

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Ishirini na Moja - 4 Julai, 2009

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010
Wizara ya Miundombinu**

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka juzi nilipokuwa naahirisha Kikao ilikuwa ni kwa madhumuni ya Kamati ya Miundombinu itusaidie kwa kukutana tena na Serikali ili kuweza kupata uhakika wa Hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo.

Kamati ilikutana, kwahiyo kabla sijawaita Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ili aweze kutupa taarifa.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU MHE. ALHAJI MOHAMMED MISSANGA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mbunge wa Ilemela, Hoja ya kufanya Mabadiliko ya Matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo ndani ya Kifungu au *Sub Vote 2005*, kinachojulikana kama *Transport Infrastrucuter Division*, Fungu 98, la Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Diallo, ya kufanya mabadiliko ya matumizi kama nilivyoeleza hapo juu.

Chini ya Kanuni ya 102 (1), Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, aliwasilisha Hoja ya kufanya Mabadiliko ya Matumizi ya

fedha za Miradi ya Maendeleo ndani ya Kifungu *Sub Vote* 2005, *Transport Infrastructure Division*, Fungu 98, Wizara ya Miundombinu kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, *Item* 4123, Dumila, Kilosa Road; ambayo imetengewa bilioni 8,760,000,000/= fedha za ndani. Na *Item* 4134, Barabara ya Handeni – Mkata, kilometa 54; ambayo ilitengewa bilioni 6,940,000,000/=. Na *Item* 2326, Magole – Turiani – Mziha – Handeni, ambayo ilitengewa shilingi milioni 200,000,000/=. Jumla ya fedha ni shilingi bilioni 15 na milioni 900, ambapo alipendekeza mabadiliko ya matumizi hayo, kuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, alipendekeza kwamba *Item* 4196, ya Dodoma – Babati; ipewe au itengewe shilingi bilioni 8,760,000,000/= na *Item* ya 4195, ambayo ni ya Dodoma kwenda Iringa; ipewe Shilingi bilioni 6. Na *Item* 4187 ya Ubungo – Chalinze; ipewe milioni 940/= na kufanya jumla ya shilingi bilioni 16 na milioni 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja hiyo iliwasilishwa mbele ya Kamati ya Miundombinu kwa kushirikiana na Wabunge wengine kwa mujibu wa Kanuni Namba 114 (8), pamoja na Serikali, ilijadili hoja hiyo kwa kina na kwa uangalifu mkubwa.

Kwanza kabisa Mtoa hoja Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mbunge wa Ilemela, alipewa fursa ya kutosha ya kuwasilisha Hoja yake na baada ya majadiliano kumalizika, alipewa fursa nyingine ya kuhitimisha hoja, ambapo alionesha kuridhishwa na namna mjadla ulivyokwenda.

Aidha, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo; naye alipewa fursa ya kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusiana na Hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kujadiliana na kutafakari kwa kina, inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, kwa siku zijazo, Mbunge mwenye tatizo au hoja mahususi katika Wizara Fulani, ni vema akaenda kwenye Kamati husika kuwasilisha hoja yake ili ijadiliwe na kuzingatiwa na Kamati husika kabla ya Kamati haijakamilisha kazi yake na kuandika Taarifa yake kwa ajili kuwasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

(ii) Mheshimiwa Spika, ni kwamba itakuwa ni jambo la busara kuendeleza Utamaduni wetu tuliouridhi kwa Waasisi wetu wa Taifa hili, wa kujenga umoja wa Kitaifa bila ya kuathiri haki ya Mbunge, ya kuwawakilisha wapiga kura wake badala ya mtazamo wa kibinadamu Majimboni.

Mheshimiwa Spika, Kamati kabla ya kufikia uamuzi wake kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, ilizingatia mambo muhimu yafuatavyo:-

(a)Serikali katika kutekeleza majukumu yake, inaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

(b)Maelezo ya Mheshimiwa Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, kuwa barabara ya Iringa – Dodoma – Babati, inahitaji fedha za kutosha ama kutoka ndani au kutoka nje kwa wafadhili.

(c)Maelezo ya Serikali kuwa kipande cha Dodoma – Iringa, Serikali imeshafikia hatua nzuri kupata ufadhili wa ADB kiasi kwamba makubaliano au Mkatata kati ya Serikali na ADB yatakamilishwa hivi karibuni. Na hivyo sio busara kuanza ujenzi kidogokidogo kwani Mfadhili anaweza kubadilisha mawazo kwa kuona kuwa kumbe tuna uwezo wa kujenga barabara hiyo wakati uwezo huo hatuna.

(d)Vilevile maelezo ya Serikali kuwa inaendelea na mazungumzo kati yake na ADB kuhusu barabara ya Dodoma – Babati na kwamba yapo matumaini ya kupata ufadhili wa Benki hiyo, lakini mazungumzo hayo hayazuwii Serikali ya Tanzania kuanza ujenzi wa awali kama vile madaraja, kwa kutumia fedha za ndani.

(e) Ni ukweli kuwa barabara ya Iringa – Dodoma – Babati, ni sehemu ya barabara ya kihistoria ya *The Grate North Road* na ni muhimu kwa ajili wa mikoa ya Kusini, Kati kwa maana ya Dodoma na Mikoa ya Kaskazini, na hivyo inahitaji hatua za haraka za ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona sio busara kufuta na kufanya mabadiliko ya matumizi ya miradi ya maendeleo ndani ya Kifungu, *Sub Vote 2005, Transport Infrastructure Division*, Fungu 98, la Wizara ya Miundombinu; kwani miradi hiyo pia ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwa ujumla. Na kwamba tukifanya mabadiliko hayo tutawakatisha tamaa na kuwasononesha wananchi wa maeneo hayo. Baada ya maelezo hayo ninayo heshima kuwasilisha ushauri wa Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, kama ifuatavyo:-

(i)Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dumila – Kilosa, kiasi cha shilingi 8,760,000,000/= pamoja na ile ya Handeni – Mkata, kiasi cha shilingi 6,940,000,000/= zinabaki kama zilivyopangwa na Serikali. (*Makofi*)

(ii)Serikali itafute fedha kutoka katika mafungu mengine kiasi cha shilingi bilioni 45,000,000,000/= ili kuanza ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati, hasa fedha itakayomwezesha Mkandarasi kufanya *mobilisation*. (*Makofi*).

(iii)Ushauri huu umekubaliwa na Mtoa Hoja, Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, wakati anahitimisha hoja yake katika Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu, kuwa baada ya kufikia uamuzi au ushauri huo, tumefanya mawasiliano na Serikali na kuitaarifu msimamo wa Kamati yangu kuwa tuuache mpango wa Serikali uendelee kama

ulivyopangwa, lakini Serikali itafute walao kiasi cha shilingi bilioni 45, ili ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati, uanze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali imepokea na kuukubali ushauri huo na kwamba itautekeleza mapema iwezekanavyo. Kutokana na ahadi hiyo ya Serikali, Kamati yangu inalishauri Bunge lako Tukufu kwamba likubali kupitisha jumla ya shilingi 841,298,364,000/= kama zilivyoombwa na Wizara ya Miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na jambo ambalo nimeletewa kama hoja kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Nzega, Lucas Seleli, ambalo ilitakiwa nilitolee uamuzi.

Nalo kwa kifupi tu, yeye anadai kwamba baadhi ya barabara ambazo Serikali imeingia Mkataba na Makampuni kadhaa kiasi cha siku nane tisa zilizopita, zilikuwa hazikutengewa fedha kwa makusudi hayo na Bunge. Kwa hiyo, zinatarajia fedha za Bajeti za mwaka huu. Kwa maana hiyo hiyo inaweza kuwa ni kasoro kubwa sana.

Sasa Maelezo ya Serikali ndio nimeyapata sasahivi hapa Mezani, na kwahiyo siwezi kutoa uamuzi wangu kwasababu ni lazima yachambuliwe na Katibu wa Bunge. Kwa hiyo nasema tu kwamba nitahitaji muda kidogo, kama tukiweza ninaweza kutoa uamuzi kabla ya saa 7.00 baada ya wataalamu kufanya uchambuzi. Vinginevyo nadhani tuisubiri hilo, tuendeleo na shughuli kwa mtiririko ambao umekwishapangwa.

Basi Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge, kuchangia kwa siku moja unusu; sasa ni wakati wa kuwasikiliza Naibu Waziri na hatimaye Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Mtakumbuka kwamba tuliirejesha ile Kanuni ya dakika 60 kwa ajili ya Wizara hii, kutokana na uzito tu na wingi wa masuala ambayo Wizara hii inayashughulikia. Yaani awali tulitengua takribani Wizara zote, ukiacha ya Waziri Mkuu, ambayo Kanuni inasema Wazi anatumia muda wowote; lakini Wizara zote nyingine zilipewa dakika zisizozidi dakika 30 kuhitimisha hoja, lakini hii tulirejesha ikawa dakika 60.

Kwahiyo, wanazo dakika 75, yaani Naibu Waziri na Waziri. Sasa Naibu nadhani anaanza kwa dakika 25 na Mtoa Hoja, Waziri kwa dakika 50.

Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Miundombinu.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nijumuike katika orodha ya wachangiaji wa hoja hii ya Makadirio ya Wizara yetu ya Miundombinu, fursa ambayo nitaitumia kwa kusaidia kujibu baadhi ya Hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, hususan zile zilizojitokeza wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Lakini kabla sijaanza kufanya hivyo naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na afya njema hadi hii leo. Na hasa kipekee kwa kuniokoa kwa ajali mbaya ya barabara iliyonipata mwishoni mwa mwaka jana, nikiwa safarini kikazi Mkoani Singida. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuninusuru katika ajali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu ya kuendeleza ridhaa yake ya kuniwezesha kutumikia nafasi aliyonipa katika Wizara hii.

Aidha namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa maelekezo na usimamizi wake wa karibu katika utendaji wangu wa kazi za Serikali zinazoihusu Wizara hii na hata Bungeni pia.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, kwa jinsi anavyoendelea kunishirikisha katika masuala mbalimbali ya kuiongoza na kuisimamia Wizara hii.

Lakini pia naomba niwashukuru watendaji wakuu na watumishi wote wa Wizara pamoja na wa Taasisi zote chini ya Wizara hii ya Miundombinu, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Injini Omari Chambo, kwa ushirikiano ambao ameendelea kunipa toka nihamishiwe kwenye Wizara hii, mwaka mmoja uliopita. Ushirikiano wao wanaonipa unanifanya nizowee kwa haraka kukabiliana na changamoto nyingi na ngumu za utekelezaji wa majukumu yangu Wizarani, nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia nishukuru sana kwa faraja kubwa ninayopata kutoka kwa Mke wangu Mpendwa Vaileth, kwa kuwa msaada mkubwa kwangu kwa kunitunza na kuwa karibu nami sikuzote katika mambo yote, magumu na mepesi.

Nimalizie shukrani zangu kwa kwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa na uvumilivu wao kwangu, na hasa wanaponikosa kwa shughuli mbalimbali za Jimboni wakati nikitumikia shughuli nyingine za Kitaifa.

Naomba waendeleo na moyo huo, nami naahidi kuendelea kushirikiana nao na kuwatumikia kwa kuwakilisha hapa Bungeni na kwingineko, na siku zote nawaomba tulenge kusonga mbele, kujiletea maendeleo katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Chamwino kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, sasa naomba nijielekeze katika mchango wangu kwa kujibu baadhi ya hoja za waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimetangulia kusema. Lakini pengine nitangulie kwa kusema kwamba, Naunga Mkono Hoja. Na ili mipango yote iliyopendekezwa kwenye hoja hii iweze kutekelezwa, naomba pia Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wote pia tuunge mkono. Wingi wa michango yenu katika hoja hii ni kielelezo tosha na cha wazi ya kwamba sekta hii ya Miundombinu, inagusa maisha ya wananchi wote wa Tanzania kwa maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi. Michango yenu yote ni ya muhimu sana, tutaifanyia kazi. (*Makofi*)

Lakini kwa vile muda hautatosha kujibu hoja zote, kwangu mimi hata kwa mtoa hoja mwenyewe, tunatangulia kuahidi ya kwamba hoja zote mlizotoa, tutazijibu kwa maandishi na kuwapatieni. Lakini ninataka tu niahidi ya kwamba kama ilivyo utamaduni wetu, wale wote aliochangia hoja hii kwa mdomo na kwa maandishi watatambuliwa rasmi na Mtoa Hoja mwenyewe. Na baada ya hayo naomba sasa nijielekeze kwenye baadhi ya majibu ya hoja hizo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ilijitokeza hoja ya kwamba serikali ijenge barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma, kwa lami ili kukamilisha Ukanda wa Kati na kuboresha bandari ya Kigoma. Hoja hii ilichangiwa na Wabunge wengi kiasi, akiwemo Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Nsanzukwanko, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Sijapata Fadhil Nkayamba na wengine waliochangia katika hoja ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa.

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba barabara hii iko katika utekelezaji katika maeneo mbalimbali. Kwanza Kigoma – Kidahwe kilometa 35.7, Mkandarasi anaendelea na ujenzi. Kidahwe – Uvinza – Ilunde kilometa 104, mazungumzo kati ya serikali ya Abudhabi kupitia *Abudhabi Fund* kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa barabara hii yamekamiliwa. Mkataba wa mkopo wa masharti nafuu unatarajiwa kusainiwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Ilunde – Malagarasi – Kaliuwa kilometa 156, maandalizi ya ujenzi wa daraja la Malagarasi na barabara zake za maingilio kilometa 48, yanaendelea chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea. Serikali inafanya mazungumzo na serikali ya Saudi Arabia, ili kupata fedha za kugharamia ujenzi wa kilometa 108 zilizobaki. Kaliuwa – Urambo – Tabora kilometa 126, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za Zabuni, ulikamilika mwaka 2007. Mazungumzo na Serikali ya Kuwait kuhusu ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami yanaendelea. Sehemu ya Tabora – Itigi – Manyoni kilometa 270, naomba mtoa hoja atakuja kuielezea kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili; serikali ijenge barabara ya Nzega – Tabora, kilometa 116 ili kuondoa kero. Nayo ilichangiwa na Waheshimiwa Mgana Msindai, Lucas Seleli, Siraju Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Juma Nkumba. Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka huu wa Fedha 2009/2010 tunaomba, Serikali imetenga

kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Nzega – Tabora, kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu; ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Mingumbi – Maswa – Bariadi na barabara ya Kolandoto – Meatu; ilichangiwa na Mheshimiwa John Momose Cheyo, Fred Tungu Mpendazoe. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2008/2009, Serikali ilitenga shilingi bilioni 7 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mingumbi – Maswa – Bariadi, sehemu ya Bariadi – Lamadi. Aidha katika Bajeti ya fedha ya mwaka 2009/2010, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Bariadi – Lamadi, kilometa 70.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne iliyojitokeza ni barabara ya Iringa – Dodoma – Babati; nayo ilichangiwa na wachangiaji wengi kweli kweli, Mheshimiwa Omari Shaban Kwangw', Mheshimiwa Kusila, Mheshimiwa Bura. Kwa kifupi tu ni kwamba kwasababu barabara hii ina maelezo mahususi, nayo vilevile nitamwachia mtoa hoja atakuja kuitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ni miundombinu ya reli, barabara na bandari, kupewa kipaumbele katika kujenga na kuchochea ukuaji wa uchumi na kuinua sekta ya kilimo. Wachangiaji walikuwa ni pamoja na Mheshimiwa Juma A. Ngasongwa, wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Susan Lyimo, na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro.

Hapa tunasema tu kwamba jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu nchini zinaendelea na mojawapo ya mikakati ya kuchochea ukuaji wa uchumi na kuinua sekta ya kilimo nchini, miundombinu bora itasaidia kupeleka pembejeo katika maeneo ya uzalishaji na kupeleka mazao kwenye masoko. Serikali itaendelea na juhudi za kuiimarisha miundombinu hiyo kadiri hali ya upatikanaji wa fedha itakavyokuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita ni kwamba pamoja na mpango wa muda mrefu uliopo wa ujenzi wa barabara ya Nata – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika.

Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Kadika Telele; na hapa tunatoa majibu ya kwamba katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.55. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 400, kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina na shilingi bilioni 1.15 zitatumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

Aidha katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 kiasi cha shilingi bilioni 1.3 zitatengwa kwa jili ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri, haukukamilika katika mwaka wa fedha wa 2008/2009,

badala yake mchakato utakamilika mwezi Julai mwaka huu. Na katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, jumla ya shilingi milioni 132 zilitengwa kugharamia matengenezo ya barabara hiyo. Matengenezo yalipangwa yafanyike kwa fedha, zimetumika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Manyoni – Isuna, ukamilishwe haraka. Mchangiaji alikuwa Mheshimiwa Juma Killimbah wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, wa Viti Maalum, Mheshimiwa Joyce Martin Massunga wa Viti Maalum; na majibu hapa ni kwamba muda wa miezi 36 kwa ujenzi wa kipande cha Manyoni – Isuna kilometa 54, ni muda ambao uliwekwa kwenye mkataba. Na ninadhani kwamba kwa muda huo barabara hiyo itakuwa imekamilika kwa mujibu wa mkataba ulivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, nane; hapa kulikuwa na pongezi kwa kutenga fedha shilingi bilioni 12.5 kwa ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongolosi. Wachangiaji walikuwa Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa na baada Mheshimiwa Benson Mpesya.

Ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongolosi kilometa 115, sehemu ya Mbeya – Luandilo kilometa 36, umeingia mgogoro wa kimkataba kati ya Serikali na Mkandarasi, na sasa suala hilo lipo Mahakamani. Lakini ujenzi wa sehemu ya mradi unasubiri maamuzi ya Mahakama.

Lakini mchakato wa kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Luandilo – Chunya kilometa 40, umekamilika na mkataba umesainiwa tayari kwa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tisa; ni kwanini barabara ya Chalinze – Segera – Tanga, inajengwa kutoka njia moja kuwa njia mbili, yaani *Dual Carriage* na inaingia barabara ya Chalinze – Dar-es-Salaam, yenye njia moja? Aidha ilishauriwa kwamba barabara ya Chalinze – Dar-es-Salaam, ndio ingefaa ijengwe njia mbili ili iweze kupunguza msongamano wa magari.

Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Selelii. Majibu ni kwamba barabara ya Chalinze – Segera – Tanga, haijengwi kwa njia mbili, yaani *Dual Carriage Way*, barabara hii ili ijengwa miaka ya 90 kwa msaada wa Serikali ya Denmark.

Wakati wa ujenzi wake ilijengwa bila ya mabega ya barabara, yaani *shoulders*, hivyo ukarabati unaoendelea sasa unafanywa chini ya ufadhili wa Serikali ya Denmark, ili kurekebisha kasoro hiyo kwa kujenga mabega na kuweka tabaka lingine la lami.

Mheshimiwa Spika, namba 10, Mheshimiwa Sadiq, wa Mvomero, aliuliza ni kwanini kipande cha Magole – Mvomero – Turiani kimeachwa, ni kwanini? Majibu ni kwamba kipande cha barabara ya Magole – Mvomero – Turiani hakijaachwa katika mpango uliopo wa kujengwa kwa lami barabara ya Korogwe – Dumila – Kilosa – Mikumi, yenye urefu wa kilometa 369. Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu hii ya Magole – Mvomero – Turiani, umesainiwa mwezi Juni mwaka 2009, tayari kwa kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, 11 ni mpango wa matengenezo ya barabara ya *PMMR* katika Mkoa wa Tanga, utekelezaji wake hauonekani, na ni hatua gani zimechukuliwa? Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, aliuliza swali hili.

Majibu ni kwamba mpango wa matengenezo ya barabara kwa muda mrefu, yaani *performance base management and maintainance of roads*, ulianza kwa majaribio mwaka 2004 katika mikoa hiyo. Lakini mkakati wa kuwapata Makandarasi kwa ajili ya mpango huu, ulianza kwa pamoja katika mikoa ya Tanga, Mwanza na Rukwa.

Kwa upande wa mkoa wa Tanga, zabuni zilizorejeshwa zilikuwa na gharama kubwa kupita Bajeti iliyowekwa, hivyo iliamriwa kurudia mchakato huo. Hii ndio sababu ya mpango huu kuchelewa katika Mkoa wa Tanga.

Hivi sasa mchakato wa kuwapata Makandarasi umekamilika na kazi zimeanza mwezi Mei mwaka huu 2009. Kazi zinaendelea na kuchonga barabara, kuweka changarawe, kujenga makalavati na kuchimba mifereji ya maji. (*Makofi*)

MICHANGO YA MAANDISHI

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa kazi nzuri inayofanyika katika kuboresha miundombinu yetu. Kipekee kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mtendaji wa *TANROADS* na Watumishi wote wa Wizara ya Miundombinu kwa kufanikisha Mkataba mpya wa kukamilisha barabara ya Kagoma – Muleba – Biharamulo – Lusahunga. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu afanye marekebisho katika barabara ambazo zimepandishwa hadhi na kuwa za Mikoa kama ifuatavyo:-

Barabara ya Kyaka – Rubale isiishie hapo, bali ifike Kimeya ikipitia Rushwa – Burungura – Mubunda – Kimeya. Aidha, barabara ya Nshamba – Biirabo – Katobago ikamilishwe ifike Kabuteigi – Mubunda na kupandishwa hadhi kuwa ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, bila shaka Mheshimiwa Waziri atagundua kuwa tamko lake la jana limeacha barabara nilizozitaja katikati. Ni vyema zikaunganishwa na barabara za Mikoa zilizopo kuliko kuacha vipande vinaingiliana. Aidha, inaweza kuleta tafsiri mbaya kwa wananchi hasa ikizingatiwa kuwa uwezo wa Halmashauri ya Muleba ni mdogo sana. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba maelezo toka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu malalamiko ya fidia kwa wananchi wa Muleba waliopisha barabara ya lami Kagoma – Muleba – Biharamulo na Chato.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MGENA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana wewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Barabara (*TANROADS*), Wakurugenzi wote, Mameneja wa Barabara Mikoa na Watendaji wengine wote wa Wizara ya Miundombinu, naomba mwendelee na kasi hiyo hiyo ya kuchapa kazi ili baada ya kipindi kifupi Tanzania iunganishwe na barabara zote za Lami na barabara za Mikoa na Wilaya ziwe zinapitika wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana kusikia maombi ya wananchi wa Iramba Mashariki, mosi, kwa kuipandisha hadhi barabara ya Kiomboi – Kisiriri – Kidaru – Ibagu – Mwangeza – Kidarata. Kwa kweli wananchi wa Iramba Mashariki wana sherekea sana.

Mheshimiwa Spika, pili, napongeza sana kuchukua barabara ya Kolandoto – Halago – Mwanuzi – Sibiti – Matala – Oldeani JCT kuwa *Trunk road*. Wananchi wa Iramba Mashariki wanapongeza sana kwani barabara hii inapitia ndani ya Jimbo la Iramba Mashariki na inaunganisha Mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Mikoa ya Singida, Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, pia mimi na wananchi wa Iramba Mashariki tunapongeza sana kwa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga Daraja la Mto Sibiti mwaka huu wa fedha. Ninaloomba ni kazi hii ianze mapema, kwani Mto huwa unafurika toka mwezi Desemba mpaka mwezi Mei mwishoni. Naomba tutumie kiangazi cha mwaka huu ili ikifika Desemba kazi iwe imefikia sehemu nzuri. Ninaomba sana pia barabara ya Singida, Ilongero, Mtinko Nkungi – Kidarata ambayo ni barabara ya Mkoa nayo ipewe uzito wa aina yake hasa kipande cha Nkungi Kidarata ambacho kinaunganisha Mkoa wa Singida na Manyara.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Iguguno – Nduguti, Gumanga ilitengenezwa vizuri sana na Kampuni ya Kichina, tatizo lililopo ni kati ya Iguguno na Kinyangiri ambako kuna mafuriko kila mwaka na *drift* au dirifuti, lililojengwa pale halihimili mafuriko ya eneo hilo. Naomba sana mahali hapo pajengwe daraja la kudumu. Pia kipande cha barabara hiyo hiyo kati ya Nduguti (Kamulungu) na Gumanga, kipande hicho hakikujengwa na Wachina, kwa hiyo, bado kinasumbua. Naomba Wizara yako itenge fedha za kutengeneza eneo hili lipitike wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa unafahamu kilio cha Wananchi wa Mji mdogo wa Iguguno baada ya barabara ya Lami kupita nje ya Mji mdogo na lami ya kuingia Mjini kujengwa upande mmoja. Mheshimiwa Rais alipotembelea Iramba Mashariki aliahidi kutoa fedha za kumalizia kipande kilichobakia na pia kutengeneza vizuri kona ya barabara inayoingia Iguguno ukitokea Singida. Kutokana na matengenezo ya barabara hiyo imeanza kuleta mafuriko maeneo ya chini ya mji wa Iguguno, naomba tatizo hilo lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba kipande cha barabara kati ya Nkungi Tambi na Nduguti itengenezwe, Daraja la Mto Ndurumo limekatika kwa chini, nalo litengenezwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ezekieli Chibulunje na wafanyakazi wao kwa hotuba yao nzuri na kazi nzuri walioifanya katika mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwa Waziri, Naibu Waziri, wafanyakazi wa Wizara ya Miundombinu na *Manager* wa *TANROAD* wa Mkoa wa Mara kwa kazi nzuri walioifanya kukarabati barabara muhimu za Jimbo la Serengeti katika mwaka 2008/2009. Kwa hakika Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wa Mara alisimamia kazi hii vizuri sana. Hongera Meneja wangu, endelea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika ilani ya CCM ya 2005 – 2010 inasema kuwa barabara ya lami itatengenezwa toka Makutano – Natta – Mugumu – Tabora B – Mto wa Mmbu hadi Arusha na itakamilika ifikapo mwaka 2010. Kinachosikitisha, hadi leo hamna kazi yoyote iliyoanza kutengeneza hii barabara kwa kiwango cha lami. Wananchi wa eneo hili wanalalamika kuwa wamesahaulika kabisa na huenda wakatolea hasira zao kwa kupiga kura kwa kinyume kichotegemewa. Tafadhali, naomba majibu ya kuridhisha kuhusu ni lini kazi ya kutengeneza hii barabara kwa kiwango cha lami itaanza.

Mheshimiwa Spika, katika ilani ya CCM ya 2005 – 2010, imeandikwa kuwa kiwanja cha Kimatatifa cha ndege kitajengwa Mugumu Wilaya ya Serengeti. Hadi sasa hamna chochote kilichofanyika. Je, ni lini kazi hii itaanza? Naomba majibu ya kuwapelekea wapiga kura wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. DUNSTAN D. MKAPA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri, nami ninaiunga mkono hoja hii.

Pili, napenda kuwapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge, niliuliza swali linalohusu ujenzi wa daraja kwenye Mto Lukwamba katika Kata ya Napacho Wilayani Nanyumbu Mkoa wa Mtwara. Serikali ilijibu kuwa daraja hilo litaanza kujengwa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ambao unaanza leo tarehe 01 Julai, 2009.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jibu hilo la Serikali ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu athibitisha wakati wa majumuisho kama daraja hilo litajengwa kama ilivyoahidiwa.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia natoa pongezi kwa Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Dr. Kawambwa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Chibulunje, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Kwa kuwa nilichangia katika hotuba ya Waziri Mkuu, ni tumaini langu nitapata majibu yangu. Sioni sababu ya kuchangia tena. Mchango wangu ulikuwa katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba barabara ya Itigi – Tabora – Kigoma iangaliwe kwa kukamilisha ahadi ya Waziri Mkuu aliyotoa katika bajeti ya mwaka 2008/2009 ya Shilingi bilioni 10 ambazo hazikukamilika katika matumizi yake. Pamoja na hayo barabara hiyo bado sehemu korofi hazikuweza kupitika masika yote. Naishauri Serikali isimamie utekelezaji wake kwa Makandarasi.

Utengenezaji wa barabara ya kwenda Tabora – Ipole, Kitunda na Ipole – Koga, kwa kutengeneza barabara hizo zitachangia kufungua Mkoa wa Tabora kwa kati ya Mkoa wa Mbeya na Rukwa. Pia itasaidia sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kufika Jimboni kwake kwa ukaribu zaidi. Naomba barabara ya Ipole – Koga – Inyongo iangaliwe, kwani ni njia anayopita Waziri Mkuu kama Mkuu wa Nchi. Wataalam hao waiangalie.

Barabara ya Tabora – Nzega kilomita 110 (80) ni vyema sasa kwa mwaka huu wa fedha ikamilike kwani kwa kujenga barabara hiyo itasaidia kufungua Mkoa wa Tabora kwa Mwanza, Shinyanga kwa kuunganika njia kubwa.

Barabara ya kilometa taty itokayo Tabora Manispaa kwenda Urambo mpaka sasa haijakamilika na inaleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo na wakazi wa pembeni ya njia hiyo. Mkandarasi huyo anasuasua sana.

Mheshimiwa Spika, niliomba ufuatiliaji wa huduma mbovu ya *TRL* kwa abiria watumiao usafiri huo. Kwani hiyo *Train ya Express* ni sumbufu, haina bafeti (*buffet*) na huondoka bila ratiba inayoeleweka. Wameondoa huduma ya usafiri na behewa la kusafirishia mizigo midogo midogo ambayo hufungwa kwenye mabehewa ya abiria (*parcel*). Ni vyema behewa hilo likarudishwa kama zamani na ilisaidia sana. Behewa hilo ni muhimu. Pia warudishe huduma ya usafi wa njia ya reli kwa wale mafundi wa njiani (pigilia) Gange ili waweze kulinda usalama wa Reli angalau kwa kilomita chache.

Mheshimiwa Spika, Uwanja wa Ndege wa Tabora ni muhimu sana kwa Taifa letu kwani kutotenga fedha za Ukarabati na kiwanja hicho ni kuvunja huduma ya ndege kwa Mkoa wa Tabora kwani wakati wa masika huwa unajaa tope.

Naishukuru sana Serikali angalu kwa mwaka huu 2009/2010 imetenga fedha za kuanzia ambazo ni za ndani. Naomba Serikali iendelee na mikakati ya kuomba wafadhili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MUSSA AZZAN ZUNGU: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza sana kwa bajeti ya mwaka huu. Mpango wa ujenzi wa *Airport* na upanuzi wa uwanja huu wa J.K. Nyerere, maamuzi yatazamwe upya, gharama ya fidia ni kubwa sana, eneo linalozungumziwa ni dogo na kwa hali ya kimataifa hakuna nchi inayojenga uwanja wa ndege mjini.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali sasa itoze *road toll* kwenye *high way* zote na pesa zitumike kujenga au kukarabati barabara na ikaribishe wawekezaji kujenga kwa gharama zao na *wa-recover through toll*.

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Miundombinu kwa jinsi wanavyojitahidi kutekeleza ilani ya CCM na ahadi zilizowekwa kwa utekelezaji wa mwaka 2005 – 2010 hali inaonyesha inaridhisha kwa maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kuishukuru Serikali ya awamu ya tatu ambayo iliacha mipango mingi ya Wizara hii na hivi sasa awamu ya nne inatekeleza kwa kasi kubwa sana. Sisi watu wa kusini tumefarijika sana kwa matengenezo ya barabara ya Kibiti – Lindi kiwango cha lami, lakini hadi sasa kilomita 60 zimesalia kukamilika. Pamoja na kazi nzuri zinazofanyika, naishauri Wizara hii, Mheshimiwa Waziri atembelee ili kujionea kazi hii nzuri lakini ili kutia msukumo, kazi hii iende kwa viwango na haraka kwani hadi sasa kazi inakwenda taratibu mno na wananchi wanaendelea kupata shida kwani eneo hili hutumia kupita kwa masaa 2 – 3 hivyo kutenda kwao kazi kwa kazi kutasaidia kuondoa kero kubwa ambayo ilikuwepo tokea tupate uhuru.

Mheshimiwa Spika, pili, wananchi wa Wilaya ya Masasi na Nanyumbu wanaishukuru Serikali kwa kuweza kutafuta wafadhili na kuweza kuanza kutengeneza barabara ya Masasi – Mangaka.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imeshaanza matengenezo kwa kiwango cha Lami lakini zipo kasoro ambazo nitaomba nipatiwe ufafanuzi.

1. Utengenezaji wa *Round – about* katika makutano ya njia nne, yaani barabara itokayo Lindi – Nachingwea – Newala – Tunduru katika eneo la *Bus stand* Masasi.
2. Uwekaji wa *Calvats* au vivuko katika maeneo muhimu kama kutoka barabara kuu kuingia katika maeneo ya Shule ya Msingi au Sekondari – Magala – Zahanati hasa katika maeneo ya sululu ambako vivuko hivyo havipo kabisa.

3. Utengenezaji wa mifereji kwa barabara yote.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu haya, kwani wananchi wamekuwa wakihoji, nasi viongozi hukosa majibu. Tunamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI alipofanya ziara Wilaya ya Masasi alisaidia sana kuona barabara hii na yale mapungufu tuliyomweleza alichukua jukumu la kumwita Meneja wa *TANROAD* ili kusaidia kutoa ufafanuzi. Katika kikao hicho, Meneja alieleza kuwa matengenezo ya *round about* hayapo katika mchoro, fedha ya matengenezo ya mifereji iliyopo haitoshi kutengeneza mifereji kwa barabara yote na vivuko ni makosa ya Mkandarasi.

Hivyo naiomba Wizara ione umuhimu wa mambo hayo matatu kwani kama sehemu ya makutano ya barabara hii, ajali nyingi tayari zimeanza kujitokeza, kukosa mifereji ya kudumu, ubora wa barabara hii utapungua na kukosa vivuko ni adha kubwa kwani maeneo hayo ni muhimu kwa matumizi ya kila siku na wakati wa msimu ambapo magari yanatakiwa kuingia hadi kwenye magHala kusomba mazao. Nategemea busara itatumika ili kuiborehsa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la *round about* ni muhimu kupewa kipaumbele; kama haiwezekani kujengwa, basi hata taa za *Solar* ziwekwe ili kuongoza vyombo vya usafiri na wananchi kupita kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi tumekuwa tukiomba kazi nyingi za ujenzi zipewe kipaumbele Kampuni za wazalendo hapa nchini ili kuwajengea uwezo na uzoefu tukiamini kuwa wao kwa kutumia uzalendo wao wanaweza wakafanya kazi vizuri zaidi na hatimaye tukaacha na kuyatumia makampuni ya nje hata katika kazi za ukarabati wa miundombinu ya maji machafu kama ilivyo hivi sasa katika jiji la Dar es Salaam linalowatumia Wachina kurekebisha mifereji ya maji machafu, haya sio maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hili, nampongeza Rais - Mheshimiwa Jakaya Kikwete na *Board* ya Wakandarasi kwa mara ya kwanza kwa kuwatunuku tuzo Wakandarasi wazalendo ambao wanafanya kazi zao vizuri ikiwemo Kampuni toka Mtwara Wilayani Masasi iitwayo *Makapo Construction*. Hongera sana. Hii imeonyesha kuwa sasa tuna makampuni bora hapa nchini ambayo yanastahili kupewa nguvu ili kuleta ufanisi wa kupunguza gharama kubwa ya kuwachukua Wakandarasi toka nje.

Rai yangu kwa Waziri ni kumwomba afanye ziara kutembelelea eneo hili lililobakia ambalo ni barabara ya Kibiti – Lindi ili kutoa msukumo na barabara ya Masasi – Mangaka ili kujionea maendeleo ya barabara hii na mapungufu niliyoyainisha katika mchango wangu. Mwisho, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. GIDEON A. CHEYO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa hotuba yake nzuri inayojitosheleza kwa kiasi kikubwa. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika ngazi ya

Wizara, Mikoa na Wilaya, kwa utendaji wao wenye ushirikiano na mwelekeo wa kuboresha sekta ya Miundombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuunga mkono hoja hii, napenda kuchangia machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kauli yake aliyoitoa juzi Bungeni kuhusu upangaji wa barabara katika hadhi stahili. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ileje, napenda kutoa shukrani kwa Wizara kukubali maombi yetu ya kupandisha hadhi ya barabara zifuatazo:-

- (a) Mpemba - Isongole (Tanzania/Malawi Border) kuwa barabara ya *Taifa (Trunk Road)*; na
- (b) Itumba – Izyila – Hansamba, kuwa barabara ya Mkoa (*Regional Road*).

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ileje iko katika harakati endelevu ya kupanua na kuimarisha biashara na nchi jirani ya Malawi na Wilaya tunazopakana nazo za Mbozi, Mbeya Vijijini, Rungwe na Kyela. Kwa hiyo, uamuzi wa kuzipandisha hadhi barabara hizo mbili utachochea jitihada hizo na kuongeza kasi ya maendeleo katika Wilaya yetu ya Ileje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo, bado tunaendelea kuiomba Wizara iendelee kuyafikiria maombi yetu mawili ambayo hayajapata kibali. Kwa kuzingatia viegezo vya kiuchumi, ulinzi na usalama, amani na utulivu na kisiasa, Wilaya yetu ya Ileje tunaomba Wizara iendelee kufikiria maombi yetu kwa barabara mbili zifuatazo:-

- Katengele/Sange – Ngulughulu – Kisyesye – Kapeta (Mgodi wa Kiwira);
- Lusisi – Bwenda – Ngulilo – Ilembo (Mbeya Vijijini).

Hizi tunaziomba kuwa barabara za Mkoa. *TANROADS* Mkoa wa Mbeya wana taarifa hizi. Kwa wakati muafaka tunamkaribisha Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri kutembelea Wilaya ya Ileje kujionea hali halisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa miradi ya barabara inaibuliwa na kuongezeka na pia fedha nyingi zinakwenda kwenye sekta ya barabara katika ngazi ya Halmashauri na kwa kuwa kuna upungufu wa Wahandisi wa barabara, tunaomba Wizara ya Miundombinu iendelee kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha wataalam wanaohitajika wanapatikana ili miradi isikwame na itekelezwe kwa viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi za pekee kwa *Engineer* Kilewo, Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Mbeya kwa ushirikiano wake mzuri na wepesi wa kushughulikia matatizo ya barabara katika Wilaya ya Ileje. Tunamtakia yeye na wenzake kazi njema.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja hii.

MHE. MERYCE M. EMMANUEL: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Miundo Mbinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa ujumla kwa kuandaa bajeti hii muhimu sana yenye kuleta matumaini makubwa sana na hasa ikitekelezwa kama jinsi tulivyoisikia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba *TANROAD* wamekuwa wakifanya kazi nzuri kabisa ya matengenezo ya barabara zetu. Lakini ningependa nichangie kidogo upande wa upangaji wa vifusi barabarani, kuwa vifusi hivyo huchukuwa muda mrefu sana bila kusambazwa vikiwa vinasubiri kuhesabiwa.

Mheshimiwa Spika, ukaaji wa muda mrefu wa vifusi hivi husababisha hata ajali kwani inabidi mabasi na magari makubwa yapite upande upande. Nashauri kuwa umuhimu wa kuhesabu vifusi ni wa msingi, ila Mkandarasi ajitahidi sana kufanya mawasiliano ili wafanye haraka kuhesabu vifusi ili viweze kusambazwa kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la barabara zetu hizi kubwa kukarabatiwa kila mwaka, hii inatokana na uzembe na kutofikia kiwango kizuri cha matengenezo yanayotakiwa. Naishauri tu Serikali kwamba wajaribu kuweka msisitizo kabisa kwa Wakandarasi waweze kufikia kiwango kinachotakiwa na zaidi tu niombe pia Serikali nayo ijitahidi pia kutoa pesa inayokidhi matengenezo hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nichangie machache kuhusu matengenezo ya barabara ambayo iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Barabara ya Mwigumbi Maswa, Baridi hadi Lamadi, ningependa kujua na wananchi wa maeneo hayo wana hamu sana kujua: Je, barabara hiyo inatarajiwa kutengenezwa lini? Je, inawezekana kufika wakati wa uchaguzi 2010 ikiwa bado na dalili zozote za matengenezo kuonekana? Naomba wananchi wa Maswa – Mwigumbi (Kishapu) baridi na Lamadi wapewe majibu yenye matumaini makubwa kwani kitabu hiki cha Ilani ni Msaafu Mtakatifu wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Waziri pamoja na Wizara, kutuondolea kero kwenye barabara ambazo ulikuwa ni wimbo hapa Bungeni. Kagoma Rusahuga haba na haba hujaza kibaba. Sasa tunakwenda kwenye Bandari zote, ifanyike mikakati madhubuti kabisa na ni kero, usafiri wa majini *Victoria* hata yenyewe kero bado ipo pamoja bandari ya Kemondo Bukoba mjini. Hizi bandari na zenyewe ni tatizo ukilinganisha na zilizopo mpakani mwa Uganda na Kenya, Rwanda na Burundi. Ikitengenezwa mojawapo itaweza kuongezea kipato kwenye Manispaa yetu. Pia tunaomba chombo cha usafiri wa majini kwani MV. *Victoria* imezeeka inanzidi umri chonde chonde tusaidiwe tunasafiri kimashaka kila usafiri kwenye Mkoa wa Kagera.

Uwanja wa Ndege sikuelewa kwa sababu umeunganishwa na kiwanja cha Mpanda. Je, wa Bukoba umetengewa shilingi ngapi na tujue tuweze kuchochea Mkandarasi aibu sana. Viongozi wetu Wakuu kushukia Geita kwa sasa hivi wanashukia Geita.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua mara kwa mara Wakandarasi wakisimamishwa na Mkandarasi anatupeleka Mahakamani Serikali akipigwa hasara: Je, tumlaumu nani? *TANROAD* au ni Wizara? Au ni njia ya rushwa? Wizara tuwe makini!

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo lingine. Kuna kivuko cha Bukoba vijijini kati ya Kijiji cha Busugo kuvuka kwenda Kasharu, tatizo kubwa sana kwa wananchi ni daraja Kalebe kutoka Mgaza kwenda Ibwera: Je, wananchi hao watasaidiwa vipi kupatiwa kivuko pamoja na daraja? Viko mashakani! Mambo yote yanaweza kufanyika kwa wakati mmoja, lakini kidogo kidogo.

Tatizo lingine ni Bukoba Stesheni ya *Bus* kwani ni finyu, pili iko katikati na mji unakuwa ni usumbufu mkubwa sana na tayari kiwanja kipo nje ya mji kidogo. Ni mikakati gani iliyopo ya kuanzisha ujenzi wa stesheni hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajali barabarani. Ajali za barabarani nyingine zinasababishwa na madereva pamoja na kukosa *parking* pamoja na kutofuata vituo vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Serikali iweke Sheria ngumu sana hasa watu wa mikokotini ya kubeba mizigo wawe na sehemu yao pamoja na barabara zao tusitumie barabara moja kwa sababu wanasababisha ajali sana. Tufanye kama nchi nyingine kama Swiden, waendesha pikipiki wana barabara zao pamoja na baiskeli, watembea kwa miguu ajali kutokea ni bahati mbaya. Namtakia Mheshimiwa Waziri utekelezaji mwema.

Mheshimiwa Spika, lingine ni *VIP*. *VIP* zina matatizo hapa nchini, naomba Serikali ijaribu kuzirekebisha tena, ni viwanja vyote Tanzania nzima, zinatia aibu kwa mfano Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam, Bukoba angalau hasa uwanja wa Kilimanjaro pamoja na Dar es Salaam ni sehemu zinazotuingizia pesa nzuri. Urekebishwaji hata kama vimewekezwa virekebishwe au kuelewana na mwekezaji huyo, sivyo ulivyo kwa kipindi cha nyuma, sasa hivi umeharibika sana.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kupongeza tena, bajeti njema.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa kuzungumza kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu nilielezea kwa kina juu ya ajali ya boti iliyotokea Tanga tarehe 14 Aprili, 2009. Kwa mchango huo ninategemea kupata maelezo juu ya uzembe uliofanyika katika uokoaji kwa waliofikwa na maafa licha ya juhudi iliyochelewa iliyochochuliwa kuanzia tarehe 16 Aprili, 2009 na 17 Aprili, 2009 ambayo haikuleta tija yoyote. Tija haikupatikana kwa sababu uokoaji ulipaswa kufanywa usiku ule ule wa ajali au hapana budi alfajiri ya tarehe 15 Aprili, 2009.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kama inataka kweli biashara ya utalii ikue kwa kiasi, ni lazima Shirika letu la Ndege la *DTCL* liimarike Kimataifa, ikiwezekana kuleta

watalii wengi sana hapa nchini kwa kutegemea mashirika mengine ya ndege. Bado shirika letu haliko makini kukidhi haja hiyo. Je, Serikali ina mkakati gani wa uhakika wa kuliimarisha Shirika hilo?

Mheshimiwa Spika, uchumi wetu ungekua haraka kwa kupitia bandari zilizopo katika nchi yetu, kama ingekuwa utendaji wa Bandari hizo ni wa kiwango kinachoridhisha. Fursa tulionayo ya kuzungukwa na nchi ambazo hazina bandari hatutumii ipasavyo, matokeo yake nchi hizo hupendelea kupata huduma hiyo kwa bandari ya nchi za jirani.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ya makusudi kuhakikisha tunabadilika, vinginevyo hatutaendelea kulalamika na umasikini wetu.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu zina mabango mengi sana ya biashara kiasi ambacho baadhi ya alama za barabarani kutoonekana na wakati mwingine kwa kutoziona alama hizo husababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, ni mkakati gani wa Wizara wa kudhibiti uwekaji wa mabango hayo kwenye maeneo yanayostahili?

Mheshimiwa Spika, kujenga barabara ni jambo zuri mno, lakini barabara hizo zihahakikishwe ziko kwenye viwango vinavyostahili, vinginevyo fedha nyingi zitatumika kwenye ujenzi huo na kipindi kifupi barabara hizo zitakamilika katika kusimamia ubora wa barabara hizo. Wizara ina utaratibu gani? Ahsante.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara ya Miundombinu hasa Waziri wake Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa na Naibu wake Mheshimiwa Hezekia Chibulunje, Katibu Mkuu pamoja na Watumishi wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri yenye maelekezo mazuri ya nini cha kufanya katika wakati mgumu kama huu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na dhana nzima kama ilivyo katika hotuba hii ila tu kuna maeneo machache ambayo naomba Waziri afanue.

Kwanza, Ujenzi wa Daraja la Nangoo, Masasi katika *Trunk Road* ya kwenda Kusini. Daraja hili lilibomolewa na mafuriko ya mwaka 1990 yaliyokumba maeneo mengi ya Kusini. Madaraja mengine yameshughulikiwa lakini hili la Nangoo ambalo ndio kubwa kuliko yote, halijatengenezwa. Tumesema mara nyingi kuwa ni kazi bure kutengeneza daraja la kuunganisha Msumbiji na Tanzania pale Mtambaswala ama kujenga barabara mpaka Songea na Mbambabay bila kujenga kwanza daraja hili. *Mtwara Development Corridor Infrastructure* yote haina maana bila ujenzi wa Daraja la Nangoo.

Naomba Mheshimiwa Waziri aeleze sana kwamba ana mpango gani wa kujenga daraja hili? La sivyo, sitaunga mkono hotuba yake kwani ni miaka 20 sasa toka daraja liaribiwe na mafuriko.

Pili, hivi sasa kuna ukarabati wa barabara ya Mtwara kwenda Masasi. Huenda mpango huu unatokana na utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na *Millenium Challenge Account (MCC)*. Inasikitisha kuona kandarasi zinazofanya kazi chini ya *TANROADS* Lindi zinafanya kazi ya kulipua kweli! Sidhani kama wanaelewa kuwa uwekaji hafifu wa lami matokeo yake ni kuharibika upesi kwa lami hiyo. Kipande hicho cha Mtwara – Lindi (Mingoyo) sio imara, baada ya miaka 2 – 3 lazima kitaharibika. Hata hivyo, Ujenzi unachukua muda mrefu sana. Sasa badala ya neema kutokana na msaada wa *MCC*, tutaachiwa kilio baada ya muda mfupi kwani matengenezo ya aina hiyo hayawezi kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Wizara isisimamie ujenzi imara wa barabara badala yake tunapoteza tu fedha nyingi kwa kazi hafifu.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo kwa haya mawili ili niunge hoja ya Waziri.

MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja ya Waziri wa Miundombinu. Barabara ni kichocheo cha Maendeleo hasa kuimarisha uchumi nchini. Bila barabara, hakuna maendeleo hata kusababisha njaa. Napenda kushukuru Wizara kwa kukumbuka kilio changu cha Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai na kuendelea Kamwanga – Sanya juu. Bila barabara hiyo kuzunguka mlima Kilimanjaro Mazao ya kilimo hayatawezekana kuletwa kwenye masoko Arusha na Moshi.

Napenda kushukuru Wizara ya hii kupandisha Barabara ya Longido – Engusero Jet – Engusero – Ketumbeine – Gelai Bomba – Engaruke Jet. Barabara hii ni muhimu kwasababu inaunganisha Wilaya ya Longido na Wilaya ya Ngorongoro. Naomba Wizara ipange fedha kwa ajili ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kikao cha Mkoa *Road Board* kilipitisha barabara mbili. Kwenye Wilaya ya Longido, naomba kueleza barabara moja iliyoachwa na Kamati yako ni muhimu sana na imekidhi vigezo vyote kwani inaunganisha Wilaya ya Siha na Longido halafu inaunganisha barabara ya Namanga – Arusha na Moshi – Arusha na Rongai – Siha. Kwa sasa, hakuna barabara ya kuunganisha Wilaya ya Siha na Longido au Wilaya ya Rombo na Longido.

Wilaya ya Longido kwa upande wa Mashariki inapakana na Wilaya zote mbili ambazo ni Siha na Rombo isitoshe barabara hiyo ndiyo itakayounganisha Longido na Mkoa wa Kilimanjaro. Bila barabara hii, Longido kwenda Mkoa wa Kilimanjaro ambayo inapakana nayo ni shida sana.

Wizara haikukumbukwa mapema kwasababu ilikuwa chini ya Wilaya ya Monduli. Napenda kukumbusha kwamba bila kupandisha barabara hii ya Siha – Longido Wananchi wa Wilaya zote mbili hawatawasiliana. Kwa kuwa Wilaya hizo mbili, yaani Longido na Siha ni mpya haikuwezekana mapema kukumbukwa kuunganisha kwa njia ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nategemea maombi yangu yatakubalika wakati wa majibu ya hoja za Wabunge nami nipate majibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Miundombinu.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa nafasi hii nami nichangie kwa hoja iliyopo mbele yetu. Namshukuru sana Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Shukuru J. Kawambwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje na wasidizi wote katika Wizara hii kwa hotuba hii ya Maendeleo ya Miundombinu.

Nianze kuchangia kwa Shirika la Reli (*TRL*). Hapo mwanzo Shirika la Reli la Tanzania (*TRC*) lilikuwa linamilikiwa na Serikali pamoja na matatizo ya hapa na pale. Lakini Shirika liliweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi ukilinganisha na mwekezaji wa sasa. Mimi mwanzoni, miaka ya themanini nilikuwa mfanyakazi wa *Tanzania Railways Corporation (TRC)*, kwa hiyo, nafahamu ufanisi na matatizo ya Reli ukilinganisha na mwekezaji wa sasa kutoka India. Sipendi sana kutaja kuwa ni Mhindi, ni vizuri tuseme kuwa ni mwekezaji, hata kama angekuwa ni Mkurya au kabila lolote, mimi kwa mawazo yangu hao wote ni wawekezaji bila kujali kabila, nchi aliyotoka, awe Mzungu au Mhindi, sisi tunachohitaji ni utendaji mzuri wa kazi.

Tangu mwekezaji (*TRL*) aingie na kufanya kazi, ameonyesha udhaifu mkubwa wa utendaji wa kazi. Huwa anashindwa kulipa wafanyakazi mishahara. Ninapenda kufahamu wakati wa majumuisho, Mheshimiwa Waziri anieleze ni nani huwa anaruhusu mishahara kwa wafanyakazi ilipwe? Yaani mishahara inalipwa kwa idhini ya nani? Kama mwekezaji (*TRL*) ameshindwa, ni kwa nini Serikali isiliendeshe hili Shirika kama hapo mwanzoni?

Nimepata taarifa kuwa wafanyakazi wa zamani, yaani walikuwa kwenye Shirika la *TRC* na baadaye waajiriwa *TRL* hawakulipwa haki zao, yaani mafao kabla hawajapata ajira mpya kwa mwekezaji mpya. Napenda kufahamu ni kweli kwamba wafanyakazi wa *TRC* hawakulipwa mafao kabla ya kujiunga na *TRL*. Napenda kupata maelezo ya kina na ufafanuzi zaidi.

Naishauri Serikali itafute mwekezaji mwingine na kama mwekezaji akipatikana Serikali iwe na hisa kubwa na upande wa *Management* Shirika liongozwe na Watanzania. Tuna Watanzania wenye uwezo wa kuongoza Shirika. Kwa mfano, wakati nafanya kazi tulikuwa na Meneja Mkuu Mtanzania aliyekuwa anaitwa Tom Mmari, alifanya kazi kubwa sana na Shirika litaleta mafanikio makubwa kwa Watanzania. Lakini kwa mwekezaji wa sasa, hakuna linachofanya ni usanii wa Serikali, nayo inakubaliana kwa kuchukua mzigo wa kulipa wafanyakazi mishahara. Nashindwa kuelewa kwamba, Serikali ione kuwa mwekezaji huyo (*TRL*) hana uwezo wa kuendesha Shirika kubwa kama hili na sielewi kama Serikali haifahamu kuwa nchi inapata hasara kubwa na hasara hiyo yote ni kodi za wananchi ambao wengi wao ni maskini wa kupindukia! Hizi si nyakati za kuwaona wananchi hawana sauti katika nchi yao.

Pili, nichangie upande wa barabara. Naishukuru sana awamu ya tatu chini ya uongozi wake Rais Mstaafu – Mheshimiwa Benjamini Mkapa kwa juhudi kubwa alizozifanya wakati wa uongozi wake kwa namna barabara zilivyotengenezwa chini ya usimamizi wa aliyekuwa Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa John Magufuli. Barabara nyingi ziliwekwa lami na kwa kweli alimudu Wizara hiyo. Nina imani kuwa Mheshimiwa Kawambwa naye anaweza kwa jinsi alivyofanya juhudi za kuimarisha barabara hapa nchini. Naiomba Serikali imalizie kipande cha barabara kati ya Singida na Manyoni ili kurahisisha usafiri katika njia ya Kata.

Barabara ya Tarime – Nyamaraga ni barabara muhimu kwa uchumi wa wananchi wa Tarime na Tanzania kwa jumla. Barabara hii ya Tarime – Nyamwaga hupita katika vijiji vya Kenyanyori, Rosana, Kemakorere, Nyerero Nyamwaga na vijiji vya jirani vya Kaisangura, Mariba, Bungurere, Kobori, Itiryo, Magucha, Kangariani, Kegonga, Masanga, Mgoto, Ntagacha ambavyo huzalisha mazao kwa wingi kama vile kahawa, mahindi, ndizi, muhogo, mtama ulezi na sasa chai na Tumbaku. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke lami barabara kwa pamoja yenye kilomita 24, kuliko kuweka kwa awamu. Kama Serikali itaiweka kwa awamu itachukua zaidi ya miaka kumi kukamilika na wakati itakapokamilika, pale ilipoanza kuwekwa lami itakuwa imeharibika. Kwa hiyo, naishauri Serikali itengeneze na kuweka lami kilomita 24 kwa pamoja kuliko kujenga na kuiweka lami kwa awamu ili kuleta ufanisi na kuleta matokeo mazuri yenye tija kwa wananchi na uchumi kwa nchi. Naiomba Serikali iweke lami barabara ya mpakani mwa Kenya na Tanzania ili kuimarisha ulinzi mpakani ili Askari waweze kupita bila matatizo wakati wa vipindi vya mvua. Barabara ambayo imepitia Kata za Burmera, Mwema, Sirari, Pemba, Nyakinga, Nyamwaga, Muriba na Nyanungu itaimarisha ulinzi na kuzuia wezi wa mifugo wa mara kwa mara ambao husababisha mapigano ya koo kwa koo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza sana uongozi wa Wizara kwa kazi kubwa na juhudi za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mujibu wa Ilani ya uchaguzi. Kwa upande wa Mkoa wangu wa Dar es Salaam na Jimbo langu la Ukonga, barabara nyingi zimejengwa na nyingine zipo kwenye mpango. Napongeza sana juhudi hizi. Hata hivyo, nina michango minne kama ifuatavyo inayohusu Jimbo langu la Ukonga.

Mheshimiwa Spika, suala la fidia kwa wananchi wa kipawa, kipunguni na kigilagila sasa lifikie mwisho kwa Serikali kukamilisha ahadi yake ya kuondoa kero hii baada ya miaka 12 ya wananchi hawa kutojua hatma/haki zao.

Barabara ya kuunganisha Wilaya ya Ilala na Temeke kwa kupitia pembezoni mwa Wilaya hizi (yaani Chanika – Mvuti – Mbande) imekuwa ikijengwa kwa kasi ni ndogo sana. Imechukua sasa miaka 16 (toka 1993) bila Serikali kukamilisha ujenzi wa barabara hii ya kilometa 29.6 tu (tena kwa *otta seal*). Hadi sasa bado kilometa zaidi ya 13 na kwa kasi ya kujenga kilometa moja kila mwaka itachukua miaka 13 ijayo kukamilisha

barabara hii. Napendekeza Serikali iamue kwa makusudi kuweka bajeti ya maendeleo mwaka 2010/2011 ya Shilingi bilioni mbili ili kumaliza kabisa barabara hii.

Katika kikao cha *Road Board* (Dar es Salaam) zilipitishwa Shilingi karibu bilioni mbili kujenga kwa lami barabara ya Ukonga – Moshi Bar. Kwenye majedwali ya hotuba sijaona fedha hizi. Barabara hii ni muhimu na mbaya sana inayohitaji kipaumbele ili kuhudumia wananchi zaidi ya 100,000 wa Kata za ukonga, Chanika, Kitunda na Msongola. Wizara iangalie upya barabara hii.

Naipongeza Serikali kutoa Shilingi bilioni 20 mwaka 2008/2009 na nyingine Shilingi bilioni 8.5 mwaka 2009/2010 kujenga barabara muhimu za Dar es Salaam kupunguza msongamano. Aidha, miradi mingine inaendelea kufanyiwa usanifu. Lakini pamoja na barabara muhimu ya Twiga/Msimbazi – Kigogo – Maziwa External, pamoja na ile ya Kimara – Kilungule –*External Mandela Road*, ni lazima barabara hizi ziunganishwe pia na barabara ya *External Mandela Road* – Mabibo Jeshini – Mazda (Kisukuru) – Tabata Chang’ombe – Baracuda – Vingunguti – *Nyerere Road* ukiacha umuhimu wa barabara hii na watu wengi wanaoishi maeneo haya, barabara hii inaunganisha barabara kuu mbili ziendazo sehemu mbili tofauti (*Nyerere Road* na *Mandela Road*). Angalia kanuni za Menejimenti ya Barabara ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN PAUL LWANJI: Mheshimiwa Spika, hakuna siri kwa wananchi kwamba barabara hii ya Manyoni – Itigi – Chaya, tenda yake ya Ujenzi ilitangazwa. Mchakato wa kumpata Mkandarasi ulishaanza lakini cha kushangaza mchakato huu umesitishwa kwa sababu zisizojulikana.

Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri amei–*relegate* barabara hii kuwa iko katika hatua za upembuzi yakinifu na usanii na kuipandisha sehemu ya Tabora – Nyahua kuwa katika hatua za kumpata Mkandarasi. Toka lini Tenda ya Barabara ya Tabora – Nyahua imetangazwa? Hii ni dhahiri Wizara imeingiliwa kubadili uamuzi wake wa kuanza kujenga barabara hii kutoka Manyoni – Itigi – Chaya. Huu ni uingiliaji wa mipango ya Serikali kukidhi sababu za kisiasa. Serikali haioni kwamba tunawapa mzigo wafadhili na Serikali yenyewe kuingia gharama zisizokuwa na tija? Kweli vifaa vya ujenzi lami na kadhalika visafirishwe mbali zaidi mpaka Tabora au Kigoma kuanza ujenzi huko badala ya kuanza kazi mara moja Manyoni? Inakera pia kuona kuwa Singida ndiyo Mkoa wa kusubiri barabara ziishie hapo kujenga (*Terminal Region*).

Naiomba Serikali/Wizara itoe maelezo ya kina juu ya mabadiliko haya ya barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya ambayo (*MOU*) imesainiwa. Kisingizio kwamba kuna machafuko *Iran* sio ya kweli kwa sababu Serikali ya Iran ni ile ile. Huu ni uonevu na hujuma kwa Mbunge wa CCM kwa sababu tayari wananchi wa Jimbo langu wanasubiri Mkandarasi aanze kazi.

Mheshimiwa Spika, maelezo nimeyatoa kwenye Barua yangu ya 1/06/2009 kwa Mheshimiwa Waziri kuomba Serikali itenge fedha za kutosha Shilingi bilioni tano kwa

ajili ya ujenzi na ukarabati wa Barabara ya barabara ya Ukiwa – Itigi – Rungwa. Hakuna majibu ambayo nimepata hadi sasa. Barabara hii ilitenga fedha za mradi wa *Elnino* kujenga upya lakini mradi huu ulifutwa baada ya Mkandarasi *M/S Badri East Africa Construction Company* kushindwa kufanya kazi. Toka ufutwe fedha chache tu zimekuwa zikitengwa kujenga barabara hii (*piece meal*), mwaka 2009/2010 imetengewa Shilingi milioni 806.8 (*Periodic Maintenance*) kiasi cha asilimia 16% tu cha ongezeko la mwaka jana. Fedha za maendeleo hazijulikani.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo/ufafanuzi.

MHE. DANIEL NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, napenda nichangie mambo machache kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa Barabara Kuu za Lami lazima zitizamwe kimkakati “*Strategic*” haitoshi kujenga barabara nyingi ndogo ndogo (fupi fupi) za kujifurahisha. Tujenge barabara ambazo kwa tafsiri pana ni za kiuchumi na zitaibua na kuchochea Uchumi wa Taifa letu.

Barabara kuu za kimkakati kwa Taifa letu kwa sasa katika mazingira ya mtikisiko wa uchumi ni zifuatazo:-

Barabara ya:-

- (i) Itigi – Tabora – Kigoma;
- (ii) Iringa – Dodoma – Singida – Minjingu; na
- (iii) Tunduma – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara hizi zijengwe kwa haraka, tena fedha za ndani zitumike. Tusijiruhusu kuleta porojo, ubinafsi na utetezi wa kizamani kuhusu matumizi ya rasilimali zetu. *Let us use our Money intelligently.* Barabara nyingine ambazo nazo ni mhimu zinaweza kusubiri kwanza. Kupanga ni kuchagua na hoja ya kizamani eti sungura ni mdogo, Bajeti finyu, kwa sasa isipewe nafasi. Tushushe ndoo hapa tulipo, tutumie fedha iliyopo vizuri, kimkakati na kwa kutazama mbele.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara na kupandisha hadhi barabara, vigezo vya kupandisha hadhi barabara vitazamwe upya. Vigezo vinavyotumika sasa ni vya kizamani kabisa! Barabara zinazokwenda maeneo ya uzalishaji chakula na mazao ya biashara na sehemu za utalii yapewe kipaumbele na viwe vigezo vya kupandisha hadhi barabara hizo. Aidha, Mikoa yenye mtandao mdogo wa barabara za *trunk roads, regional roads* kama Kigoma basi zipewe *special preference* ili nazo ziwe na barabara zaidi zenye hadhi hiyo. Kwa mfano, sielewi kabisa kwa nini barabara ya Makere – Heru – Ushingo - Kipinga – *Burundi Boarder* haikupandishwa hadhi na kuwa *trunk road*! Zaidi, sielewi barabara ya Rusesa – Nyanganga – *Kazolamimba Railway Junction* – Kandapa haikupandishwa daraja na kuwa *truck road*.

Mheshimiwa Spika, nyumba za Serikali zilizouzwa kwa makosa Wilayani Kasulu/Kigoma, kwa mfano nyumba ya *OCD* Kasulu iliuzwa, nyumba ya Hakimu wa Wilaya iliuzwa na nyumba ya *DED* Kasulu iliuzwa. Zote hizo ziliuzwa kwa makosa na ni nyumba zilikuwa sehemu maalum karibu na Bomani.

Mheshimiwa Spika, ninataka kufahamu ni lini nyumba hizi zitarudishwa Serikalini pamoja na agizo la Mheshimiwa Rais na maangalizo ya Bunge. Ninataka maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege wa Kigoma ni Uwanja *Strategic*, kwa hiyo, ujengewe *runway* ya lami. Fedha zilizopo zitumike kuimarisha na kupanua uwanja huo ili pia uweze kubeba ndege kubwa aina ya *Boeing 707* na zaidi. Uwanja wa ndege Kigoma, unaweza pia kusaidia biashara ya usafiri wa ndege katika nchi zetu za Maziwa Makubwa. Fedha zilizotengwa ni pamoja na zile za uwanja wa ndege wa Mwanza. Bajeti zipambanue ni kiasi gani cha kigoma na kiasi gani Mwanza. Mambo ya jumla jumla hayasaidii na ni mtindo wa kizamani. Jenjeni uwanja wa ndege wa kigoma lami na *infrastructure* yake kama vile ofisi na kadhhalika.

Mheshimiwa Spika, barabara za Dar es salaam za kupunguza msongamano, napendekeza barabara ya Vingunguti – Chang’ombe iliyopo Wilaya ya Ilala, hii ni barabara muhimu sana. Mbali na kuisafisha tu kwa *Grader* naomba barabara hii ipanuliwe iwe kubwa tena ya njia mbili. Ni vizuri hatua hii ichukuliwe sasa.

Barabara ya *Tabata junction* Mandera – Tabata Dampo na *Kigogo junction* ni barabara muhimu sana, kwa hiyo ijengwe na ipanuliwe na iwe ya njia mbili. Mambo haya yafanyike sasa. Manispaa ya Ilala na Kinondoni zishirikishwe kikamilifu ili zoezi hili lifanyike sasa kwa *short term*.

Barabara ya Ubungo Maziwa – *Kigogo junction* ipanuliwe na iwe ya njia mbili. *Do it now*. Barabara ya Segerea – Mbezi ambayo bado haijajengwa vizuri, barabara hii ni muhimu sana kwa hiyo, ijengwe kwa kiwango cha lami na ipanuliwe ili iwe na njia mbili. *Lets do it now, delay is costly*.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni kati ya nyingi za Dar es salaam. Kwa hiyo, ni ni ushauri wa bure, ninashauri *strongly* uzingatiwe.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kutoa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kuhusu shughuli za Wizara ya Miundombinu. Kabla ya yote, napongeza utendaji wa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kushughulikia kero za wananchi pia watendaji wote wanaounda Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu nchini baadhi hali yake sio nzuri kutokana na kutotengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nianze na barabara ya Kisesa Usagara *by Pass*. Barabara hii imeshafanyiwa upembuzi na mipango yote iko tayari. Tatizo, sifahamu ni nini kinachosababisha kutokuanza kwa kazi hiyo. Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kero inayowakumba wananchi, ni pale watu ambao maeneo yao yamekumbwa na zoezi hilo kwa maana maeneo yao yatafidiwa, lakini hadi sasa hawajui ni kiasi gani wanapewa na ni lini. Kero hii ni vyema ikamalizwa kwa kuwalipa wananchi ambao maeneo yao yatahusika katika ujenzi wa barabara. Sababau za msingi ni kuwa wananchi wameshindwa kabisa kuyaendeleza maeneo hayo kwa vile ni sehemu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandishaji wa barabara, tarehe 30 Juni, 2009 Waziri aliliambia Bunge kuwa baadhi ya barabara zimepandishwa na nyingine hazikupandishwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Misasi – Nduha – Kasololo hadi Mbarika ni barabara iliyokuwa ina daraja la ngazi ya Mkoa *No. R 165* haijatamkwa wakati Naibu Waziri wa TAMISEMI alipokuwa anajibu swali hapa Bungeni (sasa ni Waziri Mkuu) alisema barabara hiyo ni ya Mkoa: Je, ni kwa nini barabara hiyo imeachwa hewani? Naomba majibu ya Serikali, ni sababu zipi za kutoipandisha barabara hiyo na kwa sasa ni ya nani? Mkoa au Halmashauri!

Mheshimiwa Spika, mradi wa Maji wa Kahama na Shinyanga uko Wilayani Misungwi. Nimeishauri Wizara kuwa barabara inayotoka Buhingo – Seek – Nyamayinza hadi Ihelele (kwenye mradi wa maji) barabara hii iwe ya Mkoa ili kuhimili uzito wa magari yanayopeleka mizigo mizito kwenye mradi huo. Lakini hilo halikuzingatiwa: Je, Wizara inaruhusu Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi kuwa na mzani wa kupima magari yaendayo huko na kama ni zaidi ya tani 12 yatozwe ushuru?

Mheshimiwa Spika, jambo hilo ni muhimu kwa usalama wa pande zote mbili za wananchi; Kahama, Shinyanga na Misungwi. Naomba sana Wizara ifikirie hilo.

Mheshimiwa Spika barabara ya Mwanangwa - Salawe ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Jimbo la Solwa na Wilaya ya Misungwi, lakini pesa iliyopewa ni kidogo. Hivyo naiomba sana Serikali ione umuhimu wa mawasiliano hasa eneo la Busongo Sekondari kuelekea Mwangiligili, wakati wowote barabara itajifunga katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelezwa kwamba ujenzi wa barabara ya usagara – Sengerema kwa kiwango cha lami kwa sasa Sengerema hadi Busisi inaendelea vizuri:-

Je, ni lini ujenzi utanza kigongo – Usagara? Hii ni kutokana na kutoisikia katika taarifa ya Waziri. Naomba ufafanuzi, jibu hili liendane na lile la ujenzi wa barabara ya usagara – Kisesa *by Pass*, ni lini ujenzi utanza?

Mheshimiwa Spika, nawatakia utekelezaji mzuri na ninaunga mkono hoja mia kwa mia ili bajeti hii ipewe pesa za ujenzi wa barabara nchini.

MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalam na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha hotuba yao ya Bajeti ya Wizara yao kwa ufanisi na umakini kabisa. Wizara hii ni muhimu sana ndani ya nchi kwani bila ya miundombinu bora sio rahisi kupata maendeleo hasa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa kuipongeza kwa dhati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake ambao ni sahihi wa kuwaondolea shida na usumbufu waliokuwa wakiupata wakazi wa Kigamboni kwa kuwapatia kivuko kipya na kikubwa chenye uwezo wa kutosha kwa mahitaji ya wananchi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa chombo chochote kinachotumika kuchakaa ni wajibu wake, hilo lisiwe suluhisho la mwisho kwa wakazi wa Kigamboni, ni lazima ufumbuzi wa ujenzi wa daraja upewe kipaumbele kwani hilo litakuwa limeleta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la Vivuko.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imetangaza kwa nguvu zote kwa kupitia vyombo vyake vyote kwa kusema “Kilimo Kwanza.” Kauli hii ni pamoja na kuwa na barabara nzuri ili wakulima wetu waweze kusafirisha mazao yao kutoka upande mmoja na kupeleka upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, tukitekeleza hayo, kwa kiasi kikubwa kauli mbiu hiyo itakuwa na ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache napenda kuipongeza Bajeti hii. Naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya hotuba iliyotolewa. Hata hivyo, nina hoja zifuatazo ningependa kupata ufafanuzi wake.

Mheshimiwa Spika, jana tulipata orodha ya barabara zilizopangwa katika hadhi stahili. Katika orodha ile sikuona barabara ya Ifakara – Taweta kuingizwa kuwa barabara ya Taifa (*Trunk Road*) kutokana na umuhimu wa barabara hii katika uchumi wa Wilaya ya Kilombero. Barabara hii kwa siku hupikisha malori zaidi ya 50 mpaka 100 ambayo yanabeba chakula ambacho kinalisha miji yetu mikubwa kama vile Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma.

Katika mkutano wa *Road Board* Mkoani Morogoro jambo hili lilielezwa. Nafikiri hadhi ya barabara kupandishwa daraja itategemea vigezo vya matumizi ya barabara hiyo husika katika usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, katika ziara yake Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Kikwete aliwaambia wananchi kuwa barabara ya Kidatu - Ifakara itajengwa kwa vipande vipande. Ili kauli ya Mheshimiwa Rais iweze kuwafikia wananchi wote wa Wilaya ya Kilombero, ni vizuri Waziri katika majumuisho yake akaitaja barabara hii kwani Rais aliwaeleza wananchi wa Mji wa Ifakara tu.

Mheshimiwa Spika, nimeona Wizara imetenga Shilingi milioni 500 kwa kilometa 30 ambazo nahisi ni kutoka Kibaoni hadi Gereza la Kiberege. Naomba hili litamkwe na Mheshimiwa Waziri ili kusisitiza kile alichosema Mheshimiwa Rais kwamba tutajenga barabara ya Kidatu – Ifakara kwa vipande vipande ili fedha nyingi zielekezwe kwenye ujenzi wa daraja la mto Kilombero.

Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja la Mto Kilombero Mheshimiwa Waziri kama atarejea kauli yake ya Bunge la Bajeti la mwaka 2008/2009, alisema: “Upembuzi yakinifu umekamilika na kinachofuata ni ujenzi wa daraja.” Leo Waziri, anazungumzia tena hatua ya upembuzi yakinifu wa kina.

Sasa inakuwaje hatua ya ujenzi irudi tena kwenye kupembua? Naomba kwa faida ya wananchi waliomsikia mwaka jana, Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi ili wananchi waweze kuelewa kauli hizi zenye kusigana.

Mheshimiwa Spika, katika barabara ya Mkoa – Ifakara – Mlimba – Taweta – Lupembe (Njombe) ambayo nilitegemea ingepandishwa hadhi kuwa barabara ya Taifa kutokana na umuhimu wake, (kilometa 206), katika barabara hii kuna kipande cha Taweta – hadi Iramba mpakani mwa Njombe ambayo ni mpya kingeingizwa kuwa nacho kiwe sehemu ya barabara ya Mkoa kama ilivyo Ifakara – Taweta. Hii itaona na barabara ya kuunga toka mpakani Kata ya Iramba (Njombe) mpaka Lupembe ambavyo ni barabara ya Mkoa.

MHE. ELIETTA N. SWITI: Mheshimiwa Spika, nachukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kuiona Rukwa na kuitengea Shilingi bilioni 15 kwa ajili ya barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi, na Sh. 2,120,000,000/= kwa barabara ya Tunduma – Sumbawanga. Ni wazi tu kwamba Serikali imeamua kuiendeleza Rukwa kama Mkoa ambao uko nyuma. Kwa niaba ya wananchi wa Rukwa naipokea heshima ya kutuwekea barabara ya Matai – Kasanga katika hadhi ya barabara kuu. Bila kusahau kuishukuru Serikali kwa kutenga Sh. 4,560,000,000/= kwa ajili ya kiwanja cha ndege cha Mpanda na Bukoba.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni nilishuhudia kuwekwa sahihi Mikataba kati ya Serikali yetu ya Tanzania na Makampuni ya Kichina ili barabara ya Sumbawanga – Kanazi – Chizi na Chizi Kibaoni zianze kujengwa kwa kiwango cha lami. Hiyo ni hatua kwa Mkoa wa Rukwa ambao ulikuwa haujaonja barabara ya lami tangu kuumbwa dunia. (kwa kifupi tangu uhuru).Katika wakati huu ambapo Serikali imeelekeza macho yake katika Mkoa wa Rukwa, nichukue fursa hii kukumbusha kuwa barabara ya Kaengesa Mozi inatuunganisha na nchi jirani ya Zambia. Barabara ya Mwimba Mambwe – Kenya -

Mtula inatuunganisha na Zambia. Tena Mtula kuna soko la kimataifa. Iwapo barabara hizo zitaimarishwa, nchi yetu ya Tanzania itakuza biashara na *DRC* na Zambia na kuondoa umasikini Mkoani Rukwa na nchi nzima. Sumbawanga, vimejengwa viwanda vya kusaga unga na kiwanda cha nyama. Safi sana! Nashauri kwamba Soko Kuu lingekuwa *DRC* na Zambia kwa kutumia barabara hizo zikiimarishwa.

Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi sura ya 4(c) inaeleza wazi kuwa tutaunganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami. Naomba nichukue fursa hii kuiomba Serikali itimize ahadi yake hiyo kwa barabara nilizozitaja na kulinda heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia na hata kupata fursa hii ili kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara hii ya Miundombinu. Nachukua fursa hii kutoa shukrani sana kwa Waziri mwenye dhamana - Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Ezekiel Ndamami Chibulunje, Katibu Mkuu wa Wizara - Eng. Omar Chambo na Watendaji wote wa Wizara hii ya Miundombinu kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuunganisha nchi yetu hasa kwa mtandao wa barabara.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali ya awamu ya nne chini ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweka mkazo katika sekta hii ya Miundombinu kutoa vipaumbele. Nashukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara ya Singida hadi Shelui iliyokamilika mwaka 2008. Barabara hii kwa sehemu kubwa sana inapitia ndani ya Wilaya ya Iramba, hususani Jimbo la Iramba Magharibi. Pamoja na shukurani hizi, lakini naomba Wizara kupitia Wakala wa Barabara, Mkoa wa Singida (*TANROAD*) maeneo ya Sekenke (Mlimani) barabara ilijengwa kwa viwango hafifu eneo lote lililobomoka, ukarabati wa maeneo ikiwa ni pamoja na kuzirejesha zile kingo za barabara kwenye madaraja.

Mheshimiwa Spika, ili kupanguza ajali, alama za barabarani zinaonyeshe Kijiji, Kituo, vivuko vya waenda na miguu na alama nyingine muhimu ziwekwe haraka hasa maeneo yake barabara inapokamilika.

Nashukuru Serikali kwa kupandisha daraja barabara ya Jimboni kwangu (Kiomboi, Kisiriri, Kidaru hadi Kidaranga) kutoka barabara ya Wilaya na kuwa ya Mkoa (*TANROAD*). Pamoja na kupandishwa huko, naomba Wizara ianze utekelezaji kuifanyia matengenezo mara moja, kwani kukamilika kwa barabara hii kutafungua milango ya kiuchumi kwa maeneo yote yanayopitiwa na barabara hii.

Barabara ya Kiomboi kwenda Misigiri ina urefu wa kilometa 21. Tayari kilometa tano zimekewa lami (*double surface dressing*). Naiomba Serikali kupitia bajeti ya mwaka huu ikamilishe eneo lililobaki la kilometa 15. Serikali ione umuhimu wa kupeleka fedha za mfuko wa barabara kwa Halmashauri za Wilaya kwa wakati. Kwa kufanya

hivyo, itasaidia kukarabati zile barabara za *feeder road* ambazo zimeunganisha barabara kuu na barabara za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kati, Singida - Isuma hadi Manyoni, naomba Wizara ifanye kazi kwa karibu na *Contractor CHINA GEO* hasa ihakikishe uwezo wake wa vifaa kwani kilometa 60 zilizobaki ni suala la aibu kufanyiwa kazi kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Reli (*TRL*) inasikitisha kuona jinsi Shirika la Reli ambalo kwa kiwango kikubwa inaweza kuchangia ongezeko la pato la Taifa. Kwanini Reli ya Kati imeshindwa kuhamishwa? Hivi mbia *RITES* Mkataba wake kwanini uwe na mashaka? Uwezo wa *TIES* kwanini haukuchunguzwa tangu awali? Kwanini Serikali iendeleo na Mkataba wa *RITES* wakati ni dhahiri uwezo wa *RITES* kufanya mabadiliko kimuundo kwa Shirika letu la Reli ni mdogo? Iweje Serikali iendeleo kubeba mzigo mzito wa kuendelea kuhakikisha uwepo wa *TRL* wakati *RITES* inazo hisa 51% na Serikali 49%?

Mheshimiwa Spika, ninachoona, Serikali inaendelea kufanya jambo la hatari kuendelea kufanya ushirikiano na mbia asiye na uwezo. Katika dhana nzima inayohusu mfumo wa soko huria inayoruhusu wawekezaji na wabia wa maendeleo suala linalozingatiwa ni kuona uwezo wa kupata mbia mwenye uwezo anayeweza kuleta mabadiliko ya haraka katika uendeshaji wa shirika. Haingii akilini kuona mbia anakuwa na uwezo ndogo kuzidi ya mhitaji (mmiliki). Ni vyema Mheshimiwa Waziri aeleze bayana ni faida zipi tunaendelea kuwa nazo kama tutakuwa tupo na *RITES* au ni busara zipi tunaweza kupata.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutenga kiasi cha Shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha singida. Hatua hii ni nzuri sana ili kuongeza ongezeko la kufungua milango ya uchumi. Wakati juhudi hii inafanyika, Serikali ihakikishe mipango yake ya kuupanua uwanja wa ndege wa Dodoma, hii itachangia ndege za abiria kuja Dodoma na kuweka hadhi ya Makao Makuu ya nchi yetu yawe juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. R. M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Pia natoa pole na hongera kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa kazi ya kutekeleza Ilani ya CCM. Ukiwa Waziri kwenye nchi masikini na Uwaziri wako wa Sekta ikiwemo ya Miundombinu kama barabara utalaumiwa, ikiwezekana hata kulaaniwa, wakati wewe huna uwezo wako mwenyewe wa kujenga, kutengeneza barabara, kwani na wewe unategemea pesa toka Hazina na Hazina naye anategemea *TRA* kwa pamoja na wajomba zetu wafadhili.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri jambo moja kubwa hasa la utaratibu wa kumpata mkandarasi aeleze hatua/muda unaotumika kumpata mkandarasi kuanzia mwanzo hadi aende *site*, inachukua muda gani? Hili alieleze Bunge lijue ili

Waheshimiwa Wabunge tujue. Inawezekana tunaweza kuwa tunamlaumu Mheshimiwa Waziri kumbe ni utaratibu tuliojiwekea wenyewe (mchakato wa kumpata mkandarasi).

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kuwa sikivu, pale nilipoiomba isaidie ujenzi wa barabara, madaraja na vivuko katika Mkoa wetu wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali hasa Mheshimiwa Waziri, Naibu wako, Katibu Mkuu, wataalamu wako kwa kupokea ombi langu nililoliomba katika bajeti ya mwaka 2008/2009 ya ujenzi wa daraja la mto Simiyu upande wa Maligizu ambapo kwa mwaka huu Shilingi bilioni moja zimetengwa kwa ujenzi ujao huo. Nina uhakika katika mwaka ujao wa fedha 2010/2011 kiasi kilichobaki Serikali haitasita kutenga ili kazi itakayokuwa imebaki ikamilishwe. Naipongeza sana Wizara.

Pia ninaomba niipongeze Wizara kupitia kitengo cha idara ya umeme na ufundi kwa kukamilisha kwa upatikanaji wa kivuko cha Kigamboni MV Magogoni. Kivuko hicho ni mkombozi wa wananchi wa Kigamboni. Pia napongeza kwa *MV Missungwi*, *MV Kome II*, sisi wananchi wa Mwanza tunajisikia fahari kwa kupata vivuko hivyo. Vimepunguza adha kwa wananchi wa Nyakalilo na Busisi Sengerema na Geita.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali hasa idara ya viwanja vya ndege kuiangalia vizuri *Swissport*, japo malalamiko ya muda mrefu ya wafanyakazi ambao wamefunga mkataba wa miaka mitatu au miwili, lakini wanalipwa kwa masaa kama vibarua.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Mwanza tunao mradi wa ujenzi wa barabara kupitia *PMMR*. Nimeshaleta malalamiko kuhusu utendaji usioridhisha wa mkandarasi anayetengeneza barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu – Jajiro hadi Mwabuki, Meneja wa *Tanroad (M) CEO* wa *Tanroad (Mrema)* na Naibu Waziri Chibulunje nimeshawaeleza, wataalamu wetu wapo, waende wajiridhishe na kazi inayofanywa, haina ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya lami ya Mwanza – Shinyanga ambayo imetengewa Shilingi milioni 700. Barabara hii imekuwa ikitengenezwa kila mara, lakini maeneo yanayotengenezwa leo, kesho pale pale palipotengenezwa panaharibika tena. Washauri, Wahandisi wanaosimamia barabara hiyo wao hilo hawalioni?

Mheshimiwa Spika, hadhi ya *Mwanza Airport* hairidhishi hasa upande wa kushukia abiria. Nashauri kupitia mamlaka ya viwanja vya ndege iangalie upya; lakini pia katika uwanja wa JK Nyerere sehemu ya kusubiria abiria wanaosafiri ndani, viyoyozi havitoshi; siku nyingine hivifanyi kazi kabisa. Naomba utafutwe utaratibu mzuri wa kuweka viyoyozi vinavyofanana na hadhi ya uwanja wetu (*International Airport*), sote tunasafiri nje tunaona *lounge* za wenzetu zinafananaje.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Hali ya Hewa ni Idara muhimu sana kwa ajili ya kujua mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Nashauri Serikali inunue vifaa vya kisasa

kuendana na hali ilivyo, isije kazi yao ikawa ni ya kutabiri (kupiga ramli) angalau iwe na uhalisia kidogo, nikitaja kuwa kwao kutakuwa hivi, basi na iwe.

Mheshimiwa Spika, tunaomba chuo chetu cha Bahari *DMI*, Serikali isaidie sana kuiongezea fedha za ruzuku ili kuweza kukamilisha na kutekeleza majukumu yake iliyonayo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isimamie kwa karibu sana suala la mahusiano kati ya chuo chetu *DMI* na chuo kama hicho cha China ambapo kwa mahusiano yaliyopo wameahidi, kujenga chuo Kikuu cha Bahari nchini petu kwa fedha zao kazi ambayo hatua za awali zimeshafanyika za makubaliano.

Mheshimiwa Spika, naomba Bodi ya Usajili wa makandarasi pamoja na Bodi ya Usajili ya Wahandisi isimamie vizuri shughuli nzima ya kazi zinazotekelezwa na makandarasi kwa pamoja na Wahandisi ili kulinda taaluma zao. Haipendezi jengo lililokaguliwa na *Engineer* wa ujenzi kuanguka/kuporomoka au barabara ya lami iliyosimamiwa na mtaalamu wa uhandisi kuanza kubomoka muda mfupi. Hii ni taaluma, ilindeni, jilindeni ili taaluma zenu ziweze kuthaminiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu ya maswali yafuatayo kuhusu *ATCL*:-

- Tulisikia kuwa kuna mwekezaji wa Kichina anakuja kuwekeza kwenye shirika letu: Je, anafikia wapi?
- Ni lini *ATCL* itaanza safari zake za kwenda Comoro ambako kuna mfanyakazi anayelipwa URO 2000 kila mwezi bila kufanya kazi kwa zaidi ya mwaka.
- Ile ndege aina ya *Boing* ambayo ilipelekwa S.A. na baadaye Mauritius pamoja na ndege iliyoharibikia katika uwanja wa Mwanza *DH-8* zitapona lini na *Boing* itarudi lini? Kwa nini hairudi?
- Lakini naomba niambiwe *Air Bus* iko wapi? Inafanya nini? Ndege hii iliondoka na *Engineer* ambaye hadi leo hajarudi, anakula *per diem* ya Dola 250 kila siku huku Shirika linalia ukata.
- Wale *crews 70* walioajiriwa baada ya *CEO* mpya kuingia ambao wengine hawajuwahi hata kuruka mara moja nani anawalipa?
- Je, Shirika linapata faida gani kuendelea kukaa na wafanyakazi zaidi ya 352 ambao hawazalishi na ambao wanalipwa mshahara na Serikali?
- Kwa sababu hivi sasa kuna ndege moja tu inayofanya kazi *DH-8* na sheria za kurusha ndege zina utaratibu wake wa kuruka kwa masaa. Je, likitokea tatizo la kiufundi kwa ndege hiyo kama lilivyojitokeza la ndege iliyokuwa Mwanza *ATCL* ina mpango gani?

- Wale wafanyakazi walioisababishia serikali (Rais) kuingilia kati baada ya *ATCL* kukosa leseni ya ndani na ya nje hali iliyoipelekea *ATCL* kutolewa *IATA* na kusimamisha huduma zaq kurusha ndege mpaka Rais aliposema nataka kuona ndege zinaruka kuanzia kesho, wamechukuliwa hatua gani?
- Je, *CEO* wa *ATCL* David Mataka bado ni *CEO* wa *ATCL* na wakati huo huo yuko *NIC*: Je, ana mishahara miwili ya *NIC* na *ATCL* lakini stahili zake za kila siku nimeona anazilipa *NIC* na *ATCL* ambapo mishahara yake inalipwa na Serikali.
- Uendeshwaji wa shirika lolote la ndege viongozi wake wakuu lazima angalau wawe na ufahamu wa mambo ya *Aviation*. Je, *CEO*, anayekaimu U-*CEO*, Mwenyekiti wa *board* wanao mwanga wa mambo ya ndege?
- Na mwisho kwa sababu *ATCL* kwa kitendo cha kutangaza ofa ya saba saba ya kupunguza nauli ya Shs.130,000/= Dar es Salaam - Mwanza OU Dar es Salaam - *KIA* Sh.116,000/= *OW*, Dar – NW-Dar Sh. 200,000/= na Dar-*KIA*-Dar 29 179,000 bila kuweka *tax* ambayo ni Sh. 51,000/= *OW* na Sh. 82,000/= “*return ticket*” ni usumbufu kwa wateja wao. Naomba wenzetu wanapotaka kufanya vitu vizuri hivyo, basi wateja wao tujulishwe kwamba nauli hiyo ni bila *tax*.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana endapo nitajibiwa haya niliyouliza wakati Waziri atakaposimama kufanya majumuisho. Nasema tena pole na hongera kwa kuwa Waziri katika nchi masikini. Nia yetu ni kumsaidia Waziri katika kutekeleza ilani yetu. Nawaomba sana Watendaji Wakuu wa Wizara, Idara na Taasisi zilizoko chini ya Miundombinu mumsaidie Waziri katika kutekeleza ilani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Spika, napenda kuulizia kuhusu upotevu wa pesa ambazo Mhindi amekimbia nazo. Je, hayo yanaweza kutolewa ufafanuzi? Je, hatua zipi zimechukuliwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni kulikuwa na mgomo wa wafanyakazi wa *TRL* na Serikali ilitamka na kutoa maelekezo kuwepo na mkataba wa waajiri na watendaji: Je, mpaka sasa mkataba huu kati ya Watendaji na Waajiri wameshakubaliana na namna gani pesa zao za kiinua mgongo zitakavyolipwa kwa muda waliokaa kazini? Utaratibu wa wafanyakazi wa *TRL* ambao walijirwa kwa muda mrefu: Je, malipo yao yatalipwa na *TRL* kwa muda wote? Waliofanya kazi au *TRL* itawalipa kwa muda waliokubaliana nao? Kama wakilipwa kwa muda waliokubaliana nao: Je, Muda ambao walifanya kazi miaka yote ya nyuma kiinua mgongo chao watalipwa na nani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na

Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Naomba kuzidi kuwatia moyo na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo zuri sana Wizara hii imefanya, ni kutenga fedha Shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami ya Kyaka – Bugene – Kasulo. Hadi hivi sasa *detail design* ipo inaendelea. Nina imani kazi hii itakwenda kwa kasi iliyotarajiwa ili kandarasi ya ujenzi wa barabara hiyo ianze mapema iwezekanavyo. Nazidi kuomba na kusihi kazi hii ianze na iishe kabla ya mwisho wa mwaka wa 2010 na baada ya hapo fedha itengwe pia kwa kuendeleza barabara hiyo toka Bugene hadi Kasulo (Benaco).

Matengenezo ya meli ya *MV. Victoria* na *MV. Lihemba* ni ya muhimu sana kwani meli hizo ni nzuri sana. Lihemba ilitengenezwa mwaka 1913 na Victoria mwaka 1961. Pia naomba Serikali itenge fedha hata kwa bajeti ya mwaka 2009/2010 kwa ajili ya ununuzi wa meli mpya za kubadili *MV. Victoria* na *MV. Lihemba*. Kinyume na hapo, maisha ya Watanzania yatakuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, reli zetu za Tazara na Reli ya Kati ndiyo nguzo pekee ya uchumi wetu. Kwa bahati mbaya, reli zetu zinasuasua. Hotuba ya Mheshimiwa Rais imenitia moyo kuhusu kufufua reli zetu. Naomba Watendaji wetu wasituangushe.

Kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja.

MHE. EMMANUEL LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji kwa kuandaa bajeti hii na baadaye Mheshimiwa Waziri kusoma hotuba hapo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unahusu maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kupandisha barabara la Bukombe – Mfikaga yenye kilometa 32. Hata hivyo, barabara hii inafahamika kama Ushirombo – Mfikonga, naomba mfanye marekebisho, hii barabara inayounganisha barabara inayosomeka Katoro – *Bukombe border* ambapo ingesomeka Katoro – Mfikonga.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Masumbue – Lugunga – Ivumwa (Geita border) ina vigezo vyote mlivyoainisha katika kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu tarehe 30 Juni, 2009. Kwa nini barabara hii hamuipandishi hadhi? Naomba muipitie upya barabara hii kwani inaunganisha Wilaya ya Bukombe na Geita kupitia Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upandishwaji hadhi wa barabara hizi, sijaona fedha za matengenezo. Je, fedha hizi ziko wapi za barabara ya Bukonde – Mfikonga; Mwalo – Iyogelo na Runzewe – Bwanga?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza msongamono. Tatizo la msongamano, watu wengi na Waheshimiwa Wabunge na Kamati wameeleza unavyosababishwa na utendaji kazi wa *TICTS*.

Nahisi Watendaji wanaonyesha dharau hasa kwa viongozi wa kisiasa kwani Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa maoni yake juu ya mkataba wa *TICTS* ndani ya Bunge. Mkataba huu wa *TICTS* kwanza haukufuata taratibu za manunuzi, hoja ambayo hata *CAG* amependekeza. Ni vizuri bandari kavu ingezingatiwa *ICID'S* ishughulike na utoaji wa makontena kupunguza msongamano.

Mheshimiwa Spika, nafikiri *TICTS* iko juu ya sheria za nchi na watawala, kwani kama haiko juu ya sheria naamini marekebisho ya kurekebisha mkataba yangezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kumbuka sisi tunaishi katika nyakati ambazo dhambi huonekana kama ni mtindo wa maisha. Haki hutoweka, kushindwa kuwaamini watu yamkini marafiki na viongozi tuliowachagua (Mika 7:1 – 6). Tunapoteza imani kwa viongozi kutokana na utendaji mbovu wa watu wenye mamlaka na maamuzi. Hebu tufikiri yafuatayo:-

(1) Je, sababu zipi zinafanya mkataba wa *TICTS* usivunjwe?

(2) Je, ni sababu zipi Serikali imemwachia *TICTS* afanye kazi nyingine zaidi ya kupakia na kupakua mizigo?

(3) Ni sababu zipi zinazuia *ICD's* zisifanye kazi iliyokusudiwa?

Mheshimiwa Spika, hayo na mengine mengi Serikali lazima iyazingatie ili wananchi waendeleo kujenga imani kwa viongozi wake. Tusipozingatia haya, tunapoteza mapato mengi ya Taifa hili, kuacha yaingie mifukoni mwa wachache.

Mheshimiwa Spika, leo ni mara ya kwanza kusema maneno haya kwa sababu ya kuona Serikali ina jeuri, haitaki kusikiliza hoja za wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali/Mheshimiwa Waziri anapomalizia ajibu yatuatayo:-

(1) Kwa nini barabara la Masumbwe – Luginga – Ivumwa – Bukoli – Geita haipandishwi hadhi kwa kuwa vigezo vinakidhi?

(2) Ni lini barabara la Runzewe – Bwanga (Chato) itawekewa lami?

(3) Fedha za kutengeneza barabara ya Bukombe – Mfikonga, Mwalo – Iyogelo na Runzewe – Bwanga mbona hazionekani?

(4) Kwa nini mkataba wa *TICTS* haufanyiwi marekebisho kama ilivyoshauriwa?

(5) Kwa nini bandari ya nchi kavu inachelewa kufanya majukumu yake?

Pamoja na maswali hayo, naunga mkono hoja ili Serikali itekeleze yaliyokusudiwa.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kubwa na za dhati kwa Wizara hii ya Miundombinu hasa Waziri na Watendaji wake kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonyesha kwenye Wizara na kuleta maendeleo kwenye maeneo yetu ya Sengerema na Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumepata vivuko vipya viwili kwa muda mfupi sana, yaani kivuko cha Kigongo – Busisi. Eneo hili lilikuwa korofi sana. Kulikuwa na ferry moja ya *MV. Sengerema* ambayo ilikuwa imechoka sana, lakini hivi sasa kuna *MV. Misungwi* ambayo ni nzima na safi, kubwa imesaidia sana.

Tatizo moja tu ni barabara ya kutoka Geita, Sengerema, Busisi hadi Msagara ambayo ujenzi unakwenda taratibu mno kiasi ambacho kunakuwa na wasiwasi wa barabara hii kutokumalizika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Wizara hii kwa barabara zake ambazo imetengeneza kwa ustadi mkubwa. Napenda nitoe pongezi kwa kututengenezea barabara ya kutoka Kamanga, Katunguru, Nyamezugo, Nyehunge, Rwezera Nzera hadi Nkoma, pia Nzera, Igata Bugulula hadi Geita Mjini. Barabara hizi ziko chini ya mradi wa *World Bank*, zimekwenda vizuri sana. Pia Geita Ikuhura hadi Nyang’hwale imetengenezwa na inapitika vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sana vitu vifuatavyo vifanyike katika jimbo langu la Geita:-

Mheshimiwa Spika, naomba gati la Nkome ambalo katika Wizara hii mwaka 2004 zilitengwa kiasi cha Shilingi milioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa gati hili. Wakati huo Mheshimiwa Waziri alituambia na kuwaahidi wananchi wa Geita kuwa baada ya kumalizika gati la Bukondo lingefuata gati la Nkoma lakini hadi leo hakuna. Kupandishwa barabara kutoka Sungusira Idosero - Mkolani II - Ibisabagani - Ng’wabagalu - Buzilasoga - Lima hadi Sererema Mjini lipandishwe hadhi kuwa la Mkoa. Barabara ya kutoka Busisi - Nyang’hwale hadi Nyang’holongo na ile ya Katoro - Kamena hadi Kahama. Hizi barabara ni muhimu sana, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Geita haziwezi kuwa na fedha za kuwahudumia barabara hizi.

Mwisho, napenda kumwambia Mheshimiwa Kawambwa kuwa suala la *TICTS* ni muhimu sana, lishughulikiwe kuweza kufufua uchumi wa nchi yetu. Utaratibu wa kuikingia kifua *TICTS* ni aibu kubwa. Kama hawa waliotoa chochote Serikalini mnawaonea haya kuwanyang’anya tenda hii, basi Serikali imrudishie fedha zake. Ili nchi igomboke hali iwe nzuri mambo miwili yafanyike:-

(1) *TICTS* iondolewe “*exclusivity*;”

(2) Bandari zetu za nchi kavu zifanye kazi kwa kiwango cha kuridhisha.

Baada ya hayo mawili kufanyika, bandari yetu itaheshimika sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. FLORANCE ESSA KYENDESYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naipongeza kwa dhati Serikali ya awamu ya nne kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Pia nampongeza Waziri na Watendaji wake kwa kuandaa hotuba yake nzuri iliyosomwa katika Bunge lako Tukufu.

Kuhusu ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Songwe Mbeya, kama ilivyoelezwa kwenye ukurasa wa 23 katika kitabu cha hotuba cha Mheshimiwa Waziri sasa ni takribani miaka tisa tangu uwanja huo uanze kujengwa, lakini mpaka sasa bado haujakamilika. Serikali ilipanga uwanja huo ukamilike ifikapo mwezi Julai, 2009. Hivi sasa zimetengwa fedha Shilingi bilioni 32.600 ili kukamilisha ujenzi huo. Kinachonipa kigugumizi ni juu ya mkandarasi aliyepewa kazi ya kukamilisha ujenzi huo kwani ni yule aliyeshindwa kukamilisha ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Mbeya – Lwanjiro – Chunya hadi Makongorosi, wananchi wa Mbeya wanajiuliza, iweje mkandarasi huyo hana kazi ya kukamilisha uwanja wa ndege Songwe? Ieleweke kuwa uwanja huo ni wa kimataifa, nchi jirani za Kusini mwa Afrika pia zitautumia uwanja huo. Hivyo watauletea/kuiongezea mapato nchi yetu. Tunaomba uwepo ufuatiliaji wa karibu sana kuhusu maendeleo ya ukamilishaji wake.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha, pia naunga mkono hoja.

MHE. FELIX N. KIJIKO: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu kwa asilimia mia moja. Baada ya kuunga mkono hoja, napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuukumbuka Mkoa wa Kigoma kwa kuanza kazi ya kujenga barabara za lami na hasa ile ya kutoka Manyoni hadi Kigoma kupitia Tabora.

Mbali na shukrani kwa Serikali kuhusu ujenzi wa barabara kuu mbili katika Mkoa wa Kigoma, bado kilio cha wananchi wa Kasulu na Kibondo wanaionamba Serikali kuongeza juhudi za kuijenga barabara ya Kidahwe hadi Nyakonazi. Ni dhahiri kuwa upo umuhimu wa njia hiyo kutengenezwa (Kujengwa) kwa kiwango cha lami kwa sababu wananchi walio wengi na hasa wafanyabiashara wanategemea kupata na kuteleka bidhaa zao Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naungana na wazungumzaji wengine kuwa uongozi wa reli ya kati ubadilishwe na kutafuta mwekezaji mwingine ambaye anao uwezo wa kuendesha Shirika kwa sababu fedha zinazotumika kwa madhumuni ya kuwawezesha ni fedha ambazo zingefanya kazi nyingine.

MHE. MAULIDAH ANNA KOMU: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote naomba kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri na wote

ambao wanashirikiana kwenye utendaji wa kazi hii ngumu ya kuhakikisha miundombinu ya nchi yenu inajengeka kupunguza hali ya umasikini uliojikita hususani vijijini ambako ndiko kuna Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, barabara ni tegemeo la Watanzania walio wengi au tuseme wote bila kuwa na barabara zilizo nzima zinazopitika, basi umasikini utaendelea kushamiri, fedha nyingi za walipa kodi zinatumika kujenga barabara, lakini cha kushangaza barabara mara ya kujenga huharibika na hii ni kutokana na rushwa iliyojikita ndani ya nafsi za watendaji. Hakuna usawa wa fedha inayotumika na kazi inayofanyika. Kwa kweli hili inabidi liangaliwe sana. Napenda kuishauri Wizara kwamba wakati kazi za ujenzi wa barabara unapoendelea wahusika ambao ndio wasimamizi wa ujenzi huo wawe makini kupitia na kuangalia kwa udhati kazi zinapoendelea, fedha zifanane na kazi inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa ndege, ni huzuni kubwa kuona Tanzania tumeshindwa kabisa kuwa na chombo chetu kinachobeba heshima na uzuri wa nchi yetu haina haja kukaa kuangalia nini kimetokea ila sasa tuanze yajayo, hebu tuangalie kuimarisha shirika hili na tafadhalini tusianze kuweka wawekezaji kama *Railway* kwani baada ya kwenda mbele huwa tunarudi nyuma, tuangalie sana, kwani inatia simanzi kuona wenzetu jirani zetu Kenya wanarusha jina lao na bendera yao kwa ufahamu kabisa. Hivi Watanzania tuna nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli masikitiko makubwa ni gharama na hasara zinazotokana na uharibifu wa barabara. Hivi ni nini? Kwa nini hatuoni uchungu na fedha za walipa kodi? Tunatengeneza barabara kwa gharama kubwa halafu sisi wenyewe tunazivuruga baada ya muda mfupi tu wa matengenezo.

Mheshimiwa Spika, reli ni muhimu sana hasa ukizingatia bandari tulizonazo, tunasema tutengeneze bandari zetu ili tuweze kuongeza fedha za kujaza kisima chetu cha matumaini, naomba tuelewe kutengeneza bandari na kuwa na matumaini ya kupata fedha kwa kutegemea barabara tulizonazo, fedha hiyo hiyo haitafanya jambo lingine ila kujenga kwa barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tuache kauli ya hakuna pesa, sungura mdogo! Hawezi kuwa tembo madhali yeye ni sungura! Tuache upuuzi, tukae tuamue kurekebisha reli zetu kwa kujenga. Reli pana zinazotakiwa na kuleta treni za kisasa, hiyo fedha tutakayotumia kwa muda mfupi tu zitarudi. Tutakuwa tunasafirisha mizigo kwa treni, barabara zetu zitapona na mizigo itafika kwa wakati na wakulima watapata njia rahisi ya kusafirisha mazao yao, kwa sababu usafiri wa treni ni rahisi kuliko usafiri wa malori.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ni macho ya nchi hii, kila anaingia kuja Dar es Salaam kwa kuona mji ulivyo ni aibu! Tuache kusema barabara za Dar es Salaam ni za Halmashauri, lazima tuweke umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam kuondokana na barabara mbovu. Maji yanajaa, mvua ikinyesha kidogo mji haupitiki kabisa. Tunasikia barabara za mwendo kasi, hili ni la ukweli au usanii tu. Ni hadithi za Alfu Lela Ulela au siku elfu na moja.

Kila karne hadhithi ipo. Wingi wa magari Dar es Salaam ni kichaa. Nyumba zinajengwa, wahandisi hawafikirii, kulazimisha kuweka *parking* ndani, nyumba zinajengwa, njia za maji machafu hakuna, ni zile zile za zamani. Cha ajabu Mji wa Dar es Salaam majumba yanajengwa kila siku, lakini huoni upanuzi wa njia za maji machafu. Tahadhari ni kwamba kama hatutazingatia kuangalia uwezekano wa kufanya bidii ya mifereji ya maji machafu, basi kuna siku Jiji la Dar es Salaam litanuka uchafu kuliko ilivyo sasa kwa maji ya uchafu kupita juu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu simu za mkononi, kama ingelikuwa maendeleo ya nchi hii ni kama simu za mkononi, basi tungekuwa mbali sana. Kwa hili, naipongeza Wizara kwa kufanya bidii ya kuandikisha wamiliki wa simu za mkononi ili iwe rahisi kuwakamata wale wanaotumia simu vibaya. Lakini nategemea wahusika wanaoelewa fika kwamba hata huko vijijini wanatumia simu za mkononi, isiwe usajili huu ni wa mijini tu, hata vijijini shughuli hii ifanyike kama mijini.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kheri wale wote wanaofanya bidii kuhakikisha nchi yetu inaendelea kwa miundombinu ya kileo na naomba waachane kabisa na neno Rushwa kwani ni adui wa haki. *Percent* kumi ni leo, na kesho je?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. MARIA IBESHI HEWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa pongezi kwa hotuba nzuri ya bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na naunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nazidi kutoa pongezi nyingi kwa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya nchini. Mfano hai katika Mkoa wa Mwanza ni kuwa na vivuko katika Ziwa mfano *MV. Misungwi, MV. Kome* tunasema hongera sana kwa kazi nzuri hii.

Kuhusu utengenezeji wa barabara itokayo Dar es Salaam hadi Mwanza kupitia Dodoma. Manyoni na Singida, naomba nguvu iongezwe pale katikati ya Manyoni na Singida. Hapa utengenezaji unakwenda pole pole sana. Wizara iangalie kama ujenzi huu umo katika mkataba katika ukamilishaji wake.

Mheshimiwa Spika, suala la uboreshaji wa kiwanja cha ndege Mwanza linastahili pongezi kubwa. Ila ombi kwa wananchi wa Mwanza ni kupatiwa usafiri wa ndege kubwa. Zabuni zitolewe mapema ili kazi ianze kuwa nia ya kuuboresha miji/mji wa Mwanza

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kuwa na matengenezo ya uhakika na ya kudumu ya kipande cha barabara ya lami kati ya Ilula – Mabuki hadi Ukiriguru Mwanza; kuwa na matengenezo ya mara kwa mara katika vivuko vyetu ndani ya Ziwa Victoria kama *MV Sengerema, Misungwi na Kome*; uwepo usimamizi wa karibu sana wa Serikali mara zabuni kwa ajili ya uboreshaji wa kiwanja cha ndege – Mwanza itakapotangazwa ili

shughuli hiyo iweze kuanza na kuendelea vizuri; na kuwepo kuhimiza upatikanaji wa usafiri wa ndege kubwa za *ATCL* kutua mji/kiwanja cha ndege Mwanza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. JUMA ATHUMANI KAPUYA: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu wake na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa hotuba hii nzuri. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kumweleza Mheshimiwa Waziri kuwa moja ya maeneo ambayo bado yako nyuma sana ni Urambo Magharibi. Jimbo hili limezaliwa mwaka 1995 kwa hiyo, mambo yake mengi, karibu yote ya maendeleo yako katika hatua za awali.

Tatizo kubwa tulilokuwanalo na linalotukwamisha ni miundombinu hasa ya barabara. Imefikia mpaka imekuwa ni kero na ni mateso kwa wananchi wa Urambo Magharibi hasa wa maeneo ya Ufaka Ukumbi Siganga, Uyowa, Ulyankulu na Kashishi. Wakati wa masika maeneo haya huwa ni visiwa kabisa na hayafikiki. Matokeo yake huduma za wananchi huwa masikini zaidi. Wagonjwa na hasa akina mama wajawazito wanapata matatizo na mateso makubwa na hata vifo.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana hali hii ndio maana Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilileta pendekezo kwenye Wizara ya Miundombinu kuwa barabara hii ipandishwe hadhi na iwe ya Mkoa chini ya *TANROADS*. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kwa fedha za mgao wa Halmashuri haitawezekana kabisa kukabiliana na hali mbovu kabisa ya barabara.

Pendekezo hili liliungwa mkono na kupitishwa na Kamati ya ushauri ya Mkoa (*RCC*) Tabora baada ya kuidhinishwa na *Road Board* ya Mkoa.

Isitoshe, Mheshimiwa Rais alipozuru Mkoa wa Tabora, hususani Wilaya ya Urambo, wananchi walimwomba Mheshimiwa Rais barabara mbili zipandishwe hadhi ziwe za Mkoa, ile ya Tutuo – Mole – Urambo na ile ya Ugalla – Kaliua – Myowa – Ulyanku – Kashishi hadi Kahama. Mheshimiwa Rais alikubali na kuagiza lifanyike. Ila kwa mwaka huu ianze kutengenezwa ile ya Tutuo – Mole – Urambo baadaye ifute ile ya Ugalla – Kaliua – Uyowa – Ulyankulu Kashishi – Kahama.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunganisha Mikoa mitatu; Rukwa - Tabora na Shinyanga. Barabara hii ni uti wa mgongo na ni mkombozi kwa uchumi wa Mikoa hii mitatu. Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii waitambue barabara hii na waipandishe hadhi kama Halmashauri na Mkoa walivyopendekeza na kama Mheshimiwa Rais alivyowaahidi wananchi wa Urambo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. FESTUS LIMBU: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada kubwa inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, tuliomba Wilaya (mji wa) ya Magu iunganishwe na Wilaya/Mkoa ama maeneo mengine kwa kupandisha hadhi baadhi ya barabara zilizopendekezwa na Mkoa. Mkoa wa Mwanza uliomba barabara zifuatazo zipandishwe daraja (hadhi).

- i) Ng'haya – Bugatu – Salama – Shinyanga border;
- ii) Kisamba – Salama – Nasoli (Shinyanga border);
- iii) Lumeji – Nyashana – Kadashi; na
- iv) Magu Ginnery – Yichobela – Sumve.

Cha ajabu barabara (kipande cha barabara) kilichopandishwa hadhi ni Shinyanga *border* hadi Salama peke yeke!. Hii haiingii akilini. Naomba angalau kipande cha barabara kutoka Salama kwenda Ng'haya kiongezewe kwenye hii barabara iliyopandishwa hadhi.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kisesa – Usagara, wananchi wa Kisesa wanalamika kuwa hawajalipwa fidia. Kuna mpango gani mahususi wa kuhakikisha kuwa wanaohusika wote wamefidiwa?

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kutenga (shilingi) fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja Daraja la Mto Simiyu (Barabara ya Magu – Kabila – Mahaha). Naomba kupewa ufafanuzi. Katika maandiko mbalimbali ya bajeti, pengine imeandikwa zimetengwa Shilingi bilioni mbili na pengine imeandikwa zimetengwa Shilingi milioni 140. Ipi ni ya kweli? Iwapo ni milion 140: Je, kiasi kidogo hiki kitafanya kazi gani? Mbona ni kidogo sana?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ng'haya – Bugatu - Salama inaunganisha barabara ya Mkoa ya Magu – Kabila – Mahaha na ya *Shinyanga border* (Kasoli – Salama – Kisamba na Mkoa, (Magu). Tuliomba kipande hiki kichukuliwe na Mkoa, haikuwezekana. Halmashauri ya Wilaya ya Magu tayari ina Shilingi milioni 70, lakini hazitoshi. Tumeomba, (na nazidi kuomba) Serikali ituongezee pesa (barua/maombi yako Wizarani) ili angalau tuifungue njia hii halafu ndiyo tuachiwe tuendeleo nayo kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, nashauri TEMESA waongezewe pesa kulingana na maombi yao ili wanunue mahitaji ili wakarabati magari na mitambo ya Serikali. Fedha zilizotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya ukarabati wa magari na mitambo ya Serikali, miaka miwili iliyopita, mwaka huu na mwaka kesho ni nyingi saana. TEMESA wanahitaji fedha '*once and for all*', halafu watajiendesha wenyewe, hawatahitaji tena fedha toka bajeti ya Serikali. Naunga hoja mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza Wizara hii kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote, kwa kuandaa hotuba hii

ambayo imesomwa leo kwa ujumla. Naipongeza Serikali kwa jitahada za kujenga barabara za lami za kuunganisha mikoa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo ya kina kuhusu fedha zilizotengwa bajeti ya mwaka 2008/2009 ya Shilingi bilioni 12 zimefanya kazi gani kwani tayari Bunge lilishapitisha fedha hizo. Hatutaki maeneo ambayo hayatekelezi maagizo ya Bunge. Vile vile tupate maelezo ya kina kuhusu fedha hizi zilizotengwa mwaka huu 2009/2010 zitafanya kazi gani?

Barabara ya Dodoma – Iringa. Naunga mkono hoja hii. Barabara ninayoiongelea ni barabara ya Dodoma – Babati – Dodoma – Iringa. Barabara hii kubaki bila ya kujengwa kwa lami ni aibu, kwani barabara hii ni ya historia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu anieleze na afafanue fedha zinazoonekana kwenye kitabu katika *Vote 98, sub vote 2005 na item 4132* ambazo zipo Sh. 32,622,600,000/= kwa ajili ya *Regional Rehabilitation*, mgawanyo wake utatolewa lini na barabara zipi zitahusika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mzima na kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu, Katibu na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyoandika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia bajeti hii kwa kuiomba Serikali iache kujenga barabara kwa kutumia kokoto kwani barabara hizo mvua ikinyesha, zote zinakwenda na maji na pesa zote zitapotea, bora tujenge kidogo kidogo kuliko kujenga barabara nyingi na ndefu na bada ya muda zote zinaondoka. Pesa ni kodi za wananchi ambazo ni lazima tuwaonee huruma kwani Mbunge yeyote anayesimama hapa haombi barabara ya kokoto, anaomba ya lami.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zinazojengwa zinaharibika kabla hata kumaliza mwaka kutokana na waangalizi ambao hawaangalii ipasavyo *'value for money.'* Naomba Serikali wanunue chombo cha kupimia barabara na ujulikane ubora wake.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie kuhusu *ATCL*. Shirika hili linabeba mambo ya Taifa ambayo ni muhimu sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, *ATCL* inaomba Shilingi bilioni 20, inapewa Shilingi bilioni moja. Kweli tuko *serious* katika hili! Tutawalaumu watendaji bure, lakini jambo lolote linalotengeneza pesa lazima litumie pesa.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyozungumza kila siku kuwa wafanyakazi kwenye shirika hili ni wengi ambao ni 364 na wanahitaji kulipwa mafao yao, lakini mpaka leo tunaingia gharama na kungoja wawekezaji ambao wanaonekana kama ni ndoto kutokana na Serikali kushindwa kutoa fedha za kuondoa matatizo ambayo ni muhimu na kuweka shirika safi ili liweze kupata mbia wa uhakika sio wa ahadi kila siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TICS*, pamoja na Serikali kushindwa kulitolea uamuzi *TICS*, tukubali, tukatae, *TICS* ina matatizo makubwa ambayo hata vile vitendea kazi walivyosema wataleta basi, hawajaleta! Wanakodi *TPA*, na waliahidi kuongeza kina cha bahari lakini mpaka leo hakuna walichofanya. Nadhani Waheshimiwa Wabunge walio wengi hawaichukii *TICS* lakini hawatimizi viwango. Sasa huu ukiritimba mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, sio lazima waondoke *TICS*, lakini wawe na malengo ya kuondoa matatizo, sio kung'ang'ania jambo ambalo wanashindwa kutimiza malengo na kulisababishia hasara kubwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Ahsante.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza napenda kumshukuru Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Shukuru Kawambwa pamoja na Naibu Waziri wake - Mheshimiwa Chibulunje, pamoja na Watendaji wote walio kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, tatizo langu lote liko katika uwanja wa ndege wa Mwanza, kwani uwanja huu ni muhimu sana, tena Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati anatoa shukrani katika uwanja wa CCM Kirumba aliahidi uwanja huu utengenezwe ili uweze kutua ndege kubwa na ujenge mji wa Mwanza uwe ndiyo ufunguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uwanja huu hauna hata mkanda wa mizigo. Mvua ikinyesha, abiria na mizigo ni taabu tupu! Hii ni aibu kubwa katika jiji kama hili. Kuchanganya uwanja wa Mwanza na Kigoma hii ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa barabara vijijini umechelewa sana kuanza, kwani kuchelewa huku ni kuzidi kuharibika kwa barabara na kama umeamua mpango fulani, inabidi kuufanyia mkakati. Tusiishie kuandika tu. Pia naiomba Wizara iangalie sana meli ya *MV. Victoria* kwani meli hii imekuwa ni ya muda mrefu na pale tulipotembelea Kigoma, Kamati ya Miundombinu pia tuliambiwa meli ya Liemba nayo imekuwa ni ya muda mrefu. Hivi meli hizi mpaka zilete maafa ndiyo tujenge minara ya kumbukumbu? Kama ndege ya Rais imepatikana, ambaye madaraka anapewa na raia hawa, walidhutu kutamkiwa hata kama wakila nyasi lazima ndege ya Rais inunuliwe; ni vipi sasa wananchi hawa wasipate meli za uhakika ili kunusuru maisha yao na kuepuka gharama za uokoaji na ujenzi wa minara ya maafa? Naiomba Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu kuliona hili na kujali maisha ya Watanzania watumiao meli hizi? Je,

SUMATRA hawalioni hilo? Au kwa kuwa ni vyombo vya Serikali! Tunaomba *SUMATRA* iangalie meli hizi upya. Ahsante.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia hoja hii, napenda nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa maandalizi mazuri sana ya hotuba nzuri sana iliyopangika kwa misingi inayokubalika ya kuandaa bajeti inayojibu utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani kwa Serikali kutukumbuka Mkoa wa Rukwa kwa barabara za Mkoa kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami, pongezi sana zimwendee Rais wetu, Waziri na Watumishi wote wa Wizara kwa kuufungua Mkoa huu.

Mheshimiwa Spika, bado ninamwomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na wakandarasi watakaoanza ujenzi wa barabara toka Tunduma, Sumbawanga, waanze kipande cha mjini Sumbawanga kuelekea Laila. Pia kwa kuwa kuna *section* tatu za ujenzi wa barabara toka Tunduma hadi Sumbawanga, ninashauri mipango ya kuanza kulipa fidia kwa wale wote watakaoathirika na upanuzi wa barabara hii. Ni bora tukalitatusa hili mapema.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, alitoa ushauri katika ibara ya 5.2.7. ya kuitaka Serikali ione uwezekano wa kuunganisha reli kutoka Tunduma hadi Bandari ya Kasanga ili kufungua milango ya biashara na nchi jirani ya *DRC*, Rwanda na Burundi. Bandari ya Kasanga inayojengwa itazaa matunda makubwa ya kuiuchumi na kimaslahi ya kijamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mimi kama mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, ninaamini kuwa Serikali itawekea uzito mapendekezo ya kuimarisha *ATCL, TRL; TAZARA; RAHCO* na Taasisi za Wizara kama *NIT, DMI*.

Mwisho, namshauri Mheshimiwa Wazirikwamba wakati wa *winding up* – azingatie sana majibu yake yaendane kwanza na nini maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi CCM. Pili, azingatie sana pia ahadi za Rais ambazo nazo zitakuwa zinatekelezwa awamu kwa awamu kulingana na fedha zinapopatikana. Tatu, ni nia ya Serikali kufungua nchi nzima awamu kwa awamu kutegemea fedha zetu za ndani. Wahisani wao watusaidie kutuongezea nguvu pale uwezo wetu unapofikia kikomo. Nia hiyo ipo na itaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, barabara zinapoanza kutengenezwa, lazima zishirikishe uongozi wote wa maeneo husika – kuanzia viongozi wa Vijiji, Kata, Wilaya na Mkoa ili wakandarasi wakifika wasianze kazi kwa kupambana na wezi wa mali za kujenga barabara hizi wa mafuta ya mitambo na hujuma zinazofanywa na wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TEMESA* iangalie upya mpango wa jinsi ya kudhibiti wizi wa mafuta na matumizi mabaya ya magari ya Umma. Tukisimamia hilo vizuri tunaweza kuokoa fedha nyingi kwenye mafungu tuliyopewa kwenye kasma zetu ambazo ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kumwomba Mheshimiwa Waziri aendelee na kasi hiyo hiyo na ajiandae vizuri kutoa majibu fasaha.

MHE. COL. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sina budi kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa waziri kwa hotuba yake ambayo ni nzuri, iliojaa hekima na utekelezaji wa uhakika juu ya Ilani ya uchaguzi wa CCM. Aidha, nampongeza Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Wizara katika kutekeleza majukumu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kabisa, ninaomba kuchangia maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali mbaya ya kuichumi iliyoikumba dunia, tukiwa na sisi Watanzania imetukuta, ni vyema sasa tukaimarishe bandari zetu kuu hasa ya Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar na Mtwara pamoja na kuweka zana za bandarini za kisasa katika upakuaji na upakiaji wa mizigo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuikumbusha Wizara juu ya zana za uongozi wa meli za kimataifa na zile za kitaifa, yaani kuikarabati minada, maboya ambayo iko baadhi haiwaki na *land mark* imezibwa na haionekani.

Mheshimiwa Spika, viwanja vya ndege ni sehemu kubwa ya kutuongeza uchumi wa Taifa. Naomba Serikali ikubali kuelekeza kwa dhati katika viwanja vyetu ili kuimarisha uchumi wetu, lakini pia kuna haja kubwa ya kuwaweka viongozi na wataalamu waadilifu ili kuutunza vizuri uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya shirika letu la ndege la Tanzania liko hali mbaya sana na kwa kweli shirika hili ni mojawapo katika migodi mikuu ya kuchangia uchumi wa nchi yetu na sasa ninaelewa shirika hili la *ATCL* lilikuwa zuri sana na likachangia sana pato la Serikali, likisafirisha ndege zake sehemu ya Afrika hata Ulaya.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara au Serikali kwa ujumla wake ilifufue shirika hili kwa guvu zake zote.

HUDUMA ZA HALI YA HEWA: Mheshimiwa Spika, mamlaka ya hali ya hewa, pamoja na kuimarishwa kwake, lakini ninashauri mamlaka hii lazima ipewe uwezo zaidi katika kudhibiti vyombo vya bahari hasa pale wakati wanapotangaza hali ya hewa

mbaya kwa upande wa baharini, kunatokea maafa mengi ya kuzama vyombo baharini na kwa vyombo vya wavuvi kutojali taarifa ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri mamlaka hii ya hali ya hewa iwe na ushrikiano mkubwa na wa karibu na mamlaka ya udhibiti wa usafiri wa nchi kavu na majini hasa baharini.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi hali ya hewa inatangazwa kuwa mbaya bali bado watu wa *SUMATRA* hawafuatilii vyombo namna vinavyojaza watu kwenye maboti na kusafirisha bila ya kujali.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa ninaunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

MHE. DR. GETRUDE MONGELLA: Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Ukerewe wanashukuru na wana matumaini kwamba utengenezaji wa kivuko cha Rugezi – Kisonya utakamilka hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kivuko kutoka kisiwa cha Ukerewe kuelekea visiwa vya Gana, Kamasu na vinginevyo upande wa Magharibi wa Wilaya. Visiwa hivyo vina wakazi wengi na shughuli nyingi za uvuvi ziko sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba matengenezo ya uwanja wa ndege wa Ukerewe.

Naomba kukamilishwa barabara iliyoanzwa kwa lami nyembamba kama ilivyoahidiwa wakati wa Waziri Magufuli

MHE. HEMED MOHAMMED HEMED: Mheshimiwa Spika, nimuombe Mola atupe amani ya kudumu katika nchi yetu. Mheshimiwa Spika, hongera kwa kazi yako.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mbele yetu kuna hotuba ya miundombinu, hotuba ambayo imejaa nia njema ya Serikali kutaka kufanikisha usafiri katika nchi yetu, namwomba Mwenyezi Mungu amuwezeshe Mheshimiwa Waziri Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, katika kufanikisha azma yake. Ila bajeti yake ni ndogo!! Ni vyema Serikali iitupie jicho la rehema ili ipatiwe fedha za ziada kwani ili kufanikisha kauli mbiu ya Serikali ya “Kilimo Kwanza” ni lazima Wizara iwezeshe ili kauli mbiu hiyo ifanikiwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari na usafiri wa majini, bado bandari zetu hazijaweza kukidhi haja. Hii ni kutokana na ufinyu wa bajeti. Inafahamika kwamba sasa tuko katika ushindani wa biashara ndani ya Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki na *SADC*. Ukiangalia mapato ya shehena ya makontena mwaka 2007, ni makubwa kulinganisha na mwaka 2008. Kazi hii imefanyika katika bandari ya Dar es Salaam. Yote haya yanasababishwa na kushuka kwa tija ya kupakua na kupakia kwa mizigo. Ushindani wa kibiashara umepolekea majirani zetu kama bandari ya Mombasa kuongeza pato kila leo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina bandari nyingi, kwani tumezungukwa na bahari ya Indian Ocean, tuna maziwa makuu matatu, kama vile Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Tungeveza kuzikuza rasilimali zetu hizi, nchi yetu ingeweza kukua kiuchumi kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajali zinazotokea majini, watu wengi wanafariki dunia katika maji siku hadi siku. Vifo hivi vinasababishwa ama uchakavu wa vyombo vyetu na pia uzembe wa Madereva. Naiomba Serikali iwe na umakini kunusuru maisha ya watu na mali zao. Naiomba Serikali iipatie fedha *SUMATRA* ili iweze kununua zana nzuri za kileo, kwa nia ya kuweza kuokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara, pamoja na jitihada njema za Serikali kuzifanya barabara zetu kuwa ni za kiwango, ziko baadhi ya barabara zimetengenezwa vizuri lakini hivi sasa zinabomoka. Hii ni kasoro kubwa! Inaonekana ni ukosefu wa wasimamizi wazuri na kumfanya mkandarasi afanye anavyotaka. Ili hili lisiendelee *TANROADS* inatakiwa ijikite katika kusimamia ujenzi wa barabara zetu kwa kiwango ili inusuru upoteaji wa fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu reli, Shirika la Reli Tanzania lilikuwa chini ya Serikali. Hali ambayo iliweza kutoa huduma nzuri na tukaondokana na tatizo la usafiri. Mara tu Serikali ilipokubali kutia mkataba na wabia, reli hii imeelekea kufa na kushindwa kutoa huduma. Aidha, hali mbaya ya reli, kampuni ya *TRL* itasababisha msongamano wa makontena katika bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Shukuru Jamanne Kawambwa na Naibu wake, kwa nia yao njema kwa Watanzania wenzao. Mungu wabariki, ahsante.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa, kumpongeza Waziri na Naibu Waziri wa Miundombinu, kwa kazi nzuri, hongereni!

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya CCM kwa kujitahidi kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2005, kuhusu matengenezo ya barabara nyingi za lami.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kuwa barabara pale Senkenke ina mashimo, kulikoni? Inasikitisha! Barabara ya Dodoma – Singida – Mwanza, ilisahaulika sana, Mungu si Athumani, barabara ya Singida – Mwanza lami tayari, kwa nini hata miaka miwili haijaisha eneo la Senkenke kuwe na mashimo? Naomba Waziri afuatilie suala hili.

Mheshimiwa Spika, naomba sana barabara ya Mwabuki – Ngudu – Malya ijengwe. Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inaelekea Malya kwenye Chuo cha Michezo cha Afrika Mashariki. Haipendezi! Tunazalisha wataalamu wa michezo lakini wanapita eneo bovu, naomba barabara hii itengenezwe haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100%.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza sana Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara na *TANROADS* kwa kazi nzuri za ujenzi wa barabara nchini na maandalizi ya hotuba ya 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, pamoja na michango niliyotoa ndani ya Kamati ya Miundombinu, ninapenda kupata maelezo ya ziada katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuikumbusha Wizara kuhusu maombi niliyotoa mwaka 2008/2009. Wakati wa kuchangia bajeti ya mwaka 2008/2009, nilitoa maombi maalumu na majibu yaliyotolewa yalinipa matumaini kwamba katika bajeti ya mwaka 2009/2010 yatatekelezwa.

- Kuweka lami km 1.5 eneo la barabara ya Mkoa ya Pangani – Muheza, kutoka eneo la Muheza Mjini kuelekea Kilulu. Lengo ni kuupa hadhi mji mdogo wa Muheza.

- Kujenga mfereji eneo la barabara ya Mkoa kutoka Pangani – Muheza na eneo la kutoka Muheza Mjini - Kilulu, hasa ukizingatia kwamba mifereji ilijengwa upande mmoja wa barabara na kuacha upande wa pili ambapo lipo bonde kubwa linalobeba maji kutoka mlima mdogo kuanzia eneo la Benki ya *NMB* Muheza kuelekea Kilulu.

Mheshimiwa Spika, pili, mpango wa *PMMR* Mkoa wa Tanga na mapendekezo ya utekezaji – barabara ya Muheza – Amani (Kwamkoro). Napongeza sana mpango wa *PMMR* kuanza utekezaji kwa Mkoa wa Tanga baada ya kuachwa nyuma na Mikoa ya Mwanza na Rukwa. Napenda kupata ufafanuzi na kutoa mapendekezo yafuatayo:-

(a) Mpango wa *PMMR* Mkoa wa Tanga, una barabara za *Tanga East (Package 4)* na *Tanga West (Package 5)*. Je, ni barabara zipi zilizopo kati ya *package 4* na *5*?

(b) Kwa kuwa Serikali iliahidi kuweka lami barabara ya Muheza – Amani (ninavyo vilelezo vya maandishi), je, kwa mpango huu wa *PMMR* kwa lengo la kuendelea kuimarisha barabara hiyo ya Muheza – Amani hasa baada ya kuweka zege eneo la kona kali mlimani Amani, utakuwepo uwezekano wa kuweka lami angalau maeneo korofi machache hasa Mlimani Amani kwa mfano:-

- Eneo la Polisi Amani hadi Kibaoni (Njia Panda);
- Eneo la Kisiwani – Geti la Ziggi; na
- Eneo la Kiwani – Fanusi.

Mheshimiwa Spika, urefu wa maeneo hayo matatu hayazidi urefu wa zaidi ya kilomita tatu.

(c) Barabara ya Muheza – Amani kwa kawaida inaishia Kwamkoro (Amani). Mpango wa *PMMR* kwa barabara hiyo inaishia eneo la Kibaoni (Njia Panda) na kuacha eneo la barabara hiyo kutoka Kibaoni – Malaria – Kwamkoro. Je, kipande hicho kimewekewa mpango maalumu wa kukihudumia?

(d) Pendekezo la utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Muheza – Amani (Kibaoni). Kwa kuwa maeneo korofi zaidi ya barabara hiyo yapo katika maeneo ya mlimani Amani, kazi za ujenzi wa barabara ya Muheza – Amani ianze kutokea mlimani Amani kushuka chini, yaani kutokea Amani, Kibaoni hadi Lunguza – Mombani – Muheza (Mbaramo). Nashauri kwamba msimamizi na Mkandarasi anayekabidhiwa barabara hiyo ashirikishwe katika kukubali pendekezo hilo kwa mpango wa sasa wa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, tatu, barabara zilizoachwa katika Mpango wa Kupandisha Barabara za Wilaya kuwa za Mkoa, katika Wilaya ya Muheza. Barabara hizo ni:-

(a) Barabara ya kutoka Kilulu – Mtindiro – Kwabada – Mbambara – Bagamoyo – Barabara Kuu (Tanga – Segera).

- Barabara hii imejengwa kwa mpango wa *ASDP* kwa kiwango cha juu sana;
- Barabara inaunganisha kata za Kilulu, Mtindiro na Kwafungo;
- Barabara inaunganisha barabara ya Mkoa ya Pangani – Muheza na Mji wa Muheza na pia eneo la kijiji cha Bagamoyo na barabara kuu (Tanga – Segera);
- Barabara inapita katika maeneo ya mashamba makubwa ya machungwa kuliko eneo jingine lolote la Wilaya ya Muheza. Mashamba ndani ya Kata za Kilulu, Mtindiro, Kwafungo na Songa;
- Zipo shule nne (4) za Sekondari za Kilulu, Mtindiro, Kwafungo na Songa katika eneo hilo, zahanati nne (4), Mahakama nne za mwanzo; na
- Lipo soko kubwa eneo la Mtindiro, soko hilo linalohudumia biashara ya machungwa kwenda nchi jirani (Kenya/Uganda) na masoko ya Dar es Salaam, Arusha, Moshi, Dodoma, Morogoro, hadi Iringa/Mbeya. Naomba maelezo!

(b) Barabara ya Kimbo – Potwe. Hii sio barabara mpya bali ni kiungo cha barabara za Mkoa za Wilaya ya Korogwe na Muheza. Barabara ya Korogwe – Magungu – Maguzoni inajifungia Maguzoni Wilaya ya Muheza, iunganishwe Maguzoni – Potwe, Kimbo (Muheza) ili kuunganisha na ile ya Bombani – Mashewa (Kimbo).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 139, wa hotuba ya Waziri jedwali Na.2 na namba 14, Mtwara Region, kwa nini mradi wa “*detailed design*” Mangaka – Mtambaaswala,

uwekwe chini ya barabara za Mkoa na siyo Taifa? Kwa hali halisi ilivyo, barabara hii inaelekea kuunganisha nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, Waziri amesema katika hotuba yake kuwa Daraja la Umoja, linatarajiwa kumalizika mwezi Oktoba, 2009. Je, tutafikaje katika daraja bila kuwa na barabara? Je, barabara ya Mangaka hadi Mtambaaswala, inatarajiwa kuanza kujengwa lini?

Mheshimiwa Spika, mwisho, sisi wa Mikoa ya Mtwara na Lindi, tunaishukuru sana Serikali. Sisi tunawaelewa sana wenzetu wa Mikoa ya Tabora – Kigoma na Rukwa, wanavyosema humu Bungeni kuhusu barabara na sisi tulikuwa tunasema hivyo hivyo miaka kumi iliyopita, sasa tumetulia. Tungependa na wenzetu hao waangaliwe ili barabara yao ijengwe na wao waone jinsi barabara inavyokuwa kichocheo cha maendeleo. Sisi wa Mikoa ya Kusini, ni mashahidi wa jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu. Nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa (Mb) na Naibu Waziri, Mheshimiwa Chibulunje (Mb), kwa kazi na nia nzuri waliyonayo, tatizo lililopo ni uhaba wa fedha lakini uwezo mnao, ahsante.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na taasisi zake, kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa hotuba hii, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, nichukue fursa hii, kuishukuru sana Wizara ya Miundombinu, kwa kusikiliza kilio chao na kuanza kujenga kupitia *TANROADS* barabara za Igamba – Msangano – Utambalila kupitia vijiji vya Nkala na Chitete; Chapwa – Chindi na Msangano kupitia vijiji vya Namola, Chiwezi na Msamba II; Mlowo – Utambalila – Ntingwa – Itumbula – Kamsamba; na Kakozi – Kapele – Kasinde – Ilonga kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, ulikuwa ni uamuzi wa kijasiri na wa busara sana pale *TANROADS* ilipoamua kupitisha kipande cha barabara ya Igamba – Msangano – Utambalila kati ya Msangano na Tinding’oma kupitia vijiji vya Nkala na Chitete, kwenye eneo la ardhi oevu. Eneo hili lina ardhi nzuri kwa kilimo cha mpunga na mahindi na ndiko uliko mradi mkubwa wa umwagiliaji wa Naming’ongo (*Naming’ongo Irrigation Scheme*).

Wananchi wa Kata za Chitete na Msangano, wanaishukuru sana Serikali kwani huu ndio mwanzo wa kufungua sehemu ya Bonde la Ufa la Jimbo la Mbozi Magharibi. Ni matumaini ya wananchi hawa kuwa kile kipande cha barabara ya Chapwa – Namola – Chindi – Msangano kati ya vijiji vya Msamba II – Chindi – Msangano ambacho hakijalimwa, kitatengenezwa ili kufungua barabara hii kwenda Tunduma bila kulazimika kusafiri kwa umbali wa zaidi ya kilomita 130 kwa kupitia Vwawa badala ya kilomita 46 kutoka Msangano.

Mheshimiwa Spika, pia kipande cha barabara hii kati ya Nkala (Chitete) na Mkulwe Mission kama kikijengwa, kitakamilisha kilomita 40 ambazo zitawezesha usafiri kutoka Kamsamba (*Rukwa border*) na Tunduma kukamilika, ndani ya saa moja na nusu hadi Tunduma na Vwawa (Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi) badala ya saa 7 hadi 8 ambazo wananchi hutumia kwa sasa wakati wa majira ya kiangazi. Eneo hili ni ghala la chakula kwa Mkoa wa Mbeya ambalo kwa Mkoa wa Mbeya halijatumiwa hata robo yake. Barabara ya Kakozi (Ndalambo) – Kapele – Ilonga kwa upande wa Mbozi kuunganisha na ile ya kutoka Ilonga – Matai – Kasanga kwa upande wa Rukwa, ikikamilika, italeta ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Ukanda wa Juu wa Jimbo la Mbozi Magharibi. Kwenye eneo ipitayo barabara hii, kuna mradi mwingine mkubwa wa umwagailiaji wa Iyandwe ambao naamini utakapokamilika utakuwa wa kipekee kabisa nchini kwa kilimo cha mpunga wa Uwanda wa Juu. Kwa bahati mbaya, barabara hii, ujenzi wake wa mwanzo unalalamikiwa na wananchi kwa kuwa nyembamba kuliko iliyokuwa awali na kwa kiwango cha chini. Naomba usimamizi mzuri na wa karibu kwa barabara hii ili thamani ya fedha ilingane na kazi itakayofanyika.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na jedwali la mgawanyo wa fedha za barabara, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, barabara hizi zimepewa fedha kama ifuatavyo:-

Chapwa – Namola – Msangano	-	Tshs.60milioni
Ndalambo (Kakozi) – Kapale – Ilonga	-	Tshs.60milioni
Msangano – Tindingoma	-	Tshs.120milioni
Mlowo – Kamsamba	-	Tshs.60milioni
Igamba – Msangano	-	Tshs.93.818milioni

Mheshimiwa Spika, ombi la wananchi wa Jimbo hili, ni kuona fedha hizi zinatumiwa kama ilivyotarajiwa. Barabara zitengenezwe kwa kiwango tarajiwa. Wananchi wa Jimbo letu watajawa na wingi wa shukrani kwani tangu uhuru upatikane hii ndiyo mara ya kwanza wanaona barabara zao zinatengenezwe. Kilio chao kikubwa, ni kuondolewa mzigo wa usafiri wa enzi za ujima (wa miguu). Ushahidi tosha kuhusu kutokuwepo miundombinu ya barabara ni pale viongozi kuanzia wa Mkoa hadi wa Taifa, wanaposhindwa kwenda kuwatembelea wananchi walioko huko, ama wakithubutu kwenda huko wanakwama njiani.

Mfano hai, ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Chibulunje aliposhindwa kufika Kamsamba kuhimiza ujenzi wa shule mwaka juzi. Pia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri yetu, alipoambiwa na washauri wake na Kamati ya Ulinzi ya Mkoa na Wilaya ya Mbozi mwaka jana mwezi wa Oktoba kuwa Jimbo la Mbozi Magharibi halifikiki kwani barabara zake ni mbaya. Naomba Jimbo hili ambalo jioografia yake ya kuwepo Mkoa wa Mbeya inalifanya liwekwe kwenye maeneo yaliyoendelea, liwekwe kwenye kundi la maeneo ya pembezoni. Jimbo hili liko nyuma kwa kila namna kimaendeleo pamoja na kuwa na rasilimali lukuki.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Serikali kwa kuiweka barabara ya Tunduma – Sumbawanga kwenye mpango wa kujengwa kwa lami kuanzia mwisho wa mwaka huu wa 2009. Kinachonitia mashaka, ni kiasi cha fedha za ndani kilichotengwa

kwa ajili ya michoro, usanifu na ujenzi wa Tshs.2.120 bilioni bila kuonyesha kiasi ambacho Mpango wa Ushirikiano wa Changamoto ya Milenia (MCC). Barabara za maeneo mengine zimepangiwa kiasi cha fedha za ndani na nje, kwa nini siyo hii? Kuna ukweli wowote kama barabara hii itatengenezwa? Isipotekelezwa, Ilani yetu itatusuta.

Mheshimiwa Spika, naishukuru tena Serikali kwa kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mlowo – Kamsamba. Tatizo bado ni kilomita 25 kati ya Itumbula na Kamsamba. Wananchi wanafikiri kutokamilika kipande hiki inakuwa jadi ya Serikali kufanya hivyo kwa kutowajali. Naiomba Serikali itoe ufafanuzi juu ya taarifa yake ya hivi karibuni kuwa ujenzi utanza baada ya gharama za michoro na usanifu wa daraja la mto Momba unaounganisha Wilaya ya Mbozi na Sumbawanga kukokotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, naunga mkono hoja.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa, Dkt. Shukuru J. Kawambwa, kwa jitihada zake za juu za kutekeleza majukumu yake ndani ya Wizara yake. Vile vile nimpongeze kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba yake ya bajeti vizuri sana na ni imani yangu kuwa amepata mshikamano wa kutosha kutoka kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Chibulunje (Mb), Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, ni mwadilifu sana, ni imani yangu kuwa hata wanaomsaidia wamefuata nyayo zake. Hivyo, yote aliyoyaainisha, atayatekeleza ipasavyo. Mwenyezi Mungu awatie nguvu, afya, maisha marefu na mshikamano, ili utekelezaji uwe wenye tija kwa Taifa ukiwemo Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kurudia kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanyika katika kukipanua na kukarabati uwanja wa ndege wa Singida. Kazi kubwa hii iliyofanyika, itawezesha sasa ndege za biashara kutua Singida endapo kitawekwa lami. Ninaomba Serikali kuwa kazi iliyofanyika ya kutengeneza kiwanja hiki cha ndege ni kubwa na fedha nyingi sana zimetumika, hivyo, kama Serikali itachelewa kuweka lami uwezekano mkubwa wa kuharibika na fedha zote zilizotumika zitapotea bure. Ninaomba Serikali ifikirie uwezekano wa kuweka lami kiwanja hiki ili fedha nyingi zilizotumika kukitengeneza zisipotee bure. Ninamuomba kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru, wakati anafanya majumuisho yake, anipe maelezo yenye kutia moyo kwa wana-Singida.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Serikali kwa jinsi inavyojitahidi kuitengeneza barabara ya Kiomboi Bomani hadi Misigiri kwa kiwango cha lami ingawa imetengewa fedha kidogo sana. Napenda kuiambia Serikali kuwa barabara hii urefu wake ni km.21 na km.5 zilishatengenezwa na kupitia bajeti hii zimetengwa fedha za km.5, hivyo zitakuwa zimebaki km.11 tu. Ninaomba Serikali kwa kuwa barabara hii sio ndefu sana, itengenezwe yote kwani kutengeneza kidogo kidogo mpaka itakapokuja kumalizika sehemu iliyokwisha kutengenezwa itakuwa imekuwa viraka vitupu.

Kaka yangu Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, chonde chonde angalia uwezekano wa kutafuta fedha kumaliza kilomita kumi na moja zilizobaki. Nitashukuru kupata majibu mazuri kaka yangu mpendwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Shelui–Sekenke–Mingela–Doromoni–Tulia–Kidaru. Ninaendelea kuipongeza Serikali kwani zipo barabara Mkoani Singida ambazo zimepandishwa daraja kuwa za Mkoa mfano, Kiomboi – Kisiriri – Kidani – Ibaga – Mwangaza – Kidarafu. Kwa kuwa barabara niliyoandika hapa juu inakutana na hii barabara ambayo imepanda daraja, ninaomba Serikali ikubali na kuifikiria barabara tajwa hapo juu kuwa ya Mkoa kwani inakutana Kidaru na maeneo inayopitia kuna vijiji vingi vyenye wakazi wengi na ni wakulima wakubwa na wafugaji na kuna taasisi mbalimbali za Serikali. Ninategemea huruma ya Serikali juu ya ombi la wana-Iramba.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Shelui Mtoa Mtekente – Urughu – Ushora – Usule. Niendelea kuiomba Serikali kuwafikiria wana-Singida katika kupandisha barabara kwani hata hii barabara niliyoitaja hapo juu ni kubwa, kwani ina watumiaji wengi ambao ni wazalishaji wakubwa wa pato la Serikali na inapita kwenye vijiji vingi sana. Ninaiomba Serikali bajeti ya mwaka 2010/2011, barabara hii iwe ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma - Sanza. Napenda kuikumbusha Serikali kauli ya Mheshimiwa Rais alipokuwa na ziara Mkoani Singida, Wilaya ya Manyoni aliahidi, aliahidi barabara ya Dodoma - Sanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Hivyo, ninaomba Serikali ijitahidi kutekeleza ahadi ile ili isije ikakigharibu Chama cha Mapinduzi kwenye uchaguzi wa mwaka 2010, bado wana Singida wanampenda sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya – Tabora. Ninaipongeza sana Serikali kwa kutenga fedha za kujenga barabara hii. Kwa uelewa wangu, barabara hii tayari ilikwishatangaza tenda ili ianze ujenzi. Cha kusikitisha, tumeanza kupata minong’ono kuwa barabara hii sasa itanzia Tabora badala ya kuanzia Manyoni. Napenda kujua, kuna sababu gani za msingi barabara hii kujengwa kuanzia Tabora badala ya Manyoni? Kama minong’ono hii ni ya kweli, Wabunge wa Singida hatutaelewa Serikali pamoja na uongozi mzima wa Mkoa wa Singida. Ninaungana na wenzangu kusema kuwa utaratibu wa mwanzo mpaka tenda ikatangazwa ufuatwe, barabara ianzie Manyoni – Itigi – Chaya hadi Tabora.

Mheshimiwa Spika, treni ya Dodoma - Manyoni – Singida Mjini, ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Singida. Cha kushangaza ni kwamba, mwekezaji haithamini reli hii kwa madai kuwa haina faida kwake. Ninaiomba Serikali imweleze mwekezaji kuheshimu mkataba ili aendelee kuifanyia ukarabati njia ya reli pamoja na kutupa mabehewa ya kutosha na mazuri kwani wanaleta mabehewa machakavu sana na njia sio nzuri husababisha treni kuyumba na abiria kupata hofu kubwa. Nategemea majibu ya Mheshimiwa Waziri wakati akitoa maelezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya mchango wangu huo, napenda nitamke rasmi kuunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia nikiwa ninasubiri maelezo yenye kunitia moyo kutoka kwa kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Miundombinu na Mbunge wa Bagamoyo. Mungu awatangulie katika utekelezaji wa mikakati yao.

MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wengine wote hapo Wizarani, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uelewa nilionao kuhusu mambo ya barabara, ni muhimu na lazima kuzikarabati (*routine maintenance*) barabara zetu na kwa zile za lami (*tarmac*), ni lazima zaidi '*periodic maintenance*' iwepo, tofauti na hivyo, barabara zote zitaharibika na kuwa vigumu sana kuzikarabati na hivyo kuwa ghali sana kuzirudisha kwenye hali nzuri na kwa kuzingatia kuwa barabara za lami zina muda maalumu wa kuishi i.e. *10 years – 15 years*.

Mheshimiwa Spika, hongereni pia kwa kuiangalia nchi kwa ujumla wake na ndiyo maana kuna miradi nchini kote na utekelezaji mzuri wa Ilani na Ahadi za CCM zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni mwaka 2005. Nishukuru kwa kazi iliyoanza ya kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kwasadala – Masama (12.5 km) ambapo kazi iliyoanza ni ya '*detail design*' ambayo imeshakamilika na tuna matarajio ya kazi kamili ya ujenzi kuanza katika bajeti hii na ninaomba nifahamishwe rasmi kupitia bajeti hii. Nikumbushie zile barabara ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Hai, iliomba zipandishwe daraja na kuwa za Mkoa (*TANROADS*), zifikiriwe kwani hata katika Kikao cha Barabara cha Mkoa zilishapitishwa na zinakidhi '*requirements*' zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, nisisitize mambo machache kwa ustawi kwa Taifa letu; usafiri wa reli, usafiri wa majini, viwanja vyetu vya ndege pamoja na mipango yote mizuri iliyo na hapa hapa ni lazima tufuate utaalumu zaidi na kuangalia uchumi.

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote hapo Wizaran, endeleeni na kazi, hii miluzi mingi isiwababaishe yote hii ni kutokana na uwezo uliopo.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninayo barua ya Mheshimiwa Waziri (Ref.Na.MMI/GEN/2009/48), ya tarehe 17/06/2009, akinieleza kuwa *TPA* wametenga Tshs.50 million kwa ajili ya ujenzi wa gati Manda. Mbona kwenye sehemu ya 85(Uk.63) gati hii haitajwi na fedha yake iko wapi? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, pili, lengo la kuendeleza Kanda ya Maendeleo ya Mtwara, ni kuwezesha maendeleo ya miradi mikubwa ya Liganga na Mchuchuma. Katika bajeti, hii barabara ya lami (na reli) vinaishia Mbamba-Bay, kwa nini hazungumzii kupeleka miundombinu hiyo Liganga/Mchuchuma?

Mheshimiwa Spika, tatu, nashukuru kusikia kwa mara ya kwanza kuwa kuna maandalizi ya ujenzi wa barabara za lami za Itowi – Mchuchuma/Liganga – Manda. Naomba ufafanuzi; kwanza, ni maandalizi gani hayo kwa mfano na pili *time-frame* ya maandalizi na ni lini utekelezaji unaanza?

Mheshimiwa Spika, nne, niliwasilisha andiko la maombi ya fedha daraja la Mto Ruhuhu eneo la Masimavalafu, ili kupata pesa ya *Tanzania – Japan Counterpart Fund* na zile zilizotengwa na Wilaya ya Ludewa na Mbinga Mashariki, mbona Wizara yako iko kimya kwenye mchango wa Wizara?

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu usalama wa vyombo vya majini, kwa nini visitajwe vyombo visivyotimiza masharti ya ukaguzi (viwango), ili tuvifahamu na tuhakikishe havifanyi kazi?

MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, viongozi na wataalamu wa Wizara na taasisi za Wizara, kwa hotuba nzuri yenye matumaini makubwa kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa ujenzi wa barabara ya Msata – Bagamoyo – Dar es Salaam kama barabara mbadala na ya nyongeza kuunganisha Tanzania ya Kaskazini, Kaskazini Mashariki, nchi jirani za Kenya na Uganda na bandari ya Dar es Salaam, hivyo kupunguza ajali na msongamano mkubwa barabara ya Chalinze – Dar es Salaam. Vyivyo hivyo barabara ya Korogwe – Handeni – Magole – Turiani – Dumila – Ludewa kuunganisha barabara ya Morogoro – Dodoma na barabara ya Tanga – Arusha na hivyo kuwezesha matumizi endelevu ya bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ikubali kuiweka chini ya *TANROADS* Mkoa, barabara ya Dochi-Mombo (KM8) iwe barabara mbadala kati ya Lushoto Mjini na barabara kuu ya Tanga – Arusha. Barabara ya Mombo – Soni, ni finyu mno, *blind corners* nyingi na magari ni mengi sana. Tunaomba ipanuliwe na hasa Makona.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iongeze jitihada za kupata fedha na wawekezaji bandari ya Mwambani Tanga ili ijengwe na reli ya Tanga – Arusha – Musoma nayo ijengwe tukizingatia umuhimu mkubwa wa *corridor* hii kwa uchumi wa nchi yetu na usafirishaji kati ya Tanzania na nchi jirani za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, uwanja wa ndege Mombo ambao ni wa enzi za *East African Airways*, ni vema ukarabatiwe na kupandishwa hadhi kurahisisha usafiri wa watalii wanaotalii kwa wingi Milima ya Usambara na *Mkomazi Game Reserve*.

Mheshimiwa Spika, nakumbusha kilio cha wakazi wa Tarafa za Kaskazini Lushoto kwamba barabara inayounganisha miji midogo ya kibiashara ya Mlalo – Ngwelo – Mlola – Makanya – Milingano – Mashewa hadi Tanga, isimamiwe na *TANROADS* Mkoa kwani hii ndiyo njia fupi kati ya Mlalo, Mlola na Tanga Mjini. Serikali inasemaje kuhusu ombi hili?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika katika kuandaa hotubu hii na pia kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005 na hasa katika ujenzi wa barabara za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, usimamizi madhubuti katika ujenzi wa barabara za Kilwa - Sam Nujoma – Mandela - Bandarini, tunaomba kasi iongezeke kwa kuzingatia ubora wa barabara na mifereji ya maji ya mvua. Kwani katika maeneo kadhaa, ubora wake ni hafifu sana, hasa katika eneo la Mtoni, mifereji imebomoka na *'finishing'* kwa ujumla si nzuri.

Mheshimiwa Spika, tunaomba *TANROADS* Dar es Salaam na wahusika katika ujenzi wa barabara zilizoainishwa kwa madhumuni ya kupunguza msongamano wa magari katika mkoa wa Dar es Salaam, waharakishe michakato mbalimbali ili kuharakisha ujenzi wa barabara hizo zikiwemo Tabata Dampo -Kigogo, Mbezi - Kinyerezi na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa 100%.

MHE. BAKARI SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii, kumshukuru Mungu kwa kunipa uwepo na wasaa na kuweza kutoa maoni yangu japo kidogo tu kuhusu mada iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, bandari ni moja kati ya taasisi muhimu katika kuongeza pato la taifa lolote duniani. Bandari inapotumiwa kikamilifu katika idara zake zote, ni kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa nchi. Bandari ya Dar es Salaam kijiografia ipo nafasi nzuri kwa kuhudumia zile nchi zote za jirani na ambazo hazina bandari (*land-locked countries*). Bunge limekuwa likisema mara nyingi juu ya kutoridhishwa na utendaji wa bandari hii lakini ukweli unabakia pale pale kwamba bila ya ufanisi wa wadau wote pale bandarini, wakiwemo *TPA, TICTS, TRA* na kadhalika hapana kitakachofanyika.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Bunge, ni kuisimamia Serikali kwa maana ya utendaji, mapato na matumizi. Bunge limetoa Azimio kwamba pamoja na mambo mengine, basi *TICTS* haifanyi vizuri na ndio chanzo kikubwa cha uzoroteshaji na utendaji mzuri pale bandarini, likaazimia kwamba wawekezaji wale hawafai, kwa hiyo waondolewe, watafutwe wawekezaji wengine au kama hapana budi ya kuendelea basi ule

muda wa mkataba ulioongezwa usitishwe na hivyo muda wao uishie mwaka 2010 lakini muhimu ni kufanyiwa marekebisha baadhi ya vipengele vya *TICTS* ambavyo vina upungufu makubwa.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha ni kwamba Serikali mpaka sasa haijafanya hivyo. Hapa mimi nina mashaka makubwa, ninajiuliza kulikoni? Kwamba huyu *TICTS* yuko juu ya mihimili miwili yaani Bunge na Serikali? *TICTS* wanakataa kila wanaloambiwa! Tunasubiri tamko la Serikali kuhusu *TICTS* kwa hamu kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ifanye juhudi ya makusudi na hasa ya barabara, reli na hata viwanja vya ndege maana miradi hii kama itapatiwa mkazo wa aina yake, itasaidia sana sio tu kukuza uchumi wa nchi, bali na usafiri wa abiria ambao kwa sasa wanapata usumbufu mkubwa sana. Tufike mahali tuwe na miradi michache hasa ya barabara lakini ambayo tunao uhakika wa kumalizika kwa wakati, kuliko kuwa na miradi mingi ambayo kupatikana kwa pesa za kuikamilisha ni vigumu sana. Tusiwe na miradi mingi ili mradi kila mtu apate kama wanavyodai Wabunge wengi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kama inavyojulikana kwamba ajali zimezidi, hii inatokana pamoja na uzembe wa wadau husika, lakini vile vile ni kutokana na kutokuwepo na kawaida ya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo husika vikiwemo magari, meli, boti na kadhalika. Kwa hivyo, ni vyema Serikali kuliona hili na kulipangia mikakati maalumu.

Mheshimiwa Spika, chonde chonde, Serikali kwa makusudi kabisa lazima iandae mikakati mahsusi juu ya kuipatia pesa *ATCL* ili ipate kutekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia bila hivyo shirika litakwenda na maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri iliyozingatia utekelezaji wa Sera na Ilani ya CCM katika juhudi ya kuimarisha miundombinu hususan barabara ambayo inategemewa na Watanzania zaidi ya 90% na usafirishaji mizigo kwa 80%.

Mheshimiwa Spika, lakini Wilaya ya Ngorongoro imesahaulika kwa sababu zifuatazo:-

(1) Hakuna barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya na Ngorongoro (Loliondo) kwa kupitika wakati wote wa majira ya mwaka licha ya Ilani kusema hivyo;

(2) Ahadi ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 20/3/2007 kwa wananchi wa Ngorongoro kwamba watapatiwa barabara ya lami kutoka Mto wa Mbu – Engaresero – Loliondo – Musoma, haikutajwa popote katika hotuba yako;

(3) Loliondo sio mbali, ni kama kilomita 440 kutoka Arusha lakini kwa sababu ya miundombinu duni sana ni mbali na muda wa safari ni mrefu; na

(4) Barabara hii ingeunganisha Mkoa wa Arusha na Mara kwa kiwango cha lami na magari makubwa yanayopita hifadhi ya Ngorongoro na Serengeti huharibu mazingira na kugonga wanyama pori, hayatapita tena huko!

Mheshimiwa Spika, naomba majibu ya Serikali katika jambo hili.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri wa Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa na kuwasilisha hotuba nzuri na yenye kina. Aidha, ninaipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya kuboresha miundombinu mbalimbali inayoismamia hususani miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi, katika utengenezaji wa barabara nchini, ninasikitika kusema kuwa kuna baadhi ya barabara muhimu sana zinapuuzwa au zimetelekezwa. Kati ya barabara ambazo zimepuuzwa ni pamoja na sehemu ya barabara ya “*The Great North Road*”, sehemu ya Iringa – Dodoma – Babati. Kwa miaka takribani ishirini (20), barabara hii ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu lakini ujenzi haufanyiki. Wananchi wanaohudumiwa na barabara hii wamechoshwa na usanii huu, wanaomba ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami uanze. Katika bajeti ya mwaka 2008/2009, barabara ya Dodoma - Babati ilitengewa Shs.12.1bilioni lakini hakuna kilichofanyika hadi leo. Tunaomba kazi ya ujenzi wa barabara hii uanze.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2009/2010 barabara ya Dodoma – Iringa imetengewa Shs.20m/ tu, kiasi hiki ni kidogo mno! Aidha, barabara ya Dodoma – Babati imetengewa Shs.5.6bm/. Ninasikitika kusema kuwa inaonyesha kuwa Serikali haina dhamira ya kweli ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami hivi karibuni. Ninaomba Serikali itenge fedha za kutosha kuanza ujenzi wa barabara hii muhimu kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa reli, ninasikitika kusema kuwa usafiri wa reli umezorota sana. Nchi hii ilikuwa inategemea usafiri wa reli kusafirisha mizigo na abiria lakini hivi karibuni mambo ni tofauti kabisa. Mizigo na abiria wamehamia usafiri wa barabara kutokana na miundombinu ya reli kuwa mibovu sana. Hii siyo dalili njema. Serikali inashauriwa kuwekeza zaidi katika reli ili kubadilisha hali hii mbaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya machache, ninaomba kuunga mkono hotuba ya Waziri wa miundo mbinu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara, kwa kuandaa bajeti nzuri na kuiwasilisha Hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, naomba kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujua hivi ni lini hasa Uwanja wa Ndege Songwe – Mbeya utakamilika kujengwa hasa baada ya hatua (*phase*) ya tatu na ya mwisho kuchelewa kuanza kujengwa?

Pili, naomba pia kujua kama Serikali iko tayari sasa kutimiza wajibu wake wa kutoa pesa (za ndani) kama ilivyo kwenye bajeti. Wananchi wa Mbeya, wanasubiri kwa hamu sana kuona kiwanja kimekamilika mapema sana.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua umuhimu wa hali ya hewa duniani kote, sina sababu ya kueleza umuhimu huo hapa. Hata hivyo, ili shughuli za hali ya hewa ziende vizuri, tunahitaji wataalam wa kutosha katika fani hiyo. Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma, ndicho kwa sasa chuo pekee kinachofundisha wataalam wa hali ya hewa katika ngazi ya cheti. Kwa msingi huo, tunahitaji tukiimarisha chuo hicho kwa kiwango cha juu sana.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kina upungufu katika maeneo yafuatayo:-

1. Kukwama kwa jengo la chuo kwa zaidi ya miaka 12 sasa. Naomba Waziri atueleze hivi hasa jengo hilo ambalo tayari nondo zilishatumika, sementi, mchanga na kadhalika litakamilika?
2. Walimu wachache na utalam mdogo kwa baadhi ya watumishi. Kuwe na Mkakati Maalum wa kufundisha walimu wengi wenye sifa.
3. Hakuna nyumba za kutosha za walimu na watumishi wengine. Nyumba zaidi zijengwe.
4. Chuo hiki kiwe chuo kinachojitegemea, kisifanywe kama Idara chini ya Mamlaka ya Hali ya Hewa. Kwa kukifanya Chuo kamili, kitafanya shughuli za mafunzo vizuri na kwa ufanisi zaidi kuliko ilivyo sasa. Aidha, Chuo kiimarishwe zaidi ili kianze kutoa *diploma* na shahada pale pale Kigoma na siyo kuhamisha mafunzo (*diploma*) Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Mamlaka hii itengewe pesa zaidi za maendeleo ili iweze kujenga mtandao wa vituo vya hali ya hewa nchini. Mabadiliko yasiyotarajiwa ya hali ya hewa duniani, yanatufanya tuweke umuhimu mkubwa zaidi katika kujenga vituo vingi vya hali ya hewa kote nchini, ikiwa ni pamoja na kununua vifaa vya kisasa vitakavyofanya utabiri uwe wa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa ni mwaka mmoja na zaidi tangu Bunge hili lilipoazimia kusitisha Mkataba wa TICTS wa nyongeza ya pili ya miaka 15. Pamoja na kufanya marekebisho kwenye Mkataba wa awali, ambao una vipengele vibovu kama vile *exclusivity* na kadhalika, hadi leo hakuna hatua yoyote ya msingi, ambayo Serikali

imechukua katika utekelezaji wa azimio hilo. Naomba majibu ya kina katika suala hili, vinginevyo sitaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, TAZARA ni sawa na marehemu; ni kama imekufa. TAZARA imesahaulika. Leo TAZARA inafanya kazi nchini ya nusu ya uwezo wake. Ili TAZARA iweze kufanya kazi yake sawa sawa, inahitaji zaidi ya shilingi bilioni 100. Aidha, TAZARA inahitaji zaidi ya shilingi 45 bilioni, kwa ajili ya kulipa mafao ya wafanyakazi wake wastaafu/marehemu. Pamoja na hatua ambazo Serikali inachukua za kutafuta wawekezaji kutoka China, naomba Serikali ichukue hatua za dharura za kuinusuru TAZARA ili ifanye vizuri, pamoja na kulipa haki/maslahi ya wafanyakazi hasa wastaafu. Kama Serikali imeweza kuwanusuru wafanyabiashara, kwa kuwawekea dhamana kwenye mabanki na kuendelea na biashara zao; sioni kwa nini Serikali iwaache wananchi waliotumika na TAZARA, kwa miaka mingi, waendeele kuteseka kwa kutolipwa mafao yao kwa kati ya miaka miwili hadi minne. Naomba majibu ya kuridhisha. Ahsante sana.

MHE. CLEMENCE B. LYAMBA: Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii, kutoa mchango wangu katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naipongeze Serikali kwa kutimiza ahadi yake katika Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2005, kuhusu kukamilika kwa usanifu na upembuzi yakinifu wa kina wa barabara ya Mikumi – Kilosa, ambayo ina mchango mkubwa kufanikisha Mpango wa Fanya Morogoro Ghala la Chakula (FAMOGATA).

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, alithibitishie Bunge kama usanifu na upembuzi wa kina, umejumuishia madaraja mawili makubwa jirani na Barabara Kuu tarajiwa, katika Kijiji cha Uhaya Kibaoni na daraja moja katika Kijiji cha Zombo.

Mheshimiwa Spika, madaraja haya ni muhimu sana kwa sababu yanaunganisha Barabara Kuu na eneo kubwa la mashamba ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mrundikano wa makontena bandarini, unaochelewesha sana uondoshaji mizigo, hasa inayoelekea Demokrasia ya Kongo, Rwanda na Burundi; naishauri Serikali iibue mradi wa kuanzisha au kufungua Bandari Kavu katika eneo kubwa nje kabisa ya Jiji la Dar es Salaam. Eneo hili liwe na miundombinu tayari, ambayo inaweza kuboreshwa na kuongezwa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ichambue kwa kina, uwezekano wa kufungua na kujenga Bandari Kavu katika eneo la Ruvu, ambapo Reli ya Tanga – Dar es Salaam – Kigoma na Barabara Kuu ya Dar es Salaam – Tabora/Mwanza. Eneo hili ni kubwa kiasi, litatosheleza hifadhi ya mizigo hata kwa zaidi ya miaka 30 ijayo na kuepusha msongamano wa mizigo, magari na makontena mengi katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali katika kuendelea na matengenezo ya kawaida kwa barabara za kitaifa na za kimkoa, namwomba Mheshimiwa Waziri, atoe kipaumbele kwa TANROADS – Morogoro ili Barabaraba ya Mikumi – Ruaha Darajani, itengenezwe kwa kiwango cha juu zaidi kuliko ilivyokuwa awali na hususan katika maeneo ya madaraja ya Iyovi, ambako kuna mashimo mengi na maporomoko ya mawe makubwa kutoka milimani na kuangukia barabarani. Hatua za matengenezo muhimu zikichelewa, kuna hatari kubwa ya ajali kuongezeka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mji Mdogo wa Mikumi katika Barabara ya Mikumi – Ruaha (Kilombero), Reli ya Kilosa – Kidatu inakatisha barabara hizi. *Railway cross-roads* katika maeneo haya, zimekuwa katika hali mbaya mno kwa miaka mingi. Naomba Wizara iiagize TANROADS, matengenezo yafanyike. Hata Wabunge wanaosafiri kuelekea Iringa, Mbeya na sehemu nyingine za Kusini, mara kadhaa wamenionamba nihimize kuhusu haja ya kuboresha *railway cross-roads* hizo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimewaandikia TANROADS Morogoro, kuwaomba waweke jumla ya matuta manne ya kupunguza kasi ya mwendo kwa magari na pikipiki katika Vitongoji vya Simbalambwende na Ruaha (stendi ya mbuzi), ambavyo vinaambaa Barabara ya Mikumi – Ruaha, ambayo inasimamiwa na TANROADS.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya vifo sita vya watu vimetokea kwenye miteremko kwenye vitongoji tajwa katika miaka minne iliyopita na ajali nyingi, kwa sababu ya mwendo wa kasi wa magari katika maeneo haya. Nilikwishamwandikia barua mbili, Meneja wa TANROADS Morogoro, kuhusu tatizo hili, lakini anakabiliwa na upungufu wa fedha.

Kwa hiyo, naomba ujenzi wa matuta haya utekelezwe ili kuepusha vifo vya wananchi, ambao ni nguvu kazi ya Taifa letu. Ajali hizi zimekuwa zinatokea kutokana na idadi kubwa sana ya watu katika Kijiji cha Ruaha.

Mheshimiwa Spika, baada ya michango hii, naunga mkono hoja.

MHE. MCHUNGAJI DR. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naomba kuungana na wenzangu, kuwapongeza Waziri wa Miundombinu, Naibu wake na Watendaji wote, kwa Bajeti ya 2009/10; ni nzuri, imegusa kila eneo na inakidhi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu mizuri ndio maendeleo ya kila nchi. Ninaomba kuchangia kuhusu usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, *ATCL* imekufa, ina ndege moja mbovu wakati *Precesion Air* na Kenya Airways, wana ndege 32. Hii ni aibu kwa Taifa letu. Tunaingia East African Community, usafiri mkuu utakuwa ni wa anga. Kuisaidia *ATCL* ni suala la dharura na ili kuipa kipaumbele. Kutoisaidia *ATCL* ni kuwaimarisha Wakenya.

Tunaomba usafiri wa reli uimarishwe. Huu ni usafiri unaotegemewa sana na watu wa kawaida. Mbia wetu hana uwezo. Serikali imemsaidia lakini bado hawezi. Tunaomba mkataba huu utathminiwe upya. Malamamiko ya wananchi kuhusu Reli ya Kati ni makubwa sana. Rites haitaweza kuondoa kero za wananchi, ila Serikali isaidie katika management ya reli hii.

Fidia kwa Wakazi wa Kipunguni na Kiwalani, ilipwe kwa sababu pesa hizo zinapungua thamani, miaka 10 ya kungoja ni mingi. Tuwahurumie wananchi wetu.

Pongezi nyingi kwa Kivuko cha Kilombero. Tunashukuru pia kwa mpango mzuri wa daraja ila barabara zetu ni mbaya sana. Kutoka Kivukoni mpaka Ifakara ni mbaya. Kidatu – Ifakara iko katika hali mbaya. Ifakara – Mlimba, naomba zikumbukwe.

MHE. AMEIR ALI AMEIR: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, muumba mbingu na ardhi, kwa kutujalia uhai na uzima na kutuwezesha kuchangia bajeti katika kipindi hiki cha 2009/10.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji na Washauri, kwa kufanikisha na kutengeneza Kitabu hicho cha Bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kubwa na mambo yake ni makubwa, mengi na utekelezaji wake wa majukumu unamhusu kila mtu; mgeni na mwenyeji, kwa mahitaji ya kila siku. Kwa hiyo, lawama hapo ndio pao. Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake, wafanye kazi zao kwa kuzingatia vipaumbele bila upendeleo, kama inavyodawa na wachangiaji wengine. Ninasema, msikate tama, hayo yote ni wivu wa maendeleo yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kupitia Wizara hii, kwa kuliona tatizo linalozikumba bandari zetu la mrundikano wa kontena ambayo Mheshimiwa Waziri ameyataja katika hotuba yake, ukurasa wa 65 – 66.

Mheshimiwa Spika, ninaloliomba kwa Mheshimiwa Waziri na Watendaji, suala hili pia litaiongezea mapato Taifa letu na kuongeza bajeti ijayo na kuweza kufanya mengine ambayo hayatofikiwa kwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango huu, pia utaondoa mgongano ulioko bandarini hivi sasa wa kupeana lawama kwa mashirika yanayofanya kazi katika bandari zetu na hapo ndipo tutajua mchawi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba tena Serikali, suala hili lianze haraka na lisije likapigwa danadana kama Daraja la Kigamboni, ambalo utekelezaji wake unalegalega tokea 2005 na sasa unategemea kuanza 2010/11.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa Wizara hii na majukumu yalioko katika Wizara na kwa yale mengi yaliyotekelezwa na yale mengi yanayoendelea kutekelezwa, naunga mkono hoja hii, wapewe fedha wakaanze kazi. Ahsante.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waziri - Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Ezekiel Chibulunje, Katibu Mkuu – Ndugu Omari Chambo na Maafisa wote wa Wizara, walioandaa Bajeti ya Wizara yao na kuiwasilisha vyema hapa Bungeni

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali, kuipandisha Barabara ya Lucheche – Kitanda - Londo kuelekea Morogoro kuwa Trunk Road na fedha mlizotenga kuiimarisha na kuifungua barabara hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa hatua nzuri iliyofikia ya mchakato wa ujenzi wa Barabara ya Namtumbo Songea. Ninaikumbusha Serikali isijisahau, wataalam wachache wakawaponza wenzao na Wizara katika zoezi la tathmini ya fidia kwa watu watakoathirika na Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Namtumbo – Songea, kwani miradi mingi hupata malalamiko hasa katika zoezi kama hili.

Tunajua nia ya Serikali ni njema, ninachoomba, watakaokuja kulipa kulingana na tathmini, lazima wawe waadilifu na makini na wamwogope Mungu; kusiwe na dhuluma, kila mtu apate haki yake anayostahili kwani Watu wa Namtumbo ni maskini wamekubali kwa moyo mkunjufu kabisa kusogea kupisha barabara. Hivyo, naomba tuzingatie ushauri ili maendeleo yetu yasije kutokea manung'uniko yatatupunguzia baraka.

Kwa ujumla, naipongeza *TANROADS* (Ruvuma), kwa usimamizi mzuri wa barabara zetu, zinakarabatiwa na wanajitahidi kuwasimamia makandarasi kutokuwa na vifaa vya kuaminika na vya kutegemea. Nashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuwa-*gurantee*, kukopeshwa vifaa vya kazi. Makandarasi wa ndani wawe na vifaa vya kutumainiwa, kwani wana tabu sana ya kupata vifaa Mkoani Ruvuma.

Ushauri wa kupunguza msongamano wa Barabara za Dar es Salaam. Tanzania tumejaaliwa kuwa na bahari. Nashauri tuanze kufikiria ushawishi kwa watu wenye uwezo na wawekezaji wa nje, kuwekeza katika Dar es Salaam Sea Transport Net Work. Wawekeze katika kujenga magati vidogo kutoka Bagamoyo na waweke magati ya ferry boats stops, Bahari Beach moja, Kunduchi Beach moja, Kawe Beach – Msasani Beach – Masaki – Oysterbay. Mwanzoni mwa Toure Drive, karibu na mnara wa taa za kuongozea meli, karibu na China Embassy na mwisho Ferry na pale ferry, kwa kuanzia soko la samaki pana vijigati lakini tunaweza kuimarisha.

Wataalam wafikirie hili; ni jinsi gani tutaenda nalo na kuanza kulifanyia upembuzi yakinifu. Hili ni eneo la uwekezaji na litapunguza misongamano isiyo ya lazima, kuna watu wataacha magari yao au *necessary*, lakini pia ni eneo la kuongeza mapato kwa Serikali.

Lazima tufikirie njia mbadala ya kuwa *offload* watu, kutumia *land transport* tukatumie *sea transport*. Hongkong ina sqk. 7000, wana magari na watu wengi sana na wanaingiza watalii milioni mbili kwa siku, lakini wamepunguza msongamano kwa kutumia *ferry transport*, ndio kuna *fly overs* na *tunnel road*, lakini *sea transport* imesaidia sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayofanya, hasa katika kuboresha miundombinu. Pia nichukue nafasi hii, kuwapongeza Waziri na Naibu wake, kwa jinsi wanavyojitahidi.

Naunga mkono hoja hii, ila nami naona ni busara kama tutaachana na kulipa fidia nyumba zile za Kipunguni/Kipawa, kwani ni kuharibu mali. Mimi pia niliwahi kujiuliza swali hilo; kwa nini tusianzishe kiwanja kikubwa maeneo kama Chalinze au Chanika lakini hasa Chalinze ambako tayari kuna miundombinu na midomo ya maeneo ya Morogoro – South, Kaskazini, Dodoma na kadhalika. Sio lazima tuanze na majengo makubwa, la msingi ni *running ways* ambazo zinaweza kupokea ndege za aina zote, kisha watu wachukue ndege ndogo.

Mfano, nilivyoona South Africa ni Johannesburg – Capetown au Durban, Pretoria na kadhalika. Mfano mwingine ni Namibia, kiwanja kile cha Windhoek ni kikubwa sana njia zake, lakini majengo yake si makubwa. Hivyo, kwa kuanzia si lazima tuanze na majengo makubwa. Hata hivyo, Dar es Salaam sasa imejaa tuzidi kufungua maeneo mengine zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, tunashukuru kwa ajili ya barabara ya Namtumbo – Morogoro, iliyopanda hadhi. Nilisikia imetengewa bajeti toka mwaka jana, ningeshauri badala ya pesa hizo kutunzwa, kwa kuwa zinashuka thamani; ni vyema zikaanza kufanya kazi kwa kipande au madaraja makubwa.

Ziwa Nyasa, hatuna meli ya uhakika, imezeeka, ni vyema utaratibu ukaanza kufanyika wa kununua meli nyingine, yasije yakatokea kama yale ya Zanzibar.

Tunduru – Namtumbo, tutakuombeeni mzidi kutukumbuka, hali sio nzuri kabisa, lakini juhudi tunazona. Japo kuna ukweli kuwa, Mbuga za Wanyama za Selous, umaarufu wake utapatikana baada ya kuwa na barabara nzuri.

Barabara ya Mbamba Bay – Lituhi izidi kuboreshwa. Barabara ya kuunganisha Kipapa – Njombe ni ndogo, sio ya Mkoa lakini ni barabara muhimu na ni kama km. 15 tu. Kwa kuanzia ni vyema ikapewa *support* ya *special funds* ili kuipasua na baada ya hapo, iendelee na wilaya kama kawaida (Mbinga), ni barabara ambayo kiuchumi ni muhimu, kwani inaunganisha Bonde la Hagati na Nyasa. Nafahamu kuna *projects* ndogo ndogo za wahisani wadogo mnaowajua, tusaidieni.

Mheshimiwa Spika, mimi naona ni mwelekeo mzuri, Rukwa nimetembelea na kujionea mwenyewe, Kigoma hali kadhalika, mpo sawa endeleeni.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongeze juu ya Daraja la Luhekei, nadhani utaalamu wetu katika Daraja hili umeshindikana. Mara ya mwisho, nimeshuhudia watu wenu wakilinda daraja hilo, kwa madai kuwa haliwezi kupitisha mzigo mzito ikiwemo abiria, wakati ni hivi karibuni tu lilifanyiwa matengenezo. Je, kwa nini tusijaribu kupata utaalam au kujifunza kutoka kwa Askari wa JWTZ na wangelipwa wao hizo pesa? Kwa kweli kujenga daraja na kubomoa mara kwa mara ni kuharibu pesa.

Tank la mafuta ambalo lilikusudiwa kujengwa katika Kiwanja cha Ndege Songea kwa ajili ya kuwezesha kujaza mafuta ya ndege limefikia wapi? Jamani tunaumia viuno, umbali wa Songea ni km. 1078 toka Dar es Salaam; hivi mtatusaidia lini? Vile vile Songea imepanda hadhi na inatarajiwa kuingia katika Makumbusho ya Taifa. Hao watalii wetu si watapata kisingizio cha umbali?

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kutoa pongezi za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, CEO wa TANROADS, Wahandisi, pamoja na Watendaji wote, wakiwemo Mameneja wa Mikoa wa TANROADS, kwa maandalizi mazuri ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa barabara zinazojengwa na Serikali, kwa kutumia fedha zetu za ndani, zinazidi kuongezeka. Jambo hilo nalipongeza sana, kwa kutegemea wafadhili tutaendelea kubaki au kuendelea na barabara mbovu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina mtandao mkubwa sana wa barabara na nyingi ni mbovu. Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali, kuna haja ya kuongeza bajeti ya ujenzi wa barabara zetu ili kupunguza manung'uniko kwa wananchi. Hata hivyo, kutokana na uchumi wa nchi yetu, Serikali iangalie barabara ambazo zitafungua nchi yetu na zile za jirani na zile zinazounganisha mikoa.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali, kwa tukio la juzi la kusaini miradi ya kujenga barabara 10, zikiwemo zile ambazo zitajengwa maeneo ambayo yamefungika tangu nchi yetu ipate uhuru.

Mheshimiwa Spika, aidha, niipongeze Serikali kwa Miradi ya Ujenzi wa Babaraba za Kigoma – Manyovu na ile ya Kigoma - Kidahwe, ambazo utendaji wake unafanywa vizuri. Kukamilika kwa barabara hizo, kutawaongezea kipato Wananchi wa Kigoma (Mkoa), ambao kwa miaka mingi, hawakuwa na fursa ya barabara nzuri. Pia naipongeza Serikali, kwa hatua zake inazochukua, kuona kuwa nchi yetu inafunguka kwa kuunganisha barabara kwa mikoa ambayo haifikiki kwa urahisi kama Mkoa wa Tabora, Kigoma na kadhalika. Kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya Nzega – Tabora (115km), kutawapa ahueni Wananchi wa Mkoa wa Tabora hususan Mji wa Tabora, kusafirisha mazao yao kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Urambo – Kigoma na ile ya Iringa - Dodoma – Babati hadi Arusha, kama zitajengwa kwa kiwango cha lami, kwa asilimia kubwa nchi yetu itakuwa imefunguka. Naiomba sana Serikali, vipaumbele viwe kwenye barabara hizi mbili muhimu sana kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, niipongese sana Serikali, kwa juhudi inazoendelea kuzichukua ili kuona kuwa, reli zetu zinafanya kazi iliyokusudiwa. Sambamba na juhudi inazozofanya Serikali za kutenga fedha zetu za ndani kwa ajili ya ujenzi wa barabara, ifike wakati wa kutenga fedha hizo za ndani, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya reli. Tukiendelea kutegemea wafadhili, reli zetu zitaendelea kuwa magofu na hatutaweza kuondoa tatizo la mrundikano wa mizigo ulioko Bandarini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kwani gharama ya ujenzi wa reli kwa kila kilometa ukilinganishwa na ujenzi wa barabara ukoje? Reli ina faida kuu tatu; inabeba mzigo mkubwa; inahimili vishindo kwa miaka mingi (life span), miaka mingi kuharibika; na matengenezo yake ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, ijikite pia kwenye ujenzi wa reli mpya, zinazounganisha nchi za jirani ili kukuza uchumi wetu. Aidha, naiomba Serikali iwatazame kwa jicho la huruma, Wafanyakazi wa TAZARA kuhusu maslahi yao, ambayo ni ya muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mamlaka ya Hali ya Hewa, kilichoko Kigoma, Serikali ikiangalie kwani kuiachia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kukiendesha haitaweza. Chuo hicho muhimu nchini, vyeti vyake kwa wahitimu havitambuliki na NECTA. Aidha, kozi zinazoendeshwa hapo, baadhi zimehamishwa Dar es Salaam. Ni vyema Serikali ikakifanya Chuo hicho kuwa Chuo pekee nchini, kinachotoa mafunzo hayo. Ni vyema Chuo hicho kiboreshwe ili kifanane na umuhimu wa taaluma ya utabiri wa hali ya hewa, kama ilivyo kwa vyuo kama hivyo duniani.

Mheshimiwa Spika, Chuo hicho pia kipewe hadhi ya kutoa stahada ya utabiri wa hali ya hewa baada ya kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege, inajitahidi kufanya kazi kwa kadiri ya uwezo wake na kadiri ya fedha wanazotengewa, kwa ajili ya kuviimarisha viwanja vyetu vya ndege.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini, watendaji wetu sio kikwazo kwa viwanja hivyo, vikwazo ni upatikanaji wa fedha. Naishauri sana Serikali, iiongezee mamlaka hii ili wataalam wetu waweze kuonesha ufanisi wao. Tusipochukua mipango thabiti ya namna ya kuongeza bajeti katika miradi ya viwanja vya ndege, tutaendelea kuwalaumu watendaji wetu bure. Cha msingi ni fedha, kwani fedha ndio suluhisho la mambo yote hasa haya ya Miradi ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ATCL iko ICU. Naishauri Serikali, iangalie uwezekano unaofaa ama kulivunja au kutenga fedha zinazostahiki. Kwa bajeti iliyotengwa, sidhani kama kweli ATCL itaweza kufikia malengo yake iliyojipangia katika mwaka huu wa

fedha. Serikali ifanye uamuzi wake, wala isione vibaya kulivunja shirika hili na kuanza upya, kutafuta namna ya kuanzisha shirika jipya la ndege la Taifa, kwa vile uhakika wa kupata wafadhili una mashaka, kwa maoni yangu.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

MHE. DR. BINLITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali, Wizara ya Miundombinu, Waziri na Watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi ya hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Makete, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Miundombinu, Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na TANROAD Mkoa wa Iringa, kwa kusikia kilio cha Wana-Makete na kuanza ujenzi wa barabara kama ifuatavyo:-

(a) Barabara ya lami km 5 kati ya Tandala na Mang'oto kwenye maeneo sugu Barabara ya Njombe – Makete.

(b) Ujenzi wa kiwango cha kokoto km 30 Barabara ya Njombe – Makete.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa *Labour-Based Construction Programmes* kutotumika kwa ujenzi wa Barabara za Vijijini (*Rural Roads*). Teknolojia ya nguvu kazi, yaani *labour-based technology*, ina faida nyingi inapotumika katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na miundombinu ya maji, yaani *irrigation*. Faida hizi ni pamoja na kupunguza ajira; kupunguza utegemezi wa fedha za kigeni; kupunguza utegemezi wa mitambo ya nje; kujenga uwezo wa kandarasi ya Kitanzania; na kupunguza umaskini kwa kuongeza *in house income* na kuongeza uzalishaji katika kilimo, kutokana na ubora wa barabara. Kwa nini Serikali haijaonesha *commitment* kuhusu matumizi ya teknolojia hii?

Mheshimiwa Spika, maelezo kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma. Serikali itoe maelezo kwa nini na lini ujenzi wa barabara utakuwa tayari? Barabara hii ni kiungo kizuri cha uchumi kati ya Mikoa ya Kusini na Kaskazini na Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Barabara za Kikondo – Ipelele – Makate na Kikondo – Kitulo – Ndulamo, hazijawahi kupitika majira yote ya mwaka, kutokana na matengenezo kutokidhi ubora unaotakiwa. Maeneo ambapo barabara hizi zipo, mvua zinaanza kunyesha mwezi wa Oktoba, hivyo upo umuhimu wa kuanza matengenezo mapema.

Barabara hizi hazijatengenezwa mfululizo kwa miaka miwili sasa, kutokana na mvua kuanza mapema. Hivyo, tunaomba mwaka huu zipewe kipaumbele cha kuanza ujenzi mapema, yaani sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji na Viongozi wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, napenda kupongeza juhudi za makusudi, zinazofanywa na Wizara katika kuifungua Kanda ya Magharibi, kwa Mkoa ya Tabora, Kigoma na Rukwa. Naipongeza pia TANROADS, hususan Mtendaji Mkuu na Meneja wa TANROAD wa Kanda ya Magharibi.

Aidha, niipongeze pia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwa kusikia kilio chetu cha muda mrefu, kuhusu kuwepo na uwanja wa ndege wa ukakika katika Mkoa wa Rukwa na kutenga fedha katika bajeti hii kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Mpanda. Nawashukuru sana, kwa niaba ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na hususan Wakazi wa Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, yapo pia matatizo katika eneo la usafiri wa majini katika Maziwa ya Tanganyika na Victoria, kwa uchache wa vyombo vya usafiri na uchakavu wa vyombo vyenyewe; hivyo kunasababisha wananchi kutumia usafiri hatarishi wa maboti, pengine yakiwa yamepakia mizigo na kuhatarisha maisha yao. Pamoja na jitihada za SUMATRA kudhibiti hali hiyo, lakini usafiri huu si salama na wa kujivunia katika karne hii ya 21 na miaka karibu 50 tangu tupate uhuru. Aidha, lipo tatizo la mrundikano wa mizigo katika Kanda ya Kusini ya Ziwa Tanganyika, ambapo meli pekee inayofanya kazi ni MV Liemba, ambayo inasafiri aidha mara moja au mbili kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo pia la wakala na eneo katika Bandari ya Kigoma. Tatizo la wakala aliyeko, tayari nimeliwasilisha kwenye Mamlaka ya Bandari. Naamini watalifuatilia kwa makini na kama itathibitika hana uwezo wa kifedha, kiutendaji na nyenzo (vifaa), basi ni busara kusitisha mkataba kuliko kuendelea na wakala huyu ili tija iwe bora zaidi. Kadhalika, naomba Wizara kusaidia Mamlaka ya Bandari ya Kigoma na kurejesha eneo ambalo amepewa mtu binafsi, kuwa eneo la bandari. Nichukue fursa hii pia, kuipongeza TPA, kwa kumaliza tatizo la kujaa kwa mchanga katika bandari za maziwa yetu.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma, kinahitaji kupewa umuhimu unaostahili, kwa kuongezewa uwezo kwa maana ya vifaa vya kufundishia na vitabu, kuboresha maktaba na kukamilisha mradi wa mabweni, ambao ni wa miaka mingi. Serikali kwa wakati wote, imeshindwa kutenga fedha kukamilisha miradi huu, ambao gharama zake zinapanda kila wanapochelewa kutekeleza mradi huu. Kwa mara nyingine tena, napenda sasa nijikite katika eneo moja tu nalo ni reli.

Mheshimiwa Spika, nataka nipate maelezo ya kutosha na kutosheleza, juu ya reli ya Mpanda, maana nimeona fedha iliyotengwa katika bajeti ni Sh. 100 milioni, kwa reli ya Mpanda/Kaliua na Manyoni/Singida; zimekusudia kufanya nini? Naomba maelezo.

Reli ya Mpanda inahitaji matengenezo makubwa, kwa maana ya njia ya reli iko katika hali mbaya sana. Hivi mpaka Watanzania wapoteze maisha ndio tutajua tatizo lipo? Hata hivyo, kuna shehena nyingi ya kuondoshwa Rukwa (mahindi) ya WFP, kupeleka Shinyanga na Dodoma. Inawezekana vipi kuondosha hayo maelfu ya matani katika njia ambayo haina matengenezo kwa muda mrefu? Nini mpango wa Serikali kwa Reli ya Kaliua hadi Mpanda?

Mheshimiwa Spika, si Reli ya Mpanda hata Reli ya Kati ni shilingi bilioni sita tu, zimetengwa kwa ajili ya matengenezo. Sijui kama tuna dhamira ya kweli katika kuboresha usafiri wa reli ukilinganisha na barabara ambazo zimetengewa mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la mabehewa ya mizigo na abiria. Kampuni ya TRL ilipoanza, ilikuwa na mabehewa zaidi ya 1,300, leo imebaki na nusu ya idadi hiyo yanayofanya kazi; kulikoni?

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo katika mawasiliano na karakana, je, dhamira ya kuboresha maeneo haya ipo?

Mheshimiwa Spika, nataka nipate maelezo kwenye maeneo yafuatayo:-

- Kwa nini tunalipa (Kampuni) kwa mabehewa yanayokodishwa toka India lakini mabehewa ya TRC hayalipiwi?

- Kwa nini *engine* zilizokuwa za TRC zile za *89 class* zimesimamishwa; ni kwa ajili ya ku-justify uwepo wa *engine* za India ambazo gharama zake za uendeshaji ni kubwa? Naomba maelezo.

- Mkataba wa hiari ambao ulikuwa usainiwe 22 Juni, 2009 ambao haujasainiwa; nini hatima yake?

- Katika mtandao kuna taarifa za fedha za TRL kupotea/kutoroshwa; tunahitaji kupata maelezo.

Mwisho, nini matokeo ya kupitia Mkataba kati ya RITES na Government?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa mipango mizuri ya maendeleo ya Sekta ya Miundombinu, utekelezaji wa mipango hiyo, umekuwa hauridhishi kabisa. Kwa mfano:-

- Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongolosi; ni sababu ipi iliyomfanya mkandarasi aliyekuwa ameanza kujenga barabara hiyo kujiondoa kwenya kazi hiyo?

- Ahadi ya Serikali ni kuijenga Babara ya Mbalizi – Mkwajuni – Makongolosi kwa kiwango changarawe; mbona hadi sasa kazi hiyo haijaanza; badala yake barabara hiyo inakwatuliwa tu?

- Barabara ya Galula – Magamba – Namkukwe: mchanga unaochukuliwa kutoka mtoni na kuwekwa juu ya barabara, umesababisha kero nyingine zaidi. Waendesha magari hivi sasa wameamua kupasua barabara za vichocho, kwa sababu tuta lililowekwa mchanga halipitiki. Je, kwa nini kifusi cha udongo kisitumike badala ya mchanga toka mtoni?

Zipo barabara kadhaa kwenye Wilaya ya Chunya, ambazo zimewekwa vifusi kwa muda mrefu sasa, vifusi hivyo havijaondolewa wala kutandazwa. Hali hii itaendelea mpaka lini?

Serikali ilikwisha tenga fedha kuweka/kujenga sehemu korofi Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni, kwa kiwango cha lami. Sehemu hizo ni zile zilizoko kwenye Mlima wa Mbala – Jimboni Songwe. Mbona kazi ya uwekaji lami kwenye sehemu hiyo haijaanza pamoja na fedha kuwepo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri wake na wote alioshirikiana nao katika utayarishaji wa bajeti hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Kawambwa, kwa uwasilishaji mzuri wa hoja yake.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kusaini tena Mkataba wa Ujenzi wa Barabara Kuu ya Kagoma – Lusahunga. Nimepata faraja sana, maana Kagoma ndiyo mwisho wa lami toka Mtukula na Kagoma, jimbo kwangu. Sasa tutaunganishwa vizuri na Makao Makuu ya Wilaya ya Muleba na pia mikoa mingine. Hili ni jibu la ahadi yangu.

Naiomba Serikali iwe karibu na hao wakandarasi.

Naiomba Serikali ijitahidi isije kusimamisha tena mradi huu kama ilivyofanya hapo awali. Tunateseka sana kwa kukosa barabara hii. Naamini na nchi imepata hasara hata kama si kwa moja kwa moja.

Likitokea tatizo, tunashauri kwamba, Wabunge wa Mkoa wa Kagera nao washirikishwe katika kutoa maoni yao, badala ya Mkuu wa Mkoa na Mhandisi wa Mkoa, kuwa na kauli ya mwisho. Ikibidi na kwa kufaa zaidi, kwa faida ya nchi na wananchi, hoja kama hizi zipitishwe na *Road Board Commitee* na RCC pia.

Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwatambua na kuwaajiri wafanyakazi wa muda katika mradi mkubwa kama huu ili likitokea tatizo lolote, kama la kuwaachisha kazi, wapate haki zao. Hivi sasa kuna malalamiko mengi, kwa wale waliokuwa vibarua wa mradi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kuipandisha hadhi Barabara ya Rutenge – Rubale – Izimbya – Omubeweya – Buhamila - Kishoju. Barabara hii itatuunganisha vizuri na Wilaya ya Karagwe na itatuinua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ituepushe na kero ya Uwanja wa Ndege wa Bukoba. Tuliamani kwamba, shilingi 2.5 bilioni, zingewezesha mradi huu kukamilika na uwanja kuwa katika kiwango cha lami. Tunaiomba Serikali, itueleze fedha hizi zitaufikisha katika kiwango gani?

Mheshimiwa Spika, tueleze pia lini uwanja huu utakamilika? Hivi sasa ndege ndogo sana na mara nyingi zenye injini moja, zinazokwenda Bukoba – Mwanza – Bukoba. Je, Serikali haioni kuwa hii ni hatari Kubwa?

Mheshimiwa Spika, kero ya meli yenye kuaminika kutokuwepo, limeendelea kuwa tatizo. Serikali iondoe kero hii. Naishauri Serikali ithubutu, naamini inaweza kununua meli mpya, ikiamua.

Upo ushuru wa meli zinazozagaa katika bandari zetu. Sisi tunatumia mitumbwi (*engine boats*), eti nazo zinatozwa ushuru na SUMATRA. Naomba ushuru huu usitishwe na Serikali mara moja, hasa kwa mitumbwi yote inayotoa huduma katika Ziwa Victoria, bila kwenda nchi jirani. Ushuru huu ni kero.

Mheshimiwa Spika, mwendo wa kasi kwa mabasi yatokayo Bukoba – Dar es Salaam, Mwanza – Dar es Salaam na kadhalika, udhibitiwe kwa kuwapa ratiba inayozingatia usalama wa barabarani, kwa lengo la kupunguza ajali na magonjwa ya presha kwa abiria. Magari haya ya abiria, yana mwendo mkali sana na unatisha sana. Kero nyingine ni kutokuwa na usafiri mzuri wa treni toka Dar es Salaam kwenda mikoani. Sisi wa Kanda ya Ziwa na majirani zetu, tunautegemea sana.

Mheshimiwa Spika, inapotokea matengenezo/ukarabati/ujenzi wa Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Rugente, ambayo hutumika ni ile ya Ruhanga – Makongora – Nyakahama, ambayo ni ya Wilaya. Kwa kuwa viwango vya Barabara ya Ruhanga – Makongora – Nyakahama ni vya Wilaya, yakiwemo hasa madaraja yake, naiomba Serikali iyaimarishe madaraja hayo na barabara hiyo ili vifikie Kiwango cha Barabara ya Mkoa.

Naomba hivyo kwa kuzingatia kwamba, matengenezo ya Barabara ya Muhuntwe – Kamachumu – Rutenge, bado yanaendelea na kila itumikapo ya Ruhenge – Makongora – Nyakeheme, madaraja yake huvunjika. Pia uharibifu wake unakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ihimize vikundi vya ujenzi wa barabara/ukandarasi vya wanawake.

Mheshimiwa Spika, naamini Wanawake wa Tanzania, wanaweza kutoa mchango mzuri sana katika ujenzi wa barabara na majengo. Naiomba Serikali, iweke utaratibu wa kuvihamasisha, kuvisajili na kuvisaidia vikundi vya wanawake nchini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), ifanye kazi hii na itupe taarifa mwaka kesho. Nimeangalia jumla ya makandarasi 656 waliosajiliwa mwaka 2008/09, sikuona mchanganuo wa wanawake ni wangapi?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nawatakia heri. Nawasilisha.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutoka Sengerema hadi Ngoma (Wilaya ya Sengerema), inahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya hiyo.

RCC pamoja na vikao vingine, wameshaleta maombi kwako ya kupandisha hadhi barabara hiyo, ihudumiwe na TANROADS. Tunaomba barabara hii ipandishwe hadhi.

Inaonekana Mkoa wa Shinyanga umepata (umepandishiwa) barabara sita wakati Mkoa wa Mwanza ni barabara moja tu. Huu uwiano ukoje?

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kupata fursa hii, ili niweze kutoa yangu niliyonayo moyoni. Ninashukuru sana hotuba hii ni nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kutoka Stesheni Dar es Salaam mpaka Kigoma, sasa hivi hakuna *buffet car*. Kwa hiyo, wasafiri huchukua chakula chao kwenye ndoo za *plastic*, lakini wasafiri wanapofika Stesheni ya Dar es Salaam, huambiwa watoe vyakula vyao kwenye ndoo wakapime ndoo hizo.

Mheshimiwa Spika, wasafiri wale wanapata adha kubwa sana, kutoa vyakula vyao kwenye ndoo hizo na kuviweka chini na mara nyingine, vyakula hivyo vinamwangika chini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa msafiri anayesafiri kwa first class ana kilo zake, second class ana kilo zake na third class kilo zao zinajulikana; kwa nini wawe wanawanyanya kwa kubeba ndoo za plastic zilizowekwa chakula na kuwekwa chini? Ninaiomba Serikali, iweze kuliona hilo kwa macho makali kabisa ili tabia hiyo iweze kuachwa. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara ya Miundombinu, kwa kuandaa Mpango wa Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara iandae Mpango Mkakati wa Miundombinu na Mpango utazingatia Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, ATCL na barabara zote muhimu nchini. Mpango huu, ufuatwe na bajeti izingatie njia hizo ili kuweka taifa letu kwenye maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara iandae Mpango na Bajeti kwa kujenga barabara ya Minjingu – Kondo – Dodoma hadi Iringa.

Corridor ya Magharibi ifunguliwe na njia zijengwe kutoka Manyoni – Singida – Tabora na Kigoma.

Shirika la Ndege ATCL liwezeshe na kusukumwa ili lifufuke, lifanye kazi na kuwa sura ya nchi.

Serikali itengue Mkataba na TICTS na Bandari iendeshwe kibiashara na kampuni yenye uwezo na itakayoendesha Bandari ya Dar es Salaam.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba Waziri atambue umuhimu wa Barabara ya Kigoma – Kasulu Kibondo – Nyakanazi, inayofahamika kama Kigoma – Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo Barabara Kuu, yenye maslahi makubwa ya Watu wa Kigoma na Wilaya zake zote. Hivyo, sioni sababu ya kuunganishwa na barabara itokayo Sumbawanga; imekuwa *complicated* zaidi bora ingeachwa isimame peke yake kama awali. Yapaswa itengewe pesa yake yake, kama ilivyokuwa ikionekana kwenye Mipango ya Serikali zamani. Barabara hii imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, inasuburi kujengwa tu, hivyo kuiweka kwenye kundi la Barabara ya Sumbawanga, kutaifanya Barabara hiyo ichelewe kujengwa.

Nashauri Serikali iirudishe ilivyokuwa, yaani isimame peke yake kama zamani; itakuwa fupi na pesa zikitafutwa hazitakuwa nyingi, pia itasaidia hata wafadhili kuiona ni fupi na kutoa pesa kirahisi. Vile vile, hata Serikali yaweza kutumia pesa za ndani, kwani Barabara hiyo ni fupi. Eneo litakalobaki bila lami ni kuanzia Kidahwe mpaka Nyakanazi, sawa na km 136 tu. Naamini pesa za ndani zipo ila tupunguze matumizi ya kawaida, vifungu vya *allowances in kind* na vile vya takrima na vingine vingi ambavyo si vipaumbele vya Mtanzania.

Shirika la ndege Tanzania ni muhimu sana hivyo, kuna haja ya Serikali kuhakikisha linafanya kazi na kuharakisha utekelezaji wa kulifufua. Shirika hili litachochea ukuaji wa uchumi, kama litafanyakazi vizuri.

Naamini *management* ikibadilishwa, Serikali ikaendelea kuwekeza kimtaji kwenye shirika hilo, tutafanikiwa kwani nchi hii imeshaingia ubia na makampuni mengi,

ikiwemo South African Airways, lakini hatukufanikiwa, matokeo yake tumepata hasara. Tuepuke mambo ya ubia ili yasitokee yaliyokwishatokea. Serikali imesema ina mpango wa kuingia ubia na Kampuni ya China. Umakini uwe mkubwa, kama haja ya kuingia ubia ipo, ikiwa Serikali haitaona uwezekano wa kuiongezea mtaji ATCL.

Jambo ambalo naona yawezekana, kwani Serikali haikosi fedha ya kulifufua. Ukiangalia Bajeti ya Serikali, matumizi ya kawaida ni makubwa kuliko ya maendeleo; kuna haja ya kupunguza matumizi ya kawaida. Kwa mfano, vifungu vya *allowances*, *fuel*, gharama za Wakuu wengi wa Idara; wengine huja Dodoma wakati wa bajeti bila kuwa na *role* maalum wapungue, wanaokuja wawe walio na kazi za kufanya ili kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, nilitembelea Barabara Marangu hadi Tarakea June, 2009. Tulielezwa kuhusu kuvunjwa kwa mkataba wa awali na mkandarasi na kuzuia mitambo yake. Mheshimiwa Waziri, atueleze ni hasara kiasi gani itatokana na uamuzi huo hasa ukitilia maanani kwamba mkandarasi amepeleka kesi mahakamani; na uamuzi wa kumfungia ulitokana na sababu zipi? Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Bunge kama wataalam akiwemo Mwanasheria Mkuu, waliombwa ushauri kabla ya kuchukua uamuzi huo?

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kununua magari yake kupitia Wizara ya Miundombinu, unaonesha gharama zinazidi kuongezeka siku hadi siku, hasa ukiangalia Ripoti ya CAG ya 2007/2008, ambapo zaidi ya shilingi bilioni tatu zingeweza kuokolewa, kama utaratibu huu ungesimamishwa, ingawa lengo lililikuwa zuri la kupunguza gharama; kwani ilitegemewa Wizara ingekuwa inatoa oda kiwandani moja kwa moja ili bei ipungue.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje juu ya hili? Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kutoa tamko kuhusu manunuzi ya magari ya Serikali?

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo mizani za kupima uzito wa magari, lakini bado barabara zetu zinaendelea kuharibika vibaya, kutokana na uzito mkubwa. Sote tunapita maeneo yenye mizani, tunashuhudia magari yanapimwa, lakini barabara zinaendelea kuharibika.

Je, Mheshimiwa Waziri ana lipi la kueleza ukizingatia kwamba lengo la mizani sio kukusanya maduhuli bali kulinda barabara? Wizara ina pendekezo gani kwa Idara husika na mizani hiyo na kama tatizo ni udhaifu wa mizani au barabara zenyewe ni *below standard*?

Mheshimiwa Spika, naomba nipate ufafanuzi; kumekuwa na tabia ya kuwafutia mikataba Wakandarasi, kutokana na utendaji mbovu na ucheleweshaji wa malipo kwa mwaka unaoishia Juni, 2008; je, Serikali inaweza kulieleza Bunge ni hasara kiasi gani imepatikana kwa uvunjaji wa mikataba hiyo? Kwa nini Serikali inaingia mikataba mibovu inayopelekea kuivunja baadaye? Vile vile pale inapothibitika kwamba Serikali

imepata hasara ambayo ingeweza kuzuilika; ni hatua gani zimewahi chukuliwa dhidi ya wahusika?

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Watendaji Wakuu wa Idara mbalimbali na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa maandalizi mazuri, yaliyowezesha hotuba hii kuwasilishwa Bungeni. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha machache niliyonayo, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Mheshimiwa Lolesia Bukwimba (Mb), kwa ushindi mkubwa alioupata hivi majuzi katika Uchaguzi wa Jimbo la Busanda.

Aidha, napenda nitoe rambirambi zangu kwa Mufti Sheikh Mkuu Issa bin Simba na Waislam wote nchini, kwa kufiwa na mpendwa wao, Sheikh Suleiman Gorogosi, ambaye pia alikuwa Kaimu Mufti wa Tanzania. Pia ninatoa pole kwa familia, ndugu na marafiki wa Marehemu Prof. Haroub Othman, kutokana na msiba huo mzito. Tunawaomba Mwenyezi Mungu, aziweke mahali pema peponi roho za Marehemu wote wawili. Amen.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Miundombinu kwa kutekeleza kwa makini Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara kwa kuyakubali mapendezo ya Mkoa wa Shinyanga ili barabara zifuatazo ziwe na hadhi ya Barabara Kuu; Migumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi; na Kolandoto – Lalago – Mwanhuzi – Sibiti – Matala – *Oldeani Junction*. Pamoja na barabara zifuatazo kuwa na hadhi ya barabara ya Mkoa; Bariadi – Kasoli – Salawa (Magu Border); Bariadi – Budalabujiga – Gambasingu; na Luguru – Kadoto – Malya.

Aidha, naipongeza Serikali kwa kuanza kujenga kwa kiwango cha lami, Barabara ya Migumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi, kwa kuanza katika awamu ya kwanza na ujenzi wa sehemu ya Bariadi – Lamadi (kilometa 71). Ingawa kiwango cha fedha kilichotengwa na Serikali cha Sh. 1.1 katika mwaka wa fedha 2009/10, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ni kidogo, nimetiwa moyo na ahadi ya Waziri wa Miundombinu kuwa, Serikali itatafuta fedha za nyongeza, kiasi cha shilingi bilioni saba, zilizotengwa mwaka wa fedha 2008/09. Hata hivyo, suala la msingi ni kwamba, tunaanza ujenzi wa barabara hiyo.

Naipongeza Serikali kwa kukamilisha maandalizi ya rasimu ya Sera ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public – Private Partnership Policy*) katika ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege, kwa kutumia mfumo wa Jenga, Endesha na Kabidhi (BOT). Naiomba Wizara ya Miundombinu, iharakishe (*fast track*), ukamilishaji wa Sera hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wa nchi mbalimbali hata katika Bara letu la Afrika, unaonesha kuwa, Sekta Binafsi ikishirikishwa ipasavyo na kwa uwazi katika kuendeleza miundombinu na kutoa huduma muhimu, kuelemeza na mzigo katika Bajeti ya Serikali kutapungua na hivyo kuiwezesha Serikali kugharimia majukumu mengine ya maendeleo. Viongozi na Watendaji Wakuu Serikalini na Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea, lazima wabadilike haraka, waondoe woga na hisia mbaya kwa Sekta Binafsi. Lazima wajenge mahusiano mazuri na Sekta Binafsi. Fursa ni nyingi mno, tusipozishabikia, zitachukuliwa na wengine. Haipendezi mwaka ujao wa fedha, kuja na lugha ya kwamba tuko mbioni. Mheshimiwa Waziri na Timu yake, wakaze buti tusonge mbele.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia fedha nyingi za ndani na za nje, kujenga barabara kwa kiwango cha lami na mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wa Bajeti ya Serikali. Ni ukweli usiopingika kwamba, baadhi ya makandarasi wanaopewa kazi, hawakustahili kupata kazi hizo *in the first place. They bid cheap to get the contract and subsequently they become expensive through price variations ect.* Tuanze kuwa-*black list* na Makandarasi wa aina hiyo ili wasipate kazi. Kamati ya Manunuzi ya Umma ni sehemu ya tatizo, basi Wizara, TANROADS, CRB na wadau wengine, semeni msikike, maana kilio kina wenyewe. Sheria zipo ili kutumikia jamii na siyo jamii kutumikia sheria. *The least evaluated bid/tender* siyo sawa na *the lowest evaluated price.*

Tuangalie pia kazi inayofanywa na *Consultants* wakati wanafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Pamoja kuwa makadirio ya ujenzi wa mradi ni makadirio tu, hata hivyo, inatia shaka pale ambapo zabuni zinapofunguliwa, gharama za ujenzi zinakuwa juu kuliko zile za *Consultant.*

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na malalamiko mengi ya wakandarasi kutokulipwa kwa wakati, pale ambapo wanazalisha na kazi hiyo kuhakikiwa. Hali hii siyo tu inaongeza gharama za mradi, lakini pia inavuruga *cashflows* za wakandarasi husika.

Kwa kuwa fedha za ujenzi wa barabara kupitia Bajeti ya Serikali haziji kwa mkupuo, kwa nini TANROADS, MI na Hazina, wasikae kitako na kuweka mkakati utakaoiwezesha TANROADS kuongea na Mabenki ya ndani na kupata *facility* ya masharti nafuu itakayodhaminiwa na Hazina ili kuwezesha *certificates* zilizoiva kulipwa *as and when they fall due? Release* ya fedha inapopatikana, fedha hiyo itumike kulipa deni la benki.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza ukarabati wa ukarabati wa *TANZAM high way* na *Terminal I*, ambayo ilikuwa imekwama kwa muda mrefu. Hata hivyo, naiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha, iheshimu makubaliano ya kusamehe kodi mbalimbali, chini ya mikataba husika ili kumaliza mvutano uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Wakurugenzi wote na Mameneja wa TANROADS.

Napenda nitoe shukrani nyingi kwa Wizara, kwa kuipandisha hadhi Barabara ya Vikumburu – Mloka – Ikwiriri kuwa ya Mkoa. Barabara hii ni muhimu sana, kwa sababu kwa kauli ya Rais JK, alisema itafungua utalii kwa watu wa Kusini Mashariki ya Tanzania na hasa Wananchi kutoka Mozambique.

Nashukuru sana kwa kupata *allocation* ya fedha ya Barabara ya Kibiti – Utete – Nyamwage.

Naomba kuongeza shukrani zetu, kwa kuhakikishiwa tena kuwa, Kivuko cha Utete kitapatikana.

Katika Barabara ya Vikumburu – Mloka – Ikwiriri, sijaona tengeo la fedha katika bajeti hii. Barabara hii sasa ina tatizo kubwa kati ya Ikwiriri na Mkongo, kuna Daraja la Mbambe halifutiki, kwani limechakaa sana. Ni hatari kupitisha gari katika daraja lile.

Tafadhali, naomba kwa dharura, TANROADS Pwani wapeleke haraka mbao na misumari, wakafanye *emergency repairs* haraka. Nimetoka hapo juzi tu.

Altenate Trunk Road ya Daraja la Mkapa Rufiji: Kwa vile barabara ya kwenda Lindi toka Dar es Salaam ilipitia Utete (bomani) na sasa inapita juu ya Daraja la Mkapa, kwa bahati mbaya vita au balaa lolote liwalo lile ikawa daraja hilo limeathirika na halipitiki; *altenative passage to Lindi*, itakuwa kutumia barabara ya Kibiti – Utete – Nyamwage – Lindi.

Kwa hiyo, tunaomba Barabara ya Mkoa; Kibiti – utete – Nyamwage, ipandishwe hadhi na kuwa *Trunk Road Alternative to Mkapa Bridge Way*. Serikali imeshatuhakikishia upatikanaji wa Kivuko kipya cha Utete. Sasa tunaomba Barabara ya Kibiti – Utete – Nyamwage ijengewe kwa kiwango cha lami ili kuiimarisha.

Katika kufanya ukarabati wa barabara zetu za udongo/changarawe, mara nyingi huanza miezi inayokaribia majira ya mvua. Mara kwa mara barabara zinazokarabatiwa huoshwa na maji na tunapata hasara kubwa. Tunaomba kuwe na mipango, itakayowafanya wakandarasi wetu kuanza kazi za ukarabati wa barabara zetu, mara baada ya masika (majira ya mvua), badala ya kufanya kazi mwanzo wa masika.

Nashauri kuweka kitengo cha kuhakiki kila barabara inayojengwa kwa fedha ya Serikali (*value for money contracts*) za kujenga barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. RAJABU HAMAD JUMA: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii, kwa hotuba yake aliyoitoea leo hii ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka huu wa 2009/10.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu, unaanzia katika Nyumba za Kisasa, ambazo inaonesha hakuna hatua za kuziendeleza katika ule upungufu uliopo. Nyumba nzuri zina upungufu; barabara ni za vumbi, ukosefu wa taa za barabarani na upungufu wa vifaa vya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili, unahusu Bandari zetu za Tanga na Mtwara. Bandari hizo zimekosa kazi na kusababisha ongezeko kubwa la msongamano na mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.

Naiomba Serikali, ione kuwa ipo haja ya kuzifufua Bandari zetu hizo za Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeze Serikali kwa kununua Kivuko cha Kigamboni. Kivuko hicho ni ukombozi wa wananchi wengi wa Tanzania.

MHE. BUJIKU K.P. SAKILA: Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia fursa hii, ili nichangie katika hotuba kama ifuatavyo:-

Kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Nawapongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji na Watumishi wote wa Wizara hii, walioshiriki katika uandaaji wa hotuba nzuri, ambayo kwa kiwango cha kutosha iko wazi. Pamoja na uandaaji na usomaji mzuri wa hotuba hii, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa upole, usikivu na unyenyekevu, kwa watu mbalimbali. Ni matarajio yangu kuwa, hali hizo wanazionesha pia kwa matumishi wote walio chini yao, ndani ya Wizara; kama ndivyo ilivyo, ninawapongeza sana. Hali hii itadumisha mshikamano na ufanisi wa kazi ndani ya Wizara; hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuitumia fursa hii pia kumpongeza Mhandisi Kadashi – Meneja wa TANROAD Mkoa wa Mwanza, kwa usikivu wake na mipango yake mizuri, yenye kuleta tija kwa Mkoa wa Mwanza. Tangu afike Mkoa wa Mwanza, hali ya barabara Mkoani Mwanza, pamoja na usafiri majini, vimeendelea kuwa bora. Nampongeza sana. Mwenyezi Mungu, aendelee kumwongoza.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, napenda kuitumia fursa hii, kutoa shukrani kwa masuala kadhaa, yaliyotendeka hapa nchini na jimboni kwangu. Hii ni kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu.

Napenda kuishukuru Serikali, kutokana na kazi nzuri zinazofanywa na Wizara hii, kupitia TANROADS (Mwanza) na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba katika Jimbo

langu la uchaguzi. Eneo linalohusika hapa hasa ni katika ujenzi wa barabara, baadhi ya barabara ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kupitia PMMR ambazo ni Mabuki - Malampaka; Jojiro – Ngudu – Magu.
- (b) TANROAD (M) ambazo ni Mwamhaya – Itongoitale; Hungumalwa – Nyamilanya – Ngudu.
- (c) Halmashauri za Wilaya ambazo ni nyingi sana ikiwemo ya Ilula – Milyungu.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa Barabara za Hungumalwa – Ngudu na Ilula – Milyungu, ambazo bado zinajengwa, barabara nyingi jimboni mwangu zinapitika vizuri. Naipongeza sana Serikali kupitia ni Wizara hii kwa hali hiyo.

Shukrani nyingine kwa Serikali zinatokana na Wizara kukubali kupandisha daraja Barabara ya Hungumalwa – Nyamilama – Ngudu, iliyokuwa ya Halmashauri na kuifanya kuwa ya Mkoa. Nashukuru sana, kibali hicho kimezifanya barabara kutoka Magu hadi Hungumalwa sasa zihudumiwe na chombo kimoja, yaani Serikali Kuu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Mwanza, tofauti na awali lilipokuwa likihudumiwa na Halmashauri ya Kwimba kwa Hungumalwa, Ngudu na Wakala kwa upande wa Ngudu – Magu. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongeze na shukrani zilizotangulia, ninayo maombi na ushauri kama ifuatavyo:-

Barabara kutoka Hungumalwa – Nyamilama – Ngudu hadi Magu kujengwa kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Spika, barabara hii ambayo sehemu ya Hungumalwa–Ngudu, iliyokuwa ikisimamiwa na Halmashauri ya Kwimba, imepandishwa daraja kuwa ya Mkoa, inafanya barabara yote niliyoitajwa yenye urefu wa takriban km 67 hivi, inakuwa chini ya Mkoa. Barabara hii inazo sifa zifuatazo: Inaunganisha Makao Makuu ya Wilaya mbili; Kwimba (Ngudu) na Magu; inaunga barabara kuu mbili (Musoma – Mwanza na Shinyanga – Mwanza); inaufungua Mji wa Ngudu – Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba na kuwezesha Wananchi wa Ngudu kufikia Miji ya Mwanza, Shinyanga na Magu kwa urahisi; na inatumiwa na magari mengi makubwa, yenye uzito mkubwa nyakati zote.

Faida zifuatazo zitapatikana kutokana na ujenzi huo:-

- Ni njia fupi kwa magari mengi makubwa na madogo yatokayo na kwenda Shinyanga hadi Musoma. Barabara hii inapunguza umbali wa kilomita takriban 40 kwa atakayezungukia Mjini Mwanza. Hivyo, barabara hii itapunguza sana msongamano wa magari Jijini Mwanza.
- Itaufungua Mji wa Ngudu.

- Kwa kuwa itakuwa ikitumiwa na magari makubwa na mengi ambayo yatakuwa mazito, kuiweka lami itaipunguzia Serikali gharama za mara kwa mara, kukarabati barabara hii, kutokana na uharibifu unaosababishwa na magari hayo hasa nyakati za mvua.

Mheshimiwa Spika, ninamsihi sana Mheshimiwa Waziri na Washauri wake Wakuu, wazingatie kwa makini zaidi ushauri huu, kwa kuangalia mantiki ya ombi hili mahususi la kuufungua kimaendeleo, Mji wa Ngudu, ambao kwa muda mrefu, umejifunga kwa kulazimishwa na mazingira yanayouzunguka mji huo. Ninashauri ikiwezekana, ushauri na maoni ya Uongozi wa Mkoa wa Mwanza, akiwemo Mkuu wa Mkoa na Meneja wa TANROAD Mwanza, pamoja na wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, wakashirikishwa kwa karibu zaidi, kuweza kufikia muafaka wa nafasi ya ombi hili katika vipaumbele vya maeneo hayo. Ni vyema hili likafikiriwa hata kama ni kuanza kwa kuijenga kwa kiwango cha lami nyepesi.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimekuwa nikiangalia Jiji la Mwanza, kasi yake ya ukubwa na umuhimu wake, kwa maeneo ya Kanda ya Ziwa. Kila nikiangalia Uwanja wa Ndege, ninahitaji sana kushauriwa ujenzi wa Uwanja katika eneo wazi na jipya, badala ya kuendelea kujibana katika eneo ambalo katika siku zijazo ni dhahiri haitakuwa rahisi hata kuuongeza. Haiwezekani ukaendelea kuupanua uwanja huo kuelekea Ziwani au kwenye eneo la jeshi au kwenye maeneo ya makazi yanayozidi kuusonga uwanja huo.

Aidha, haitakuwa rahisi kuendelea kulipa fidia kwa wakazi kutokana na ukubwa wa gharama za fidia. Kila nilipokuwa nikishauri, nimekuwa nikipendekeza uwanja ujengwe katika eneo la Ranchi ya Babuki; hilo ni eneo kubwa, bado linaweza kumegwa kwa fidia kidogo. Kama haiwezekani, Serikali itafute eneo muafaka mapema tena kwa gharama nafuu.

Ninaipongeze Serikali, kwa kujenga na kuwauzia watumishi nyumba. Ni jambo jema sana. Ninaomba Serikali inapowauzia nyumba watumishi, waonunua nyumba hizo wasiruhusiwe kuharibu mazingira na mandhari za miji. Iangalie uharibifu utokeo Oysterbay.

Barabara chini ya PMMRA, kwa mwaka huu zimetengewa kiasi gani? Je, Barabara za Mabuki - Malampaka na kutoka Jojiro kupitia Ngudu hadi Magu, kwa pamoja zimetengewa kiasi gani cha fedha?

Barabara za Mwamhaya – Itonguitale na Hungumalwa – Ngude, zinahitaji madaraja mapya ili kuziwezesha zipitike kwa mwaka mzima. Madaraja yanayohitajika ni ya Mto Buyogo (Mwamhaya Itonguitale) na Mto Ndagwasa (Hungumalwa – Ngudu).

Katika maelezo ya awali ya Serikali kupitia Wizara hii ya Miundombinu, yalieleza kuwa yanashughulikiwa. Nilitegemea fedha yake ionekane katika bajeti ya mwaka huu sijazona; kuna nini kwa madaraja haya? Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri anipatie maelezo na hatima ya ujenzi wa madaraja haya na Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuunga mkono hoja.

MHE. USSI AMME PANDU: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri, pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa kuleta bajeti ambayo ni nzuri na yenye kutia matumaini kwa Watanzania. Lakini pia; ni bajeti ambayo inatekeleza kwa kiasi kikubwa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, ukurasa Na.101 wa kitabu hiki, unaelezea ushirikiano mzuri kati ya SMT na SMZ, kwa mambo yanayohusu Wizara hii, hasa pale Mheshimiwa Waziri alipoamua kukutana na Mheshimiwa Machano O. Said, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar.

Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamini W. Mkapa, wakati anafungua Barabara ya Amani - Mtoni kwa awamu ya kwanza huko Zanzibar, aliwaahidi wananchi wa huko kwamba, ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu ya pili ataamaliza yeye kama Rais wa Muungano, kabla hajaondoka madarakani. Matokeo ni kwamba, kaondoka na barabara haikujengwa.

Mheshimiwa Rais Jakaya M. Kikwete, naye alipokuja jimboni kwangu Mtoni, Zanzibar, mwezi wa Januari, 2009, pia alisema barabara hii ambayo aliahidi Mheshimiwa Mkapa, sasa nitaimaliza mimi kama alivyoahidi Rais huyo. Je, Mheshimiwa Waziri kwa ushirikiano mzuri mlionao ni kwa nini barabara hiyo mpaka leo haijajengwa?

Je, Mheshimiwa Waziri huoni kwamba tunawakatisha tamaa wananchi na ahadi za viongozi na kuona kwamba hazina ukweli? Naomba majibu. Ahsante.

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nilishawapongeza viongozi wote wa Wizara. Nina moja nililisahau.

Mheshimiwa Spika, kuna Mawakala wetu; TANROAD – Wakala wa Barabara; TBA – Wakala wa Majengo; na TAMESA – Wakala wa Ufundi.

Mheshimiwa Spika, hizi zote ni watoto wa Wizara moja, bahati mbaya sana kuna tofauti kubwa ya mishahara yao, nitaomba ufafanuzi. Kwa nini kunakuwa na *gap* kubwa kati ya TANROAD, TBA na TEMESA?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anieleze hatima ya Watumishi wa TEMESA, aliyeajiriwa ni Mkurugenzi tu wengine wote wa muda. Naomba ufafanuzi. Kwa kuwa tuna TEMESA; kwa nini Wizara isiwawezeshe Mawakala hawa ili wamudu kutengeneza magari yote ya Serikali badala ya kupeleka magari ya Serikali kwenye *garage* za watu binafsi na Serikali kutumia fedha nyingi?

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi ni lini sasa TEMESA itawezeshwa kifedha imudu kazi zake?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HASNAIN G. DEWJI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Nampongeza Waziri na Naibu wake, kwa kazi mzuri katika Wizara hii. Naishukuru Serikali kwa kumpata Mkandarasi km 60 Nundu – Somanga na kazi imeanza vizuri na inaendelea kujengwa. Bado mkandarasi analalamika kutokulipwa malipo yao. Hivi mpaka sasa M. A. Khalafi hajalipwa na nina wasiwasi kazi inaweza kusimama kwa kufanywa hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awe makini kumlipa mkandarasi. Tatizo lingine kwa Barabara ya Somanga kwenda Ndundu, mkandarasi hajapata GN kwa ajili ya msamaha wa kodi ya mafuta. Leo ni miezi sita GN haipo na hii inasababisha mkandarasi kulipa kodi hiyo na kukosa fedha za kazi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ahimiza kibali hicho ili kazi ya barabara hiyo itengenezwe haraka sana. Kuhusu ATCL, kampuni hii itakuwa mzigo mkubwa na tunaweza kupata hasara. Mheshimiwa Waziri, aunde Tume kwa Shirika hilo la ATCL, wananchi wajue hali halisi ya Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, Mheshimiwa Waziri apeleke Waraka kwa Halmashauri zote, kuwataka Wakurugenzi wote wasiwe wanachukua wakandarasi wasio na uwezo, kwa kuwa wanaitia hasara Serikali.

Mwisho, naipongeza Bajeti ya Wizara na naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Spika, naanza kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, pamoja na Mashrika (Taasisi) zake, kwa matayarisho mazuri ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii. Adhiha, nawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya, pamoja na matatizo mengi yanayoambatana na utendaji wa kazi zao.

Ama baada ya pongezi, napenda kutoa ushauri kwa maeneo yafuatayo:-

Serikali/TPA bado ina kazi kubwa ya kufanya kwa madhumuni ya kupanua na kuboresha huduma zitolewazo na Bandari zetu (Dar es Salaam, Tanga na Mtwara). Mkazo mkubwa, uwekwe kwenye Bandari ya Dar es Salaam katika kipindi cha muda mfupi na baadaye katika kipindi cha muda mrefu.

Ili kufanya hivyo, Serikali/TPA haina budi kukaribisha wawekezaji binafsi (wa ndani na nje) ili kuongeza ushindani katika utoaji wa huduma za kupakuwa na kupakia mizigo bandarini.

Aidha, eneo la kupandishia mizigo moja kwa moja kwenye mabehewa ya mizigo bandarini ni budi lipanuliwe, kuwezesha zaidi ya *train* moja ya mizigo kupakiwa mizigo kwa siku moja.

Serikali iruhusu TPA inunue eneo lililokuwa linamilikiwa na NASACO ili liweze kutumiwa kwa madhumuni ya kupanua shughuli za Bandari ya Dar es Salaam.

Naipongeza Serikali (Wizara), kwa mikakati yake ya kuboresha huduma za *train* katika Reli ya Kati.

Pamoja na mikakati hiyo, napendekeza yafutayo yazingatiwe:-

Mtaji wa sasa wa Shirika la Reli (TRL) (*Authorized Capital*) ni Sh. 20 bilioni.

Serikali pamoja na Rites, wanazungumzia uwezekano wa kuongeza mtaji wa TRL. Nashauri mtaji (*Authorised Capital*) wa Kampuni hii, uongezwe mpaka takriban Sh. 200 bilioni. Kwa kuanzia, mtaji utakaohitajika (kuchangiwa) kuwekezwa (*issued and subscribed capital*) na wabia wawili kwa viwango vya uwiano wa 51% (Rites) na 49% Serikali, usipungue Sh. 100 bilioni.

Nina imani kuwa, ukubwa wa mtaji huu ninaoupendekeza, ndiyo utakuwa jawabu la upungufu wa uwezo wa fedha za kuiendeshea Kampuni ya TRL. Vile vile itatuwezesha kupima uwezo wa wabia, kukidhi mahitaji ya kifedha ya kampuni.

Aidha, ongezeko hili la mtaji, litawapa moyo wa matumaini wakopeshaji kwenye Kampuni hii ya TRL. Vinginevyo, hata wakopeshaji watasita.

Manegement Agreement baina ya Rites na TRL, iangaliwe upya, kwa madhumuni ya kurekebisha vifungu vya *management fees*. Uongozi wa kampuni, pamoja na maeneo mengine muhimu kwa manufaa ya pande zote mbili za wabia (wana hisa), Serikali na Rites.

Maboresho ya Reli ya Kati: Utekelezaji wa Mradi huu muhimu kwa taifa letu, usimamiwe kwa karibu zaidi na hasa ikizingatiwa kwamba, reli hii ni mali yetu (Serikali). Tuongeze jitihada ya kupata misaada na mikopo toka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Wafadhili wengine duniani, kwa ajili ya kuirekebisha Reli yetu.

Kwa nini sehemu ya Reli ya Tabora – Kigoma itaboreshwa kwa uzito wa ratili 60 kwa yadi badala ya uzito wa ratili 80 kwa yadi kama inavyofanywa kwenye sehemu nyingine za reli hii?

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kutangaza kwamba, Serikali imekwisha kubaliana na IFC ili mkopo wa \$ 44.0 milioni kwa TRL, uweze kuendelea kutolewa. Napendekeza Serikali/TRL, iharakishe utimizaji wa masharti yote mapema ili mkopo huu uweze kutolewa na kuiwezesha Kampuni ya TRL, kuanza kutumia fedha za mkopo huu kwa ajili ya kuboresha shughuli zake.

Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma: Kwa maoni yangu, kwa kuwa taratibu zote za kumpata Mkandarasi wa sehemu ya Manyoni – Itigi – Chaya zimekamilika, ujenzi wake uendelee kama ulivyopangwa.

Wakati huo huo, Serikali itafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya Tabora – Kigoma – Chaya ili ujenzi wake nao uanze katika kipindi cha bajeti ya 2009/10.

Mheshimiwa Spika, mantiki ya ushauri wangu ni kwamba, tukibadilisha mpango wa sasa wa Serikali na kusisitiza kuwa ujenzi uanzie Tabora kuja Chaya, hofu yangu, ujenzi wa barabara hii utachelewa kuanza kwa takriban miezi saba mpaka minane, kwa sababu ni lazima taratibu zote zianze upya; yaani upembuzi yakinifu, usanifu, utayarishaji wa nyaraka za tenda, kuitisha tenda, kutathmini tenda na hatimaye kumpata Mkandarasi. Haya yote yamekwishafanywa kwa kipande cha Manyoni – Itigi – Chaya. Kilichobaki ni kumpata Mkandarasi na kazi kuanza.

Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Nzega uanzie Tabora, mara tu taratibu za usanifu na kadhalika zitakapokamilika. Ili ujenzi huu uweze kuanza haraka; ni budi mradi huu uwe miongoni mwa miradi itakayotekelezwa kwa kutumia fedha zetu za ndani. Ni kipande kifupi (116km), lakini ni moja ya viungo muhimu kwa mawasiliano ya Tabora na sehemu nyingine za nchi, kupitia Barabara Kuu ya Dar es Salaam - Mwanza.

Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Sikonge – Mbeya nao uanzie Tabora, kwa utaratibu wa DDB. Fedha zake zitafutwe na ikiwezekana tuanze na fedha zetu za ndani. Usanifu wa Kiwanja cha Ndege Tabora umekamilika, lakini hakuna fedha za ujenzi kwenye Kitabu cha Maendeleo. Naomba maelezo ya Serikali, kuhusu mipango ya ujenzi wa kiwanja hiki kikongwe hapa nchini. Ili tuweze kupata fedha za ujenzi wa baadhi ya miundombinu yetu (Barabara na Viwanja vya Ndege), Serikali haina budi kuharakisha upatikanaji wa *infrastructure bonds* kama alivyotangaza Mheshimiwa Rais, kwenye hotuba yake ya kuunusuru uchumi wetu. Aidha, Serikali iuze hisa zake za Zain (Celtel) NMB, Tanzania Cigarettes Company, NBC na kadhalika ili kupata fedha zitakazowekezwa kwenye miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH: Mheshimiwa wanza, naomba niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, kwa kuanza rasmi, utekelezaji wa ahadi zake, ilizozitoa kwa Wananchi wa Mafia.

Nawashukuru sana Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje (Mb), Katibu Mkuu, Ndugu Omari Chambo, Wakurugenzi wote wa Wizara hii, Wakuu wa Idara zote zilizo chini ya Wizara hii, Wakurugenzi wote wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii, pamoja na Wataalamu wote walio chini ya Wizara hii ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, mimi binafsi na kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Mafia, kwa Serikali yetu kuwa na nia ya kuondoa kero zilizokuwa zinatukabili Wilayani kwetu Mafia. Nashukuru kwa dhati ya moyo wangu, kwa ukarabati mzuri wa Uwanja wa Ndege wa Mafia (awamu ya kwanza) na kumalizia awamu ya pili ya uwanja huu wa ndege. Pili, nashukuru kwa kuendeleza ujenzi wa barabara ya lami toka Bandari ya Kilindoni hadi Utende, yenye urefu wa kilomita 14 au 16 .

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa nia kabisa, imekusudia kuanza ujenzi wa Bandari ya Mafia (Jetty), ambalo ni tegemeo la usalama wa wananchi na mali zao kwa Wakazi wa Mafia, kwa asilimia 85. Kwa hilo basi, naomba na kushukuru sana. Sambamba na vifaa vya ujenzi wa barabara, yaani Greda, Shindilia na hata utaalam.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo basi, sina budi kuiombea Serikali yetu na kuwaombea Viongozi wote wa Serikali hii, kuanzia Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete; Makamu wa Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda (Mb); Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Shukuru Kawambwa; Naibu wake; Katibu Mkuu wa Wizara; na wote wanaohusika na Wizara hii.

Nasema Allah (Mola), atawalinda kwa mabaya yote na akuongozeni kuyafanya ya kheri katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. JUMA SAID OMAR: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Viongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa kutuongoza vizuri. Pia nawapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kuwasilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, ni vigumu kwa nchi yetu, kufikia malengo ya MKUKUTA, kutokana na kasi ya ukuaji wa uchumi kuwa chini ya viwango vinavyotakiwa. Hii inatokana na utawanyaji wa rasilimali tulizonazo kila mahali, bila ya mikakati maalum. Ni vyema tukaangalia mipango mikubwa zaidi ya nchi kuliko mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, barabara ni kufungua nchi. Ni vyema barabara za mikoa, zikapewa kipaumbele kwani zinaunganisha mikoa na hivyo kufanya shughuli za uchumi na maendeleo, kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi. Barabara zinawezesha kusafirisha mazao ya wakulima kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Spika, barabara zinawezesha huduma mbalimbali kama vile afya, elimu, benki, usambazaji wa pembejeo za kilimo na kadhalika, kuwafikia wananchi kwa urahisi zaidi, iwapo kuna barabara nzuri.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa anga nao ni muhimu sana katika kukuza uchumi wetu na kuleta maendeleo. Ni vyema viwanja vya ndege katika maeneo mbalimbali hapa nchini, vikaimarishwa ili tuwe na usafiri wa uhakika kupitia njia ya anga. Kupitia njia ya anga, tunaweza kusafirisha mazao ya kilimo na mifugo kwa urahisi zaidi kutoka hapa nchini kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tuna samaki wengi katika bahari na maziwa yetu makuu; ni vyema Serikali ikawa na vyombo vya uhakika vya kufanya doria ili kulinda na kuhifadhi samaki wetu na rasilimali nyingine za baharini na katika maziwa zisiibiwe au kuharibiwa kwa njia yoyote. Pia kuwe na vyombo vya kusaidia usafiri wa wananchi kwa maeneo yanayohitaji vivuko kama vile meli, *speed boats* na kadhalika. Ahsante.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, naomba kupongeza juhudi za Wizara, kujenga barabara za lami kwa Mikoa ya Magharibi; Rukwa, Tabora na Kigoma. Hapa mnatekeleza kufungua uchumi wa kijiografia.

Naomba Wizara ifikirie upya, kupandisha Barabara ya Wilaya ya Mbozi ya Kakozi hadi Ilonga katika Wilaya ya Sumbawanga katika Jimbo la Kalambo, ambapo huko ni ya Mkoa wa Rukwa, lakini Mbozi ni ya Wilaya na ni kiungo muhimu kwenda Bandari ya Kasanga, bila kupitia Sumbawanga ambayo ni mzunguko mkubwa mno.

Kuhusu reli zetu; reli ni chombo kitakachosaidia kupunguza bei ya bidhaa nchi nzima kama zitaimarishwa na pia itasaidia kuokoa uharibifu wa barabara ambazo hivi sasa zinabeba uzito mkubwa mno, isivyo kifani, kwani reli zetu ni hoi.

Serikali ifikirie kujenga reli ya Mpanda hadi Karema ili reli ya Mpanda isaidie kuchukua mzigo toka Kongo. Bandari ijengwe pale Karema. Serikali pia izungumze na Wachina, wasaidie kujenga reli toka Tunduma hadi Kasanga ili mizigo toka Katanga Lubumbashi, isipitie katika nchi mbili hadi Dar es Salaam Port.

Kuhusu msongamano bandarini, ijengwe ICD kubwa eneo la Ruvu na ziwepo treni maalum, kuhamisha mizigo na makabrasha kwenda Ruvu ICD. *Clearing* yote ifanyike huko ili magari makubwa yanayoingia Dar es Salaam, yaishie huko kupunguza msongamano, kelele na *carbon* mjini, ambao unazidi kuongezeka.

TICTS ichunguzwe kabla haijawa kansa ya usafirishaji na upakuaji bandarini. Sasa ni donda ndugu, kwani mkataba wake ni wa ovyo na Serikali mtaendelea kuchafuka.

Kiwanja cha Ndege cha Songwe na Sumbawanga vikamilishwe ili Nyanda za juu Kusini, nasi tufanye biashara na mataifa mengine, kwa kuuza *perishables* kama ilivyo kwa KIA; maua na mbogamboga.

Ujenzi wa barabara zote katika Mkoa wetu wa Rukwa, usimamizi wa karibu uwepo ili *value for money* ionekane wazi. Barabara za Mkoa na Wilaya, fedha zisimamiwe kwa karibu hasa wilaya ambazo zinapotea ovyo. Wizara itupatie wahandisi wilayani na wasiofaa waondolewe.

Barabara ya Kaegesa - Mwimbi iongezewe fedha ili iwekewe changarawe yote, pamoja na Laela – Mwimbi – Matai. Kalepula – Ilonga, ikiungana na ile ya Konga – Kakozi Wilayani Mbozi, ambayo nimeisemea.

TAZARA ipewe fedha nyingi zaidi.

MHE. DR. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, pamoja na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, kwanza, kwa utendaji wao mzuri, pamoja na hotuba nzuri ya Bajeti ya 2009/2010. Aidha, nawapongeza Watendaji wao wote, akiwepo katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya, pamoja na utayarishaji wa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuipongeza Serikali, inayoongozwa na Rais Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Wasaidizi wake Wakuu; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote.

Mheshimiwa Spika, Mke wa Rais wetu, amekuwa mfano wa kuigwa, kwa kujituma hususan juhudi zake za kutafuta rasilimali kwa ajili ya miradi ya maendeleo hasa miundombinu na huduma za kijamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, aiangalie barabara ya kutoka Morogoro Mjini kuelekea Kisaki. Ubovu wa barabara hii, umechangia sana kudumaza maendeleo ya Wilaya ya Morogoro Vijijini. Wananchi wanalima, lakini wanakosa masoko kwa ajili ya ubovu wa barabara. Vile vile huduma za afya zinaathirika pia kutokana na kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Morogoro Vijijini, inaongoza kwa vifo vya akina mama wajawazito katika Mkoa wa Morogoro, sababu kuu ni ukosefu wa usafiri, pamoja na kushindwa kumudu gharama za usafiri, ambazo zimekuwa kubwa mno, kutokana na ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri aiangalie hii barabara, kwa nia ya kuboresha huduma za jamii na kukuza uchumi wa nchi hususan kilimo. Zaidi ya yote, hii ni barabara ambayo inaenda katika Mbuga ya Solous, ambayo ni kubwa kuliko zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuomba Wizara iangalie namna ya kuboresha huduma ya reli ya kati, kwani wananchi wangu wa Kilosa, hususan wakulima wa vitunguu, wanategemea sana usafiri wa treni. Hii ndiyo njia pekee kwa wananchi wa vijijiji vingi vya Kilosa, kuweza kufika Mjini Kilosa, Mpwapwa na Morogoro. Ninaomba hili liangaliwe kwa makini, kwani hata wenzetu wa Mkoa ya Kati na Magharibi, wanategemea sana usafiri huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia haya machache, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. SIGFRID S. NG'ITU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu, Watendaji pale Wizarani na bila kuwasahau TANROADS.

Mheshimiwa Spika, naomba nikueleze tatizo ambalo linauwinda Ubunge wangu na ushindi wa Chama chetu cha CCM pale 2010.

Mheshimiwa Spika, sasa nikueleze hilo tatizo:-

(i) Mradi wa Barabara ya Nanganga hadi Ruangwa; kuna nyumba ambazo zimebomolewa au kuhitajika kubomolewa ili kupisha huu mradi. Wananchi wanalalamika.

(ii) Wanacholalamikia zaidi ni kifuta machozi bado hakijatolewa. Makisio kiduchu na wengine hawatapata chochote kile.

(iii) Je, waathirika akina Mkopa kule Nandagala watanipa Kura au akina Njinjo na Wazee wenzake kule Ruangwa nao watatupa kura CCM?

(iv) Wazee waliojenga nyumba zao Likunja enzi za ujana wao, sasa wamezeeka sana na hawana wajukuu wenye uwezo wa kuwajengea nyumba za kuishi au hata kuwatunza kwa kuwapa uji wenye sukari.

(iv) Ruanga ilikuwa ni kijiji tu enzi za Wilaya ya Lindi Vijijini, baadaye ikawa Kata, Tarafa na Wilaya pale 1995. Hii barabara imewakuta katika yale majumba yao, yanayohitajika kubomolewa.

(v) Barabara hii tunaihitaji sana kwa vile inaturahisishia kufika pale Nanganga ili tukaikute barabara ya lami itokayo Masasi kwenda Mtwara. Nasi inaturahisishia kufika mapema Mnazi Mmoja ili twende Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Lindi kule Lindi.

Mheshimiwa Spika, najua Waziri atanijibu kwa maandishi, lakini naomba ruhusa yako ili awapokeee waathirika wa zoezi hili na hasa akina Mkopa na Wazee wenzake, wamwelezee kisawa sawa. Busara zako naamini zitapoza hasira zao.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali, kwa jinsi ambavyo imeonesha utekelezaji wa Ilani ya CCM katika upande wa barabara. Naamini hata Bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu, imelenga kwenye kutekeleza Ilani ya CMM. Hivyo, naomba utendaji usituangushe. Baada ya hayo, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Naomba Barabara ya Isuna – Manyoni, isimamiwe vizuri, angalau ifikapo 2010 Juni tukabidhiwe.

Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora inafanyiwa upembuzi yakinifu kwa miaka mingapi kwani hata bajeti zilizopita ni upembuzi yakinifu?

Kuna matatizo gani ATCL? Je, wamefanya nini tangu waanze? Je, fungu la fedha wanazotengewa zinawatosha kutimiza azma yao?

Kwa nini Bandari isiwe Wizara ili iweze kusimamia vizuri usafirishaji wa majini?

Nini kusudio la Wizara kuhusu Reli ya Dodoma – Singida? Je, ipo kweli katika mipango yenu kwani ninaingia shaka kuwa hamna taarifa hiyo?

Ni vigezo gani mnamumia kujenga nyumba za watumishi Mikoani kwani naona mnarundika majengo kwenye mkoa iliyo na majengo, ukiacha Pwani na Dodoma? Kwa nini isiwe ghorofa Singida?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono.

MHE. ELISA D. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali, kwa juhudi zinazofanywa katika kuendeleza miundombinu hasa barabara.

Napongeza usimamizi mzuri wa TANROADS katika miradi mbalimbali katika nchi yetu na hususan katika Mkoa wa Arusha na Jimbo langu la Uchaguzi la Arumeru Magharibi, Barabara ya Mbanda – Oljoro – Losinyai, ambapo amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, jitihada na juhudi za Serikali zinazoonekana katika miundombinu ya barabara ni vyema pia zielekezwe kwenye miundombinu mingine ya Reli, Viwanja vya Ndege na upanuzi wa Bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Lindi, ili kukuza uchumi wa nchi yetu, kwa kuwa miundombinu yote tajwa hapo juu, inategemeana. Ninashauri Serikali kuwa, ni vyema jitihada za makusudi ziandaliwe, kujumuisha miundombinu hii kwa pamoja ili kukuza na kuboresha uchumi wetu kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuendeleza miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na kadhalika, taifa litahitaji fedha nyingi, ambazo uchumi wa nchi yetu hauwezi kubeba kwa wakati mmoja na kwa muda mfupi ujao; na kwa kuwa bajeti yetu ni tegemezi kwa wahisani wa nje kwa asilimia 32, hasa katika

miradi ya maendeleo, ikiwepo miundombinu ya aina mbalimbali. Nashauri Serikali, kwa kadiri itakavyowezekana, itumie fursa mbalimbali kama vile *Build, Operate and Transport (BOT)* na kujumuisha Sekta Binafsi (PPP), pamoja na Serikali kuibua na kujenga miundombinu mbalimbali katika nchi yetu; hivyo kuleta maendeleo ya haraka katika ujenzi wa miundombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya mikataba mibovu, isiyo na tija kwa maslahi ya taifa letu. Kumekuwa na mikataba mingi, ambayo Serikali imeingia na Wawekezaji wababaishaji na ambao hawakutekeleza makubaliano ya kimkataba kati yao na Serikali. Mashirika hayo ni pamoja na TICTS, TRL, IPTL, pamoja na ATCL/SAA. Nashauri Serikali ichukue hatua za kisheria, kwa wote hawa, kwa maslahi ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu tatizo kubwa la msongamano wa mizigo, hasa makontena katika Bandari ya Dar es Salaam. Msongamano huu hasa unasababishwa na utendaji wa Kampuni ya TICTS, wenye upungufu. Aidha, kuna mamlaka na masharika mengine, ikiwepo Mamlaka ya Bandari yenyewe, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Kampuni ya T-Scan, pamoja na Mawakala wa kutoa mizigo bandarini.

Naishauri Serikali, kupitia Mamlaka ya Bandari, kuwakutanisha wadau wote ili kutafuta na kuweka mikakati sahihi ya kupunguza urasimu wa kuondoa mizigo bandarini ili kuondoa adha kwa wajasiriamali walio na mizigo yao bandarini.

Aidha, Mikataba na Watendaji wa Kampuni za TICTS na T-Scan, ambazo ndio zinahusika na kuandaa mizigo bandarini, iangaliwe upya, kwa nia ya kuboresha utendaji wao na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Spika, ningependa kupata maelezo ya kina, juu ya Barabara ya Natta – Mugumu – Loliondo, ambayo kwa muda mrefu sasa hatujapatiwa maelezo ya juu ya nini kinaendelea kwenye barabara hiyo.

Katika mwaka uliopita wa fedha, barabara hii ilitengewa pesa kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Pesa iliyotengwa kwa mwaka huu ni kwa ajili ya kazi hiyo hiyo. Tulitegemea mwaka huu, ujenzi wa barabara hiyo ungeanza. Je, ni kitu gani kinakwamisha ujenzi wa barabara hiyo? Namwomba Waziri, anipatie maelezo ya kina juu ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kupata ufafanuzi wa Kivuko cha Kisorya, Wilayani Bunda, ambacho ni chakavu sana na kwa sasa kinatumika kwa kuvutwa na boti ndogo. Hali ambayo imejenga hofu kubwa kwa Wakazi wa Kisorya na Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, mara kwa mara, Kivuko hiki kimekwama na kushinda majini na abiria kwa siku nzima. Gharama ya kukivuta kwa boti ni kubwa mno. Je, kwa nini

Wakazi hao wa Kisorya na Ukerewe hawapatiwi kivuko kipya? Naomba Waziri anieleze ni nini hatima ya kivuko hicho chakavu na kibovu kupindukia?

Ahsante, naomba kuwakilisha.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote.

Napenda kuipongeza Serikali, kwa juhudi zake za kusimamia Ilani hasa kwa ujenzi wa barabara, madaraja na vivuko.

Mheshimiwa Spika, napenda kuweka msisitizo wa kuhimiza ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Daraja hili litakuwa mkombozi wa wananchi wanaoishi Kigamboni na hata wa mikoa jirani. Kuweka daraja hilo kujengwa mwaka wa fedha 2010/11, iwe ahadi ya uhakika ili kupunguza adha kwa wananchi. Daraja hili ni mkombozi.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikajizatiti katika kuziimarisha na kusimamia vizuri bandari zetu, kwani ni njia pekee ya kutuongezea kipato katika nchi yetu. Nchi nyingi za jirani, ambazo hazina bandari (*Landlock*), zinatumia bandari yetu, lakini ukiritiba uliokuwepo bandarini tunapoteza kipato. Pia kuna bandari nyingi zimezunguka nchi yetu, kama Tanga, Mtwara, nazo zingetumika na kufikiria jinsi gani Bandari ya Lindi itafufuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, napongeza juhudi za Serikali katika kuimarisha na kufufua barabara za ndani za Jiji la Dar es Salaam, ambazo zinaunganisha wilaya nyingine, kitu ambacho kitasaidia kupunguza msongamano wa magari hasa nyakati za asubuhi, jioni na hata nayakati za msimu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb), Waziri wa Miundombinu, kwa hoja yake nzuri, aliyoisoma kwa ufasaha na yenye takwimu muhimu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Aidha, napenda kuwapongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Taasisi chini ya Wizara hiyo, kwa kumsaidia Waziri wao kwa uaminifu, uadilifu na ufanisi wa hali ya juu na kumwezesha kusoma hotuba nzuri sana humu Bungeni.

Vile vile naipongeza Wizara hii, kwa kusimamia Wakandarasi kwa karibu na kuwafutia mikataba wale wabovu na wakorofi kama BECCO, ambaye alichelewesha ukarabati wa Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii tena kwa dhati.

MHE. MWANAWETU S. ZARAFI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hii, pamoja na Watendeaji wake, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Shukrani nyingi kwa Wizara, kwa kuweza kuendeleza eneo lililobaki la Barabara ya Kibiti – Lindi.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Nangurukuru – Liwale, inaunganisha Wilaya ya Liwale na Wilaya ya Kilwa. Kilio cha Wananchi wa Wilaya ya Liwale ni kusafiri toka Dar es Salaam hadi Liwale, kwa kutumia njia ndefu ya Dar es Salaam – Kilwa – Lindi – Masasi – Nachingwea hadi Liwale, wakati *short-cut* ipo na hata gharama ni kubwa kuliko Dar es Salaam – Kilwa – Liwale.

Kama barabara hii hatikauwa rahisi kutengenezwa kwa kipindi cha karibu, basi naomba muwasisitize TANROAD Lindi, waitengeneze kwa kiwango cha changarawe ili ipitike vizuri kama ilivyo kwa barabara za Mwanza – Maswa hadi Meatu.

TANROAD Mkoa wa Lindi, wamekuwa wakirasha rasha katika baadhi ya Barabara za Mkoa wa Lindi.

MHE. ENG. LAUS O. MHINA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hotuba yao nzuri. Vile vile niipongeze Wizara nzima kwa jumla, ikiongozwa na Katibu wake, Eng. Omar Chambo, kwa kuiongoza Wizara hiyo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, naelewa ni kwa kiasi gani Serikali inavyojitahidi kujenga, kukarabari na kufanya matengenezo katika barabara zetu kwa viwango mbalimbali. Vile vile naelewa jitihada zinazofanywa na TANROADS, hususan Uongozi wa Mkoa wa Tanga, katika kukarabari na kufanya matengenezo ya Barabara za Mkoa, pamoja na madaraja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote hizo, hebu TANROADS itazame kwa karibu, uwezekano wa kuzifanyia matengenezo makubwa maeneo ya Barabara ya Kogorowe - Mtoni - Mombo, hususan eneo la Korogwe - Mashewa na Barabara ya Slab - Maguzoni hususan eneo la Kwagunda - Mnyuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kupitia TANROADS, iendeele na juhudi zake za kudhibiti uzito wa mizigo inayopitishwa kwenye barabara zetu. Hata hivyo, Wizara isifumbie macho malalamiko ya wananchi, kuhusu watumishi wachache wasio waaminifu, wanaotumia mizani za barabarani kuwanyanyasa wahusika wa magari, kwa lengo la kujinufaisha wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za matengenezo ya barabara zetu hususan za Mikoa ni vyema kuanzisha Kitengo cha Barabara Vijijini (*Rural Roads Agency*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na huduma isiyoridhisha ya Shirika la Reli (TRL) kwa ujumla, nashauri iangalie hali ya miundombinu ya vituo vya *train* (stesheni), pamoja na majengo yaliopo na yale ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, uchukuzi na huduma za baharini na katika maziwa ziko hoi. Lazima kuinua uwezo wa bandari zetu, kwa kukarabati vifaa na maeneo ya kuhudumia meli, mizigo na abiria.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*), naipongeze Wizara kwa kuongeza nguvu katika ujenzi wa nyumba za watumishi na za biashara. Kutokana na mahitaji makubwa ya nyumba za kuishi; ni vyema mkazo ukawekwa zaidi kwenye ujenzi wa nyumba za ghorofa (*flats*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na jukumu la kusajili Wahandisi na Makampuni ya Ushauri wa kihandisi, ni vyema Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), ikaweka mkazo zaidi kwenye usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu. Kwa juhudi zao, karibu Halmashauri zote sasa katika Idara ya Ujenzi, husimamiwa na wahandisi waliosajiliwa; hili ni la kupongezwa. Hatua kali zichukuliwe kwa watu wanaotumia jina (*title*) la mhandisi, bila ya kuwa na sifa hiyo. Huku ni kudhalilisha taaluma ya uhandisi.

Majukumu ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), yasiishie kwenye kusajili na kukagua tu, bali waweke mkazo zaidi kwenye kutoa mafunzo na kuangalia ni jinsi gani ya kuwawezesha makandarasi wazalendo, kuingia kwenye soko la ushindani. Majengo mengi bado yanajengwa kienyeji, bila kutumia makandarasi hata katika Miji Mikuu; hii ni hatari, lazima ikomeshwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA: Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango ambao nimeshautoa, naomba serikali ifanye utaratibu wa kuiokoa ATCL. Hivi inakuwaje hata Watumishi wa Serikali wanaposafiri wanakodi ndege binafsi badala ya ndege ya Serikali?

Je, tutakuzaje utalii kama hatuboreshi ndege za nchi hii?

Je, Serikali inawezaje kukanusha kama baadhi ya watendaji wanashiriki kuihujumu ATCL kwa kushirikiana na ndege binafsi?

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe fedha/mtaji wa kuiwezesha ATCL ili iweze kujiendesha. Mheshimiwa Waziri, anaposema kuwa, wamewahi kutoa zaidi ya 13 bilioni; hawaoni kwamba hizo hela zilitolewa wakati wa Mkataba na Makaburu? Hii inaonesha jinsi gani Serikali (watendaji baadhi), kuheshimu na kuamini zaidi watu toka nje ya nchi hasa weupe kuliko watanzania. Hata bodi iliyopo walikuta kuna hasi (-) ya mahesabu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itueleze ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kuendesha ATCL? Je, kiasi hicho kinatosha kulikwamua? Je, kwa nini Shirika la Serikali linazidiwa na mashirika binafsi; huu sio mpango wa kuhujumu?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini ATCL ikwamuliwe.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Spika, naipongeza serikari, kwa kazi kubwa inayoifanya katika kushughulikia utengenezaji wa barabara, uliosambaa kwa mtandao mpana hapa nchini. Pamoja na pongezi hizo, ninao ushauri ufuatao kwa Wizara:-

Kwa kipindi kirefu, Wizara hii imejitahidi kusimamia usafiri wa majini hasa katika Maziwa ya Victoria na Tanganyika. Muda umefika sasa, Serikali isaidie usafiri katika Ziwa Nyasa. Kwa kuwa imeonekana wazi kuwa, wawekezaji wengi hawajawa tayari kuwekeza na kununua meli za abiria na mizigo na hivyo kuchangia katika kukwamisha usafiri wa wananchi waishio kando kando mwa Ziwa Nyasa hasa wa Mikoa ya Mbeya, Iringa na Ruvuma. Meli (maboti) ya abiria, yanayotumika hivi sasa ni machakavu sana na ni hatari kwa usafiri wa Ziwa Nyasa, ambalo huchafuka kwa dhoruba kali za mara kwa mara. Ninaishauri Serikali kwamba, katika mazingira haya ya kulegalega kwa uwekezaji katika Ziwa hilo, Serikali ifanye maamuzi ya kununua meli za abiria ili kuepusha maafa yanayoweza kujitokeza wakati wowote.

Kwa wakati huu tunaosubiri, Serikali iangalie uwezekano wa kuzungumza na nchi jirani ya Malawi, ambao kwa miaka ya sitini na saba ni meli zao zilikuwa zinatoa huduma pia kwa wasafiri wa upande wa Tanzania. Malawi wana meli mbili kubwa na za abiria katika Ziwa Nyasa na meli kubwa ya mizigo. Lengo ni kuhakikisha Watanzania hao wanapata huduma kama wenzao waishio kandokando ya Maziwa mengine. Wakati huo huo, nashauri magati yaendele kutengewa fedha ili meli zilizopo ziweze kupata maeneo salama ya kutia nanga ndani ya bandari. Tangu Serikali itenge fedha kujenga Gati la Mbamba Bay/Manda, hakuna fedha nyingine tena inayoendelea kutengwa.

Barabara ya Katumba – Lwangwa – Mbambo – Tukuyu (Wilaya ya Rungwe), ambayo imepewa fedha ya *Detailed Engeneering Design*, imeendelea kupewa uzito. Tunaishukuru sana Serikali kwa hatua hiyo iliyofikiwa. Hata hivyo, tunaomba uharaka katika kulifanyia kazi suala la utekelezaji wa mradi huu haraka, kutokana na matengenezo yake kuhitaji fedha nyingi sana. Hii inatokana na mvua nyingi sana, inayonyesha mara kwa mara Wilayani Rungwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nashukuru Barabara Songea – Mitomoni – Mkenela kupanda hadhi. Nashukuru Barabara ya Winoifinga pia kutengewa fedha. Nampongeza sana Meneja Barabara Mkoa wa Ruvuma, kwa kazi nzuri.

Ningependa kufahamu, katika ukaguzi wa ujenzi wa Daraja la Mkenda kuvukia Msumbiji, Mheshimiwa Rais, aliagiza barabaraba hiyo nayo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami na wakati nauliza swali katika mkutano uliopita, Mheshimiwa Naibu Waziri alisema na kuliambia Bunge, agizo la Mheshimiwa Rais ni utekelezaji. Ningependa kujua ni kiasi gani sasa kimetengwa ili kujua uwezekano wa kuanza upembuzi yakinifu wa kujenga barabara hiyo kwa lami. Wenzangu Msumbiji, bado wako mbele yetu kwa kuanza kuweka lami katika barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi kubwa zilizokwihafanyika za miundombinu hususan barabara na kadhalika nchini kote.

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge lililopita, nilikwishaulizia kuhusu Airport ya Bukoba, itaanza kujengwa lini huko Mkajunguti kwani ni muhimu ili kubeba mazao kama vile ndizi, mboga, samaki fresh toka International Airport Bukoba kwenda Dubai na kadhalika, kupeleka mazao.

Pili, kilio cha Wananchi wa Mwanza, Shinyanga, Kigoma na Tabora, kuhusu treni ni muhimu sana, kwani usafiri huu unachukua mizigo mingi sana na kusaidia barabara zetu zisiharibike.

Kipindi cha Bunge hili pia nilikwisha changia kuhusu *flyovers* za Jijini Dar es Salaam. Huu ni wakati sasa tupate wafadhili na kadhalika, tuweze kutengeneza barabara za *flyovers* ili kukidhi msongamano wa magari Jijini. Aidha, nilichangia pia kutafuta uwezekano wa usafiri wa majini, kutumia maboti toka Kunduchi na sehemu nyingine mpaka karibu na bahari ili kusaidia katika usafiri. Sehemu kubwa ya Jiji la Dar es Salaam, barabara zake nyingi hazijakidhi kiwango kinachotakiwa. Ili jiji lionekane safi na zuri, tujali barabara zake kwanza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. STEPHEN J. GALINOMA: Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika, japo kuna upungufu katika vipaumbele. Nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu nzima, pamoja na TANROADS.

Mheshimiwa Spika, nimesema kuna upungufu. Hili limejidhihirisha katika majadiliano tangu jana. Nitaeleza eneo linalonihusu hapa chini na kura yangu itategemea majibu kutokana na mapendekezo yafutayo:-

LAMI IR – DO: Tulipokuwa Kilolo nilikumbushia jambo hilo, ambalo limekuwa linapigwa danadana toka 1996. Ulinithibitishia kimaandishi kuwa, zimetengwa 20m/= kwa kukamilisha *contact documents* na kwamba, kazi iengeanza mwaka ujao. Nikataka ufafanuzi ni mwaka upi (2009/10 au 2010/11) ambao sijaupata?

Nikumbushe tu kwamba, Wabunge karibu wote waliozungumza, wanailaumu Wizara kwa kupiga chenga. Hata Wapinzani wanailaumu kwa taarifa yako, kama hakuna majibu yanayotosheleza, Mkoa wangu na ya jirani, tumepanga kupinga mpaka mwisho.

Kwa hiyo, naomba jibu la wazi, *in specific terms*, barabara hiyo itawekwa lami lini? Mchango wa Mheshimiwa Malangalila ni maoni yetu wote. *We feel extremely bitter and that we are being victimized for not being vocal.*

IR – MSEMBE: Sikuridhika na majibu ya Naibu Waziri ya tarehe 29 Juni, 2009. Nilimwomba *Regional Manager* katika *Road Board*, atufanyie angalau *preliminary study*, itusaidie kuona tunakokwenda. Majibu ni kwamba, hana fedha wala watu na hawezi kufanya lolote bila amri ya Wizara.

Ruaha National Park ndiyo kubwa kuliko zote nchini na *potential* yake kiutalii/kiuchumi ni kubwa sana. Ndiyo hii barabara inayotengenezwa @ 250 metres a year au 400 years! Naomba Wizara itusaidie.

Njia Panda – Ipanda Hospital: Hiki ni kipande kidogo cha 5 - 6 km na kinaunganisha Makao Makuu ya Wilaya na Hospitali ya Wilaya. Majibu ya 29 Juni, 2009; kwamba ni jukumu la Halmashauri hayasaidii. Sote tunajua kuwa, Halmashauri kuweka lami ni ndoto. Naomba Wizara ibadili msimamo wake.

Vigezo vya Grading of Roads: Vigezo vya kufanya gredi za barabara, baadhi yake ni vikwazo vikubwa. Si lazima iwe kati ya Mkoa na Mikoa au Wilaya na Wilaya. Barabara zinaweza kuwa na umuhimu wa pekee; kijamii au kiuchumi kama barabara hizo mbili katika para 2 na 3. Nashauri tuwe *open minded* ili pale ambapo kuna umuhimu wa kiuchumi au kijamii, barabara husika zipewe kipaumbele stahili.

MHE. ABDUL J. MAROMBWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii, iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Kwa kiasi kikubwa, imelenga kuboresha miundombinu ya nchi yetu, kwa kutoa vipaumbele, ambavyo kama vitatekelezwa kwa ukamilifu; napenda kuishauri Serikali kuwa ni vizuri kusimamia kwa karibu miradi hii ili iweze kukidhi mahitaji ya wananchi wa nchi hii. Pamoja na hayo, ningependa nami kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Kwanza, nianze kwa kuishukuru sana Serikali, kwa kutimiza ahadi ya Rais ya mwaka 2005 na aliitoa tena mwaka 2007 Desemba, kwa kusema kuna Barabara ya Nyamisati – Tuaruke – Kibiti, iliyojengwa kwa kiwango cha changarawe. Kwa mwaka huu, barabara hii imepewa pesa kiasi cha Sh.105 milioni. Kiwango hiki cha pesa ni kidogo sana, kwa kujenga km 42, lakini naamini ni mwanzo mzuri. Naamini kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali itaweza kumalizia ujenzi wa barabara hii muhimu kwa maendeleo ya Wananchi wa Wilaya za Rufiji na Mafia.

Mheshimiwa Spika, jambo/mchango wangu wa pili ni kuhusu Barabara ya Kibiti – Utete – Nyamwage. Barabara hii ni ya Mkoa na tunaishukuru sana Serikali, kwa kuipatia barabara hii fedha kila mwaka. Tunashukuru pia kwa kutupatia Kivuko cha Utete, ambacho kitarahisisha kwenda Makao Makuu ya Wilaya. Jambo ambalo ningependa kushauri ni kuwa; ni vizuri Serikali ikaipandisha daraja barabara hii na kuifanya kuwa *alternative Trunk Road*, kwani endapo Daraja la Mkapa litapata matatizo, barabara hii itumike ili kuunganisha na Mikoa ya Kusini. Kwa hiyo ni vizuri barabara hii ya Kibiti – Utete – Nyamwage iwe ya lami badala ya changarawe.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Barabara ya Kilwa (toka Bandari - Mbagala Rangi Tatu). Tunaishukuru sana Serikali, kwa matengenezo makubwa ya barabara hii. Kwa kiasi kikubwa, barabara hii ina kasoro za kiufundi, kwani baadhi ya maeneo ya barabara yana mashimo na inaleta usumbufu mkubwa! Maeneo hayo ni pamoja na makutano ya Barabara ya Mandela na Kilwa. Eneo hili lina mashimo makubwa na ni hatari hata kwa magari. Ni vizuri basi eneo hili litengenezwe ili kurahisisha usafiri.

Aidha, eneo la Mbagala Rangi Tatu, nalo lina matatizo makubwa sana. Barabara hii ya Kilwa, matengenezo yake yameishia hapo; ni vizuri Serikali ikaongeza kutengeneza barabara hii hadi kufika Milima Mzinga. Kwa kufanya hivyo, kutasaida sana kuondoa msururu wa magari pale Mbagala Mwisho. Kwa sasa eneo hili lina adha kubwa, hasa kwa wasafiri waendao Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie Daraja la Kigamboni. Ujengaji wa daraja hili ni ukombozi mkubwa wa wananchi; si wa Kigamboni tu bali hata waendao Mikoa ya Kusini. Ni vizuri Serikali ikaharakisha mchakato wa ujenzi wake ili ulete ukombozi kwa watu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, miundombinu ndio moyo wa maendeleo ya nchi yoyote ile. Ni jambo la kusikitisha, kuona sekta hii bado haijaleta maendeleo kwa nchi hii, kwani miundombinu ni mibovu mno na bado haijaendelezwa kwa muda mrefu.

Nchi zote zilizoendelea duniani, ziliwekeza katika miundombinu ya barabara, reli na bahari/maziwa. Waliamini nchi au watu, hawawezi kufanya chochote cha maendeleo, bila kusafiri na kusafirisha watu, mizigo; ikiwemo vyakula na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, suala la reli ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote ile. Tanzania tulikuwa na reli Dar es Salaam – Moshi – Arusha, lakini imekufa. Matokeo yake, barabara ndio imekuwa ikibeba mizigo na hivyo kuharibu sana barabara zetu. Tunaomba reli ziboreshwe. Tuna uhakika, reli zikiimarishwa barabara zetu zitapona.

Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ni nembo ya Taifa letu, lakini inasikitisha kuona Shirika hili likifa na kuwa kama yatima. Ni jambo la ajabu, kuona mashirika binafsi yakilizidi Shirika la Taifa. Tuliambiwa kuna ndege mbili zimekodishwa, lakini mpaka leo bado hazijafanya kazi. Je, Serikali inaweza kutuambia ni hasara kiasi gani Serikali inapata kutokana na ukodishwaji huu lakini hazifanyi kazi ndego hizo?

Mheshimiwa Spika, SUMATRA ni chombo kinachosimamia usafiri wa nchi kavu na majini, lakini kimekuwa na tatizo kubwa sana la ajali za mara kwa mara; si tu za barabara bali hata za majini. Tunaomba SUMATRA, iwe inakagua mara kwa mara vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kufuta mpango wa barabara tatu Dar es Salaam, kwani kilio cha wananchi kilikuwa ni ajali za mara kwa mara na msongamano mkubwa sana. Naamini jawabu la msongamano Dar es Salaam ni kuwa na *flyovers*. Je; ni lini Serikali itaanza mchakacho wa ujenzi huo? Nchi kama Ethiopia imeweza kwa nini sisi tushindwe?

Mheshimiwa Spika, suala la bandari ni la msingi sana, kwa mustakabali wa nchi yetu. Tanzania ni nchi iliyopo katika mazingira mazuri kijiografia. Niseme tu, Mwenyezi Mungu, alitupendelea sana kuwa na bandari na kuzungukwa na nchi sita zisizo na bandari. Ni jambo la kushangaa, kuona pamoja na kuwa na bandari tena si moja bali tatu na zile za maziwa, lakini bado bandari hizi hazijaboreshwa na hivyo kufanya nchi hizi, sizitumie ipasavyo bandari zetu na hivyo kupoteza fedha nyingi sana. Baya zaidi, watendaji wamekuwa si waadilifu na baadhi yao, wamekuwa hata wakiiba vifaa hususan magari kama *distributors, boosters, radio cassetts, DVD* na kadhalika. Wizi huu umefanya baadhi ya wateja kuhamia katika Bandari ya Mombasa na Lamu. Tunaomba Serikali isimamie vizuri bandari zetu ili kudhibiti wizi huu. Kwani kama itaendelea hivi, tutapoteza wateja wengi na tutaijengea jina baya nchi yetu.

Naishauri Serikali, iangalie upya suala la mabasi yaendayo kasi, tuliyoambiwa yanakuja. Yatapita njia zipi?

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naishukuru Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu, kwa kutupatia fedha za ujenzi wa Daraja la Kalulu na kuifungua Barabara ya Mkoa, kipande cha kutoka Lukumbule hadi Kijiji cha Tulingane (Makande).

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sikufarijika na barua niliyoletewa na Wizara hii, yenye Kumb. Na. MI/Bunge 16 ya tarehe 26 Juni, 2008, iliyosainiwa na Mheshimiwa Chibulunje (Mb), Naibu Waziri wa Miundombinu. Ndani ya barua hiyo, kuma maelezo yafutayo nanukuu: "... Barabara ya Mangaka – Tunduru (km 146), *studies* zake bado hazijaanza. Barabara hii inapendekezwa ijengwe kwenye ADF 12 kama AfDB wataafiki."

Mheshimiwa Spika, kauli hizi mbili, hazifurahishi na hazileti matumaini hata kidogo kwa Wananchi wa Tunduru, ambao kwa kipindi kirefu, wamekuwa wakivuta

subira. Miaka takriban miwili mfululizo, Serikali imekuwa ikitenga fedha zipatazo Sh. 500 ml kila mwaka, kwa ajili ya *studies* za babaraba hiyo. Leo tunaambiwa *studies* za barabara hazijaanza! Namwomba Waziri atueleze; hizo fedha zilizotengwa zimetumika kwa shughuli gani? Kwa nini babarabar hii haijafanyiwa *studies* ilhali ni moja ya barabara iliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, Waziri anasema, barabara hii inapendekezwa ijengwe kwenye ADF 12 kama AfDB wataafiki; je, kama AfDB hawatakubali nini wazo mbadala?

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri, atueleze wazo mbadala kama AfDB hawataafiki wazo lao. Wananchi wote wa Tunduru hawatashiba maelezo ya Serikali kama maelezo hayo hayaoneshi dira ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Mangaka – Tunduru. Ahsante sana.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb), kwa hotuba nzuri. Pia naishukuru Wizara, kwa kazi nzuri zinazofanyika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Serikali, kwa kuwezesha Barabara ya Minjingu – Babati – Singida, kuanza kutengenezwa kwa lami. Tunashukuru sana. Hata hivyo, kuna matatizo madogo madogo ya hapa na pale, kama vile mahusiano ya kikazi kati ya mkandarasi na wafanyakazi wake na jamii; ni ya kurekebisha tu, si makubwa. Kwa upande wa Serikali, kuna baadhi ya wananchi kandokando ya barabara, hawajalipwa fidia kwa mazao yao hasa miti kama wenzao wengine.

Mheshimiwa Spika, nazidi kushukuru kwa fedha zilizotolewa kwa Barabara ya Dareda – Dongobesh na Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iondoe kwa namna yoyote ile, aibu ya Shirika la Ndege Tanzania na Shirika la Reli nchini. Inatosha tu kusema, hali ni mbaya na kazi kubwa inatakiwa kufanyika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tunayo hamu kubwa sana kuona barabara nyingi za lami zikijengwa nchini na hii ni muhimu sana. Ujenzi wa barabara unategemea pia uchumi wa nchi; hivyo kile kidogo kilichopo, lazima kitumike kwa makini. Wakati nachangia Bajeti ya Serikali, nilielezea wasiwasi wangu mkubwa, juu ya gharama kubwa za ujenzi hapa nchini; jambo ambalo limetokea ghafla. Leo kilomita moja ya barabara, inajengwa kwa shilingi zaidi ya bilioni moja kutoka Sh. 300 hadi 500 milioni kwa kilomita moja. Katika Afrika Mashariki, wastani wa ujenzi wa kilometa ni Dola za Marekani 500,000 hadi 600,000.

Siku tatu zilizopita, mikataba kadhaa imetiwa saini ili kujenga kilomita 563.30 kwa shilingi 584.324, hii ni ghali mno!

Mheshimiwa Spika, *trend* iliyopo ni kwamba, *contractors* wengi wa kimataifa hivi sasa ni Wachina na wamepandisha mno *rates* zao. Historia inaonesha katika ushindani wa tenda, Wachina wamekuwa chini siku zote na kuwa kimbilio letu kiuchumi, leo ni *total about turn!* Kuna haja ya maelezo.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonesha kila mara Serikali inapoingia kwenye mgogoro na *contractors*, Serikali imekuwa ikishindwa katika *cases* au *arbitrations* zinazotokea na hivyo kuingia hasara kubwa.

Kuna suala la *contractors* angalau saba, ambao wanayo dispute na Serikali na kuna kila dalili ya Serikali kushindwa na hatimaye kulipa madeni au fidia au faini kubwa. Wataalam wa TANROADS/Ujenzi, wawe makini katika kufikia maamuzi ya ku-*terminate contractors*. Tungependa kufahamu; hadi sasa kilichotufikisha katika *disputes* nyingi ni kutofahamu *contract conditions* au ni nini hasa? Tutaendelea kufuatilia ili kuhakikisha ufanisi unakuwepo katika taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, Ili *Organization* yoyote ifanikiwe katika majukumu yake ni lazima iangalie utendaji kazi wa *employees* wake. Lazima wafanye kazi kwa ushirikiano na ushirikishwaji wa kutosha. Mwaka jana wakati wa bajeti, nilihoji juu ya jambo hili katika TANROADS.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushirikishwaji wa watumishi katika TANROADS katika maamuzi yanayowahusu, niliuliza kama lilikuwa linafanyika. Mheshimiwa Waziri, aliahidi kutoa maelezo ya jinsi ambavyo angeshughulikia suala hili, lakini bado hajatufahamisha jinsi alivyoshughulikia hoja zetu kwa kina, bila utani na bila kusitasita. Hii ni kwa mujibu wa rekodi za Hansard ya Julai 3, 2008, ukurasa wa 269.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri basi kuelezwa katika ujumla wake, juu ya hayo niliyohoji, ikiwa ni pamoja na utafiti juu ya *comparative rates* za ujenzi wa barabara zetu za lami.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuunga mkono hoja kwa maendeleo ya nchi yetu.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Chunya, nimeambiwa kuwa, sehemu ya pili ya Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi, yaani Lwanjilo – Chunya, mkataba tayari na mkandarasi atianza kazi mara moja. Mimi sidhani, kwani sehemu ya kwanza ya barabara hiyo, ilianza mwaka 2007 na mwaka 2008 Mheshimiwa Rais aliweka jiwe la msingi; lakini mkataba umevunjwa na pande zote mbili, mwezi wa nne mwaka huu; na hakuna hata mita moja ya lami imewekwa!

Hii barabara imo kwenye Ilani ya CCM. Itatuwia vigumu sana kupata kura kwa wananchi mwakani. Naomba sana, mtoa hoja aniambie ni nili sehemu hiyo ya pili

itaanza kuwekwa lami? Pia ile sehemu ya kwanza, baada ya mkataba kuvunjwa, sheria inawataka aidha waende kwa mzabuni aliyekuwa wa pili au wafanye *sole sourcing*. Naomba mtoa hoja aseme ni lini mkandarasi wa sehemu hiyo atapatikana na lini ataanza kazi?

Mheshimiwa Spika, Reli ya TAZARA ina umuhimu sana kwa nchi ambazo hazina bandari kama Zambia na Malawi, lakini ina ushindani mkubwa sana na reli za Msumbiji na Namibia. Naomba mtoa hoja aseme ni lini reli hii itapewa wawekezaji ili ianze kazi kwa ufanisi na kuweza kuongeza kipato cha taifa?

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Watendaji wote wa Wizara hii ngumu na nyeti, katika jitihada zao za kutekeleza miradi mbalimbali, tukianza na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi hasa Mkurugenzi wa TANROAD.

Jitihada zenu na uwezo wenu sisi tunauthamini sana, kama baadhi ya Wabunge wenzangu walivyochangia. Changamoto na lawama zinazoelekezwa kwenu ni shauku ya baadhi ya Wabunge na Wananchi ya kudai maendeleo, maeneo yale ambayo maendeleo hayapatikani, hasa miundombinu ya barabara.

Ninawashauri yafuatayo: Msimamie kikamilifu, ufanisi wa shirika la reli na *railways* yenyewe; muangalie tena Mikataba ya TICTS na namna gani mnaweza kujumuisha *Agency* nyingine; kukubali na kuruhusiwa *ICDs* za watu binafsi na kwa kuwa wana mipango ya kutengeneza za kwao, hivi ni vikwazo vikubwa viondoeni.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalowashauri Wizara hii ni kuimarisha bandari zetu na usafiri wa majini. Tuimarisha Bandari za Tanga, Kigoma, Mtwara, Dar es Salaam na hata Bandari ya Zanzibar. Hivi kuna tatizo gani pale? Msongamano wa *containers* unapotokea, meli ziruhusiwe kushusha Zanzibar!

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kwa makusudi, iweke msisitizo wa juu ya vyombo vya abiria majini vidhibitiwe; ni hatari sana. Hali ilivyo hivi sasa, vyombo hivi vinapakia abiria bila ya idadi ipasavyo, hasa Dar es Salaam, Zanzibar au kwenye Maziwa kama Lake Victoria. Zaidi ya hayo, uangalifu wa kutosha unahitajika kwa vyombo hivi, kwa maana ya kuviangalia uwezo na uzima wake. Watu wanapoteza maisha yao, hakuna fidia wala malipo; si kutoka kwa wenye vyombo wala Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwa nchi yetu kuwa haina ndege zinazopeperusha Bendera ya Taifa hili kubwa na lenye heshima kubwa duniani.

Shirika la *ATCL*, limeingia mkenge halijui lini litafufuka. Tunaiomba Serikali, pamoja na jitihada zake zote, ilione tatizo hili na kulishughulikia. Tunafahamu juhudi na jitihadi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali, lakini kasi zaidi inahitajika.

Mheshimiwa Spika, haya yakifanyika, nadhani Serikali itakuwa inapiga hatua kubwa sana katika uchumi wa nchi hii. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Ahsante.

MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI: Mheshimiwa Spika, katika kipengele namba 20(m), kumbe kuna mafunzo yanayoendelea kutolewa ya matumizi ya nguvu kazi katika ujenzi wa barabara za vijijini (*Upscaling of Labour Based Technology Programme*).

Kwa vile Wilaya ya Ludewa ni nchi ya milima sana, pamoja na ile ya Livingstone, ujenzi wa Barbara kwa kutumia nguvu kazi ni muhimu na unatumika sana Wilayani. Naomba tuletewe mafunzo ya ujenzi wa nguvu kazi, kwa vijana wetu Wilayani Ludewa ili kuboresha elimu yao na kuleta ufanisi zaidi. Nitapenda kujua kama hili litawezekana na kwa utaratibu upi?

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, nina mambo mawili naomba Wizara iyafanyie kazi (utekelezaji).

Kuhusu kulipa fidia Wananchi wa Kipawa ili kuwezesha uwanja wa ndege kupanuliwa; ni muda mrefu sana wananchi wa eneo hilo wamekuwa wakiishi kwa shida sana, kutokana na kutokulipwa fidia na kuzuiwa hata kuzifanyia matengenezo nyumba zao.

Inawezekana gharama za kulipa fidia ni kubwa sana, kwa nini Serikali isitafute eneo lingine kando ya Dar es Salaam ambalo halihitaji fidia kubwa ili uwanja mpya wa kisasa ujengwe huko na huu wa sasa wa J. K. Nyerere Airport utumike kwa ndege za Serikali na zile zinazotoa huduma ndani ya nchi?

Mwaka 2005 wakati wa kampeni, Mheshimiwa Rais, aliahidi kujengwa kwa kiwango cha lami, Barabara ya Kagera hadi Mburahati. Mheshimiwa Rais Kikwete, alitoa ahadi hiyo wakati akihutubia mkutano wa kampeni pale Mburahati.

Naiomba sana Wizara, ijitahidi kutekeleza ahadi hiyo kwani imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu, wanaiulizia kila siku ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais Kikwete.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, napenda kujua zaidi juu ya ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Makongorosi na naomba kujikita zaidi katika fidia ya wahanga wa barabara hii. Napongeza kwa jitihada za awali za kulipa fidia; hata hivyo, yapo malalamiko ya wakazi wengi wa maeneo ya Isanga, Iganzo na Mwansenkwa, Jiji la Mbeya. Naomba Wizara ipitie upya malipo haya ili wajane na yatima, ambao nyumba zimebolewa na miti mbalimbali na *fence*, zipewe uzito kwa malipo halali.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na kuunga mkono

MHE. DR. CRYIL A. CHAMI: Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote. Kiujumla, nawapa pole Viongozi na Watendaji wote wa Wizara hii, kwani mzigo mnaoubeba kwa niaba ya Watanzania ni mzito.

Ukitembelea nchi mbalimbali, utaona zenye barabara nzuri ni zile zenye *road toll*. Hapa Tanzania, magari yanayopita katika barabara zetu kupeleka mizigo nchi jirani ni mengi sana. Faida wanapata wananchi wa nchi hizo, lakini mzigo wa kujenga barabara ni wa Watanzania. Nashauri, Wizara ione uwezekano wa kuyalipisha magari haya ili wenye magari hayo (*foreigners*), nao wachangie katika uboreshaji wa Barabara za Tanzania. Turudishe *road toll*.

Hivi hatuwezi kuuza *shares* za ATCL (*assuming* tumezi-*float*) kwa Watanzania tukapata mtaji wa kuliendesha shirika hili? Naamini tukifanya hivi, *shares* zitakuwa *oversubscribed*, mtaji tutapata na wateja watakuwa wengi kutokana na *loyalty* itakayotokana na wenye pesa wengi kuwa *shareholders*.

My two cents!

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuboresha miundombinu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri hiyo, naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Barabara ya kutoka Ludewa hadi Lupingu iko chini ya Wilaya, lakini barabara hii inapita katika milima mikali. Niliwahi kuuliza swali Wizara ya miundombinu, kutokana na mazingira ya barabara hii, nikiomba iwe Barabara ya Mkoa, kwani gharama za matengenezo ni kubwa, kwa Wilaya yenye mapato madogo kama ya Ludewa kumudu. Ninaelewa vigezo vimetolewa vya barabara kuweza kupandishwa daraja. Napenda kushauri kwamba, pamoja na vigezo vilivyowekwa, tuangalie pia barabara ambazo ni ngumu au zina mazingira magumu ya matengenezo. Hivyo basi, Barabara ya Lupingu ifikiwiwe ili wananchi, wakiwemo wanawake, waweze kupata huduma za usafiri mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu zimekuwa hazina maeneo ya abiria kupumzika, hasa kwenye Barabara Kuu na hii imepelekea wasafiri kujisaidia porini na kuharibu mazingira na kujenga utamaduni miongoni mwa wananchi kwamba, kujisaidia porini ni kama utamaduni. Ukarabati wa barabara na ujenzi, uendane na kuweka vituo vya wasafiri kupumzika. Hii itasaidia pia kuongeza ajira kwa wananchi kuendesha biashara na kujenga utamaduni wa usafiri.

Mabasi/magari kuwa na vifaa vya kutupa takataka ili kusaidia kulinda mazingira. *Traffic* wakague pia kama magari yana vyombo vya kutupa taka.

Barabara ya Kitonga ifanyiwe ukarabati. Barabara hii imeharibika kwa muda mfupi baada ya ujenzi. Serikali iwe makini na makandarasi wanaopewa tenda ili kujenga barabara bora. Kwa vile barabara hii imeanza kuharibika, basi ifanyiwe marekebisho haraka.

Vituo vya matibabu na ushauri nasaha kwa madereva wa magari makubwa: elimu ya UKIMWI, itolewe kwenye vituo vitakavyojengwa. *Clinics* zijengwe Makambako, Iringa, Chalinze na Nyololo kwa kuanzia. Vituo hivi vitasaidia madereva kupumzika na kupima afya zao.

Elimu kwa watumia barabara itolewe, kuhusu usalama barabarani kwa watumia barabara na wanaoishi kando kando ya barabara ili kupunguza ajali, kwani wananchi waishio kando kando ya barabara wakati mwingine wanalala barabarani na kadhalika. Elimu ni muhimu ikibidi vijiji hivyo viwe na kamati ya kuangalia usalama wa barabara ili kupunguza ajali.

Iringa ipate huduma za usafiri wa ndege.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa hotuba nzuri iliyochambua kila eneo.

Tokea kuanzishwa *TANROADS*, kumekuwa na matokeo mazuri ya ujenzi wa barabara na madaraja. Lakini inaelekea hakuna tathmini sahihi inayofanywa, juu ya matumizi halisi ya miradi hiyo. Kwa mfano, Barabara ya Dodoma – Manyoni, kilomita 126, ilianza Machi, 2003. Mjenzi Konoike Construction, ambaye alisitisha mkataba 16 Desemba, 2008, baada ya kukamilisha kilomita 110 kutoka Dodoma hadi Kilimatinde na kubaki kilomita 16, bila ya kufanywa tathmini halisi, *TANROADS kumpa Letter of content, Estim Construction Co. Ltd.*

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kuwa, tarehe 5 Januari, 2009 hadi 12 Januari, 2009, Mkataba wa Tenda ulikwishatiwa saina na kazi kuanza. Ingelikuwa miradi yote ya barabara ilishughulikiwa kama huu, basi nchi yetu ingekuwa imekwishafunguka.

Mheshimiwa Spika, naomba atueleze kuwa ndio utaratibu wa tenda kupewa mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikisema kuwa, barabara kwa kiwango cha lami kilomita moja ni kuanzia Sh.300,000,000 hadi Sh.800,000,000, kulingana na mazingira ya barabara hiyo inakojengwa.

Mheshimiwa Spika, ni vipi kilomita 16 ziharimu Sh.1.5 billion kwa kilomita moja? Naomba maelezo ya kina ni vipi TANROAD wamempa kazi ya zaidi ya kiwango cha 50 million kama walivyoruhusiwa na Sheria ya Manunuzi?

Kilomita 16 au 17 zingekuwa 15 billion; ni kwa vipi malipo yalifikia 25 billion? Hii ziada ya 12 billion imepelekwa wapi? Tathmini ya mradi huu imefanywa na nani?

Upanuzi wa bandari ni muhimu sana; cha kushangaza, tunaanzisha miradi mipya wakati tuliyonayo hatujaikamilisha! Bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na Pemba, zote zinahitaji upanuzi tu na tungelipata fedha za kujenga bandari nyingine.

Tupanue Bandari zilizopo kwanza, kabla ya kujenga nyingine. Aidha, suala la *Dry Dock* ni muhimu, kwani hivi sasa huduma hiyo inapatikana Mombasa na Madagaska. Sisi ndio wenye meli nyingi, lakini hatuna chelezo hadi leo. Hii ni aibu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasemaje juu ya bandari na chelezo?

Sheria ya kuhamisha fedha za bajeti kwenda kwenye mradi mwingine imekuwa chanzo wa mgogoro na Wabunge. Ni vyema mkawasiliana na Waziri wa Fedha ili msipate mgongano na Wabunge.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu 2005, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, akiwa Mjini Mpwapwa, aliahidi kuwa, Barabara ya Mbande hadi Mpwapwa, itawekwa lami kupitia Kongwa Mjini. Naomba ahadi hiyo itekelezwe.

Mheshiwami Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda, akiwa ziarani mwaka huu 2009, Jimboni Kongwa, alishauri kuwa, tuanze kwa Barabara za Mjini Kongwa na Mjini Mpwapwa, kwa kilomita tano kila mji. Naomba sana, jambo hili lipewe kipaumbele katika bajeti ya mwakani.

Mheshiwami Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi kubwa waliyofanya katika kuandaa hotuba yao nzuri na yenye malengo ya kuimarisha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, lazima tukumbuke kwamba, mawasiliano ni maendeleo, bila mawasiliano hakuna maendeleo, iwe ya barabara, ya anga, reli ama maji. Hivyo basi, naomba sana Serikali ione umuhimu na kutenga fedha na maeneo mahususi ya kuyasimamia ili kuondoa kero zinazolalamikiwa kila siku.

Hivi kwa nini Serikali haichukui hatua za makusudi, kushughulikia barabara moja baada ya nyingine ili wananchi waweze kufaidika na maendeleo ya nchi yao kuliko kujenga kipande kipande?

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo ambayo sina ulazima wa kuyataja, hawajawahi kujengewa barabara tangu awamu zote zilizopita hadi leo hii.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam kuna tatizo kubwa la matumizi ya barabara, naiomba Serikali ifikirie suala la kujenga barabara za *flyovers* ili kuwapunguzia Wakazi wa Dar es Salaam, adha ya usafiri wanayoipata.

Nchi yetu itaendelea kubaki na kutowajali wananchi wake hadi lini? Mbona hatuwafikirii sana wananchi wanasafirisha bidhaa zao kwenda sokoni kwa kutumia muda mrefu zaidi kuliko kawaida kama tungekuwa na wepesi wa usafiri? Tukipoteza muda, tunachelewesha maendeleo, kwa sababu shughuli za kijamii zinazorota.

Mheshimiwa Spika, naomba sana tujitahidi.

MHE. DORAH H. MUSHI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uzima nami niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu.

Nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Miundombinu, Naibu Waziri, pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii, kwa hotuba yao nzuri waliyoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu, kwa kuweka lami barabara nyingi nchini na pia kuweka kipaumbele kwenye kilimo Kwanza, lakini Kilimo Kwanza pasipo barabara; mazao yetu yataoza mashambani na ghalani. Mazao yetu lazima yaende kwenye masoko ya mbali. Hivyo, Miundombinu ya barabara ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nipongeze barabara zote zilizopandishwa hadhi kwa mfano, Barabara ya KIA kwenda Mirerani.

Mheshimiwa Spika, Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwenye ziara Mkoani Manyara, alitimiza ahadi yake kwa kutamka wazi kuwa, barabara hii sasa iwekwe lami na akaahidi mbele ya wananchi kuwa, fedha zitatafutwa popote. Sasa fedha iliyotengwa ni kidogo mno haitoshi. Hivyo basi, ningepomba kauli aliyoitoe Rais wetu, itekelezwe na barabara hiyo ianze ujenzi mara moja.

Mheshimiwa Spika, Mirerani imepata hadhi na kuwa mji mdogo. Isitoshe naipongeze sana Serikali kwa kuitambua Mirerani, Mji Mdogo na kulitenga eneo hilo kuwa maalum kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda (EPZ).

Mheshimiwa Spika, hii ni neema kubwa kwa Wananchi wa Mirerani. Wengi wao walikata tamaa na kuhama, lakini sasa kutokana na eneo hilo kupata hadhi kubwa namna hiyo, naamini sasa watarudi wananchi watapata ajira.

Mheshimiwa Spika, kutokana na eneo la Mji wa Mirerani kupata hadhi ya kuwa eneo maalum kwa uwekezaji wa viwanda. Serikali ifanye jitihada za kuhakikisha ujenzi wa miundombinu mizuri, hasa barabara ili kuweza kuwavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kuwa kauli ya Rais ni ya mwisho, hakuna wa kubadilisha; Barabara ya KIA - Mirerani ipatiwe fedha za kutosha. Ujenzi uanze mara moja.

Eneo Maalum la EPZ liheshimiwe ili kutoa nafasi kwa wawekezaji.

Kutokutenga fedha za kutosha kujenga barabara hiyo ni kudhoofisha maendeleo ya Wananchi wa Mirerani.

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Ishirini na Moja - 4 Julai, 2009

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010
Wizara ya Miundombinu**

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka juzi nilipokuwa naahirisha Kikao ilikuwa ni kwa madhumuni ya Kamati ya Miundombinu itusaidie kwa kukutana tena na Serikali ili kuweza kupata uhakika wa Hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo.

Kamati ilikutana, kwahiyo kabla sijawaita Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ili aweze kutupa taarifa.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU MHE. ALHAJI MOHAMMED MISSANGA: Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mbunge wa Ilemela, Hoja ya kufanya Mabadiliko ya Matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo ndani ya Kifungu au *Sub Vote 2005*, kinachojulikana kama *Transport Infrastructer Division*, Fungu 98, la Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Diallo, ya kufanya mabadiliko ya matumizi kama nilivyoeleza hapo juu.

Chini ya Kanuni ya 102 (1), Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, aliwasilisha Hoja ya kufanya Mabadiliko ya Matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo ndani ya Kifungu *Sub Vote 2005*, *Transport Infrastructure Division*, Fungu 98, Wizara ya Miundombinu kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, *Item 4123*, Dumila , Kilosa *Road*; ambayo imetengewa bilioni 8,760,000,000/= fedha za ndani. Na *Item 4134*, Barabara ya Handeni – Mkata, kilometa 54; ambayo ilitengewa bilioni 6,940,000,000/=. Na *Item 2326*, Magole – Turiani – Mziha – Handeni, ambayo ilitengewa shilingi milioni 200,000,000/=. Jumla ya fedha ni shilingi bilioni 15 na milioni 900, ambapo alipendekeza mabadiliko ya matumizi hayo, kuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, alipendekeza kwamba *Item 4196*, ya Dodoma – Babati; ipewe au itengewe shilingi bilioni 8,760,000,000/= na *Item* ya 4195, ambayo ni ya Dodoma kwenda Iringa; ipewe Shilingi bilioni 6. Na *Item 4187* ya Ubungo – Chalinze; ipewe milioni 940/= na kufanya jumla ya shilingi bilioni 16 na milioni 100. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja hiyo iliwasilishwa mbele ya Kamati ya Miundombinu kwa kushirikiana na Wabunge wengine kwa mujibu wa Kanuni Namba 114 (8), pamoja na Serikali, ilijadili hoja hiyo kwa kina na kwa uangalifu mkubwa.

Kwanza kabisa Mtoa hoja Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, Mbunge wa Ilemela, alipewa fursa ya kutosha ya kuwasilisha Hoja yake na baada ya majadiliano kumalizika, alipewa fursa nyingine ya kuhitimisha hoja, ambapo alionyesha kuridhishwa na namna mjadla ulivyokwenda.

Aidha, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo; naye alipewa fursa ya kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusiana na Hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kujadiliana na kutafakari kwa kina, inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, kwa siku zijazo, Mbunge mwenye tatizo au hoja mahususi katika Wizara Fulani, ni vema akaenda kwenye Kamati husika kuwasilisha hoja yake ili ijadiliwe na kuzingatiwa na Kamati husika kabla ya Kamati haijakamilisha kazi yake na kuandika Taarifa yake kwa ajili kuwasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

(ii) Mheshimiwa Spika, ni kwamba itakuwa ni jambo la busara kuendeleza Utamaduni wetu tuliouridhi kwa Waasisi wetu wa Taifa hili, wa kujenga umoja wa Kitaifa bila ya kuathiri haki ya Mbunge, ya kuwawakilisha wapiga kura wake badala ya mtazamo wa kibinadamu Majimboni.

Mheshimiwa Spika, Kamati kabla ya kufikia uamuzi wake kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, ilizingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Serikali katika kutekeleza majukumu yake, inaongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

(b) Maelezo ya Mheshimiwa Kawambwa, Waziri wa Miundombinu, kuwa barabara ya Iringa – Dodoma – Babati, inahitaji fedha za kutosha ama kutoka ndani au kutoka nje kwa wafadhili.

(c) Maelezo ya Serikali kuwa kipande cha Dodoma – Iringa, Serikali imeshafikia hatua nzuri kupata ufadhili wa ADB kiasi kwamba makubaliano au Mkatata kati ya Serikali na ADB yatakamilishwa hivi karibuni. Na hivyo sio busara kuanza ujenzi kidogokidogo kwani Mfadhili anaweza kubadilisha mawazo kwa kuona kuwa kumbe tuna uwezo wa kujenga barabara hiyo wakati uwezo huo hatuna.

(d) Vilevile maelezo ya Serikali kuwa inaendelea na mazungumzo kati yake na ADB kuhusu barabara ya Dodoma – Babati na kwamba yapo matumaini ya kupata ufadhili wa Benki hiyo, lakini mazungumzo hayo hayazuwii Serikali ya Tanzania kuanza ujenzi wa awali kama vile madaraja, kwa kutumia fedha za ndani.

(e) Ni ukweli kuwa barabara ya Iringa – Dodoma – Babati, ni sehemu ya barabara ya kihistoria ya *The Grate North Road* na ni muhimu kwa ajili wa mikoa ya Kusini, Kati kwa maana ya Dodoma na Mikoa ya Kaskazini, na hivyo inahitaji hatua za haraka za ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona sio busara kufuta na kufanya mabadiliko ya matumizi ya miradi ya maendeleo ndani ya Kifungu, *Sub Vote 2005, Transport Infrastructure Division*, Fungu 98, la Wizara ya Miundombinu; kwani miradi hiyo pia ni muhimu kwa uchumi wa nchi yetu kwa ujumla. Na kwamba tukifanya mabadiliko hayo tutawakatisha tamaa na kuwasononesha wananchi wa maeneo hayo. Baada ya maelezo hayo ninayo heshima kuwasilisha ushauri wa Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, kama ifuatavyo:-

(i) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Dumila – Kilosa, kiasi cha shilingi 8,760,000,000/= pamoja na ile ya Handeni – Mkata, kiasi cha shilingi 6,940,000,000/= zinabaki kama zilivyopangwa na Serikali. *(Makofi)*

(ii) Serikali itafute fedha kutoka katika mafungu mengine kiasi cha shilingi bilioni 45,000,000,000/= ili kuanza ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati, hasa fedha itakayomwezesha Mkandarasi kufanya *mobilisation*. *(Makofi)*.

(iii) Ushauri huu umekubaliwa na Mtoa Hoja, Mheshimiwa Dr. Anthony Mwandu Diallo, wakati anahitimisha hoja yake katika Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu, kuwa baada ya kufikia uamuzi au ushauri huo, tumefanya mawasiliano na Serikali na kuitaaruifu msimamo wa Kamati yangu kuwa tuuache mpango wa Serikali uendelee kama ulivyopangwa, lakini Serikali itafute walao kiasi cha shilingi bilioni 45, ili ujenzi wa barabara ya Dodoma – Babati, uanze mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali imepokea na kuukubali ushauri huo na kwamba itautekeleza mapema iwezekanavyo. Kutokana na ahadi hiyo ya Serikali, Kamati yangu inalishauri Bunge lako Tukufu kwamba likubali kupitisha jumla ya shilingi 841,298,364,000/= kama zilivyoombwa na Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na jambo ambalo nimeletewa kama hoja kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Nzega, Lucas Selelii, ambalo ilitakiwa nilitolee uamuzi.

Nalo kwa kifupi tu, yeye anadai kwamba baadhi ya barabara ambazo Serikali imeingia Mkataba na Makampuni kadhaa kiasi cha siku nane tisa zilizopita, zilikuwa hazikutengewa fedha kwa makusudi hayo na Bunge. Kwa hiyo, zinatarajia fedha za Bajeti za mwaka huu. Kwa maana hiyo hiyo inaweza kuwa ni kasoro kubwa sana.

Sasa Maelezo ya Serikali ndio nimeyapata sasahivi hapa Mezani, na kwahiyo siwezi kutoa uamuzi wangu kwasababu ni lazima yachambuliwe na Katibu wa Bunge. Kwa hiyo nasema tu kwamba nitahitaji muda kidogo, kama tukiweza ninaweza kutoa uamuzi kabla ya saa 7.00 baada ya wataalamu kufanya uchambuzi. Vinginevyo nadhani tusisubiri hilo, tuendelee na shughuli kwa mtiririko ambao umekwishapangwa.

Basi Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge, kuchangia kwa siku moja unusu; sasa ni wakati wa kuwasikiliza Naibu Waziri na hatimaye Mtoa Hoja, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.

Mtakumbuka kwamba tuliirejesha ile Kanuni ya dakika 60 kwa ajili ya Wizara hii, kutokana na uzito tu na wingi wa masuala ambayo Wizara hii inayashughulikia. Yaani awali tulitengua takribani Wizara zote, ukiacha ya Waziri Mkuu, ambayo Kanuni inasema Wazi anatumia muda wowote; lakini Wizara zote nyingine zilipewa dakika zisizozidi dakika 30 kuhitimisha hoja, lakini hii tulirejesha ikawa dakika 60.

Kwahiyo, wanazo dakika 75, yaani Naibu Waziri na Waziri. Sasa Naibu nadhani anaanza kwa dakika 25 na Mtoa Hoja, Waziri kwa dakika 50.

Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Miundombinu.

NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi nijumuike katika orodha ya wachangiaji wa hoja hii ya Makadirio ya Wizara yetu ya Miundombinu, fursa ambayo nitaitumia kwa kusaidia kujibu baadhi ya Hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, hususan zile zilizojitokeza wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Serikali na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Lakini kabla sijaanza kufanya hivyo naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia uhai na afya njema hadi hii leo. Na hasa kipekee kwa kuniokoa kwa ajali mbaya ya barabara iliyonipata mwishoni mwa mwaka jana, nikiwa safarini kikazi Mkoani Singida. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuninusuru katika ajali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kipekee pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, kwa imani yake kwangu ya kuendeleza ridhaa yake ya kuniwezesha kutumikia nafasi aliyonipa katika Wizara hii.

Aidha namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, kwa maelekezo na usimamizi wake wa karibu katika utendaji wangu wa kazi za Serikali zinazoihusu Wizara hii na hata Bungeni pia.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa, kwa jinsi anavyoendelea kunishirikisha katika masuala mbalimbali ya kuiongoza na kuisimamia Wizara hii.

Lakini pia naomba niwashukuru watendaji wakuu na watumishi wote wa Wizara pamoja na wa Taasisi zote chini ya Wizara hii ya Miundombinu, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Injiniya Omari Chambo, kwa ushirikiano ambao ameendelea kunipa toka nihakimishiwe kwenye Wizara hii, mwaka mmoja uliopita. Ushirikiano wao wanaonipa

unanifanya nizowee kwa haraka kukabiliana na changamoto nyingi na ngumu za utekelezaji wa majukumu yangu Wizarani, nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nishukuru sana kwa faraja kubwa ninayopata kutoka kwa Mke wangu Mpendwa Vaileth, kwa kuwa msaada mkubwa kwangu kwa kunitunza na kuwa karibu nami sikuzote katika mambo yote, magumu na mepesi.

Nimalizie shukrani zangu kwa kwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa na uvumilivu wao kwangu, na hasa wanaponikosa kwa shughuli mbalimbali za Jimboni wakati nikitumikia shughuli nyingine za Kitaifa.

Naomba waendeleo na moyo huo, nami naahidi kuendelea kushirikiana nao na kuwatumikia kwa kuwawakilisha hapa Bungeni na kwingineko, na siku zote nawaomba tulenge kusonga mbele, kujiletea maendeleo katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Chamwino kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi, sasa naomba nijielekeze katika mchango wangu kwa kujibu baadhi ya hoja za waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimetangulia kusema. Lakini pengine nitangulie kwa kusema kwamba, Naunga Mkono Hoja. Na ili mipango yote iliyopendekezwa kwenye hoja hii iweze kutekelezwa, naomba pia Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wote pia tuunge mkono. Wengi wa michango yenu katika hoja hii ni kielelezo tosha na cha wazi ya kwamba sekta hii ya Miundombinu, inagusa maisha ya wananchi wote wa Tanzania kwa maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi. Michango yenu yote ni ya muhimu sana, tutaifanyia kazi. (*Makofi*)

Lakini kwa vile muda hautatosha kujibu hoja zote, kwangu mimi hata kwa mtoa hoja mwenyewe, tunatangulia kuahidi ya kwamba hoja zote mlizotoa, tutazijibu kwa maandishi na kuwapatieni. Lakini ninataka tu niahidi ya kwamba kama ilivyo utamaduni wetu, wale wote aliochangia hoja hii kwa mdomo na kwa maandishi watatambuliwa rasmi na Mtoa Hoja mwenyewe. Na baada ya hayo naomba sasa nijielekeze kwenye baadhi ya majibu ya hoja hizo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ilijitokeza hoja ya kwamba serikali ijenge barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma, kwa lami ili kukamilisha Ukanda wa Kati na kuboresha bandari ya Kigoma. Hoja hii ilichangiwa na Wabunge wengi kiasi, akiwemo Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Kaboyonga, Mheshimiwa Nsanzukwanko, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Sijapata Fadhil Nkayamba na wengine waliochangia katika hoja ambayo Mheshimiwa Waziri aliitoa.

Mheshimiwa Spika, majibu ni kwamba barabara hii iko katika utekelezaji katika maeneo mbalimbali. Kwanza Kigoma – Kidahwe kilometa 35.7, Mkandarasi anaendelea na ujenzi. Kidahwe – Uvinza – Ilunde kilometa 104, mazungumzo kati ya serikali ya Abudhabi kupitia *Abudhabi Fund* kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa barabara hii

yamekamilika. Mkataba wa mkopo wa masharti nafuu unatarajiwa kusainiwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Ilunde – Malagarasi – Kaliuwa kilometa 156, maandalizi ya ujenzi wa daraja la Malagarasi na barabara zake za maingilio kilometa 48, yanaendelea chini ya ufadhili wa Serikali ya Korea. Serikali inafanya mazungumzo na serikali ya Saudi Arabia, ili kupata fedha za kugharamia ujenzi wa kilometa 108 zilizobaki. Kaliuwa – Urambo – Tabora kilometa 126, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za Zabuni, ulikamilika mwaka 2007. Mazungumzo na Serikali ya Kuwait kuhusu ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami yanaendelea. Sehemu ya Tabora – Itigi – Manyoni kilometa 270, naomba mtoa hoja atakuja kuileleza kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili; serikali ijenge barabara ya Nzega – Tabora, kilometa 116 ili kuondoa kero. Nayo ilichangiwa na Waheshimiwa Mgana Msindai, Lucas Seleli, Siraju Juma Kaboyonga na Mheshimiwa Juma Nkumba. Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya Mwaka huu wa Fedha 2009/2010 tunaomba, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Nzega – Tabora, kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu; ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Mingumbi – Maswa – Bariadi na barabara ya Kolandoto – Meatu; ilichangiwa na Mheshimiwa John Momose Cheyo, Fred Tungu Mpendazoe. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2008/2009, Serikali ilitenga shilingi bilioni 7 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mingumbi – Maswa – Bariadi, sehemu ya Bariadi – Lamadi. Aidha katika Bajeti ya fedha ya mwaka 2009/2010, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Bariadi – Lamadi, kilometa 70.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne iliyojitokeza ni barabara ya Iringa – Dodoma – Babati; nayo ilichangiwa na wachangiaji wengi kweli kweli, Mheshimiwa Omari Shaban Kwangw', Mheshimiwa Kusila, Mheshimiwa Bura. Kwa kifupi tu ni kwamba kwasababu barabara hii ina maelezo mahususi, nayo vilevile nitamwachia mtoa hoja atakuja kuitolea maelezo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ni miundombinu ya reli, barabara na bandari, kupewa kipaumbele katika kujenga na kuchochea ukuaji wa uchumi na kuinua sekta ya kilimo. Wachangiaji walikuwa ni pamoja na Mheshimiwa Juma A. Ngasongwa, wa Ulanga Magharibi, Mheshimiwa Susan Lyimo, na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro.

Hapa tunasema tu kwamba jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu nchini zinaendelea na mojawapo ya mikakati ya kuchochea ukuaji wa uchumi na kuinua sekta ya kilimo nchini, miundombinu bora itasaidia kupeleka pembejeo katika maeneo ya uzalishaji na kupeleka mazao kwenye masoko. Serikali itaendelea na juhudi za kuiimarisha miundombinu hiyo kadri hali ya upatikanaji wa fedha itakavyokuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita ni kwamba pamoja na mpango wa muda mrefu uliopo wa ujenzi wa barabara ya Nata – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu, Serikali itenge fedha kwa ajili ya kuifanyia matengenezo barabara hiyo ili iweze kupitika.

Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Kadika Telele; na hapa tunatoa majibu ya kwamba katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.55. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 400, kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina na shilingi bilioni 1.15 zitatumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

Aidha katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 kiasi cha shilingi bilioni 1.3 zitatengwa kwa jili ya usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni. Mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri, haukukamilika katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, badala yake mchakato utakamilika mwezi Julai mwaka huu. Na katika mwaka wa fedha wa 2008/2009, jumla ya shilingi milioni 132 zilitengwa kugharamia matengenezo ya barabara hiyo. Matengenezo yalipangwa yafanyike kwa fedha, zimetumika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Manyoni – Isuna, ukamilishwe haraka. Mchangiaji alikuwa Mheshimiwa Juma Killimbah wa Iramba Magharibi, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, wa Viti Maalum, Mheshimiwa Joyce Martin Massunga wa Viti Maalum; na majibu hapa ni kwamba muda wa miezi 36 kwa ujenzi wa kipande cha Manyoni – Isuna kilometa 54, ni muda ambao uliwekwa kwenye mkataba. Na ninadhani kwamba kwa muda huo barabara hiyo itakuwa imekamilika kwa mujibu wa mkataba ulivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, nane; hapa kulikuwa na pongezi kwa kutenga fedha shilingi bilioni 12.5 kwa ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongolosi. Wachangiaji walikuwa Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa na baada Mheshimiwa Benson Mpesya.

Ujenzi wa barabara ya Mbeya – Makongolosi kilometa 115, sehemu ya Mbeya – Luandilo kilometa 36, umeingia mgogoro wa kimkataba kati ya Serikali na Mkandarasi, na sasa suala hilo lipo Mahakamani. Lakini ujenzi wa sehemu ya mradi unasubiri maamuzi ya Mahakama.

Lakini mchakato wa kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Luandilo – Chunya kilometa 40, umekamilika na mkataba umesainiwa tayari kwa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, tisa; ni kwanini barabara ya Chalinze – Segera – Tanga, inajengwa kutoka njia moja kuwa njia mbili, yaani *Dual Carriage* na inaingia barabara ya Chalinze – Dar-es-Salaam, yenye njia moja? Aidha ilishauriwa kwamba barabara ya Chalinze – Dar-es-Salaam, ndio ingefaa ijengwe njia mbili ili iweze kupunguza msongamano wa magari.

Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Seleli. Majibu ni kwamba barabara ya Chalinze – Segera – Tanga, haijengwi kwa njia mbili, yaani *Dual Carriage Way*, barabara hii ili ijengwa miaka ya 90 kwa msaada wa Serikali ya Denmark.

Wakati wa ujenzi wake ilijengwa bila ya mabega ya barabara, yaani *shoulders*, hivyo ukarabati unaoendelea sasa unafanywa chini ya ufadhili wa Serikali ya Denmark, ili kurekebisha kasoro hiyo kwa kujenga mabega na kuweka tabaka lingine la lami.

Mheshimiwa Spika, namba 10, Mheshimiwa Sadiq, wa Mvomero, aliuliza ni kwanini kipande cha Magole – Mvomero – Turiani kimeachwa, ni kwanini? Majibu ni kwamba kipande cha barabara ya Magole – Mvomero – Turiani hakijaachwa katika mpango uliopo wa kujengwa kwa lami barabara ya Korogwe – Dumila – Kilosa – Mikumi, yenye urefu wa kilometa 369. Mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu hii ya Magole – Mvomero – Turiani, umesainiwa mwezi Juni mwaka 2009, tayari kwa kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, 11 ni mpango wa matengenezo ya barabara ya *PMMR* katika Mkoa wa Tanga, utekelezaji wake hauonekani, na ni hatua gani zimechukuliwa? Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, aliuliza swali hili.

Majibu ni kwamba mpango wa matengenezo ya barabara kwa muda mrefu, yaani *performance base management and maintainance of roads*, ulianza kwa majaribio mwaka 2004 katika mikoa hiyo. Lakini mkakati wa kuwapata Makandarasi kwa ajili ya mpango huu, ulianza kwa pamoja katika mikoa ya Tanga, Mwanza na Rukwa.

Kwa upande wa mkoa wa Tanga, zabuni zilizorejeshwa zilikuwa na gharama kubwa kupita Bajeti iliyowekwa, hivyo iliamriwa kurudia mchakato huo. Hii ndio sababu ya mpango huu kuchelewa katika Mkoa wa Tanga.

Hivi sasa mchakato wa kuwapata Makandarasi umekamilika na kazi zimeanza mwezi Mei mwaka huu 2009. Kazi zinaendelea na kuchonga barabara, kuweka changarawe, kujenga makalavati na kuchimba mifereji ya maji. (*Makofi*)

Hoja nyingine ilikuwa ni Serikali ifanyie marekebisho ya barabara ya uchumi ya Mtwara Nanyamba, Tandahimba, Newala, hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum. Lakini vilevile Mheshimiwa Njwayo Mbunge wa Tandahimba naye alichangia.

Majibu ni kwamba katika mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali imetenga jumla ya shilingi 377 milioni kwa ajili ya matengenezo ya muda maalum katika barabara ya Mtwara, Nanyamba, Tandahimba, Newala. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara kutoka Mtwara hadi Mwanza kwa kiwango cha lami. Je ahadi hiyo imetimizwa? Hili swali liliulizwa na Mheshimiwa Halima Mdee. Hapa Serikali inajibu ya kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara ya kutoka Mtwara hadi Mwanza yenye urefu wa kilomita 1710 kwa kiwango cha lami imetimizwa. Hadi sasa sehemu kubwa ya barabara hiyo imekamilika na sehemu chache zilizobaki ziko katika hatua za mwisho za ujenzi kwa kiwango cha lami kama ifuatavyo.

Kipande cha Ndundu, Somanga, kilomita 60 kazi zinaendelea na zitakamilika mwaka 2011. Manyoni Isuna kilomita 54 kazi zinaendelea na zitakamilika mwaka 2011, Ilula Mwanza, kipande kati ya Ilula na Mwanza ambacho kimeharibika mapema kitafanyiwa ukarabati mkubwa. Kwa hiyo, kwa vipande hivyo vichache vilivyobakia nataka kujibu kwa uhakika kabisa kwamba ahadi ya Rais imetekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwamba ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Tabora Urambo kilomita tatu, ulikuwa ukamilike mwezi Aprili, 2009 haujakamilika vigezo gani vilivyotumika katika kuteua mkandarasi kutoka Musoma kuja kujenga kilomita tatu badala ya kuteua mkandarasi wa kutoka huko huko Tabora? Na hoja hii ilitwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Kazi ya ujenzi wa barabara ya Tabora Urambo yenye kipande cha kilomita tatu, ulianza mwezi Aprili, 2008 na ulipangwa kukamilika Juni, 2009. Mradi huu umechelewa kukamilika kutoka na ulazima uliojitokeza wa kuhamisha huduma za kijamii ambazo ni mabomba ya maji na nguzo za umeme. Kwa sasa huduma hizo zimehamishwa na mkandarasi anaendelea na kazi.

Kutokana na sababu hizo mkandarasi ameongezewa muda wa miezi miwili na sasa kazi zitakamilika mwezi Agosti mwaka huu. Kazi zilizofanyika ni Ujenzi wa tuta wa barabara umekamilika kwa asilimia 90, msingi kwa asilimia 70, ujenzi wa makaravati umekamilika kwa asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imejitokeza katika michango ya Waheshimiwa Wabunge ni barabara ya Kagoma, Lusahunga ijengwe haraka kwani imekuwa kero kwa wananchi. Hili lilitolewa na Mheshimiwa Wabunge Savelina Mwijage, baadaye alikuja kulisisitizia Mheshimiwa Masilingi. (*Makofi*)

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali imetengewa shilingi bilioni 19 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha baada ya mkataba wa awali kusitishwa mwaka 2008 kutokana na mkandarasi kushindwa kazi, zabuni ziliitishwa upya na mkandarasi mpya amepatikana sasa mkataba mpya umesainiwa mwezi Juni, 2009 na kazi zinatarajia kuanza mara moja.

Dhana ya *Mtwara Corridor* haitaieleweka kwa wananchi wa Ruvuma mpaka hapo barabara ya Tunduma Songea itakapojengwa kwa kiwango cha lami, na hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Devota Likokola. Majibu ni kwamba katika kutimiza azma ya kufungua ukanda wa *Mtwara Corridor* Serikali itaendelea na utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa barabara ya Mtwara, Masasi, Tunduru, Namtumbo, Songea *Mbamba Bay* kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Masasi Mangaka kilomita 54 kazi ya ujenzi inaendelea na jumla ya kilomita 15 za lami zimekamilika hadi sasa katika mwaka wa fedha 2009/2010. Serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa barabara hii na jumla ya shilingi bilioni 9.6 zimetengwa, mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Japan.

Katika mradi wa *Mtwara Corridor* kuna daraja la umoja, kazi ya ujenzi inaendelea na zinatarajiwa kukamilika Oktoba, mwaka huu hadi sasa kazi imefikia asilimia 85. Kipande cha Mangaka Mtamba wa Swala, usanifu wa kina wa barabara ya Mangaka Mtamba Swala umekamilika ndiyo sasa Serikali inatafuta fedha za kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Mangaka Tunduru kilomita 146 upembuzi yakinifu umekamilika Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami. Tunduru Namtumbo kilomita 194 upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Tunduru Namtumbo umekamilika. Benki ya Maendeleo ya Afrika *ADB* pamoja na shirika la maendeleo la Japan *JAICA* wamekubali kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi, mazungumzo yanaendelea kwa lengo la kusaini makubaliano ya mkopo. Kipande cha Namtumbo Songea hadi Mbinga kilomita 139, barabara ya Namtumbo Songea kilomita 61 na Songea Peramiho *junction* Mbinga kilomita 78 zitajengwa kwa kiwango cha lami kwa ufadhili wa Serikali ya Marekani kupitia *MCC*. Mchakato wa kuwapata makandarasi unaendelea na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kusainiwa Desemba 2009. (*Makofi*)

Mbinga *Mbamba Bay* kilomita 68 usanifu kwa kina umekamilika, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kugharimia ujenzi kwa kiwango cha lami. Kukamilika kwa miradi ya barabara iliyotajwa hapo juu kutaibua na kuchochea fursa mbalimbali za kiuchumi katika ukanda huu wa *Mtwara Corridor* ikiwa ni pamoja na wananchi wa Ruvuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali iboreshe huduma za usafirishaji wa abiria wa mizigo na reli eneo hili nitamwachia mtoa hoja kuja kulitolea maelezo ya ufasaha zaidi. Eneo lingine ni mkataba wa *TRL* hilo nalo naomba nimwachie mtoa hoja aje alitolee maelezo, miundombinu ya reli, Serikali kuipa fedha *TRL* yote haya naomba niyaruke ili Mheshimiwa Mtoa hoja atakapokuja ayatolee maelezo kwa ufasaha.

Sasa eneo linalofuata ni huduma mbovu na usalama mdogo wa abiria na mizigo ndani ya treni na hili lilitolewa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Sijapata Fadhihi Nkayamba na wengine pamoja na Mheshimiwa Tatu Ntimizi.

Kwa safari za treni kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza *TRL* ina *Buffet Car* moja tu kwa ajili ya kutoa huduma za chakula ndani ya treni, safari ya Dar es Salaam kwenda Kigoma kwa sasa haina *Buffet Car* kutokana na kusimamishwa na *SUMTRA* kwa sababu za kiusalama. Aidha *Buffet Car* hiyo iko kwenye matengenezo ya katika karakana ya Dar es Salaam. Hata hivyo kampuni imeajiri kampuni binafsi kutoa huduma za chakula ndani ya treni na imepewa behewa moja kwa ajili ya huduma hiyo, ambayo ni hatua ya muda tu lakini jitihada za kuboresha huduma hii zinaendelea chini ya usimamizi wa *SUMTRA*.

Hoja nyingine wastaafu wa TAZARA hawalipwi mafao wanapostaafu na hii ilitolewa na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, kwa kuzingatia hali mbaya ya fedha inayoikabili TAZARA menejimenti imepanga utaratibu kuwalipa mafao stahili wastaafu kwa mafungu madogo madogo kila mwezi kupitia taasisi za mifuko ya hifadhi ya jamii. Lakini kwa ujumla tu niseme matatizo ya shirika la reli la TAZARA ni makubwa ya kifedha na kimejimenti Serikali zetu mbili ya Zambia na Tanzania zinalifanyia kazi kwa jitihada ya kuhakikisha yanafanyika marekebisho makubwa na hasa kutafuta mwekezaji ambaye ataendesha shughuli za shirika hili la reli ya TAZARA, na hivi sasa mchakato wa kusaini *protocol* mpya kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli hii utafanyika muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, nyingine ilikuwa ni kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za bandari, hii hoja ilichangiwa na wachangiaji wengi Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kiongozi wa upinzani, Mheshimiwa Ali Salum, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na wengine.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi nataka kusema kwamba Wizara yangu imekamilisha mpango kabambe wa uendelezaji wa bandari zote za mwambao na maziwa yaani *Port Master Plan*. Mpango huu wa miaka 20 umeanza kutekelezwa mwezi Machi, 2009 lengo la mamlaka ya bandari nchini ni kuziboresha na kuendeleza na kukaribisha wawekezaji kuendeleza huduma za mizigo. Bandari ya Dar es Salaam itaendelezwa ili iweze kuhudumia meli kubwa zenye uwezo wa kuchukua mizigo mikubwa pamoja na kuanza kutekeleza mpango wa kuendeleza bandari nchini. Pia Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za mizigo ili kuongeza ufanisi wa kuhudumia mizigo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie lakini sio kwamba hoja ndiyo zimekwisha, kwa kusema hoja iliyojitokeza ya kwamba tuangalie uwezekano wa kuunda Wizara ya Bandari pekee ili kuboresha huduma za bandari na hoja hii ililetwa na Mheshimiwa Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Kilonsi Mporogomyi na Ahmed Ali Salum.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kwamba kwa kuwa Serikali inaendelea kufuatilia na kutatua matatizo mbalimbali ya bandari haioni sababu ya kuunda Wizara ya Bandari peke yake kwa hivi sasa, lakini kwa sababu suala la kuunda Wizara ni la ridhaa ya muunda Serikali, hilo kusema kweli kwa sasa hivi tusingependa kuendelea kulisemea chochote.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimesema mwanzo, hoja ni nyingi na wachangiaji ni wengi na sisi kama tulivyoahidi kwamba hoja tunazitambua kwamba zina umuhimu zinagusa majimbo yetu wote, ahadi za Rais zinagusa kila jimbo katika nchi yetu yote, tutaendelea kuzitekeleza kwa kadri uwezo wa Serikali utakavyokuwa unaruhusu.

Kwa hiyo, naomba tu nirudie kwa kusema kwamba tuiunge mkono hoja hii na hasa wale wenzangu waliokuwa wanasema kwamba kwa sababu mradi huu ni ahadi ya ilani, ni ahadi ya Rais kwa hiyo siwezi nikaunga mkono mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba miradi hii pamoja na ahadi hizi ziko katika majimbo yote ya Uchaguzi, kwa hiyo kama tukija na msimamo huo kwamba mradi au ahadi iliyoko kwenye jimbo langu kama halijatekelezwa basi kuunga mkono kutakuwa na mashaka, mipango yetu haitakwenda naomba tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja hii ili mipango iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sasa namwita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu anazo dakika 50 nitaondoa muda wote ule ambao atatumia kutaja majina ya wachangiaji kwa maandishi, na kwa kuchangia humu Bungeni ili abaki na dakika hamsini za kushughulikia hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe mwenyewe na Mheshimiwa Jenista Mhagama Mwenyekiti kwa jinsi ambavyo mmesimamia majadiliano ya Bajeti ya Wizara yangu takribani sasa leo ni siku ya tatu. Usimamizi wako mahiri katika majadiliano haya yanaonyesha jinsi gani Chama cha Mapinduzi (CCM) kina hazina kubwa ya viongozi katika ngazi zote. (*Makofi*)

Pia nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaji Mohamed Missanga, kwa maoni aliyotoa ya Kamati yake ambayo yamejaa uzoefu, busara na hekima kubwa, utaalum wa sekta na mawazo ya upeo wa muda mrefu wa kisera ambayo kwa ujumla wake yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha sekta hii kwa siku zijazo. (*Makofi*)

Aidha namshukuru msemaji mkuu wa Kambi ya Upinzani Sekta ya Miundombinu, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kwa maoni na mapendekezo yake kuhusu Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano ya hotuba ya Serikali Waheshimiwa Wabunge 44 walitoa michango yao kuhusiana na sekta ya miundombinu. Aidha wakati wa majadiliano ya hoja ya Waziri Mkuu Waheshimiwa Wabunge 44 pia walitoa maoni mbalimbali na ushauri kuhusu sekta ya miundombinu. Kwa ujumla michango ya Waheshimiwa Wabunge kwa Bajeti hizi mbili kuhusu sekta ya miundombinu ilihusu maeneo makuu yafuatayo.

Kwanza ni barabara. Waheshimiwa Wabunge 72 walichangia. Usafiri wa majini. Waheshimiwa Wabunge 30: Usafiri wa reli, Waheshimiwa Wabunge 19 na usafiri wa anga, Waheshimiwa Wabunge 11 walichangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa tutazingatia sana ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge na nitatoa ufafanuzi kwa yale ambayo yatahitaji kutolewa ufafanuzi. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa michango yao waliyoitoa kwa maandishi na kuzungumza hapa Bungeni wakati

wakijadili hoja ya Wizara yangu. Michango hii ni michango mizuri na itatusaidia sana katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti hii pamoja na kuboresha sekta ya miundombinu katika siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, naomba basi kama ilivyo ada yetu kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza na kwa maandishi hapa Bungeni kama ifuatavyo.

Awali waliochangia kwa kuzungumza wakati wakichangia Hoja ya Serikali, Bajeti ya Serikali na hoja ya Waziri Mkuu ambao ni Wabunge 88 kama ifuatavyo.

Wabunge waliochangia wakati wakichangia Hoja ya Bajeti ya Serikali kuu na Hoja ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalasa, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Ahamed Ali Salum, Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw', Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Benadeta Kasabango Mshashu, Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, Mheshimiwa William Jonathan Kusila, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Magale John Shibuda, Mheshimiwa Lazaro Samweli Nyalandu, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Arch. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

Wengine ni Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Mwanawetu Zafari, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Godfrey Zambi. Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Josephine Ngezabuke, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Elieta Switi, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Eng. Louse Mhina, Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

Wengine ni, Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Mhonga Ruhanywa,

Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyr, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Ana Maulidah Komu, Mheshimiwa Abbas Zubeir Mtemvu, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza wakati wa kuchangia hoja ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu ni 47 na naomba niwatambue kama ifuatavyo. Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo.

Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Benito Wiliam Malangalila, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Brg. Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Ramadhan Athuman Maneno, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw', Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Victor Mwambalasa, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Idd Mohamed Azan, Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Dorah Mushi na Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi wakati wakichangia Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu ni 93 na naomba niwatambue kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, Mheshimiwa Dustan Mkapa, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Mercy Emmanuel, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Charles Mwera, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Paul Lwanji, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibiliti, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Elieta Switi, Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Anna Magareth Abdallah, Mheshimiwa Dr. Lucas

Siyame, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Archt. Fuya Kimbita, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi, Mheshimiwa Bakar Shamsi Faki, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya,

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Khadija Ally Al-Qassimy, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Col. Fete Mgeni, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Benedict Nangoro, Mheshimiwa Muhonga Ruhanywa, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia,

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Ussi Ameir Pandu, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Hasnain Dewji, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Sigrif Ng'itu, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi, Mheshimiwa Eng. Louse Mhina, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Cythia Hilder Ngoye, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa Janeth Kahama, Mheshimiwa Abdul Jabiri Marombwa, na Mheshimiwa Stephen Galinoma. (*Makofi*)

Labda kabla sijaendelea na sehemu hii baada ya ya kusoma orodha hiyo ndefu, niwatake samahani Waheshimiwa Wabunge ambao bila ya kukusudia pengine nimetaja majina yao kwa makosa. Naomba radhi kwa wale ambao nimewakosea katika kuyataja majina yao. Sikufanya hivyo kwa makusudio bali kwa uharaka wa kusoma na kwa changamoto ya kiti hiki ambacho nimesimama sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia ujumbe ambao Wabunge wengi wamekwisha kutoa kwamba miundombinu ya uchukuzi pamoja na huduma zake ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa letu na kuleta maisha bora kwa wananchi wote. Miundombinu hiyo ni ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na vivuko. Nachukua fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imepokea kwa moyo mkunjufu michango hiyo na tunaahidi kuifanyia kazi michango hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunaahidi kufanyia kazi michango hiyo yote, michango hiyo itakuwa dira yetu katika utendaji kazi kila siku. Pale ambapo tutaona kuna umuhimu wa kujifunza kwa kina au kupata maelekezo ya ziada kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge hatutosita kuonana nao mmoja mmoja au kwa kikundi au hata Kamati nzima ya Bunge ya Miundombinu. Kwa kutumia njia hii nina imani kwamba tutaendeleza ushirikiano mzuri kati ya Wizara yangu na Bunge lako Tukufu. Napenda pia kuchukua fursa hii kukuhakikishia kwamba tumekuwa na ushirikiano mzuri na Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Waheshimiwa Wabunge wote. Tutaendeleza ushirikiano huo hata baada ya vikao hivi vya Bunge katika kuboresha na kuimarisha sekta hii ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ya Miundombinu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu wakati akiwasilisha maoni ya Kamati yake alisisitiza utekelezaji wa Ilani ya CCM. Serikali kuweka mikakati ya kudhibiti ajali za majini na barabarani ambazo zinaleta athari kubwa kwa taifa. Pia alisisitiza kuwa Serikali iangalie utendaji usioridhisha wa bandari ya Dar es Salaam hasa katika kitengo cha kontena kinachoendeshwa na *TICTS*, kuufanyia marekebisho mkataba wa *TICTS*, matumizi ya vituo vya mizigo ama *ICD* na kushirikisha wadau wote katika kutatua matatizo.

Kuhusu usafiri wa reli Kamati ilishauri kuwa Serikali itafute fedha ili kuimarisha reli ya Tanga, Arusha, Tabora, Kaliuwa, Mpanda na Manyoni - Singida. Serikali pia ichukue hatua ya kuvunja mkataba wa *TRL* kutafuta mwekezaji mwingine.

Katika sekta ya usafiri wa anga Serikali itoe fedha za kutosha kuweza kuendeleza viwanja vya ndege nchini na iongeze fedha katika Shirika la *ATCL*. Aidha, ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa Bagamoyo au Mkuranga upewe msisitizo.

Maoni ya Kamati yamezingatiwa na baadhi ya hoja nitazitolea ufafanuzi wakati nikijibu Hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Maoni ya Kambi ya Upinzani. Pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto ambaye ni msemaji mkuu wa Kambi ya Upinzani Sekta ya Miundombinu kwa ushauri wake. Mheshimiwa Kabwe Zitto alitaka Serikali ieleze ni fedha kiasi gani mwekezaji *RITES* amewekeza kwenye kampuni ya *TRL* na Hoja ya Serikali kulipa shilingi bilioni 4.4 kwa *RAHCO* ili kufidia madeni mbalimbali yaliyokuwa ya *TRC* bila idhini ya Kamati ya Madeni ya Taifa.

Alitaka pia kujua Serikali imefikia wapi katika kuupitia Mkataba na pia Serikali imepata wapi nguvu ya kununua hisa wakati *KADCO* ilikopeshwa shilingi bilioni 5 kwa dhamani ya Serikali.

Kuhusu Sekta ya Usafiri Majini, Kambi ya Upinzani ilitaka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ili iweze kushindana na Bandari ya Mombasa na kuhusu usafiri kwa njia ya maji katika ziwa Victoria ambao umekuwa hauridhishi.

Maoni ya Kamati yamezingatiwa na baadhi ya hoja nitazitolea ufafanuzi wakati nikijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, ningependa kutolea ufafanuzi juu ya hoja ya *KADCO* na usafiri katika Ziwa Victoria kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, *KADCO* ilipatiwa mkopo wa shilingi bilioni 3.9 na *European Investment Bank* na kuchukuliwa dhamana na Serikali kuanzia mwaka 2003 *KADCO* ilianza kulipa mkopo huo na hadi sasa imelipa jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 1.6 kama inavyotakiwa na mkataba. Aidha, kwa kuwa, *KADCO* kama kampuni itaendelea hata baada ya hisa za wanahisa wawili kununuliwa ni dhahiri kwamba *KADCO* kama kampuni itaendelea kulipa mkopo huo.

Kuhusu mapitio ya mkataba baada ya Serikali kubaini kuwa kulikuwa na vipengele vya mkataba ambavyo vilikuwa na mapungufu Serikali ilianzisha majadiliano na *KADCO* ya kuupitia mkataba. Katika vipengele 49 vilivyopitiwa vilisalia vipengele vitatu tu ambavyo havikupata muafaka wakati ambapo wanahisa wakuu wawili *Mott Mac Donald* na *Saif* walitaka kujitoka katika kampuni. Ni kweli Serikali inataka kununua hisa za wanahisa hao katika *KADCO*, hii inatokana na wanahisa hao *Mott Mac Donald* mwenye hisa 41.4% na *Saif* mwenye hisa 30% kutaka kujitoka na kuuza hisa zao. Wanahisa hao walitaka hisa zao ziuzwe kwa kampuni ya *Omni port* ya Uingereza lakini Serikali ilipotathmini uwezo wa kampuni hiyo ilionekana haina uwezo kifedha wa kuendeleza kiwanja cha Kilimanjaro. Hivyo Serikali ikafanya uamuzi wa kununua hisa hizo kwa lengo la kuzitunza kwa muda ikimtafuta mwekezaji mwingine mwenye uwezo. Kwa sasa hisa za Serikali ndani ya *KADCO* ni 24%, hisa za 4.6% ni za kampuni ya *Inter Consult* ya Tanzania.

Kuhusu usalama wa usafiri wa Meli katika Ziwa Victoria ni kwamba meli zote hufanyiwa matengenezo makubwa na yale ya kawaida mara kwa mara na kukaguliwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini yaani *SUMATRA* na zinazokidhi viwango vya cheti cha ubora. Meli ya *MV Victoria* ilifanyiwa matengenezo makubwa kuanzia mwezi Juni, 2007 hadi Februari, 2008 na kwa sasa inaendelea na safari zake bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, Hoja za Wabunge. Sekta ya Barabara. Baada ya kutoa maelezo kuhusu hoja za Kamati ya Miundombinu na Kambi ya Upinzani sasa naomba nitoe michango ya Wabunge waliochangia hoja yangu nikianza na hoja zilizoelekezwa kwenye sekta ndogo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ya ujenzi wa Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma ambayo imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao.

Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba, Mheshimiwa John. P. Lwanji, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Juma Nkumba na Mheshimiwa Aziza S. Ally.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamehoji kisitishwa kwa mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kujenga sehemu ya barabara kutoka Manyoni – Itigi hadi Chaya. Aidha, walitaka kujua mipango iliyopo ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora hadi Kigoma kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kujenga barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora hadi Kigoma kwa kiwango cha lami, Kwa kuwa barabara hiyo ni ndefu sana na uwezo wa Serikali ni mdogo, juhudi zimeelekezwa katika kutafuta msaada au mikopo kutoka nchi za nje. Aidha, katika hatua ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii, Serikali ilianzisha mchakato wa kuitisha zabuni za ujenzi wa kiwango cha lami sehemu ya Manyoni, Itigi, Chaya baada ya kutiliana saina Hati ya maelewani ama *MOU* kati ya Serikali ya Iran na Serikali ya Tanzania Desemba, 2008. Kwa bahati mbaya, mkataba wa kupata fedha kutoka Serikali ya Iran haukuwa umesainiwa. Kutokana na hali hiyo basi Serikali ililazimika kusitisha mchakato wa kumpata mkandarasi wakati tunasubiri mkataba huo usainiwe. Mategemeo ya kusaini mkataba huo bado yapo na barabara ya Manyoni – Itigi mpaka Chaya itajengwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa juu ya ujenzi wa Barabara ya Iringa – Dodoma – Babati hadi Minjingu hoja ambayo ilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao. Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Felister A. Bura, Mheshimiwa Eng. Benito Malangalila, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Zabein M. Mhita. Hawa waliochangia hoja hii walitaka kujua mipango ya ujenzi wa barabara ya Iringa – Dodoma – Babati – Minjingu. Aidha pia walitaka kufahamu jinsi fedha iliyotengwa mwaka 2008/2009 shilingi bilioni 12 ilivyotumika na kwamba fedha iliyotengwa mwaka 2009/2010 ya bilioni 5.6 itafanya kazi gani.

Mheshimiwa Spika, dhamira ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kama ilivyoanishwa katika Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005. Hata hivyo barabara hii ina urefu wa jumla ya kilomita 528. Hivyo haiwezekani kutumia fedha za ndani pekee kutokana na gharama kuwa kubwa na Serikali haina uwezo huo. Ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami, Serikali imekamilisha makubaliano ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ama *ADB* kutoa fedha za ujenzi kwa sehemu ya barabara ya Iringa – Dodoma. Kuhusu sehemu ya barabara ya Dodoma – Babati katika Bajeti ya mwaka 2008/2009 Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 12, mwaka wa fedha 2009/2010 Serikali imepanga kuanza ujenzi kwa madaraja kwa kutumia fedha zake za ndani wakati juhudi zinaendelea kutafuta fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma – Babati imetengewa fedha na fedha hizi hazitoshi Serikali imetoa ahadi ya kuongeza katika fungu hili ili kazi ianze katika ujenzi wa barabara hiyo ya Babati – Dodoma lakini pia Serikali itaendelea na juhudi za kuapata pesa za wahisani ili tuweze kuwa na hela za kutosha kutimiza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya utendaji wa makandarasi na ubora wa ujenzi wa barabara nchini hili ni eneo kuu ambalo limehojiwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao ni hawa wafuatao.

Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Raymond A. Mrope, Mheshimiwa Hemed Hemed, Mheshimiwa Janeth Massaburi na Mheshimiwa Maria I. Hewa.

Waheshimiwa Wabunge hawa wameonyesha wasiwasi wao juu ya utendaji mbovu wa makandarasi hususan ubora wa kazi na ucheleweshaji wa kukamilisha kazi hivyo kusababisha migogoro ya mikataba.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuimarisha usimamizi wa utendaji wa kazi za makandarasi kwa kupitia Sheria na Taasisi za udhibiti wa kazi za ujenzi. Aidha, Wakala wa Barabara *TANROADS* itahakikisha inasimamia na kuzingatia kwa umakini utendaji wa makandarasi na kuchukua hatua zinazofaa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limehojiwa ni eneo la mipango ya kupata fedha za ujenzi wa barabara na Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hoja hii ni hawa wafuatao.

Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Anthony Diallo na Mheshimiwa Brig. Hassan Ngwilizi.

Waheshimiwa Wabunge hao wametoa mchango wao wa mawazo kuhusu namna ya kuongeza upatikanaji wa fedha zaidi kwa ajili ya miradi ya barabara ikiwa ni pamoja na kupunguza 15% ya matumizi ya kawaida kwa Serikali nzima na kutumia hisa zake iliyowekeza katika mashirika kuweka tozo za utumiaji wa baadhi ya barabara na madaraja.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeyapokea mawazo hayo kwa nia ya kuona uwezekano wa namna ya kuyatekeleza. Tumeyapokea mawazo hayo mazuri, tutaendelea kuyatafakari ndani ya Serikali ili tuone namna ambavyo tungeweza kimuafaka kabisa kuyatekeleza kwa faida ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa ni usalama barabarabani na udhibiti wa uzito wa magari na kupunguza msongamano. Eneo hili limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao.

Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Vita R. Kawawa na Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya ajali za Barabarani, udhibiti wa uzito wa magari na msongamano wa magari mijini, Serikali itaendelea kusimamia kikamilifu juhudi za kupunguza ajali kwa kuisitiza na kusimamia Sheria za usalama wa barabarani.

Serikali pia itaendelea kutumia mizani iliyopo na kuongeza mingine ikibidi ili kudhibiti uzito wa magari yanayopita katika barabara. Aidha, Serikali kuanzia mwaka wa fedha 2008/2009 imeanza kutekeleza mradi wa kuboresha barabara za Jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano wa magari.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa ni fidia kwa miradi ya barabara na Waheshimiwa waliochangia hoja hii ni hawa wafuatao.

Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Vita R. Kawawa na Mheshimiwa Wilson M. Masilingi. Ulipwaji wa fidia kwa watakoathirika na ujenzi wa barabara unazingatia Sheria. Hivyo kama kuna malalamiko yoyote ya wale wote ambao hawakuridhika na fidia wana haki ya kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana na sekta hii. Naomba Waheshimiwa Wabunge wawaelimisha wananchi ili kuwaepushia usumbufu na kero zinazoweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limechangiwa ni kupandisha hadhi barabara. Hoja hii ilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao kwa sababu ya muda naomba nisiwataje wote lakini jumla yao ni 25 kwa sababu nilishawataja katika orodha ya jumla.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme yafuatayo. Upandishaji wa hadhi za barabara umezingatia vigezo vilivyotumishwa katika Sheria ya barabara Namba 13 ya mwaka 2003 na Kanuni za Management za mwaka 2009. Aidha, barabara ambazo hazikupandishwa hadhi hazikukidhi vigezo ambavyo vimeanishwa. Hata hivyo, vigezo vilivyotumika katika kupandisha hadhi barabara vimetumwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote, kama kuna barabara ambayo inakidhi vigezo hivyo na haikupandishwa daraja inaweza kuletwa Wizarani ili iliangukiwe na Kamati ya Kitaifa tuliyoichagua kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa zoezi hili ni endelevu na tutaendelea kupanga barabara katika hadhi stahili mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa njia ya Reli. Waheshimiwa Wabunge walichangia kuhusu hoja ya kuvunja kwa mkataba wa ukodishwaji wa Reli ya Kati unaoendeshwa na *TRL* kwa kuwa imeshindwa kutoa huduma za kuridhisha. Aidha, walishauri Serikali kuanza mkakati mpya wa kumtafuta mwekezaji mwingine. Wakati mwekezaji mpya anatafutwa uendeshaji wa huduma za usafiri wa reli ukabidhiwe kwa kampuni ya Serikali ya *RAHCO* na kwamba iwezeshe kwa mtaji wa kutosha badala ya kuendelea kuipa fedha kampuni ya *TRL*.

Waheshimiwa waliochangia hoja hii jumla yao ni kumi na saba. Naomba nisiwataje majina kwa sababu ni wengi na hasa kwa vile tayari nimeshawataja wachangiaji katika orodha ya jumla.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe maelezo yafuatayo.

Wana hisa wa *TRL* ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *RITES* wanaendelea na majadiliano ya kuifanyia marekebisha mikataba ya ukodishaji wa

TRC. Wanahisa wameunda vikundi viwili ili kuharakisha majadiliano, kikundikazi kimoja kazi yake ni kutayarisha Mpango wa Biashara ama *Business Plan* ya kampuni ambapo wanahisa watajua mahitaji halisi ya kuongeza mtaji wa kampuni na kurekebisha mikataba kwa lengo la kuondoa upungufu mbalimbali uliojitokeza ikiwa ni pamoja na kutatua tatizo la *management* ya kampuni.

Vikundikazi viwili vimeundwa kimoja cha kuangalia *Business Plan* au Mpango wa Biashara wa kampuni na kingine kinaangalia mikataba ambayo Serikali imeingia katika kukodisha miundombinu hii ya Reli.

Mwekezaji *RITES* katika kampuni ya *TRL* mpaka sasa amewekeza dola za Kimarekeni milioni 10.2 kama sehemu ya mtaji. Serikali imewekeza dola za Kimarekeni milioni 9.8 kama Sehemu ya mchango wake kwa mtaji.

Vilevile Serikali itaimarisha njia ya Reli kupitia *RACO* kwa kutoa kiasi cha dola za Kimarekeni milioni 33 na wanahisa wote wawili wataongeza mtaji kwa kiasi cha dola za Marekeni milioni 80. Aidha, Serikali iko katika hatua ya upembuzi yakinifu ya kuboresha Reli ya Kati ya Dar es Salaam hadi Isaka na kuijenga na baadaye kuunganisha Reli hiyo na ile Reli itakayojengwa kati ya Isaka hadi Keza kwenda Kigali nchini Rwanda na kati ya Keza hadi Igitaga mpaka Msongati nchini Burundi.

Maamuzi kuhusu mkataba huu yatatolewa baada ya kuhitimisha majadiliano kati ya Serikali na mwanahisa *RITES* wa nchini India.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Usafiri wa Anga. Imetokea hoja kuhusu *ATCL* na hoja hii imechangiwa na Waheshimiwa wabunge kumi. Naomba pia nao nisiwataje majina ili kuokoa muda. Waheshimiwa wabunge walitaka kujua juhudi zinazofanywa na Serikali za kuimarisha *ATCL* ili ichangie katika kukuza utalii na biashara. Aidha, walitaka *ATCL* iongezewe fedha katika Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kuimarisha kampuni ya ndege ya Tanzania. Hatua ambazo Serikali imechukua ni pamoja na katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali ilichukua hatua ya kubadili deni lake kiasi cha shilingi bilioni 17.5 ndani ya kampuni hiyo kuwa mtaji hivyo kuimarisha mizania ya Shirika la *ATCL*.

Katika mwaka 2008/2009 Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 12.25 kwa ajili ya uendeshaji wa *ATCL* pamoja na kulipia baadhi ya madeni yakiwemo madeni ya mafuta.

Wakati *ATCL* iliponyang'anywa cheti cha uendeshaji ama *Air Operator Certificate* mwezi Desemba mwaka 2008, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu iliingilia kati na kuunda timu ya Wataalamu ambao iliharakisha mchakato wa *ATCL* kurejeshewa tena chetu hicho na *ATCL* iliweza kurejeshewa cheti hicho na Mamlaka ya Usafiri wa Anga yaani *TCAA* tarehe 30 Desemba, 2008. (*Makofi*)

Katika mwaka wa 2008/2009 Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kutathmini thamani ya kampuni na ukaguzi wa hesabu za ATCL zinazoishia mwezi Juni, 2008. Mazoezi haya mawili yalikuwa ni muhimu kwa ajili ya kujindaa kwa kampuni hiyo kubinafsishwa na kupata mwekezaji katika kampuni hiyo.

Serikali imekuwa na mazungumzo na *China Sonangol Internationa Ltd.* ili iweze kununua 49% ya hisa za Serikali ndani ya ATCL ili mwekezaji aweze kutoa mtaji unaotakiwa katika kutekeleza mpango wa biashara wa kampuni. Matumaini ya Serikali ni kwamba mazungumzo yatakamilika mapema na ATCL iweze kuchukua nafasi yake katika jamii. Ni kweli mazungumzo yamechukua muda. Kazi haikuwa nyepesi lakini walau sasa tunaweza kusema tumeanza kuona Mwanga mwisho wa *tunnel* hili.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu fidia kwa wananchi waliojenga ndani ya kiwanja cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo ilichangiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya.

Mheshimiwa Spika, Hoja hii inawahusu wananchi wa Kipawa, Kigilagila, Kitunda na Kipunguni wanaongoja fidia ya kuhama, Waheshimiwa Wabunge walihoji, kama gharama ni kubwa, Serikali itafute sehemu nyingine ya kujenga kiwanja na Wabunge hao pia walitaka kupata maelezo kuhusu wananchi wanaotakiwa kuhama ambao walipewa viwanja katika maeneo ya Pugu, Kajiungane, Buyuni na Majohe kwamba wanasumbuliwa kwani viwanja walivyopewa vina mgogoro.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ulipaji fidia kwa wakazi wa maeneo ya Kipawa, Kipunguni na Kigilagila ambao watatakiwa kuhama ili kupisha upamuzi wa kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius K. Nyerere kilinza kufanyiwa kazi tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000. Changamoto kubwa kwa Serikali tangu wakati huo ni ukubwa wa gharama zinazotakiwa kama fidia kwa wakazi hao kwa mujibu wa Sheria na uhaba wa fedha kutokana na kuchelewa kulipa fidia hizo, gharama zilikuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka wakati gharama za fidia kwa mwaka 2004 zilikadiriwa kuwa shilingi bilioni 22.9, mwaka 2007 zilifikia shilingi bilioni 27.8 Kwa kuwa hivi sasa tunapongea gharama za fidia zinakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Spika, gharama za ulipaji fidia kwa wakazi wa maeneo yote matatu zitajumuishwa katika mradi mzima wa upanuzi na uendelezaji wa kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius K. Nyerere unaotarajiwa kufanyika kwa ubia kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa niaba ya Serikali na kampuni ya *China Sonangol* kutoka Jamhuri ya watu wa China.

Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, kati ya viwanja 7000 vilivyopimwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege eneo la Pugu Kajiungeni, Buyuni na Majole, viwanja 1600 vililipiwa fidia na Mamlaka hiyo ili kuwapatia wakazi 1300 wa Kipawa ambao wamepangwa kuhama

katika awamu ya kwanza, kati ya viwanja hivyo vipo viwanja 400 ambavyo vimevamiwa na wananchi walioko maeneo ya jirani. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imewasiliana na Mkuu wa Wilaya ya Ilala ili wale wote waliovamia viwanja hivyo waweze kuondolewa kwa mujibu wa Sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lililochangiwa ni eneo la kutaka kujua kwa nini Serikali itumie fedha nyingi kulipa wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila badala ya kutafuta eneo jipya la kujenga kiwanja kipya cha kimataifa. Eneo hili lilichangiwa na Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni na Mheshimiwa Dr. Anthony M. Diallo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na Chuo Kikuu cha Ardhi kuhusu thamani ya kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Mwalimu J. K. Nyerere pamoja na miundombuni yake imeonyesha kwamba tathmini ya kiwanja hicho ni zaidi ya shilingi bilioni 500. *(Makofi)*

Aidha, Miundombinu ya kiwanja yaani barabara za kutua na kurukia ndege, maegesho na viungio vyake kwa maana ya *run ways* na *tax ways* vina uwezo wa kuhudumia abiria milioni 20 na idadi hii ya biria itaweza kufikiwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 20 ijayo. *(Makofi)*

Hii ina maana kwamba miundombinu hiyo inaweza kutumika kwa zaidi ya miaka 20, upanuzi unaokusudiwa ni ujenzi wa jengo la tatu la abiria ama *terminal building three* kwani jengo la sasa *terminal building two* limefikia ukomo wa uwezo wake. Tathmini inaonyesha kwamba gharama ya fidia kwa wananchi wa Kipawa, Kipunguni na Kigilagila ni sawa na 8% ya gharama ya kujenga kiwanja cha kimataifa chenye miundombinu kama ile ya kiwanja cha kimataifa cha Mwalimu Julius K. Nyerere.

Tunakubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge ya kuanza kutafuta eneo jipya kwa ajili ya kiwanja kipya cha kimataifa kwa ajili ya miaka ijayo.

Serikali imetafuta na kupata maeneo mapya katika Mkoa wa Pwani na moja ya maeneo hayo yalipatikana katika Mkoa wa Pwani katika Wilaya ya Bagamoyo na Wilaya ya Mkuranga. Maeneo hayo yatatumika kujenga kiwanja kipya cha kimataifa kitakachokidhi mahitaji ya usafiri wa anga kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, sasa twende kwenye sekta ya usafiri kwa njia ya maji. Sekta hii ya usafiri kwa njia ya maji, hoja ya kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za bandari ilichangiwa na Wabunge 26 pamoja na Mheshimiwa Mohammed Hamisi Misanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti Kamati ya Bunge, Fedha na Uchumi na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekamilisha mpango Kabambe wa Uendelezaji wa Bandari zote za mwambao na maziwa ama *Port Master Plan*. Mpango huu ni wa miaka 20 na umeanza kutekelezwa mwezi Machi mwaka 2009.

Lengo la Mamlaka ya Bandari nchini ni kuziboresha na kuendeleza na kukaribisha wawekezaji kuendesha shughuli za mizigo. Bandari ya Dar es Salaam itaendelezwa ili iweze kuhudumia meli kubwa zenye uwezo wa kuchukua makasha 5000 ama *TELLS*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanza kutekeleza mpango wa kuendeleza bandari nchini pia Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuboresha huduma za mizigo ili kuongeza ufanisi wa kuhudumia nyaraka, kupunguza muda wa kontena kukaa bandarini na kupunguza mrundikano wa makasha hayo bandarini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuboresha utendaji, kuongeza ushindani na mkataba mbovu wa *TICTS* ilichangiwa na Wabunge kumi na tatu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeunda Kamati ya Mawaziri ili kufanya majadiliano na *TICTS* kwa madhumuni ya kuondoa kipengele cha ukiritimba kilicho ndani ya mkataba na hivyo kutoa fursa ya wawekezaji wengine kuja na kuwekeza katika huduma za Meli zinazobeba makasha ili kuongeza tija, ushindani na hivyo kuongeza pato kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Ali Khamis Seif kuhusu ajali ya kuungua moto kwa boti ya *Amana Pemba* iliyotokea Tanga tarehe 14 Aprili, 2009 akiitaka Serikali kutoa maelezo kuhusu kuchelewa kwa Mamlaka zilizo Tanga kushughulikia suala hili mapema hadi kusababisha vifo vya abiria.

Mheshimiwa Spika, Boti ya *MV Amana Pemba* iliondoka Bandari ya Tanga tarehe 14 Aprili, 2009 saa 3.45 usiku ikiwa na mizigo ya aina mbalimbali. Kutokana na uchunguzi uliofanyika Boti hiyo ilipita tena bandari bubu Sahare na kuchukua abiria ambao idadi yake haijulikani. Boti hii ilipata ajali ya moto siku hiyo ikiwa safarini kuelekea Pemba. Taarifa za ajali za Pemba zilitumwa kwa njia ya simu ya mkononi kwa boti dada ya *MV Amana* Tanga saa 6.15 usiku tarehe 15/4/2009.

Aidha, nahodha wa *MV Amana Pemba* alipaswa kutoa taarifa kwa kutumia simu ya *VHF* ambayo inasikika na Bandari, Polisi na vyombo vingine vya majini ili kupata msaada wa haraka.

Juhudi za uokoaji zilianza mara tu baada ya *TPA* kupata taarifa kupitia *MV Amana* Tanga na kutuma chombo chake cha *MV Aida Kondo* ambacho kiliongozana na *MV Amana* kwenda eneo la ajali kuwahi uokoaji. Hali ya mawimbi na upepo mkali vilizuia vyombo hivyo kufika eneo la ajali na kulazimika kurudi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15/4/2005, asubuhi, Kikosi cha Utafutaji, kikiongozwa na Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Tanga, kilianza kazi kwa kutumia boti za *TPA*, Polisi na magari kwa upande wa nchi kavu na helikopta ya Polisi angani. Maeneo mengi yalifikiwa hadi Ras Moa karibu na mpaka wa Kenya. Aidha, watu 32 waliokolewa kutoka kwenye ajali hii, baadhi yao waliokolewa na wavuvi na wengine waliokoka kwa kutumia majaketi ya kuokolea maisha ama *life jackets* na magodoro yaliyokuwa yamebebwa kama mizigo. Timu ya uokoaji wa Mkoa wa Tanga, haikupata mtu wa kuokoa wala maiti kwa muda wa siku mbili za juhudi za utafutaji na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, zoezi la kutafuta na kuokoa hatuwezi kusema lilichelewa. Hata hivyo, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa utafutaji na uokoaji pamoja na kuwaagiza waendesha vyombo, kuzingatia Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003 na Kanuni zake, kutumia vifaa vya mawasiliano na viashiria ajali wanavyokuwa navyo mara tukio la ajali linapoanza kujitokeza na kuwa na vifaa vya kuokolea maisha. Aidha, kwa upande wa Serikali, tutaendelea kutoa elimu ya usalama majini na kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu *Meli ya MV Victoria* kutengewa fedha kwa ajili ya matengenezo katika bajeti hii ili kuimarisha usafiri katika Ziwa Victoria, ilitolewa na Mheshimiwa Gosbert Blandes na Mheshimiwa Savelina Mwijage. Serikali haikuweza kutenga fedha kwa ajili ya matengenezo ya *Meli ya MV Victoria*, kupitia bajeti hii kutokana na ufinyu wa bajeti yetu. Hata hivyo, *MV Victoria* itaendelea kufanyiwa matengenezo kutokana na fedha za kampuni ya *MSC*. Sambamba na hatua hiyo, Serikali itaendelea kutafuta vyanzo vingine ili kuiongezea nguvu Kampuni ya *MSC* kwa kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni juu ya Serikali kununua *Meli* mbadala ya *MV Victoria* na *MV Liemba*. Serikali itaendelea na juhudi za kuzifanyia matengenezo meli hizi, ili ziwe salama na kuwa na ubora unaotakiwa. Aidha, itaendelea kuhamasisha wawekezaji binafsi kuwekeza kwenye vyombo vya usafiri majini kulingana na Sheria ya Usafiri Majini ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kuhusu Halmashauri za Manispaa ya Dar es Salaam kupewa mrahaba kutoka katika mapato ya Bandari. Hoja hii, ilitolewa na Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi. Serikali kupitia Sheria ya Bunge Na. 17 ya mwaka 2004, iliyounda Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*), *TPA* imepewa jukumu la kusimamia na kuendeleza bandari zote za mwambao na bandari za maziwa ya Tanzania, hivyo mapato yake yote yanaelekezwa katika kuendeleza miundombinu ya bandari nchini.

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam, ipo katika Manispaa za Temeke na Ilala. Licha ya kuwa ni kichocheo kikubwa cha shughuli za kiuchumi katika maeneo yanayoizunguka, pia *TPA* inalipa kodi za aina mbalimbali kwa Halmashauri za Manispaa hizo, ikiwemo *City Service Levy* na *Property Tax*.

Mheshimiwa Spika, takwimu za kipindi cha miaka minne iliyopita, yaani mwaka 2005/2006 mpaka 2008/2009 zinaonyesha kwamba, Mamlaka imechangia zaidi ya shilingi bilioni 1.608 kwa Manispaa ya Temeke na shilingi milioni 29,000,692 kwa Manispaa ya Ilala. Mamlaka pia katika kipindi cha miaka minne iliyopita, imetoa jumla ya shilingi Milioni 915, 000, 364 kusaidia shughuli za kijamii katika Manispaa hizo, kwa ajili ya ujenzi wa shule, hospitali na uchimbaji visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, hayo ni maeneo makuu ambayo nimeona niyatolee ufafanuzi wa jumla kwa kuunganisha michango ya Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Ufafanuzi ambao umetolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ni ufafanuzi wa mchango mmoja mmoja uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Naomba niseme kwamba, michango mingine ambayo sikuitolea ufafanuzi, ama haikutolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Naibu Waziri, yote itatolewa ufafanuzi kwa njia ya maandishi ambayo yatasambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo na ufafanuzi huo, naomba sasa kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. OMARI S. KWAANGW’: Mheshimiwa Spika, mwongozo!

SPIKA: Mwongozi wa Spika, Kanuni?

MHE. OMARI S. KWAANGW’: Kanuni ya 68(1) kuhusu utaratibu.

SPIKA: Endelea.

MHE. OMARI S. KWAANGW’: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 102, Ukurasa wa 65, inasema hivi:-

“Katika Kamati ya Matumizi Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kutaka kufanya mabadiliko katika Makadirio ya Matumiizi ya Serikali iwapo mabadiliko hayo hayatabadili madhumuni ya Fungu au sehemu yoyote ya Fungu husika”.

Mheshimiwa Spika, kidogo nilishtuka niliposikia ushauri wa Kamati ya Miundombinu kwamba, Mbunge akiwa na hoja na bahati nzuri ipo kwenye hoja yao, amesema kwamba, Mbunge akiwa na hoja, kwanza, aipeleke kwenye Kamati. Sasa ninataka mwongozo wako, Kanuni hii inamtaka Mbunge anayetaka kutoa maelezo yake wakati wa Kamati ya Matumizi, iwe wakati huo, sasa ina maana gani Kamati inaposema kwa siku zijazo Mbunge mwenye tatizo au hoja mahsusi katika Wizara fulani ni vyema akaenda kwenye Kamati husika kuwasilisha hoja yake ili ijadiliwe na kuzingatiwa na Kamati husika, kabla Kamati haijakamilisha kazi yake na kuandika taarifa yake kwa ajili ya kuwasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu? Najua Kamati inafanya kazi kwa niaba ya Bunge, lakini Kamati haiwezi kufanya kazi ya Bunge. Sasa naomba mwongozo wako

kabla hatujaingia kwenye Kamati ya Matumizi, maana inaweza ikatokea Mbunge tena akasimama.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Omari Kwaangw'. Pendekezo la Kamati ya Miundombinu linaleta mkondo mwingine ambao ni hiari kwa Mbunge kuufuata. Mkondo uliopo kwenye Kanuni hauwezi kuzuiwa na Maazimio tu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, kwa sababu hii ni haki iliyomo ndani ya Kanuni. Kwa hiyo, huu ndiyo utaratibu wa kufuata Mbunge akiridhika kwamba, ana haja ya kuleta hoja ya kuhamisha fedha bila kubadili madhumuni ya kifungu anachotaka, basi utaratibu haukubadilishwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia Kamati ya Miundombinu ilichofanya si kibaya, inatoa mkondo mwingine ambao kama Mbunge anataka kuungwa mkono na Kamati, basi aweze kufikisha kule, yote mawili yanaweza kufanyika. Ahsante sana. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji kuhusu hoja iliyo mbele yetu, kuna kitu ambacho katika Kanuni zetu hizi, Kanuni ile ya 101(2) inasema hivi:-

"Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika, wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi".

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 101(3), kinakataza hawezi kuzungumzia mambo zaidi ya mawili. Sasa nawaelekeza kwenye kile Kanuni ya 101(5), ambacho kinasema:-

"Muda wa kusema katika Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kutoa ufafanuzi hautazidi dakika tano".

Waheshimiwa Wabunge, pia Kanuni ya 101(4) inasema:-

"...Mbunge anayetaka ufafanuzi anaweza kuzungumza si zaidi ya mara mbili juu ya suala hilo".

Sasa Kanuni ya 101(4) na (5), tulizitengua na kusema kuwa ni dakika tatu, halafu Mbunge asiseme zaidi ya mara moja.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Bunge, ni mahali pa demokrasia, nadhani hapa kidogo tulikwenda mbali mno. Kwa hiyo, kwa kuwa leo tuna muda wa kutosha, nataka kupendekeza kwamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, alete hoja ya kutengua kile tulichotengua ili Wabunge waweze kuzungumza kwa dakika tano (5) na pale wanapokuwa hawakuridhika na ufafanuzi, waweze kurejea tena kusema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ile ya kwanza tuliyokuwa tunaitumia, ilikuwa inafanya Kiti kionekana kama kinatumia uimla (yaani nguvu tu), ambapo si vizuri. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, ili atoe hoja hiyo.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO: Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni ya 150, naomba kutoa hoja kwamba Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kuzungumza zaidi ya dakika tano na pia wapewe nafasi ya kutoa hoja zao zaidi ya mara moja wakati wa Kamati ya Matumizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Nisahihishe hapo siyo zaidi ya dakika tano, ni usiozidi dakika tano. Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo mbele yetu, ni kurejea kwenye Kanuni kama ilivyo, yaani Kanuni ya 101...

WABUNGE FULANI: Haijaungwa mkono!

SPIKA: Eeh, haijaungwa mkono kweli.

MHE. BALOZI DR. GERTUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika!

MHE. BALOZI DR. GERTUDE I. MONGELLA: Mheshimiwa Spika, kabla hoja hiyo haijaungwa mkono, ninapenda unipe mwongozo. Tukienda kwa utaratibu wa kutengua Kanuni, wakati kipindi hiki chote tumetumia Kanuni hiyo na mimi jana nilipewa maelekezo na Naibu Spika na nikayaheshimu kwamba, nisisimame tena mara ya pili na nisizungumze zaidi ya dakika zilizowekwa. Naomba mwongozo wako kama hii haitatupa hatari ya kwamba, kila wakati tunatengua Kanuni na Kanuni hii ni muhimu na ni msingi mkubwa katika kuendesha Bunge hili, isingekuwa vizuri iletwe *specifically* halafu tuijadili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tulikwishatengua Kanuni, tulichonacho hapa ni Wizara ambayo kwa namna ya pekee, imechukua mambo mazito mengi...

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliguna)

SPIKA: Aah! Mnisikilize basi. Sasa kwa nia njema tu, nilitaka muweze kupata nafasi, inavyoelekea hamtaki na isitoshe kwa mujibu wa Kanuni, hoja hii haikuungwa mkono. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tunarejea, nitawahoji kuhusu hoja iliyopo. Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo, ni ya kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2009/10. Hoja hiyo ilitolewa na kuungwa mkono, lakini kwa mujibu wa utaratibu uliomo katika Kanuni ya 100 na 101, nitamwomba sasa katibu atuelekeze hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 98 – WIZARA YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU

Kif.1001 - *Administration and General*..... Shs. 2,878,169,500/=

MHE. AZIZA S. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kifungu hicho hicho Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize, tangu *TRL* ichukue Shirika la Reli, kulikuwa na wafanyakazi ambao wameshafanya kazi miaka 28 nyuma, mpaka sasa wafanyakazi wale ajira yao haijulikana kwa sababu hawamo kwenye *pay-roll*. Lakini Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004, inaeleza wazi nafasi za wafanyakazi na haki zao, je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatueleza hatima ya wafanyakazi wale mpaka sasa hivi ikoje?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, naomba nitambue mchango wa maandishi wa Mheshimiwa John Cheyo, ambaye sikumtaja jina wakati nawatambua wale waliochangia hoja hii. Lakini pia naomba nitambue kuchangia kwa Mheshimiwa Ephraim Madeje, ambaye amechangia kwa kuongea, pia naye sikumtaja wakati nawataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watumishi wa *TRL*. Wakati *TRL* imechukua uendeshaji wa miundombinu ya *TRC*, wafanyakazi wale wote ambao walitakiwa kupungua kwa wakati huo, walipunguzwa na wale wengine ambao walibaki wameendelea kuwa katika ajira ya *TRL* na kuwa na makubaliano mbalimbali ndani ya *TRL*. Sina uhakika kama kuna wafanyakazi ambao mpaka hivi sasa hawajaingia katika *pay-roll* ya *TRL*, kama wafanyakazi hao wapo, basi tutahakikishe kwamba, wameingizwa kwenye *pay-roll* ili waweze kuwa wafanyakazi rasmi ndani ya shirika hilo.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati natoa mchango wangu katika Wizara ya Fedha, nilizungumzia suala la *TICTS*. Bandari jukumu lake kubwa ni kupakua na kupakia mizigo na siyo kuhifadhi. Hivi sasa bandari ya Dar es Salaam, kuna mlundikano mkubwa sana wa makasha kwa sababu tu, kampuni ya *TICTS* imeamua kukumbatia kuhifadhi makasha badala ya kuyaondoa na vilevile ukizingatia kwamba, Serikali ilishawishi kuwaambia Watanzania kuwekeza katika ujenzi wa *ICDs* na Watanzania wamefanya hivyo. Naomba Serikali itoe ufafanuzi, inasema nini juu ya

kutotumika kwa zile *ICDs*, ilihali kuna mlundikano mkubwa wa makasha bandarini ambao unasababisha ufanisi mbovu wa bandari yetu, jambo ambalo linasababisha baadhi ya watumiaji wa bandari hii kutotumia bandari yetu na kuhamia bandari zingine za nje ya nchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtutura, hebu tuelimisha *ICDs* Mwenyekiti pia hajui, ni nini hii? Ili na wenzio tufahamu.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: *ICDs* ni *Inland Container Terminal*.

MWENYEKITI: Ni nini?

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: *Inland Container Depots*

MWENYEKITI: Aah, *Inland Container Depots*, ok! Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri kwa ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mtutura, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kwamba, Serikali imeendelea kuhamasisha bandari iweze kutumia *ICDs* zilizopo au maeneo yale ya kuhifadhi makasha nje ya bandari. Mpaka hivi sasa sekta binafsi imejenga vituo vya makasha nje ya bandari vinavyofika Kumi (10) na kwa msisitizo, Serikali imeelekeza *TICTS* na wadau wanao Shirikiana na *TICTS* ili kuweza kuondosha makasha haya bandarini na kuyapeleka kwenye vituo vya makasha vile vya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakifanya hivyo mpaka hivi karibuni kulipotokea mzozo kidogo kati ya *TICTS* na wale wenye vituo vya kuweka makasha. Lakini tatizo hili sasa limetatuliwa. Limetatuliwa kwa maana *TRA*, Mamlaka yetu ya Mapato, imetoa maelekezo mahususi ya namna ya kutumia *ICDs* hizi. Kwa hivyo, siyo utashi wa mdau yoyote kule bandarini wa kupeleka makasha kwa namna anavyopenda ama kwenye *ICD* hii au katika *ICD* ile, bali *TRA* imetoa maelekezo mahususi na imetoa matangazo hayo kwenye magazeti, Kwa mpango huo, tuna imani kubwa kwamba, utaondosha utata wa kuhamisha makasha na kuyapeleka katika vituo vya nje ya bandari.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kifungu hicho hicho. Wakati nachangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimezungumzia barabara ya Kisesa-Usagara, ambayo iko kwenye *package* moja na ile ya Nyanguge - Musoma. Mwaka huu haijatengewa pesa yoyote, imetengewa shilingi milioni 100 tu, lakini miaka miwili iliyopita ilikuwa inatengewa shilingi bilioni 1.4. Sasa nilitaka nielewe hii barabara, itajengwa na nani na lini itaanza kujengwa sambamba na kulipa wananchi ambao tayari maeneo yao yameishaanishwa, kwa maana ya kwamba, yamewekewa alama 'X',

hawajafidiwa na haweelewi. Naomba jibu ili wananchi wa maeneo hayo waweze kufahamu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ya Mheshimiwa Jacob Shibiliti, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika mwaka huu wa fedha tumeshindwa kutenga fedha katika barabara zote kama ambavyo tulikuwa tumefanya mwaka jana na mwaka juzi. Kufuatana na ufinyu wa fedha, kuna maeneo ambayo imebidi tupunguze na kuna maeneo ambayo imebidi tupeleke hela sehemu ambazo mwaka jana hatukupeleka fedha. Kwa hivyo, hili ni eneo mojawapo. Tunasikitika kufanya hivyo lakini hatukuwa na njia ya kufanya zaidi ya kugawa kile ambacho kilikuwepo kwa maeneo ambayo yanahitaji kujengwa barabara zake. Nakushukuru sana Mwenyekiti.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nazungumzia Fungu hilo hilo, mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazungumzo yangu wakati nachangia hoja hii, niliuliza kwa nini barabara ya kutoka Musoma kuunganisha na Arusha, haijatengewa fedha yoyote, ijapokuwa kwa miaka mingi sana Serikali ilikwishatoa uamuzi kwamba, barabara hiyo ijengwe lakini inaonekana kwamba, Serikali inasita.

Wakati Mheshimiwa Waziri analeta hoja yake hii alisema anazungumzia tu mambo ambayo yako kwenye *manifesto* ya Serikali, kama haiko kwenye Ilani ya Chama, basi hasemi. Sasa hii haijaandikwa kwenye Ilani ya Chama mwaka huu, wala mwaka jana, je, ni kigugumizi gani kimetokea? Hiyo barabara itajengwa lini? Mbona fedha ziliwahi kutengwa huko nyuma na Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani ulikuwa Waziri wa Miundombinu na ulifanya hata *bridge* ya Kirumi, leo ni miaka 45 sioni chochote kinakwenda, utawambiaje watu wa Mara? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima sana, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mkono, Kaka yangu, amenifuata mara nyingi kwa suala hili na suala hili la barabara ya Nata – Mugumu - Roliondo hadi Mto wa Mbu Arusha kuunganisha Musoma pamoja na Arusha, amelizungumzia mara nyingi.

Ni kweli kwamba ni mradi wa siku nyingi na ni mradi ambao Serikali imeendelea kuutafutia pesa awamu kwa awamu. Mwaka wa fedha uliopita, tuliutengea pesa jumla ya shilingi bilioni 1.5, mwaka huu wa fedha, sio kweli kwamba, mradi huu hatukuutengea pesa, mradi huu umetengewa fedha. Mwaka wa fedha 2009/2010, ukurasa wa 186, kifungu kidogo cha 4149, katika *Volume IV*, zimeonyeshwa jumla ya shilingi milioni mia tisa (900,000,000/=), na kazi ambayo inaweza kufanywa. Hii ni barabara ndefu sana, ina zaidi ya kilomita 450, kwa hivyo, ni mradi mkubwa. Ili iweze kujengwa, taratibu zote za

ujenzi wa barabara inabidi zitekelezwe, moja, ikiwemo upembuzi. Namba mbili, ikiwemo usanifu ama *design*, halafu ndiyo uje katika hatua ya ujenzi wa barabara hii ngumu ambayo inabidi ujenzi wake uwe makini sana.

Sasa pesa ambazo zilitengwa mwaka jana na Bunge likaidhinisha, ni kwa ajili ya *design* shilingi 1.5 bilioni, pesa ambazo zimetengwa mwaka huu pia milioni mia tisa (900,000,000) ambazo zinaonekana kwenye vifungu hivyo, Bunge lako Tukufu, likipitisha ni kwamba pesa hizi milioni mia tano (500,000,000) zitakwenda kuongezewa katika deni la *design* ili *Designer* aweze kukamilisha kazi, lakini pesa nyingine iliyobaki katika kasma hiyo, itaenda kufanya matengenezo ambayo yataiwezesha barabara hii ipitike wakati utaratibu wa ujenzi unaendelea. Kwa hivyo, si kweli kabisa kwamba hatukutenga hela. Hela zimetengwa na mimi mwenyewe hii barabara naifahamu vizuri sana, nilipanga mwaka huu kuitembelea tarehe 02/05/2009 lakini najilaumu kwamba nilikubali ushauri wa Mheshimiwa DC wa Serengeti. Nilipofika Musoma, akaniambia Mheshimiwa wala usiende huko, huwezi kupita. Nikakubali kutokwenda, najilaumu sasa, bora ningekwenda halafu nikakwama ingekuwa vizuri zaidi. Nakushukuru Mwenyekiti.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kifungu hicho kinachohusika, Mshahara wa Waziri. Mimi nashukuru majibu ya Serikali, kuhusu barabara hii ya Manyoni –Itigi – Chaya - Tabora, yamekaa vizuri lakini ili kumbukumbu zikae vizuri, ninapenda Waziri aanishe wazi kwamba, *Status* ya barabara hii ikoje, iko katika hatua ya kupata Mkandarasi au iko katika hatua ya upembuzi yakinifu na la muhimu zaidi, inaanzia kujengwa kutoka wapi? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ungeuliza kama inajengwa tu, hii kutoka wapi...

Waheshimiwa Wabunge, katika mambo ya utawala, kuna kitu kinaitwa *Zero-Sum-Game* yaani unataka kusema sehemu moja kikipatikana, kwingine iwe sifuri. Moyo wa namna hiyo hausaidii chochote, sema tu sehemu yangu itajengwa, hiyo ndiyo hoja yenyewe.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya ndugu yangu, Mheshimiwa Lwanji kama ifuatavyo:-

Barabara ya Manyoni - Itigi itajengwa na itajengwa kutokea Manyoni. Sasa hivi tuna makubaliano na nchi ya Iran, tunangoja kusaini mkataba ule wa kutoa fedha. Tukifanikiwa kuingia mkataba na nchi ya Iran na hata kama hatukufanikiwa bado mradi wa Manyoni – Itigi – Chaya, utajengwa kwa kuanzia Manyoni.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba ufafanuzi, kifungu hicho hicho.

Katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza pamoja na mengine, kumshauri Waziri au Wizara kwamba tatizo kubwa la *TRL* ni mtaji. Katika majibu yake ya ufafanuzi hapa, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba kwa kweli mtaji ni dola milioni 20 tu ambazo zimechangiwa kwa uwiano wa 10.2 kutoka *RITES* na 9.8 kutoka Serikalini.

Katika mchango wangu wa maandishi, niliishauri Serikali kwamba ili tuweze kuona *seriousness* ya *investor* na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya mradi huu wa reli, tupandishe *authorised capital* mpaka takribani 200 *millions dollars*. *They so called initially issued and called capital*, isiwe chini ya milioni 100, hapo ndio tutapima *seriousness* ya *investor* na ndio tutajua kama anaweza au hawezi.

Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri ameeleza tu kwamba tuko mbioni kuongeza mtaji, sawa, lakini bado naomba ufafanuzi juu ya huu mtaji unaongezwa kwa kiasi gani, Serikali itazingatia ushauri wangu au watakuwa chini ya hapo? Naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa kaka yangu Siraju Kaboyonga kama ifuatavyo:-

Hesabu ambazo nimezitoa katika majumuisho yangu ni zile *contributions* ambazo zilitolewa na wanahisa hawa wawili wakati wanaiunda *TRL*. Lakini ni kweli kwamba mahitaji ya mtaji ili kuweza kuiendesha reli hii ya *TRL*, ni makubwa kushinda *contributions* hizo ambazo zimetolewa. Serikali ilielewa hivyo na iliingia katika ubia huu mahsusi kwa kujua kwamba mahitaji ya kuiendesha reli hii ni makubwa sana na hakuna katika walioomba kuendesha miundombinu hii walikuwa na uwezo wa fedha hizo nyingi.

Kwa hivyo, Serikali imeingia pale ili kuwezesha kupata mtaji huu. Mtaji ambao mpaka sasa umekisiwa una jumla ya Dola za Kimarekani 160 na katika hizi milioni 33 tayari zilishakopwa kutoka *World Bank*, shilingi milioni 44, mkataba wake ulishasainiwa na *IFC* na sehemu ya mkopo huo imeshaanza kutumika. Shilingi milioni 14 zilishaidhinishwa, shilingi milioni 7 zimetolewa na *TRL* walishaanza kuzitumia ingawa sasa hivi tumesimamisha kwa ajili ya mchakato wa majadiliano kati ya wanahisa kwa maana ya Serikali na *RITES* na pia *IFC* ambayo ni wakopeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali imeazimia kukopa na imekubaliwa na *World Bank* kuikopesha Dola za Kimarekani milioni 40 na tofauti katika hiyo maana yake ni Dola za Kimarekani 43 milioni, Serikali imechukua jukumu hilo la kuzitafuta hizi Dola milioni 43 ili ziweze kuunganishwa na Dola milioni 40 tutakazokopa *World Bank* ambazo zitakuwa dola milioni 83. Hayo ndiyo mahitaji ya mtaji kwa kipindi cha miaka kama mitatu inayokuja. Mchakato huo umefanywa, tuna imani kwamba kila kitu kimekaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko katika kuhakikisha kwamba mpango wa biashara umekaa vizuri na mpango wa biashara ndio unaotoa mahitaji ya mtaji ni nini na kwa

sababu kikundi kazi mahsusi kinafanya kazi hiyo, tutapata kujua kama ni Dola 200 au Dola milioni 160 au nyingine. Lakini pia mazungumzo ya mkataba yenyewe utatuwezesha sisi kufanya maboresho yale ya kimkataba ambayo yatawezesha reli hii sasa kwenda kwa kasi hiyo ambayo inahitajika kwa Watanzania. Nakushukuru sana.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Awali ya yote, nimpe sana pole Mheshimiwa Dr. Shukuru kwa changamoto alizopata lakini nimpongeze kwa jinsi ambavyo amekuwa akijibu hoja zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia kwa maandishi, nilielezea masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo kumekuwa na ajali nyingi sana hasa katika miteremko mikali na kona katika madaraja yanayojengwa sasa hivi. Nikatolea mfano wa pale Nduruma, Arusha lakini vile vile nikatolea mfano wa kule Sekenke na sasa hivi pale Daraja la Ruvu. Kwa kweli kumekuwa na ajali nyingi lakini vile vile kumekuwa na ujambazi wa kutisha. Nimeona pia katika nchi nyingine kwa kweli katika miteremko ya aina hiyo, huwa kuna matuta, unakuta matuta haya mara nyingi ndiyo yamekuwa yanasababisha ajali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie wana mikakati gani kuhakikisha kwamba wanapunguza ajali pamoja na wizi katika maeneo ambayo wameweka matuta makubwa sana?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu hoja za Mheshimiwa Lyimo kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu nikubaliane naye kwamba kweli hizi ajali zinatokea katika haya madaraja na kwenye miteremko mikali. Lakini kuhusu suala la matuta, tulishatoa maelezo hapa kwamba tunataka kuweka mfumo wa matuta unaofanana badala ya kuwa maeneo mengine matuta makubwa, maeneo mengine matuta madodo, nimesema na Kigogo, ili kuhakikisha kwamba magari yanakwenda kwa mwendo mzuri. Lakini vile vile tunataka kukubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutashirikiana na wenzetu wengine katika suala la kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo ili hata kama ajali imetokea basi tuweze kukabiliana na tatizo hilo la ujambazi. Lakini vile vile ulinzi shirikishi ambao wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani wanauendesha, nadhani unaweza kusaidia sana kwa kushirikiana na wenzetu wanaoishi katika maeneo haya. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Lugha ya Kiswahili inaendelea kukua na hapa tuko Makao Makuu, wenyeji wa hapa badala ya madogo huwa wanasema madodo, kwa hiyo tunaweza kulikubali hili.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu hilo hilo, mshahara wa Waziri.

Katika mchango wangu wa maandishi na maoni ya Kamati ya Bunge, nilizungumzia juu ya reli ya kutoka Kaliua – Mpanda na kwa kuwa kuna shehena kubwa ya chakula ambacho kinataka kihamishwe kutoka Mpanda kupelekwa Dodoma na hali ya reli ni mbaya sana na kwa kuwa kuna fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya

utengenezaji wa reli, nataka kusikia kauli ya Mheshimiwa Waziri, ana mpango gani juu ya kuimarisha reli ya kutoka Kaliua - Mpanda ili iweze kufanya kazi ambazo zimekusudiwa?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa ndugu yangu Arfi kama ifuatavyo:-

Suala lake ameliwasilisha kwetu kimaandishi katika michango yake na kwa kipande hiki cha Kaliua mpaka Mpanda kiko ndani ya mpango wa *TRL* wa maboresho ya njia ya reli yenyewe. Kwa bahati mbaya sana, sina takwimu za kifedha, kiasi gani ambacho tunategemea kukiweka kule lakini naweza kumhakikishia kwamba katika mwaka huu wa fedha, kuna mpango huo wa kuimarisha miundombinu ya reli katika njia hiyo. Lakini pia kwa umuhimu wa hoja aliyotoa, mimi kama Waziri mwenye dhamana, nitalifuatilia suala hili ili kuhakikisha kwamba kipindi hiki ambacho chakula kwetu ni muhimu sana wakati kuna tishio la uhaba wa chakula duniani hatuna kimbilio la urahisi, usafiri wa chakula tutaupa *priority* katika kutekeleza miundombinu yetu ya usafirishaji. Nakushukuru Mwenyekiti.

MHE. OMARI S. KWAANGW’: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ni suala la ufafanuzi. Kwanza namshukuru Waziri kwa kueleza kwamba barabara hii ya Dodoma - Babati wako kwenye mazungumzo na *ADB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka ufafanuzi juu ya ushauri wa Kamati ya Miundombinu ambayo sijasikia kama Waziri ametoa ufafanuzi. Kamati ya Miundombinu imesema hivi:-

“Serikali itafute walau kiasi cha shilingi bilioni 45 ili ujenzi wa barabara ya Dodoma - Babati uanze mapema iwezekanavyo”.

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu akaendelea kusema kwamba:-

“Mheshimiwa Spika, nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imepokea na kukubali ushauri huo na kwamba itautekeleza mapema iwezekanavyo”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasikia kauli ya Waziri kwamba hizi shilingi bilioni 45 ambazo Kamati imesema hapa, kama kauli hii ni sahihi na kwamba Serikali imekubali na itatekeleza mapema iwezekanavyo au namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Omari Kwaangw’ kama ifuaatavyo:-

Suala hili limekuwa ni suala la joto sana na mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na wataalamu wenyewe, tumeshiriki kikamilifu katika mjadala na Kamati ya Miundombinu. Hoja hii kama ilivyotolewa ushauri na maelekezo ya Kamati ya Miundombinu, imepokelewa na Serikali na kwa kuanzia Bunge hili Tukufu likipitisha bajeti hii, kuna shilingi bilioni 5.6 ndani ya kifungu hicho.

Lakini kusema kwamba Serikali imekubali jukumu hili maana yake tutatafuta fedha zinazopungua katika kifungu hicho cha barabara ya Babati - Dodoma ili kutimiza kiwango ambacho kimetajwa cha shilingi bilioni 45. Jukumu hilo Serikali imekubali na tutatafuta ili tihakikishe kwamba kazi katika barabara hiyo imeanza mapema iwezekanavyo.

MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika hotuba ya Waziri Mkuu, nilisema na katika hotuba hii nikaandika, kwa kuwa wasafiri wanaotumia njia ya treni kuanzia Dar es Salaam kwenda Kigoma wakifika pale stesheni kwa kweli wananyanyasika vibaya sana na kwa kuwa sasa hivi hakuna *buffet car* ambayo huwa inatengwa kwa ajili ya kwenda Kigoma na wananchi wanalifahamu suala hilo. Kwa hiyo, wakati wanaposafiri huwa wanachukua ndoo za plastiki wanahifadhia chakula chao lakini wanapofika pale stesheni Dar es Salaam wananyanyaswa vibaya sana, wanaambiwa watoe kile chakula ndani ya ndoo waweke chini halafu zile ndoo zikapimwe. Kwa kuwa Serikali hii iko chini ya Chama cha Mapinduzi na wanaonyanyaswa ni wananchi wa Chama cha Mapinduzi, naiomba Serikali leo iweze kuwafafanulia wananchi hao ni kitu gani kinachoendelea kati yao. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ikiwa hilo linatokea, ni wananchi wote tu linawapata kwa sababu hatuasafiri kwa vitambulisho vya vyama.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nikiri kwamba Mheshimiwa Sijapata Nkayamba tumeshazungumza naye kuhusu kero hii ya vyakula vya wasafiri katika Shirika la reli. Nilipokuwa najibu hoja za Wabunge hapa, nilikiri kwamba kwa sasa hivi hakuna *buffet car* ya kwenda Kigoma lakini jitihada zinafanyika kufanya ukarabati na hatimaye huduma hiyo ya *buffet car* kwa kwenda Kigoma iweze kurejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili suala la kumwaga chakula, kusema kweli tulipolifuatilia, tuliona kwamba kinachofanyika pale kwanza ni usalama wa abiria wenyewe kuona kama chakula hicho kinaweza kikawa kinawafaa, lakini nataka tu niseme sisi tutakuwa karibu sana kufuatilia kuona kwamba mtu ambaye amebeba hifadhi ya chakula chake cha kumwezesha kwenda nacho safarini wakati huku mbele hakuna huduma nyingine yoyote, viweze kukubalika ili wasafiri waweze kupata huduma hiyo kwa kujitegemea wenyewe.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1001, mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu, nilieleza kuhusu kutokuwa na mafuta katika injini na kusababisha treni kusimama njiani tena maporini. Hapa Waziri

hajasema anachukua hatua gani ili kusahihisha suala hili ili wasafiri wasipate adha kama nilivyoizungumza, kusimama porini pia magenge yamefungwa hawana usalama kabisa.

Kwa bahati, leo asubuhi nimepiga simu Tabora, treni huwa inaondoka saa 1.45 mpaka saa 3.45 hawajaondoka, mafuta hamna kwenye injini, je, suala hili litatazamwa namna gani? Kama reli inatengenezwa lakini je usafiri wa hawa watu, usalama wao uko wapi? Wanaweza wakaondoka Tabora wakafika porini wakasimama kama walivyosimama wiki iliyopita. Naomba ufafanuzi wa Waziri na hatua anayochukua?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa dada yangu Tatu Ntimizi kama ifuatavyo:-

Kwa lile ambalo alikuwa amelitolea maelezo ni kwamba treni hiyo ambayo ilisimama kwa hoja kwamba imeishiwa mafuta tokea Tabora, nimetaka maelezo kwa wataalam na wamesema sio kwamba iliishiwa mafuta. Kichwa cha treni hiyo kilikuwa kimepata hitilafu kwa hiyo ikabidi ipigwe simu ili treni ya mizigo ambayo ilikuwa inaelekea Tabora igeuze njia ivute treni hii ya abiria ili wasikae pale kwa sababu ya hitilafu ya kichwa kile cha treni. Sasa hicho ndicho kilifanyika, treni ya mizigo ikaenda kuvuta lakini kwa sababu ilikwishatoka safarini, kasma yake ya mafuta katika hesabu za kudhibiti mafuta ndani ya vichwa hivi vya treni, kwa sababu tunapokwenda watu wanakuwa na mahesabu mengi na tofauti, kwa hiyo mafuta yake yakawa sio ya kutosha, ndiyo maana nayo ikaja ikapata matatizo wakati inavuta kichwa kile ambacho kilikuwa kimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna tatizo la fedha za kununulia mafuta kwenye Shirika letu la *TRL*. Tunaendelea kufuatilia tuhuma hizi ambazo zinatokea na hii ya karibuni tutaendelea kuifuatilia kwamba inatokana na kitu gani. Lakini naomba Bunge lako Tukufu liamini kwamba tatizo la ununuzi wa mafuta ndani ya Shirika letu la *TRL*, halipo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*.....Shs.755,132,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning*.....Shs.1,099,019,500/=

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwenye *sub-vote* 221200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoelewa, Kitengo cha Sera na Mipango, ni Kitengo nyeti sana katika Wizara. Katika kifungu hiki cha Usafiri wa Ndani (*Travel – In*

– *Country*), ukiangalia fedha zimepungua kwa takriban shilingi milioni 400 ukilinganisha na mwaka jana. Ninavyoelewa, sasa hivi kuna barabara nyingi sana zinajengwa na hivyo nilifikiri kwamba hiki kifungu ni kwa ajili ya wataalamu kwenda kuangalia Wakandarasi wetu wanavyofanya kazi, sasa naomba kuelewa ni kwa nini kifungu hiki kimepungua kwa zaidi ya karibu shilingi 400 ukilinganisha na mwaka jana?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Mbunge, ni sahihi kabisa lakini kama ambavyo tulishataarifiwa kuanzia wiki iliyopita, kulikuwa na mabadiliko ya muundo wa Wizara. Katika miaka ya nyuma kwenye hiki kipengele cha Sera na Mipango zilikuwepo Idara zingine ambazo zilikuwa zinaangukia katika kifungu hiki, kwa mfano, majengo na watu wa TEMESA walikuwa wanaangukia hapa. Kwa hiyo, fungu lilikuwa kubwa katika kipindi cha nyuma lakini baada ya mabadiliko ya muundo, vifungu vile vingine vimehamishiwa katika sehemu zingine, kwa hiyo fedha zikapungua pia.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Information, Education and
Communication*Shs.127,366,900/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 – *Procurement Management Unit*.....Shs.129,966,510/=

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba tu nifahamu kidogo. Kwa kuwa katika manunuzi imeonekana kidogo hali ya utaalamu hasa katika kuandaa mikataba na kuhakikisha kwamba mikataba hiyo inatangazwa kwa wakati kumekuwa na upungufu. Nilikuwa naomba tu nipate ufafanuzi kwamba Wizara imechukua hatua gani katika kuboresha Kitengo hiki?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Kitengo hiki cha *Procurement Unit*, ni Kitengo ndani ya Wizara yenyewe, kwa sababu ile Idara nyingine ya *Procurement perse* imeshahamia Wizara ya Fedha kuanzia mwaka huu. Lakini vile vile niseme tu kwamba ndani ya Wizara katika kuhakikisha kwamba Kitengo hiki kinafanya kazi ipasavyo kwa maana ya kuhudumia Wizara, tunazingatia tu ile Sheria ya Manunuzi ambayo iko kwa mujibu wa sheria.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - <i>Internal Audit Unit</i>Shs.283,113,000/=
Kif. 1007 - <i>Legal Services Unit</i>Shs.118,947,000/=
Kif. 1008 - <i>Management Information System Unit</i>Shs. 98,207,000/=
Kif. 2002 - <i>Technical Services Division</i>Shs. 7,647,177,200/=
Kif. 2003 - <i>Transport Division</i>Shs.0/=
Kif. 2004 - <i>Communication Division</i>Shs.0/=
Kif.2005- <i>Transport Infrastructure Division</i>Shs.211,929,946,690/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 2006 - *Transport Service Division*.....Shs. 45,296,099,700/=

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye programu hii ya 20, *sub-vote* 2006, kifungu kidogo 230400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kupanga mpango wa kununua kivuko kipya cha Lugezi Kisolya. Lakini katika masuala ya *maintenance*, kivuko kile kwa sasa kina hali mbaya na kinavutwa na kamba. Fedha ninazoziona hapa ni shilingi milioni 21, naona kama ni kidogo. Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi, je, kivuko hiki kwa sasa kitapewa kipaumbele katika kufanyiwa *maintenance*?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Kirigini. Serikali kwa kutambua changamoto zilizopo kwenye kivuko hiki cha Kisolya, imefanya maamuzi ya kununua kivuko kipya. Lakini mpaka kivuko kipya kitakapopatikana, tutaendelea na kukifanyia matengenezo kivuko hicho ili kiweze kutoa huduma inayofaa. Najua tumeitengea fedha zaidi ya hizi shilingi milioni 21, tumetenga jumla ya shilingi milioni 100, za matengenezo, lakini sasa hivi kwa haraka haraka sijui ni kifungu gani ambacho tumeweka fedha hizi. Tunaelewa tatizo hilo na tutalishughulikia na fedha zimetengwa za kutosha kwa ajili ya kazi hiyo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - <i>Supplies and Services</i>Shs. 0/=
Kif. 5002 - <i>Safety and Environment Division</i>Shs.404,185,000/=
Kif. 6002 - <i>Road Division</i>Shs.0/=

MPANGO WA MAENDELEO

FUNGU 98 – WIZARA YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU

Kif. 1001 - *Administration and General*.....Shs.280,000,000/=
Kif. 1003 - *Policy Planning*.....Shs. 4,914,900,000/=
Kif. 2002 - *Technical Services Division*.....Shs.24,685,000,000/=
Kif. 2003 - *Transport Division*Shs. 0/=
Kif. 2004 - *Communication Division*.....Shs.0/=
Kif. 2005 - *Transport Infrastructure Division*....Shs. 537,368,334,000/=

MHE. DR. SAMSON F. MPANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi naulizia barabara ya kutoka Kipatimo kwenda Njia Nne. Hii barabara ilipangiwa fedha kutoka *HIPC* na matokeo yake barabara ile ilitokea Kipatimo ikaishia Chumo kutokana na upungufu wa pesa, Serikali inasema nini kuhusu kipande kilichobakia kutoka Chumo mpaka Njia Nne.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufafanuzi kuhusu hoja ya Mheshimiwa Dokta Mpanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kumbukumbu zangu, barabara hii ni barabara ambayo haikuwa kwenye mpango wa *TANROADS* wa kuhudumiwa na Wizara, inayofahamika ni ile ya kutoka Tingi – Kipatimo. Sasa katika mpango huu wa *HIPC*, barabara hii haikufika Njia Nne ikaishia tu pale Chumo. Hivyo niseme kwamba nitashirikiana na TAMISEMI ili kupata ufafanuzi wa suala hili ili mamlaka husika ziweze kuikamilisha hiyo barabara na kuwaridhisha wananchi wa maeneo hayo.

MHE. ELIZABETH N. BATENGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 98, Kifungu cha 2005, kifungu kidogo cha 4287, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Bukoba na Mpanda umepangiwa shilingi bilioni nne, milioni mia tano na sitini. Nilipokuwa nachangia, niliomba kufahamu kwa nini vimechanganywa lakini pia nijue na wananchi wajue uwanja wa ndege wa Bukoba umetengewa kiasi gani cha fedha? Naomba ufafanuzi huo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi ufuatao kwa hoja ya Mheshimiwa Batenga, ni kweli kwamba viwanja hivi viwili vimetengewa pesa kwa pamoja katika kifungu hiki kidogo cha 4287 kwa viwanja vya Bukoba na Kiwanja cha Mpanda. Viwanja hivi, ni muhimu sana na tuna mpango wa kuhakikisha kwamba hatua kwa hatua tunaenda kuviboresha mpaka viwe viwanja ambavyo vinaweza vikatoa huduma inayoendana na matarajio ya wananchi. Mchanganuo wake ambao tutajitahidi katika miaka inayofuatia iwekwe tofauti, ni kuwa kiwanja cha Bukoba chenyewe kimetengewa jumla ya shilingi bilioni mbili, milioni mia tano na sitini na kile cha Mpanda kimetengewa jumla ya shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo ndiyo huo, TAA ndiyo itasimamia kazi hii, wao watatumia kasma hizo kwa ajili ya viwanja viwili tofauti.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, *subvote* ya 4117, katika mchango wangu, nilikuwa nazungumzia barabara kutoka Nangurukuru kwenda Liwale, hapa ipo Nangurukuru lakini siyo kwenda Liwale, kuna maeneo mengine, nashangaa katika barabara hii ambayo pia ni ahadi ya Rais kwamba itumike kipindi chote cha mwaka kwa kiwango cha chngarawe, Serikali haijasema chochote, je, hata hiki kiwango cha changarawe kinashindikana Mheshimiwa Waziri? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki nilikuwa sijakipata, tuko nadhani ukurasa 188.

MWENYEKITI: Ni ukurasa wa 187, pale juu, arudie swali?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba haijatengewa pesa siyo kweli kwa sababu katika kifungu hicho 4117 Nangurukuru – Mbwemkulu, imetengewa fedha kwa mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi milioni mia moja na sabini, kifungu hicho kimetengewa fedha siyo kweli kwamba hakijatengewa fedha.

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakujibu swali ni Nangurukuru – Liwale, siyo Mbwemkulu?

MWENYEKITI: Huruhusiwi kusimama mara ya pili, hilo ndilo tulilikataa, basi tena, tunafungwa na Kanuni.

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi, *Vote 98, Subvote 2005, Item 4180*, ukurasa 189, ni kuhusu barabara ya Tunduma Sumbawanga. Kwenye *item* hii, inaonekana barabara hii imepewa shilingi bilioni mbili na milioni mia moja ishirini kwa ajili ya *detailed design na construction* wakati barabara hii kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, tumeambiwa itanza kutengenezwa mwezi Disemba, je, wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi na wale wa Rukwa waamini kwamba michoro hiyo na usanifu itakwisha katika miezi minne ijayo na barabara ianze kutengenezwa mwezi Disemba?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Dokta Luka Siyame kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Tunduma –Sumbawanga, ni moja katika miradi ambayo inafadhiliwa na wenzetu wa Marekani chini ya Shirika la *MCC*. Kazi ya uandaaji imefikia hatua nzuri na hivi sasa tunategemea tuingie kwenye hatua ya ujenzi kwa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *MCC* wanapotoa pesa ya kigeni kwa ajili ya ujenzi, sisi Serikali tuna dhamana ya gharama zingine kama vile za kulipa fidia kwa wananchi wale ambao wapo katika maeneo yale ambayo yatatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.

Hizo pesa ndiyo ambazo tumeziweka katika kifungu hiki, zimeandikwa *detail design and construction* lakini *construction* hailipwi na Tanzania na *detail design* imemalizika, kwa hivyo, ni mlolongo wa taratibu za usanifu pamoja na *construction* lakini kwa *component* ya Serikali. Kwa hivyo, hizi ni hela tu za Serikali kwa ajili ya kulipa fidia wananchi katika maeneo hayo.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Fungu 98, *subvote* 2005, *Transport and Infrastructure* ukurasa 188, *item* 4209, nilikuwa na mawili lakini Kanuni kama inavyotukataza nitasema moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *construction of Mwanza and Kigoma Airport*, mwaka juzi na mwaka jana, utaratibu ulikuwa huu huu, kwamba fedha za Mwanza na Kigoma Airport ziliwekwa pamoja. Mwaka juzi 2007 na 2008, ilikuwa ni hivyo hivyo, matokeo yake ikawa kwamba uwanja wa ndege wa Kigoma tuliishia kufyekewa majani na hatimaye tukaambulia mashine ya *screening* hii ya dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa sababu zimewekwa pamoja na kwa sababu ile ile, sisi tufyekewe nyasi halafu uwanja wa ndege wa Mwanza ukaimarishwe *runway*, naomba ufafanuzi kwa Waziri, je, sasa si ni zamu yetu Kigoma ili hizo fedha sasa shilingi bilioni 6.6 zipelekwe kutengeneza *runway* ya lami, maana nakumbuka wenzangu wa Mwanza wamekiri wenyewe kwamba *runway* yao ni kati ya *runway* zilizo bora katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni zamu ya Kigoma sasa, hizi shilingi bilioni 6 zipelekwe Kigoma zikatengeneze *runway* ya Kigoma kwa sababu tumesubiri miaka miwili, naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mwenyekiti amekwishakuwaasa Waheshimiwa Wabunge, tusiwe na utaratibu wa *Zero-Sum Game*, yaani nipate mimi wale wa upande wa pili wasipate chochote, lakini Waziri labda unaweza kueleza vinginevyo.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hoja hii aliifikisha Mheshimiwa Mbunge na kama katika kasma zingine ambazo viwanja vimeunganishwa na hii pia ningependa kuitolea ufafanuzi kwamba kasma hii ambayo hapa inaoneshwa kwa hela za ndani, milioni mia saba themanini na mbili, mgao wake ni kama ifuatavyo. Kwa kiwanja cha Kigoma kimechangiwa jumla ya shilingi bilioni mia mbili kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya *runway* lakini pia tunaushirikiano na *MONAC* kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya kiwanja kile. Bado hakijafikia hatua ambayo tutaweza kuanza kuwekea lami *runway* lakini kwa kasma hii na kwa ushirikiano na shirika hili la kimataifa ambalo linahudumia wenzetu kule wa *DRC*, ni kwamba wao pia watachangia kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya miundombinu ndani ya mwaka huu wa fedha, kwa hiyo tunategemea tutakuwa tumefikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mwanza zimetengwa shilingi milioni mia tano na themanini na mbili na pia kasma ile *foreign* inaonekana hapa *forex* katika kifungu hicho hicho, kwa sababu tuna mkataba mahsusi pamoja na *BADEA* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika kiwanja cha Mwanza. Hatuna uwezo wa kuhamisha hela zile za *BADEA* kuzipeleka Kigoma, lakini tutaendelea kujitahidi kiwanja hiki cha Kigoma kitafanyiwa kazi vizuri na kinaendelezwa ili kufikia kiwango cha kuridhisha siyo tu kwa watu wa Kigoma lakini kitaridhisha Tanzania nzima katika harakati za kujenga uchumi wetu.

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza ufafanuzi juu ya suala la Kiwanja cha ndege cha Tabora. Ufafanuzi ninaouomba, kwenye hotuba ya Waziri alipotamka katika ukurasa wa 80 wa kitabu chake cha hotuba kwamba kiwanja cha Tabora ni moja ya viwanja ambavyo upembuzi yakinifu umekwishakamilika, lakini katika kitabu hiki tunachokijadili sasa hivi naona viwanja ambavyo upembuzi yakinifu umekamilika vimetengewa pesa lakini Tabora haimo, naomba ufafanuzi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi wa hoja ya kaka yangu Mheshimiwa Kaboyonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tabora, ni moja katika viwanja saba ambavyo vilikuwa vimepata ufadhili wa *World Bank* kwa ajili ya usanifu na upembuzi yakinifu na tumefanya hivyo kwa sababu viwanja hivi ikiwemo cha Tabora, Serikali ina nia thabiti ya kuviendeleza na kuvijenga ili miundombinu yake ikidhi haja na matarajio ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa ambazo zinaonekana hapa ni zile ambazo Serikali, kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ndiyo imeweka pesa katika viwanja hivi. Kitu ambacho ninaweza nikamdokezea ndugu yangu Kaboyonga ni kwamba Mamlaka ya TAA, pia ina bajeti yake ambayo inatenga kwa ajili ya matengenezo katika viwanja vya ndege, wao wameikasimu Tabora, wakairuhusu Serikali Kuu iweke kwenye viwanja vingine. Bahati mbaya sina kasma ambayo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekasimia mwaka huu wa fedha lakini wamenihakikishia kwamba wameikasimu vizuri, kwa hivyo bila shaka wana Tabora watakuwa na faraja.

MWENYEKITI: Nikumbushe tu Mheshimiwa Waziri kwamba mwaka 1978, Serikali ilikwishatoa zabuni ya kujenga uwanja wa Tabora na Mkandarasi Aulagaden Rose wa Kenya alifika pale akaleta lami na kototo, ikatokea vita ya Nduli Idd Amin, mradi wote ukahamishiwa Mwanza. Naweka tu historia vizuri ili msishangae. (*Kicheko*)

Halafu kuna jambo, unajua Mwenyekiti asipoelewa mambo, nayo si vizuri. Nataka nielewe jambo moja. Pale kwenye ukurasa wa 186, *Subvote 2005, item 4112*. Kidahwe –Malagalasi – Tabora. Nilielewa kwamba ndani ya hii, ndiyo ule mpango wa kujenga barabara kuanzia Tabora kwenda Kaliua unianza kwa maana kwenda Tabora,

kwenda Tumbi, si ndiyo zimo humu? Nataka kufahamu, unajua Mwenyekiti asipofahamu mambo mengine... (Kicheko)

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Kiti kina haki ya kupata ufafanuzi mzuri ili kiweze kuongoza kwa njia ambayo itaridhisha Bunge lako la viwango.

Ni kweli kabisa katika kifungu hiki cha 4112 Kidahwe –Malagalasi –Tabora, humu ndani yake, moja ni kwamba tuna mpango ambao tunaujadili sasa hivi pamoja na wenzetu wahisani wa nje kwa ajili ya kujenga barabara ya Tabora – Urambo mpaka Kaliua. Majadiliano haya hayajafikia ukamilifu lakini kwa kipindi hiki ambacho hatujakamilisha majadiliano hayo, tumechukua kipande katika barabara hiyo hiyo ili kuonesha kwa wahisani kwamba tuna kiu ya kujenga barabara ya Tabora na tumekasimia pesa kwa ajili ya kujenga walau kilomita 16 kuanzia Tabora kuelekea Kaliua ambayo itatufikisha mpaka Tumbi. Kwa hiyo, hiki kipande kimo humu.

MWENYEKITI: Prof. Kapuya, unasikia mambo hayo na Dr. Msekela, unajua sisi watatu, wote hatuwezi kuuliza. Kwa hiyo, basi kwa niaba ya wenzangu, nimepenyeza na kuchomeka hapo. (Kicheko)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif.2006 - *Transport Services Division* Shs.2,000,000,000/-

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif.5002 - *Safety and Environment Division*Shs.1,282,800,000/=

MWENYEKITI: Samahani Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, huwa ni vigumu kuona kama amesimama au? (Kicheko)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Angalau sauti yangu inasikika. Ninaomba katika kifungu hiki cha 5002, nipatiwe ufafanuzi, kwa kuwa kinazungumzia usalama na mazingira, je, katika hizi pesa zilizotengwa zinahusisha ujenzi wa vyoo barabarani? Kama ambavyo tumeshuhudia katika tangazo la TIGO, watu wanavyoachwa njiani na hivyo simu kuwasaidia na vilevile kuwaelimisha akina mama ambao wengi wao wanajihusisha sana na shughuli za ujenzi na kama sivyo, je, kuna mpango wowote au Wizara iko tayari kuwaomba TIGO baada ya lile tangazo na kuona tatizo la watu wanaotoka Songea kama walivyoonesha basi kikajengwa choo angalau kimoja katika barabara ile?

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa hoja ya Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuna tatizo hili la kuchimba dawa katika barabara zetu kuu wakati tun safiri katika maeneo mbalimbali na swali hili limejitokeza mara kadhaa kwa Wabunge tofauti katika mikutano yetu mbalimbali ya Bunge.

Sasa kwa ajili ya kujibu hoja hizo, katika vifungu hivi hapa hatuna kifungu maalum ambacho kitatumika kwa ajili ya kazi ya kujenga vyoo. Lakini Serikali imetoa maelekezo tayari kwa msimamizi wa ujenzi wa barabara hizi za kitaifa ambaye ni Wakala wetu wa *TANROAD* kwamba kuanzia sasa *design* zozote ambazo zinaandaliwa ama usanifu wowote unaoandaliwa uambatane na ujenzi wa vyoo katika barabara zile kuu ambazo zinatengenezwa ili ziweze kujenga mazingira salama kwa ajili ya wasafiri na wananchi kwa ujumla.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 6002 - Road Division Shs.0/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa, kabla Katibu hajasema kitu, nilikuwa napokea kwa maandishi hapa baadhi ya hoja, sasa natoa majibu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Dr. Diallo. Ni hivi, kungekuwa na mabadiliko, ndiyo Sekretarieti hapa ingeweza kusimama kuomba hiyo hoja isemwe maana ya mabadiliko halafu tupitishwe. Kwa kuwa Kamati ya Miundombinu wamekubaliana na Serikali baada ya kusikiliza hoja ya Mheshimiwa Dr. Diallo, wamekubaliana kwamba hakutakuwa na mabadiliko na badala yake zitatafutwa fedha shilingi bilioni 40 kuongezea kwenye shilingi bilioni 5 kwa ajili ya barabara ya Dodoma - Babati. Kwa hiyo, hoja ya kupunguza kwenye sehemu mbalimbali inakuwa imefutika yenyewe kwa wakati huu. Kwa hiyo, ndiyo sababu hatukusimama kuweza kujadili hoja hiyo. Ahsante sana, Katibu kwa shughuli inayofuata. *(Makofi)*

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mtoa hoja kuweza kutoa taarifa kuhusu kazi iliyofanyika kwenye Kamati, naomba kusema kwamba majibu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Selelii bado sijayapata. Kwa hiyo, siwezi kutoa mwongozo wowote. Namwomba mwenzetu awe na subira Bunge bado linaendelea, yakishakamilika basi tutayatoa hapa.

Sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kuhusu taarifa ya kazi ya Kamati.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi imepitia makadirio ya Bajeti ya Wizara

ya Miundombinu kwa mwaka 2009/2010, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe makisio ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu
kwa Mwaka 2009/2010 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge na nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri umechangia sana kuwezesha hoja hii kuweza kupita kwa sababu wewe ni mtu msikivu, ni Waziri ambaye kwa kweli hubabaiki, unafanya kazi yako kwa uaminifu mkubwa, kwa kweli tunashukuru sana kwamba hali hii umeweza kuidhibiti vizuri na sasa tumemaliza shughuli hata kabla ya wakati. (*Makofi*)

Sasa baada ya pongezi hizo, naomba mzingatie yaliyozungumzwa ili Mungu akitujalia katika mwaka ujao basi mjadala wa Wizara hii usiwe mgumu kama ilivyokuwa mwaka huu.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo, ile Semina ambayo ilikuwa ifanyike leo kwa sababu dhahiri, imebidi tuiahirishe na inaelekea sasa TCRA, Mamlaka ya Mawasiliano, watashauriana nasi kuhusu tarehe 19 au tarehe 26, ili semina hiyo iweze kufanyika. Kwa hiyo tuzingatie hilo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Chama cha Hiari cha Wabunge Wawakilishi wa Wafugaji, anawatangazia Wabunge wote wa maeneo ya wafugaji, kuwa leo tarehe 4 Julai kutakuwa na kikao muhimu katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya kuahirishwa kikao hiki cha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, nawaarifu kwamba wakati wa majadiliano wa hotuba ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, hasa kwenye lile suala la mazingira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, aliahidi kwamba Wajumbe kutoka Kamati mbili watakwenda North Mara hivi punde. Sasa nafurahi kuwafahamisha kwamba safari hiyo ni leo kwa ndege na wanaokwenda kutuwakilisha kutoka Kamati hizo mbili wakiongozwa na Mheshimiwa Job Ndugai ni wafuatao:-

Yeye mwenyewe Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa na Mheshimiwa Charles Mwera. Mipango yote ya kuwapokea huko wakaone athari zilizotokea ama vinginevyo basi wataikuta huko, tunawatakia safari njema na kazi njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, anaomba leo na yeye kaomba Ukumbi wa Pius Msekwa, nadhani itabidi msikilizane au ukumbi wa Pius Msekwa sehemu (b) inawezekana. Kwa hiyo, Kamati ya Huduma za Jamii mara baada ya kuahirisha Bunge wakutane Ukumbi wa Pius Msekwa (b).

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Klabu ya Kulenga Shabaha, *Bunge Range Club*. Mnajulishwa kuwa zoezi la kulenga shabaha lililopangwa kufanyika Jumapili tarehe 5 Julai, limeahirishwa mpaka Jumapili inayofuata ya tarehe 12 Julai. Kwa hiyo, kesho hakutakuwa na zoezi hili kule Makutupora badala yake litafanyika Jumapili ijayo na kuahirishwa kwa zoezi hilo kumetokana na kusomwa kwa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa yaani wenyeji wenu wamo katika maandalizi ya hotuba yao ambayo ni siku ya Jumatatu, kwa hiyo hadi hapo tarehe 12.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wetu hapa, wachezaji na viongozi wa timu ya mpira wa miguu ya *Arusha Wazee Sports Club*. Timu hii imetokea Mkoani Arusha na iliwasili jana kwa ajili ya mechi itakayochezwa leo saa 10.30 jioni. Naomba *Arusha Wazee Sports Club*, tafadhali na viongozi msimame. Wale pale, karibu sana. Tunafurahi sana ushirikiano wa wananchi wa rika mbalimbali kuweza kufika Bungeni na kushiriki pamoja na Waheshimiwa Wabunge, tunawapongeza sana ndugu zetu wa Arusha karibuni sana. Ila nasikitika kwamba jioni sijui kama mtatoka mmefurahi. Maana hii timu ya Bunge ni kabambe kwelikweli. Kwa hiyo, kwa tangazo hili, naomba Waheshimiwa Wabunge wote tufanye jitihada, tukashangilie tuone mpira mzuri, yeyote atakayepata nafasi basi muweze kuwa kule.

Saa moja na nusu leo usiku, kutakuwa na tafrija ya Wizara ya Miundombinu pale *St. Gaspers*. Kwa hiyo, saa kumi mpira, saa moja na nusu unakwenda kupata; na mnajua tena Wizara ya Miundombinu mambo yake sio madogo. Kwa hiyo, mnaalikwa kwenye hafla ya Wizara ya Miundombinu pale *St. Gaspers*.

Waheshimiwa Wabunge, huku nikiwatakia *weekend* njema, naahirisha sasa Bunge hadi Jumatatu tarehe 6 Julai, 2009, Saa Tatu Asubuhi.

(*Saa 6.03 Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,
Tarehe 6 Julai, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)

